

# Uachiliaji wa Uwezo wa Vijana Chipukizi



Taasisi ya Ruhi





Kitabu cha 5

# Uachiliaji wa Uwezo wa Vijana Chipukizi

Taasisi ya Ruhi

Vitabu katika mlolongo:

Hapo chini yapo majina ya vitabu vilivyopo kwa sasa katika mlolongo ulioandaliwa na Taasisi ya Ruhi. Vitabu hivi vinakusudiwa kutumika kama mlolongo mkuu wa kozi katika juhudi ya kimpangilio ili kuimarisha uwezo wa vijana na watu wazima kuhudumia jumuiya zao. Taasisi ya Ruhi pia inakuza seti moja ya kozi zinazochepua kutoka kitabu cha tatu katika mlolongo kwa ajili ya kuwafunza walimu wa madarasa ya watoto ya Kibahá'í, na halikadhalika seti nyingine kutoka Kitabu cha 5 kwa ajili ya kuinua wahuishaji wa vikundi vya vijana chipukizi. Hizi, pia, zimeoneshwa katika orodha hapo chini. Inapaswa kukumbukwa kwamba orodha hii inaweza kubadilika kadiri uzoefu uendeleavyo ugani, na majina ya ziada yataongezwa kadiri idadi ya vipengele vya kimtaala vinavyoendelea kukuzwa vifikiapo hatua ambapo vinaweza kusambazwa kwa upana.

| | |
|---|---|
| Kitabu cha 1 | *Mawazo juu ya Maisha ya Roho* |
| Kitabu cha 2 | *Uinukaji kwa Kuhudumu* |
| Kitabu cha 3 | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 1* |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 2* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 3* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 4* (kozi ya mchepuo) |
| Kitabu cha 4 | *Wadhihirishaji Pacha* |
| Kitabu cha 5 | *Uachiliaji wa Uwezo wa Vijana Chipukizi* |
| | *Msukumo wa Awali: Mchepuo wa kwanza wa Kozi ya Kitabu cha 5* |
| | *Duara Lipanukalo: Mchepuo wa pili wa Kozi ya Kitabu cha 5* |
| Kitabu cha 6 | *Ufundishaji Hoja* |
| Kitabu cha 7 | *Kutembea Pamoja kwenye Njia ya Huduma* |
| Kitabu cha 8 | *Agano la Bahá'u'lláh* |
| Kitabu cha 9 | *Kupata Mtazamo wa Kihistoria* |
| Kitabu cha 10 | *Kujenga Jumuiya Hai na Zenye Kupuma* |
| Kitabu cha 11 | *Nyenzo za Kimwili* |
| Kitabu cha 12 | *Familia na Jumuiya* |
| Kitabu cha 13 | *Kujihusisha katika Shughuli za Kijamii* |
| Kitabu cha 14 | *Kushiriki katika Mjadala wa Umma* |

Hakimiliki © 2015, 2022 na Ruhi Msingi, Colombia
Haki zote zimehifadhiwa. Toleo la 2.1.2.PE.PV (tafsiri ya muda) zilizochapishwa Mei 2023
ISBN 978-628-95545-0-2

Kilichapishwa awali kwa Kihispania kama *Liberando los poderes de los prejóvenes*
Hakimiliki © 2006, 2014, 2022 na Ruhi Msingi, Colombia
ISBN 978-628-95102-2-5

Taasisi ya Ruhi
Cali, Colombia
Barua pepe: instituto@ruhi.org
Tovuti: www.ruhi.org

# Yaliyomo

Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi ........................ v

Msimu wa Mchipuo wa Maisha .......................................... 1

Rika la Matumaini ............................................................ 47

Kuhudumia kama Mhuishaji ............................................. 87

# Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi

Tangu kuanzishwa kwake mwanzoni mwa miaka ya 1970, Taasisi ya Ruhi imejitahidi kuhudumia kupitia shughuli zake za kielimu vijana wenye umri wa miaka kati ya 12 na 15, aghalabu maarufu kama "vijana chipukizi", ambao huwakilisha kundi hilo maalum la jamii. Kama ilivyo shuhudiwa udhanifu na uwezo wa wengi katika rika hili, Taasisi ilishawishika juu ya umuhimu wa kuwapatia fursa ya kuchunguza idadi fulani ya dhima na dhana ambazo zingewawezesha kushughulikia michangamano ya maisha, kupambana na majeshi ya uozefu wa maadili yanayopata nguvu kila mahali, na kuwa mawakala hai wa mabadiliko ya kijamii. Miongo kadhaa iliyofuata ilijumuisha kipindi cha vitendo na tafakari kilichofaidika zaidi na zaidi kutoka uzoefu wa ulimwengu mzima katika kuhudumia vijana chipukizi kutoka kwenye usuli tofauti, ikijumuisha juhudi katika uwanja huu wa maendeleo, haswa zaidi katika eneo la uwezo wa kusoma na kuandika. Hadi kufikia mwaka 2000, dhana ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi ilikuwa imeshaibuka na, pamoja nayo, sura tofauti za programu ya miaka mitatu inayotafuta kuachilia uwezo wao wa akili na wa kiroho katika huduma kwa jamii ya wanadamu.

Kama jitihada nyingine za Taasisi ya Ruhi, programu ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi inatolewa mashinani kupitia utaratibu wa elimu ya mbali ambayo hujumuisha, katika suala hili, vipengele vitatu vikuu: "kikundi cha vijana chipukizi", "mhuishaji", na seti mahsusi ya nyenzo. *Uachiliaji wa Uwezo wa Vijana Chipukizi*, kitabu cha tano katika mlolongo mkuu wa Taasisi, kimekusudiwa kuwasaidia wale ambao wangependa kutoa programu ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi katika vijiji na ujirani wao. Ni cha kwanza katika mlolongo wa kozi, kinachochepuka kutoka mlolongo mkuu, ambacho kitawasaidia watu binafsi kukuza uwezo unaohitajika kuhudumia kama "wahuishaji" — jina ambalo, ndani yake lenyewe, huongelea asili ya tendo la huduma linalohusika nalo. Wakati siyo kila mmoja atakaye soma kitabu ataingia katika uwanja huu wa jitihada, inatumainiwa kuwa wote watapata msukumo kutoka mada zinazojadiliwa na watatambua umuhimu wa kuwa makini ipasavyo kwa matumaini bora ya vijana chipukizi — hili, kama suala nyeti la ujengaji wa utamaduni ambao utaendeleza mielekeo kwa vijana ambao ni tofauti kabisa kuliko ule uliyodumishwa katika jamii nyingi hivi sasa. Katika mazingira kama hayo, basi, yatawafanya hata wale ambao hawahusiki moja kwa moja katika program kuwa tayari kutoa msaada wao kwenye shughuli zinazoendelea kushamiri.

Wale ambao wanahudumu kama wakufunzi wa Kitabu cha 5 wanachopaswa kutambua ni kwamba, miongoni mwa washiriki, watakuwepo vijana wengi walio mwishoni mwa ujana wao au mwanzoni mwa miaka ishirini ambao waliingia katika mlolongo mkuu wa kozi kwa shauku iliyowazi ya kutoa huduma kama wahuishaji, na pamoja na uwezo wote uliofichika unaohitajika kufanya hivyo. Baadhi watakuwa wamekutana na Imani kupitia majadiliano pamoja na wanarika wenzao ambao walitilia mkazo nafasi wanayoweza kuwa nayo katika kuwaelimisha vizazi vichanga. Wengine watakuwa wamepitia program ya uwezeshwaji wa kiroho wao wenyewe kama vijana chipukizi na walianza kusoma Kitabu cha 1 punde tu baada ya hapo. Haijalishi kwa namna gani wameletwa kwenye mchakato wa taasisi, sasa wao wataunda sehemu ya kiini kinachoendelea kukua cha watu binafsi katika kijiji au ujirani wao

wakijidhatiti kwenye uboreshwaji wake na, katika muktadha huu, watapata uzoefu wa kutembelea kaya kwa minajili ya kuchunguza pamoja na familia mada kuu za Imani—tendo la huduma lililoelezwa katika Kitabu cha 2. Kama sehemu ya kiini hiki, idadi yao kubwa pia itahusishwa kwa karibu na angalau kikundi kimoja cha vijana chipukizi katika eneo na watamsaidia mhuishaji kutekeleza shughuli tofauti na kuungana naye katika ziara za mara kwa mara kwa wazazi kwa ajili ya kujadili juu ya dhana na mbinu zinazohusiana na programu. Kufikia hapa, wao wote watakuwa wamepata ujuzi mwingi kuhusu mafundisho ya Kibahá'í, ambayo yatakuwa yameimarisha kina cha ujuzi kupitia usomaji wa Kitabu cha 3 na cha 4, na watadhihirisha stadi, uwezo, mielekeo na sifa za kiroho zinazohitajika kuanzisha na kudumisha maongezi yenye maana pamoja na marafiki na majirani. Ni hususan hapa, wafikapo kwenye Kitabu cha 5, kwamba umuhimu wa mchakato wa ujengaji uwezo ambao kiasili umo katika mlolongo mkuu wa kozi za Taasisi ya Ruhi — mchakato uliotungwa kwa ajili ya kutembea njia ya huduma — utakuwa dhahiri. Kuhusisha kikundi cha vijana chipukizi katika program ya miaka mitatu kwa ajili ya uwezeshwaji wao wa kiroho ni tendo muhimu la huduma, na juhudi za wahushaji wachanga za kufanya kazi hiyo itategemea, kwa kiasi kikubwa juu ya uwezo walioujenga kiuthabiti katika njia hadi sasa.

Kitengo cha kwanza cha kitabu, "Msimu wa Mchipuo wa Maisha", humakinikia juu ya sifa ambazo maandiko ya Imani huonesha zinahitaji kuainisha kipindi cha ujana. Kutoka uchambuzi uliofanywa, polepole muono unaibuka wa mchango uliyofanywa na kila kizazi cha vijana katika huduma kwa Hoja ya Mungu na kwa jamii ya wanadamu. Mkufunzi atataka kuhakikisha kwamba washiriki waondoke katika masomo ya kitengo wakiwa wameamshwa na muono unaoendelea kukunjuka, kwani ni muono huu unaotaarifu program ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi na ambao unatoa mwelekeo kwa jitihada zao za kuwahusisha vijana wadogo katika shughuli zake.

Kwa uhakika, kitengo kinafunguliwa kwa kuwaomba washiriki kufikiri juu ya zile tabia ambazo wanatumaini kuwa vijana wadogo watakuza hadi kufika mwisho wa programu ya miaka mitatu watakapokuwa na umri wa miaka 15 — ambao unaonwa kama kizingiti cha ukomavu katika mafundisho ya Kibahá'í — na kuingia katika "upevu" wa ujana wao. Mkufunzi anapaswa kuelewa kwamba kusudi la zoezi siyo la kuchunguza katika vipengele vya program au kufikiria uwezo usiodhihirika wa vijana chipukizi, uchunguzi ambao utafuatiliwa katika kitengo cha tatu na cha pili, kwa mfuatano. Bali, kusudi ni kuleta kwenye umakinifu wa papo hapo taswira ya kijana mdogo alie tayari kuchukua nafasi yake miongoni mwa kizazi kijacho cha wale ambao wataendeleza Hoja ya Mungu na kujidhatiti wao wenyewe kwa maendeleo ya ustaarabu. Kwa washiriki, zoezi litaongeza uthamini wao wa asili ya shughuli ambayo wataanza kuifanya baada ya muda mfupi kama wahuishaji na watayapa majadiliano yao yatakayofuata, maana yenye undani zaidi.

Dhidi ya mandhari hii, kwa hiyo, kitengo hiki kinawasilisha idadi fulani ya vifungu kutoka kwenye maandiko ambayo yanaweka wazi baadhi ya dhana zinazohusu kipindi cha ujana. Miongoni mwa dhana zilizotambulishwa mapema katika kitengo ni mwingiliano kati ya huduma, elimu na maandalizi ya siku za baadae, suala ambalo linaweza wakati mwingine kutawala akili za vijana. Kile kinachowekwa wazi ni kwamba, pale ambapo maisha yanaangaliwa kwa ujumla wake, sura zake tofauti, badala ya kufarakana moja kwa nyingne, zinaweza kutumika kuimarishana. Zoezi la Sehemu ya 10 litawasaidia washiriki kufikiria juu ya nini hili humaanisha kivitendo. Sharti uangalifu ufanyike, isijetokea kwamba wao wanayapitia mazoezi bila kufikiri na wanashindwa kufahamu jinsi chaguo fulani za kimaisha na jinsi ya kufikiri zinavyoweza kuibua mikanganyiko ya kufikirika na mvutano wa kimawazo wanaoutengeneza.

Dhana nyingine inayoongelewa katika kitengo, moja kati ya lengo lake, ni ile ya kusudi la kimaadili lenye pande mbili. Washiriki, bila shaka watakuwa wanafahamu dhana hii kutokana na masomo ya vitabu vilivyotangulia. Hapa inaongelewa kwa kina zaidi, na inawapasa kuweka umakini zaidi kwa zile sehemu zinazohusu uchunguzi wake, ambazo zinaanza kwa kueleza ubadilikaji wa aina mbili — kwenye ngazi ya mtu binafsi na katika muundo wa jamii — kama ilivyotarajiwa katika maandiko ya Kibahá'í. Kitengo kinapendekeza, katika mwangaza huu, kwamba vijana wawe wamejawa kusudi la hisia kali la kuchukua wajibu wa ukuaji wao wenyewe wa kiakili na wa kiroho na kutoa michango ya kudumu kwa maendeleo ya jamii. Pia inadai, zaidi, kwamba sura hizi mbili za kusudi la kimaadili zinakamilishana na kimsingi haziwezi kutenganishwa, kwa sababu viwango na tabia za watu binafsi hubumba mazingira yao na hayo, kwa upande mwingine, hubumbwa na miundo ya kijamii na michakato. Baadhi ya washiriki pengine watapata changamoto kuthamini matokeo ya dai hili, ambalo limechunguzwa katika Sehemu ya 16. Mitazamo ya kiulimwengu inayotawala — ambayo, kwa upande mmoja, huweka mkazo mkubwa juu ya ubinafsi na uhuru wa mtu binafsi au, kwa upande mwingine huweka mkazo wa kupindukia juu ya nguvu za kijamii na michakato ya kisiasa — zinazoweza kupinda uhalisi na kubumba itikadi na ruwaza za fikra, aghalabu hazionekani. Wakati wa kufanya mazoezi pamoja na kikundi, mkufunzi anapaswa kutambua changamoto inayoweza kuibuka na kuwasaidia wajumbe, ikihitajia, kutambua madai ambayo hayana uwiano na tamko la Mlinzi lililonukuliwa katika sehemu hiyo. Uchunguzi wa dhana yenye kusudi lenye pande mbili kwa hiyo unafikia tamati, hivyo, kwa kupendekeza kuwa ni katika uwanja wa huduma peke yake kwamba kusudi hili linaweza kutambuliwa. Huduma, kitengo hueleza, huunganisha ukamilishaji wa uwezo wa mtu binafsi pamoja na maendeleo ya jamii.

Kitengo cha pili kinaitwa "Rika la Matumaini", na kinahusu vijana chipukizi na uwezekano mwingi walio nao. Kinajaribu kuimarisha katika akili ya wale wanaokisoma, uelewa kwamba vijana chipukizi ni wajumbe wa kikundi cha rika maalum ambacho kina sifa zake mahususi — sifa ambazo haziachi shaka kwamba, japokuwa lingekuwa kosa kuwachukulia kama watoto wadogo, vilevile ingekuwa ni ya kupotosha kuwahamasisha kuiga mienendo ya kiutu uzima ambayo kiasili ni ya juujuu, ambayo inaendelea kuota mizizi katika maeneo mengi zaidi na zaidi. Kitengo hiki kinatumaini kuweka wazi kwamba mbinu iliyochukuliwa na jumuiya ya Kibahá'í kuelekea kundi rika hili, ikiwa imebumbwa na maandiko ya Imani na kuchochewa na mifano kama ile ya kijana Rúḥu'lláh, ni tofauti kabisa kuliko mbinu zilizo wekwa juu ya dhana na nadharia, ambazo zimeenea, ambazo nyingi kati ya hizo huonesha kuwa vijana chipukizi ni waasi na wamezoea kukabiliwa na hatari.

Sambamba na malengo yaliyopo hapo juu akilini, kitengo kinachukua fursa ya kuangalia kwa kifupi asili ya ujana wa awali na halafu huwaambia washiriki kutafakari juu ya changamoto ya kuelekeza utambuzi unaoendelea kukua wa vijana wadogo wa rika hili, ipasavyo. Katika hili, kitengo hiki kinatoa angalizo: jitihada kama hizi lazima ziepukane na mitego ya baadhi ya programu, ambazo badala ya kuelekeza utambuzi binafsi unaoendelea kuongezeka uliomo katika kipindi hiki cha mtungo cha maisha kuelekea kwenye huduma pasina ubinafsi kwa wengine, kuigeuza juu ya "nafsi" na, inasikitisha kwamba, mwishowe inawafanya mateka wa "nafsi ng'ang'anizi". Sehemu ya 5 hadi ya 9 inajaribu kuwatahadharisha washiriki kuhusu baadhi ya hatari za hila za mtego huu kwa kuwapitisha katika mfuatano wa dondoo husika kutoka katika maandiko ya Kibahá'í. Kitengo hiki kisha kinaenda kufikiria athari za mazingira ya kijamii juu ya maisha ya vijana wadogo, hutambulisha dhana ya "kikundi cha vijana chipukizi" kama mazingira ya msaada wa pamoja, na kinaeleza mwelekeo unaopaswa kufuatwa na wale wanaoinuka kuhudumu kama wahuishaji wa vikundi kama hivyo.

Kitengo cha tatu, “Kuhudumu kama Mhuishaji”, kinaendeleza kwa namna fulani pale ambapo cha pili kinaishia na hujaribu kuwafahamisha zaidi washiriki juu ya asili ya tendo la huduma. Baada ya kupitia baadhi ya vipengele vya kikundi cha vijana chipukizi, kitengo hiki kinaanza majadiliano kuhusu nyenzo, ambazo usomaji wake huwakilisha kiini cha programu. Sehemu kubwa ya kitengo hiki imetumika kwa ajili ya majadiliano haya, na mkufunzi anapaswa kuelewa vizuri azma yake, ambayo si ya kuwaeleza tu nyenzo washiriki, bali kuwapa umaizi katika kile kinachohusika katika mchakato wa uwezeshwaji wa kiroho na jinsi nyenzo zinavyotafuta kulea utendaji wake. Nukuu kutoka kwenye nyenzo zimejumuishwa kote, lakini vitabu viwili vimechambuliwa kwa ujumla wake — *Pepo Nyanana za Uthibitisho* na *Roho ya Imani* — na washiriki watahitaji kuwa na nakala za vitabu.

Suala la uwezeshwaji wa kiroho linahitaji, kwa ujumla, mawazo na tafakari kutoka kwa wakufunzi. Hakika, mchakato wa kielimu unaoanzishwa na kozi za taasisi unaweza, katika uchambuzi wa mwisho, kuonwa kama mbinu ya uwezeshwaji wa kimaadili na wa kiroho, ule ambao kupitia humo, watu wa kila tabaka la maisha na kila usuli wanawezeshwa kuinuka kushiriki katika ujenzi wa ulimwengu mzuri zaidi. Dhana ya uwezo inayotumika hutofautiana kwa kiasi kikubwa kutoka fafanuzi zilizoenea ambazo zinahusisha madhumuni ya kutawala au kuchochea wengine wakubali matakwa yake na mahitaji. Kusudi, badala yake ni kuwa mifereji kwa ajili ya kutiririsha uwezo wa kiroho wa mtu: uwezo wa umoja, wa upendo, wa huduma yenye unyenyekevu, wa vitendo safi. Jinsi ya kuchangia kwenye mabadiliko yanayohitajika kwa ajili ya uendelezaji wa mchakato kama huo — la, kuchapuza — ni kiini cha tendo la kuhudumia kama mkufunzi, pamoja na tajiriba katika kuhusisha kikundi baada ya kikundi katika usomaji wa kozi, kila mkufunzi anaweza kupata vianga katika vichocheo vingi vinavyohusika vinavyoingiliana, ambavyo hakuna hata kimoja ambacho ni muhimu zaidi kuliko uleaji wa uelewa wa kweli.

Katika kitabu hiki, bila shaka, shauku ilioko mbele ya mkufunzi husonga mbele zaidi, hadi kizazi kinachofuata na kwa asili ya mchakato wa kielimu ambao utawawezesha vijana wadogo kutumia uwezo wao uibukao ipasavyo. Kwenye moyo wa mchakato huu upo uwezo wa fikra na kauli unaoimarishana. Uwezo wa akili unaohusisha kufikiri kinadharia, ambao unaongezeka kwa kasi katika kipindi cha ujana wa awali, unapata nguvu zaidi ndani ya vijana chipukizi kadiri wanavyojifunza kutumia dhana husika za kisayansi, kimaadili, na kiroho katika uchambuzi wao wa ulimwengu unaowazunguka na kwa jitihada zao za mwanzo za utendaji katika jamii. Walakini, japokuwa ni wa muhimu kiasi gani, uwezo wa uchambuzi wa kimantiki unahitaji mtazamo wa kiroho. Kupitia humo, njia za uelewa, ambazo hazipatikani kupitia utumiaji wa uwezo wa kiakili peke yake, hufunguka. Vijana chipukizi, kwa hiyo, wanapaswa kusaidiwa kutambua nguvu za kiroho na kubaini kanuni za kiroho katika hali wanazokutana nazo ikiwa wanataka kufanya chaguzi sahihi za kimaadili. Kwamba muundo wa kimaadili unaoongoza mawazo na tabia ya mtu unaungana kwa karibu na muundo wa lugha ambao huelezea wazo ni nguzo ya kimsingi inayoonwa na mchakato wa kielimu. Wowote uwao umaizi ambao umetolewa katika vitengo viwili vya Kitabu cha 5 katika mchakato huu, Sehemu ya 5 hadi ya 19 ya kitengo cha tatu inajitahidi kuziweka wazi sura zake tofauti, ikichota kutoka mifano kutoka katika vitabu vinavyotumika katika programu, kama inavyohitajika. Kila mkufunzi angepaswa kupitia sehemu hizi kwa uangalifu wakati akijiandaa kuongoza kundi lolote kupitia humo. Inatumainiwa kwamba washiriki watapata kutoka masomo yao uelewa wa uwezo wa vitabu kuwezesha vijana chipukizi kutoka tamaduni tofauti tofauti.

Katika mwanga wa majadiliano haya, hivyo, kwamba washiriki wanapewa fursa ya kuchambua vitabu vyote viwili, kimoja kinachoangukia kwenye kipengele cha “mwelekeo wa Kibahá’í’’ na kingine kinachowakilisha kipengele dhahiri cha Kibahá’í cha programu.

Vipengele hivi viwili hutambulishwa kwa washiriki mapema katika kitengo hiki, na mapitioyao yao ya *Pepo Nyanana za Uthibitisho* na *Roho ya Imani* hukusudiwa kuwasaidia kuona jinsi, katika mada na dhana zilizoongelewa na katika lugha iliyotumika, vitabu vyote viwili vinachangia kwenye madhumuni ya program yaliyoelezwa hapo juu. Dhana ya uthibitisho inayoongelewa katika kitabu cha kwanza, kwa mfano — kwamba kama mtu atafanya jitihada kuelekea kwenye malengo stahiki, yeye atavutia uthibitisho mtakatifu — huvuma ndani ya mioyo na akili za vijana wadogo kila mahali. Uelewa wanaoupata kupitia usomaji wa kitabu unaelekea kuwasaidia, pale wanapoanza kazi mpya zenye changamoto, kushinda woga na kutojiamini ambavyo aghalabu huambatana nayo, bila kujenga desturi haribifu, ambazo ni ishara ya mkazo mwingi unaotiliwa juu ya "nafsi". Kwa njia hii, hadithi ya kawaida lakini ya kina ikunjukayo katika kitabu, ambayo kwa kawaida ni miongoni mwa ya kwanza kusomwa na vijana chipukizi, huwaweka wengi katika njia ambayo huwalinda, angalau kwa kiwango fulani, kutokana na nguvu za ubomoaji zinazopasua mfumo wa jamii, nguvu ambazo zingewanyang'anya utambulisho wao wa kweli kama viumbe bora.

Vivyo hivyo, ufafanuzi wa dhana uliotolewa kwenye *Roho ya Imani* huwasaidia vijana chipukizi kutoka kila usuli kutafakari kwa kina juu ya masuala ya kifalsafa ambayo yanaanza kuingia akilini mnamo kipindi hiki cha maisha na kuona muunganiko tata uliyopo kati ya mambo ya kiroho na ya kimwili. Miongoni mwa dhana hizi ni, kwa mfano, mabadiliko ya kimwili na muonekano wa roho ya mwanadamu. Kile ambacho mkufunzi anapaswa kuthamini ni kwamba, kwa vijana wengi wadogo, wanaosoma Kitabu cha 5 na kuvuviwa kuwa wahuishaji, isipokuwa tu wamemaliza program ya uwezeshwaji wa kiroho wao wenyewe kama vijana chipukizi, mapitio ya *Roho ya Imani* yatajumuisha fursa ya kwanza kwa ajili yao kuchunguza kimpangilio dhana zilizowasilishwa, na wao sharti wapewe muda uhitajikao kufikiri kupitia athari zake.

Katika kuhitimisha mapitio haya, washiriki wanahamasishwa kutafakari juu ya kanuni ya upatano kati ya sayansi na dini, siyo tu kama dhana iliyoongelewa kwa uwazi katika kitabu, bali kama msingi wa majadiliano yote. Kile kinachopendekezwa ni kwamba sayansi na dini zinaweza kutazamwa kama mifumo miwili ya ujuzi na utendaji inayokamilishana ambayo kwayo ustaarabu huendelea. Umuhimu wa tafakuri hii inapaswa izingatiwe na washiriki, hususan wale wanaojiandaa katika uwanja huu wa huduma. Baada ya yote, kama upatikanaji kamili zaidi wa uelewa wa uhalisia ni sehemu nyeti ya mchakato wa uwezeshwaji wa kiroho, basi vitabu kwa ajili ya vijana chipukizi havina budi kuchota kutoka kwa vyanzo hivi vyote viwili vya ujuzi.

Wakati usomaji wa nyenzo utaunda shabaha ya msingi ya kikundi chochote cha vijana chipukizi wanaoshiriki katika program hii, wao pia watabeba shughuli nyingine zozote pamoja. Hizi zinajumuisha miradi ya huduma, michezo, sanaa, ufundi stadi, na tukio maalum mara moja moja. Sehemu ya 25 na 26 zinawakilisha kanuni na mawazo machache yanayohusiana na shughuli hizi lakini huzuia kwenda kwa maelezo ya kina zaidi, zikitanabahi kuwa maelezo yao mahususi yangehitaji kujitokeza kufuatana na hali za mahali. Licha ya hivyo, inatumainiwa kuwa mtindo na utekelezaji wa miradi ya huduma itatiliwa mkazo katika program, kwa kuwa huduma hutoa uwanja ambamo kusudi la kimaadili lenye pande mbili lililotajwa hapo awali liweze kujidhihirisha lenyewe. Kwenye hili, washiriki wanapaswa kuelewa kwamba miradi kama hiyo itakua mada ya mara kwa mara ya ushauriano kwenye mikutano na wahuishaji wenzi.

Kitengo hiki kinafikia mwisho kikiongelea masuala kadhaa yanayohusiana na kazi ya mhuishaji, kushiriki umaizi kuhusu namna ya kusaidia uundwaji wa kikundi cha vijana

chipukizi, jinsi ya kuendesha mikutano michache ya mwanzo, na jinsi ya kufanya mazungumzo na wazazi juu ya asili ya programu na maendeleo ya vijana wao wa kiume na wa kike. Tangu mwanzo, washiriki sharti watambue kwamba uwezo unaohitajika kuhudumu ipasavyo kama mhuishaji huongezeka kadiri muda upitavyo kupitia tajiriba na usomaji endelevu wa kozi zinazochepuka kutoka Kitabu cha 5. Hili linadai kiwango fulani cha kujidhatiti kwenye elimu ya vijana chipukizi ambao wengi wao wakiwa katika rika la miaka ya mwisho wa ujana wao na mwanzoni mwa umri wa miaka ishirini — katika msimu wa mchipuo wa maisha yao — wameonesha uwezo wa kufikia. Ni kutoka katika safu zao kwa hiyo, kwamba itaibuka idadi iongezekayo ya watu wale ambao watabobea kwenye njia hii maalum ya huduma, wakihusisha kikundi hadi kikundi kwenye program ya uwezeshwaji wa kiroho, na ambao, kwa namna hii watahakikisha kwamba matamanio ya kizazi kijacho yanafikiwa.



# Msimu wa Mchipuo wa Maisha

## Kusudi

Kupata uelewa fulani wa baadhi ya tabia ambazo zitawaainisha vijana, kama kigezo cha kuwahusisha vijana chipukizi katika program kwa ajili ya ya uwezeshwaji wao wa kiroho

## SEHEMU YA 1

Kipindi kati ya miaka kumi na mbili na kumi na tano huwakilisha muda maalum katika maisha ya mtu, kwani ni katika miaka hii ambapo yeye huacha utoto nyuma na hupitia mabadiliko makubwa. Wakati bado hawajafikia ujana wao kamili, watu katika rika hili kwa kawaida huitwa "vijana chipukizi". Kuwahusisha vijana chipukizi katika shughuli ambazo zinalenga kuongeza uwezo wao wa kiroho na kiakili na kuwaandaa kushiriki kikamilifu katika mambo ya jumuiya zao, ni kitendo cha huduma cha maana kabisa. Vitengo vitatu vya kitabu hiki vinalenga kwenye baadhi ya dhana, stadi, sifa, na mielekeo ambavyo uzoefu unaonesha kuwa vinahitajika na wale wanaotaka kutekeleza programu ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi iliyopendekezwa na Taasisi ya Ruhi.

Shughuli zinazounda programu hii kwa kawaida hufanyika katika vikundi vidogo, kwenye ngazi ya umma. Kama mhuishaji wa jitihada za kikundi kama hicho, utahusika na ukuaji wa vijana wadogo kadhaa ambao katika muda mfupi tu watafikia umri wa miaka kumi na tano, kizingiti cha ukomavu, ambapo watapata majukumu mapya. Katika kitengo hiki cha kwanza hatutotafakari sana juu ya sifa za vijana chipukizi bali juu ya aina ya vijana wapaswavyo kuwa kufuatana na ushauri kutoka maandiko ya Imani. Kinachopaswa kuwa wazi kabisa kutokana na vifungu mtakavyovisoma ni kwamba kuna idadi kadhaa ya tabia ambazo zinatakiwa kutofautisha kila kizazi cha vijana na hususani nguvu ambazo lazima zibumbe maisha yao. Inawezekana kabisa, bila shaka, kwamba ninyi wenyewe ni vijana mlio katika umri wa miaka ya mwisho ya ujana wenu na mwanzoni mwa umri wa miaka ishirini na, katika hali ambayo nyenzo zilizowasilishwa katika kitengo hiki zitawapatia fursa ya kuchunguza malengo yenu wenyewe na hali kadhalika vipaumbele vyenu.

## SEHEMU YA 2

Kwa kuanza, fikiria kikundi cha vijana chipukizi ambao hivi punde utafanya nao kazi. Kwa miaka mitatu ijayo utakutana nao kila mara kama rafiki wa kweli na utawasaidia katika kusoma na kuchunguza mawazo pamoja, katika ufanyaji mipango na kutekeleza miradi rahisi ya huduma, na katika kutafakari juu ya yale wanayojifunza kama kikundi kutoka uzoefu kama huo. Ingekuwa yakufaa kwako kuchukua muda sasa kufikiria mbele mwishoni mwa kipindi hicho cha miaka mitatu, wakati watakapokuwa wamehitimu programu. Kukusaidia kuweka wazi akilini mwako mwenyewe tabia unazotumaini zitakuja kuwatofautisha marafiki zako wadogo, fanya mazoezi hapo chini na washiriki wenzako wa kozi hii.

1. Je, vijana unaowatazamia wanaweza kuainishwa na kusudi lenye hisia za juu? Je, wangefikiria kusudi hilo ni lipi? ____________________________________________

   ________________________________________________________________________

   ________________________________________________________________________

2. Je, unatumaini kuwa wataelekeza nguvu zao kwenye kitu gani hasa?______________

   ________________________________________________________________________

   ________________________________________________________________________

3. Ni kitu gani kitakacho wapa hamasa kufanyia kazi malengo yao? ________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

4. Jinsi gani unatarajia wao watakua wanatambua changamoto zinazowakabili wanadamu katika wakati huu? Je, wanaweza kushawishika kwamba wana uwezo kwa uhakika wa kuchangia kwenye kuufanya ulimwengu mahali bora zaidi? ______________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

5. Wewe bila shaka ungependa marafiki zako vijana wawe wamepata, katika kipindi chenu cha pamoja, mwelekeo fulani kuelekea ujifunzaji. Mwelekeo huu unaakisika katika matamko yaliyopo hapa chini. Je, unaweza kuongeza mawili au matatu zaidi?

- Watapenda kusoma na watajaribu kuweka katika vitendo yale waliyojifunza.
- Watakuwa na tabia ya kutafakari juu ya matokeo ya matendo yao.
- Watakuwa na akili iliyo wazi na kuuendea ujifunzaji kwa unyenyekevu.
- Watakuwa na shauku kubwa ya kukuza uwezo wao wa kuhudumia wanadamu.
- Watatamani sana kupata ubora katika chochote wafanyacho.
- Watakuwa na shauku kuhusu usomaji wa masomo ya sayansi na sanaa.
- Watapata furaha kubwa kujifunza kufanya kazi kwa ajili ya maendeleo ya wanadamu kama ilivyo kwenye ukuaji wao wenyewe wa kiakili na kiroho kama watu binafsi.

- ____________________________________________________________________
- ____________________________________________________________________
- ____________________________________________________________________

6. Ni zipi kati ya kauli zifuatazo zinaelezea namna ambavyo unatarajia vijana unaowafikiria watajiongoza wenyewe?

_____ Viwango vyao vitakaribia zaidi au kidogo vile vinavyowekwa kwa ajili ya vijana na mielekeo ya duniani na mitindo.

_____ Watatazama vyombo vya habari mashuhuri kwa ajili ya kupata viwango vya kusimamia maisha yao.

_____ Watafuata katika nyayo za wale wanaojitahidi, licha ya changamoto ngumu kuishi kufuatana na viwango vya juu vya maadili.

_____ Wataweza kugundua pale ambapo matendo yao yanakwenda kinyume na imani zao kama mkanganyiko huo utatokea.

_____ Wataamini katika dhana kama umoja wa jamii ya wanadamu, usawa kati ya wanaume na wanawake na haki, lakini vitendo vyao vingeakisi kwa karibu zaidi desturi zilizokubaliwa na jamii ambazo zinaonesha ustadi katika mazungumzo ya dhana kama hizo, lakini hushindwa kutekeleza dhana hizo katika vitendo.

_____ Wataachana na fikra za viwango vya juu ili waishi kwa raha katika mazingira ya kijamii ambamo fikra hizo hazifuatwi.

7. Matamko yaliyopo hapa chini yanaeleza baadhi ya athari za maisha safi na ya kibikira. Je, unadhani itakuwa na umuhimu wa kiasi gani kwa vijana unaowafikiria kuweza kutafakari juu ya athari kama hizi? Je, unaweza kuongeza nyingine chache katika orodha?

- Kutokuwa na mienendo ya kipuuzi
- Kujitenga na starehe za kipuuzi na potovu
- Kutoruhusu anasa za ulimwengu kutawaondoa kutoka kusudi lao la juu
- Kutofuata vivutio na mitindo kama ni kinyume cha viwango vya usafi na ubikira
- Kutofikiria kuwa usafi maana yake pekee ni kutokufanya tendo la ndoa nje ya ndoa
- Kuwa wakadirifu katika namna wanavyovaa
- Kuwa wakadirifu katika namna wanavyoongea
- Kuwa wakadirifu katika chaguo zao za burudani
- Kutambulika kwa staha na unyenyekevu wao
- Kutokuwa na wivu na husuda
- Kutambulika kutokana na usafi, uungwana na akili safi
- Kuwa waangalifu kudhibiti tamaa zao za chini
- ____________________________________________
- ____________________________________________
- ____________________________________________

8. Katika miaka michache ambayo utakuwa pamoja na rafiki zako, ni imara kiasi gani unatumaini kuwa uwezo wao, kote kiakili na kiroho, utakuwa

- kushinda changamoto?
- Kustahimili katika jitihada zao za kufanikisha malengo yao?
- Kustahimili katika jitihada zao za kufanikisha malengo yao?

## SEHEMU YA 3

Hebu sasa tugeukie vifungu vichache kutoka maandiko ya Imani na kuchunguza jinsi vinavyomuelezea kijana. 'Abdu'l-Bahá husema:

**"Enyi wapendwa wa 'Abdu'l-Bahá! Maisha ya mtu yana msimu wake wa mchipuo na yamejaliwa utukufu mzuri mno. Kipindi cha ujana kinatofautishwa na nguvu na juhudi na hujulikana kuwa muda bora kabisa wa maisha ya mwanadamu. Kwahiyo jitahidini mchana na usiku ili kwamba mkiwa mmejaliwa nguvu za kimbinguni, mkisukumwa na nia angavu na kwa msaada wa uwezo Wake wa mbinguni na neema ya kimbinguni na uthibitisho, muweze kuwa mapambo ya ulimwengu wa jamii ya wanadamu, na mashuhuri miongoni mwa wale walioanzishwa katika elimu ya kweli na upendo wa Mungu. Inabidi mtofautishwe miongoni mwa watu kwa utakatifu wenu na kujitenga, ubora wa nia, ukarimu mkuu, dhamira, akili bora, ung'ang'anivu, uinuaji wa malengo yenu na sifa zenu za kiroho; ili muweze kuwa njia ya utukuzwaji na utukufu kwa Hoja ya Mungu na mahali pa mapambazuko ya majaaliwa Yake ya mbinguni; ili muweze kutenda kufuatana na ushauri na maagizo ya Uzuri Uliobarikiwa — maisha yangu yawe dhabihu kwa wapendwa Wake — na kwa kuakisi sifa za Kibahá'í na amali, muweza kutofautishwa kutoka wengine. 'Abdu'l-Bahá anatarajia kwa shauku kuwa kila mmoja wenu atakuwa mithili ya simba asiye mwoga anayetembea katika malisho ya ukamilifu wa mwanadamu na upepo mwanana uliojaa manukato ya miski unaovuma juu ya konde za sifa njema."[1]**

1. Kamilisha sentensi zifuatazo kulingana na teuzi hapo juu:

   a. Msimu wa mchipuo wa maisha ya mtu umejaliwa na ________________________ .

   b. Kipindi cha ujana kinabainishwa na ________________ na ______________ .

   c. Kipindi cha ujana hujulikana kuwa _________________________ katika maisha ya mwanadamu.

   d. Katika kipindi cha ujana sharti tujitahidi mchana na usiku ili kwamba tukiwa tumejaliwa __________________ , tukisukumwa na ________________________ na kwa msaada wa ______________________ na __________________________ na ____________________ , tuweze kuwa ______________ ya ulimwengu wa jamii ya wanadamu.

e. Katika kipindi cha ujana sharti tujitahidi mchana na usiku ili tuwe mashuhuri miongoni mwa wale walioanzishwa katika ______________________________ na ___________________ .

f. Katika kipindi cha ujana sharti tutofautishwe kwa _____________ wetu na _______________ .

g. Katika kipindi cha ujana sharti tutofautishwe kwa ______________________ la kusudi.

h. Katika kipindi cha ujana sharti tutofautishwe kwa ________________________ , ________________ , _________________ , ubora __________________ , uinuaji wa _____________ yetu na _________________ zetu za kiroho.

i. Katika kipindi cha ujana lazima tuwe _______________ za utukuzwaji na utukufu kwa __________________ na __________________ pa _____________ Yake.

j. Katika kipindi cha ujana lazima tujitahidi kujisimamia wenyewe katika _________ kwa ____________________ na __________________ wa Uzuri Uliobarikiwa.

k. ‘Abdu’l-Bahá anatarajia kwa shauku kuwa kila kijana aweze kuwa mithili ya ________________ anayetembea katika malisho ya _____________________ na __________________ upepo mwanana uliojaa manukato ya miski unaovuma juu ya konde za __________________________ .

2. Bila shaka mmewahi kusikia msemo mmoja au dhana nyingine maarufu kwamba vijana wanapaswa kumakinikia kwenye starehe, kwa sababu muda si mrefu watakabiliana na mambo muhimu ya maisha. Ni wazi kuwa fikra hizo haziwiani na maelezo ya hapo juu ya ‘Abdu’l-Bahá. Ni zipi baadhi ya hisia zinazozungukia dhana maarufu kama hii? Jadilini swali hili na kikundi cha marafiki ambao unasoma nao leo na andika hitimisho lako hapa.

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

## SEHEMU YA 4

Katika sala ifuatayo, 'Abdu'l-Bahá hueleza baadhi ya matumaini Anayowatakia vijana.

**"Ewe Bwana mwema! Kwa neema jalia jozi ya mabawa ya mbinguni kwa kila mmoja wa makinda hawa, na uwape nguvu ya kiroho ili waweze kuruka kupitia katika anga hili lisilo mipaka na kuingia kwenye vilele vya Ufalme wa Abhá.**

**"Ee Bwana! Imarisha miche hii michanga ili kila mmoja uwe mti uzaao, wa kijani na unaositawi. Zipe ushindi roho hizi kupitia uwezo wa majeshi Yako ya mbinguni, ili waweze kuvunja nguvu za makosa na ujinga na kukunjua viwango vya upatano na mwongozo miongoni mwa watu; ili waweze, sawa na pumzi ihuishayo ya msimu wa mchipuo, kuburudisha na kuhuisha miti ya roho za wanadamu na sawa na mvua za vuli wazifanye konde za eneo hilo kijani na zenye rutuba.**

**"Wewe ni Muweza na Mwenye uwezo; Wewe u Mpaji na Apendaye-wote."[2]**

1. Kamilisha sentensi zifuatazo kufuatana na teuzi hapo juu:

   a. 'Abdu'l-Bahá huwafananisha wale waliomo katika ujana wao kama makinda yahitajio jozi ya ____________________________ na anamuomba Mungu awape __________________________ ili waweze ________________ kupitia anga lisilo na mwisho na waweze ________________________________ Ufalme wa Abhá.

   b. Huwafananisha wale wenye umri mdogo kama ________________ michanga na anamsihi Mungu kuwaimarisha ili kwamba kila mmoja uwe ________________ , ________________ , na ____________________ .

   c. Anamuomba Mungu kuwapa ushindi ili waweze kuvunja ______________ za _______________ na _________________ na kukunjua ________________ vya _________________ na _________________ .

   d. Anaomba kwamba waweze, sawa na __________________ ihuishayo ya msimu wa ____________________ , kuburudisha na __________________________ miti ya ________________________ na sawa na _____________________________ wazifanye konde za eneo hilo ________________ na _____________________ .

2. Katika sala 'Abdu'l-Bahá anamuomba Mungu kuwajalia vijana uwezo wa kiroho. Ni zipi miongoni mwa zifuatazo unazihusisha na uwezo wa kiroho?

| | |
|---|---|
| ______ ubora wa kusudi | ______ ukarimu mkuu |
| ______ kumtegemea Mungu | ______ ubembe |
| ______ ubikira | ______ dhamira ya kutekeleza shughuli |
| ______ ujanja | ______ ubora wa akili |

| | |
|---|---|
| ______ ukarimu mkuu | ______ ukarimu |
| ______ ubembe | ______ shauku ya kutawala wengine |
| ______ tabia nyoofu | ______ uthabiti na dhamira |
| ______ tamaa ya kidunia | ______ unyenyekevu |
| ______ tamaa ya cheo cha kijamii | ______ ufahari katika mafanikio ya mtu |
| ______ upendo wa Mungu | ______ kiburi |
| ______ upendo wa anasa | ______ usafi wa nia |

3. Katika sala hii ‘Abdu’l-Bahá anamuomba Mungu kumuwezesha kijana kuvunja nguvu za makosa na ujinga. Amua ni upi kati ya ufuatao utawasaidia vijana katika jitihada zao dhidi ya nguvu kama hizo:

______ uwezo wa kutenganisha kilicho sahihi kutoka kosa

______ uwezo wa kulaghai wengine

______ uwezo wa kueleza mawazo ya kina kwa uwazi

______ uwezo wa kutambua na kushinda ubaguzi

______ uwezo wa kutumia nyenzo za kimwili kwa matumizi sahihi

______ uwezo wa kuwadhibiti wengine kwa ajili ya kufanikisha malengo ya mtu binafsi

______ uwezo wa kudhibiti tamaa za hali ya chini

______ uwezo wa kuchangia kwenye umoja wa mawazo

______ uwezo wa kutopendelea katika uamuzi wa mtu

______ uwezo wa kuendeleza haki

4. Katika sala ‘Abdu’l-Bahá anamuomba Mungu kuwawezesha vijana kukunjua viwango vya upatano na mwongozo. Amua ni upi kati ya ufuatao utawasaidia vijana katika juhudi kama hizo:

______ uwezo wa kusitawisha fundo za urafiki

______ uwezo wa kuwasikiliza wengine kwa uangalifu

______ uwezo wa kukabiliana na shida kwa utulivu na umakini

______ uwezo wa kubaini makosa na mapungufu ya wengine

______ uwezo wa kupuuzia makosa na mapungufu ya wengine

______ uwezo wa kuhudumia jamii bila ubinafsi

______ uwezo wa kufurahia mafanikio ya wengine

______ uwezo wa kuwapa wengine tumaini

______ uwezo wa kushirikiana pamoja na wengine

_____ uwezo wa kuendeleza maslahi ya mtu binafsi bila kujali sana ustawi wa wengine

_____ uwezo wa kuendeleza ustawi wa jumuiya

## SEHEMU YA 5

Mateuzi tuliyosoma katika sehemu mbili zilizopita yanatupatia umaizi fulani katika sifa ambazo vijana wanapaswa kuwa nazo. Ni dhahiri kuwa kadiri vijana wadogo wafikiapo umri wa miaka kumi na tano, mambo mengi yatatarajiwa kutoka kwao. Hakika tunaelewa kuwa Maandiko yanauelezea umri wa miaka kumi na tano kama mwanzo wa ukomavu. Ni katika umri huu ambapo sheria za Kibahá'í kama vile kusali na kufunga vinakuwa vitu vya lazima kwa kila mtu. Kuhusu kuelekea ukomavu 'Abdu'l-Bahá anasema:

> **"Mtoto mchanga anyonyaye hupitia hatua mbalimbali za kimwili, akikua na kuendelea katika kila hatua, hadi hatimaye mwili wake unafikia umri wa ukomavu. Baada ya kufika katika ngazi hii yeye hupata uwezo wa kudhihirisha ukamilifu wa kiroho na wa kiakili. Miangaza ya uelewa, akili na maarifa huanza kuonekana ndani mwake na nguvu za roho yake hukunjuka."**[3]

Na pale ambapo mtu hufikia umri wa ukomavu, 'Abdu'l-Bahá hutuambia kuwa:

> **"yeye huelewa uhalisi wa mambo na kweli za ndani. Hakika, katika uelewa wake, hisia zake, maamuzi yake na uvumbuzi wake, kila siku ya maisha yake baada ya kufikia ukomavu ni sawa na mwaka mmoja kabla yake."**[4]

1. Zipo fikra nyingi kuhusu vijana ambazo zinaweza kuchunguzwa kufuatana na kauli ya hapo juu ya 'Abdu'l-Bahá. Ni zipi kati ya zifuatazo unafikiri zinamuhusu mtu mwenye miaka kumi na tano? Mvulana au msichana

_____ ana uwezo wa kiroho kutafakari juu ya maana ya uhai na kifo.

_____ anaweza kufikiria dhima za kina ikiwa tu zitawekwa katika mfumo wa mzaha.

_____ ana uwezo wa kiakili kubaini na kuchambua nguvu zinazoshawishi maisha yake.

_____ ana uwezo wa kutekeleza majukumu kwa umakini.

_____ ana uwezo wa kiroho wa kukabiliana na changamoto ngumu.

_____ ana uwezo wa kuendesha madarasa kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto.

_____ ana uwezo wa kueleza mafundisho na kanuni za Imani kwa ufasaha na kujiamini.

_____ hahitaji msaada na upendo wa wazazi.

_____ anaweza kuchukua wajibu wa kutekeleza sheria za Kibahá'í.

_____ ana uwezo wa akili wa kuelewa michakato ya kijamii.

_____ anaweza kujihusisha katika huduma muhimu kwa jamii.

2. Unaweza kupenda kukariri sala ya hapo chini:

> **"Ee Bwana! Mfanye kijana huyu mwangavu, na ujalie baraka Yako juu ya kiumbe huyu maskini. Mjalie ujuzi, mpe nguvu ziongezekazo kwenye mapambazuko ya kila asubuhi na mlinde ndani ya himaya ya ulinzi Wako ili kwamba aweze kuwekwa huru kutoka makosa, ajitolee mwenyewe kwa huduma ya Hoja Yako, awaelekeze wapotofu, awaongoze waovu, awafungulie mateka na kuwaamsha wazembe, ili wote wabarikiwe kwa kumbukumbu Yako na Utukuzo. Wewe u Mwenye Nguvu na Mwenye Uwezo."[5]**

## SEHEMU YA 6

Baadhi ya uwezo wa kimwili, kiakili, na kiroho unawekwa wazi pale vijana wanapovuka kizingiti cha ukomavu wafikishapo umri wa miaka kumi na tano. Wanapotakiwa kuacha nyuma mielekeo, mawazo na tabia za kitoto, sharti wakuze uwezo mpya. Uelekezaji wa nguvu hizi katika huduma kwa Hoja ya Mungu na kwa wanadamu hupaswa kuanza mwanzoni mwa ujana wa mtu. Bahá'u'lláh husema:

> **"Amebarikiwa yule ambaye mwanzoni mwa ujana wake na katika kilele cha maisha yake atainuka kuitumikia Hoja ya Bwana wa mwanzo na wa mwisho, na ataupamba moyo wake kwa upendo Wake. Udhihirisho wa neema ya aina hiyo ni mkubwa kuliko kuumbwa kwa mbingu na dunia. Wamebarikiwa walio thabiti, na heri ni kwa wale walio imara."[6]**

Huduma inayotolewa kwa Hoja na kila kizazi cha vijana ni ya muhimu kwa maendeleo. Ikitilia mkazo umuhimu wa mchango wanaoutoa, barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi husema: "Ni juu ya mabega yao kwamba huweka majukumu yote ya kutunza roho ya huduma isiyo na ubinafsi" miongoni mwa wale wanaojitahidi kuendeleza malengo ya Hoja ya Mungu. "Bila roho hiyo", barua inaendelea, "hakuna kazi inayoweza kukamilishwa kwa mafanikio."

Kuhusu sifa zile zinazohitajika kuwafanya vijana haswa kustahili kwa ajili ya uwanja wa huduma, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu katika ujumbe kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa huandika:

> **"Ustahimilivu wa vijana katika hali ngumu, utendaji wao na nguvu, na uwezo wao wa kuendana na hali za mahali, kukabiliana na changamoto mpya, na kutoa vuguvugu lao na shauku zao kwa wale wanao watembelea, vikiunganishwa na kiwango cha tabia kinacho dumishwa na vijana wa kibahá'í, huwafanya vyombo vyenye uwezo kwa ajili ya utekelezaji wa mipango na miradi iliyofikiriwa. Hakika, kupitia sifa hizi bainifu wanaweza kuwa waanzilishi wa shughuli yoyote na nguvu shinikizi ya juhudi yoyote ambamo wanashiriki, iwe ya mahali au ya kitaifa."[7]**

Na, ikiwaasa vijana ulimwenguni kote, Nyumba ya Haki inaeleza zaidi:

> **"Ingawa uhalisia wenu unabumbwa na utofauti mpana wa hali, walakini shauku yenu ya kuleta mabadiliko chanya na uwezo wa huduma yenye maana, tabia zote**

**za hatua ya maisha yenu, hazijazuiliwa kwa mbari yoyote au utaifa, wala havitegemei nyenzo za kimwili. Kipindi hiki angavu cha ujana mnachoshiriki kinashuhudiwa na wote . . .”**[8]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo kufuatana na mateuzi yaliyopo hapo juu:

   a. Wale wainukao kuhudumia Hoja ya Mungu mwanzoni mwa ujana wao na wameipamba mioyo yao kwa upendo wame ________________ .

   b. Juu ya mabega ya vijana limewekwa jukumu la kutunza ______________ ya _______________________________ miongoni mwa wale wanaofanya kazi kuendeleza Hoja ya Mungu.

   c. Bila moyo wa huduma usio na ubinafsi, ambao uendelezaji wake huwekwa juu ya mabega ya vijana, hakuna kazi inayoweza____________________________ .

   d. _____________________ wa vijana katika hali ngumu na _________________ wao na ________________ huwafanya vyombo vyenye uwezo katika kutekeleza mipango na miradi.

   e. Kama vyombo vyenye uwezo kwaajili ya utekelezaji wa mipango na miradi, vijana wanaweza kutumia uwezo wao wa ___________________ wenyewe kwa hali wazikutazo, ku _________________ na changamoto mpya, na ku __________ vuguvugu lao na shauku kwa wale wawatembeleao.

   f. Kupitia sifa zao bainifu vijana wanaweza kuwa __________________ wa shughuli yoyote na ____________________________ ya juhudi yoyote wanayo shiriki.

   g. Zozote ziwazo hali zinazobumba uhalisi wa vijana kote ulimwenguni, shauku ya ___________ kuhusu ___________________________ na uwezo kwa ajili ya _______________________________ ni tabia bainifu za wale wote waliomo katika hatua hii ya maisha.

## SEHEMU YA 7

Dhana nyingi kiujumla huhusishwa na huduma zifanywazo na vijana, miongoni mwa hizo, hali ya papo kwa papo, msisimko na uhuru wa kufanya chochote kile kivutiacho fikira zao. Ingawa kuna uhalali katika uhusishaji wa dhana hizi na huduma, tunapaswa tuwe waangalifu tusitilie mkazo mwingi kupita kiasi. Ni rahisi mno kuingia katika mazoea ya kupunguza shughuli za vijana kuwa mlolongo wa matukio ya kusisimua tu na kupuuza thamani ya kuelewa asili ya mchakato na hitaji la kujifunza nidhamu ya utendaji wa kimpangilio. Fikiria michakato ya kimpangilio ambayo kupitia humo mafundisho na kanuni za Imani zinatumika kuongeza nguvu za misingi ya kiroho ya vijiji na ujirani — kwa mfano, elimu ya kiroho ya Watoto, uimarishaji wa maisha ya jumuiya, na ukuzaji wa rasilimali watu. Sasa, pamoja na rafiki zako mnaosoma kozi hii, fikirieni baadhi ya vitendo vya huduma ambavyo vinaweza

kufanywa na vijana vinavyochangia kwenye michakato hii. Kwani shughuli hizi hazipelekei kwenye furaha? Je haziruhusu kiasi fulani cha utendaji wa papo kwa papo? Je hazihamasishi ubunifu kupitia kutumia jitihada za kinidhamu?

## SEHEMU YA 8

Mara nyingi tunasikia kuwa kipindi cha ujana ni wakati wa maandalizi. Kauli hii ni kweli kabisa. Ikirejea kwenye mabadiliko yahitajikayo duniani leo, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu inaandika kuwa, "mabadiliko yanayotarajiwa kutokea katika utendaji wa jamii, kwa sehemu kubwa yatategemea juu ya ubora wa maandalizi vijana wafanyayo kwa ajili ya ulimwengu watakao urithi." Tunachopaswa kuuliza basi, ni, jinsi gani vijana wanaweza kujiandaa vyema zaidi kwa ajili ya majukumu watakayo beba kadiri wanavyoelekea kwenye utu uzima. Ujumbe ulioandikwa na Nyumba ya Haki hueleza:

> **"Kwa mtu yeyote, kama ni Mbahá'í au la, miaka yake ya ujana ni ile ambamo yeye atafanya maamuzi mengi ambayo yataweka mwelekeo wa maisha yake. Katika miaka hii, yeye atachagua kazi ya maisha yake, atakamilisha elimu yake, ataanza kupata riziki yake mwenyewe, atafunga ndoa na kuanza kulea familia yake mwenyewe. Muhimu zaidi ya yote, ni katika kipindi hiki kwamba akili yake itakuwa na maswali mengi na kwamba zile thamani za kiroho ambazo zitaongoza tabia zake za siku za mbele huchukuliwa."[9]**

Kwa mwangaza huu, barua iliyoandikwa kwa niaba ya Mlinzi ikirejelea kwa hitaji la vijana kukuza yote mawili uwezo wa kiroho na wa kiakili kama sehemu ya maandalizi yao ya baadae. "Mtahitajika kujiandaa vyema" barua huonesha. "Mtahitajika kuwa mlioendeleza pande zenu za kiakili na vilevile za kiroho sawa sawa".

Aghalabu, swali hili la maandalizi huibua maswala mengine yanayohusu uhusiano kati ya masomo — iwe ni ya kitaaluma, kiufundi, au kitaalamu — na huduma kwa Imani. Hususani, wakati mwingine haiko wazi ni kiasi gani cha nguvu vijana wanapaswa kutumia juu ya kila kimoja. Upande mmoja zaidi ni kuwashauri vijana kujidhatiti wenyewe kikamilifu kwa elimu

yao na kusubiri mpaka watakapopata tajiriba zaidi ya maisha kabla ya kujihusisha kwa dhati katika eneo moja au maeneo zaidi ya huduma. Ni kweli "kwa hali zote, upataji wa elimu ndani ya uwezekano wa mtu na kupata biashara au utaalamu ambao utamsaidia kupata mahitaji ni lazima vipewe umuhimu mkubwa". Walakini, kama ambavyo Nyumba ya Haki huweka wazi, "kueleza miaka ya mafanikio ya vijana pekee" kama hatua ya maandalizi ya kuanza biashara au utaalamu, ingekuwa

> **"kupuuzia nguvu za ubunifu zinazopatikana ndani ya vijana kwa kiwango hicho kikubwa. Baada ya yote, mashujaa wengi wa awali wa Imani walikuwa vijana wa kiume na wa kike ambao waliinuka kutimiza matendo makubwa kabisa katika njia ya Mpendwa wao."[10]**

Kwa upande mwingine zaidi ni kuwahamasisha vijana kuachana na elimu ya kitaaluma au ufundi stadi kwa pamoja na kutumia nguvu zao, hususan katika wakati huu wa fursa, katika uwanja wa huduma kikamilifu. Kwamba huduma inapaswa kuwa muhimu katika maisha ya kila kijana ni dhahiri kutokana na aya nyingi, kama zile tulizosoma katika sehemu zilizotangulia. Kwamba kipindi shadidi cha huduma, ikiwa unahusisha usitishaji wa muda wa masomo au la, kinaweza kuwa "kipengele chenye thamani cha maandalizi yao" pia ni dhahiri. Kwa wakati huohuo, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu husema:

> **"Wakati ni sahihi kutarajia mambo makubwa kutoka kwa wale ambao wana mengi ya kutoa katika njia ya huduma, marafiki wanapaswa kulinda dhidi ya kuchukua mtazamo mfinyu juu ya maana ya ukuaji hadi ukomaavu. Uhuru wa kujongea na upatikanaji wa muda unawawezesha vijana wengi kutoa huduma katika njia ambazo zinahusika moja kwa moja kwa mahitaji ya jumuiya, lakini kadiri wanavyosogea mbele zaidi kwenye miaka yao ya ishirini, peo zao hupanuka. . . . Kwa wengi, kipaumbele cha haraka kitakuwa elimu zaidi, ya kitaaluma au ufundi, kutokana na uwezekano uliopo mbele yao, na nafasi mpya za mwingiliano pamoja na jamii zitafunguka. . . . Maamuzi muhimu watakayofanya kuhusu mwelekeo wa maisha yao ya utu uzima yataamua kama huduma kwa Hoja ya Mungu ilikuwa sura fupi ya kukumbukwa ya miaka yao ya ujana, au kiini imara cha uwepo wao wa kidunia, lenzi ambayo kwayo vitendo vyote vinaletwa katika taswira."[11]**

Kabla ya kufikiria zaidi uhusiano kati ya elimu na huduma, pengine ungependa kusita kidogo na kuandika kauli fupi ambayo huakisi uelewa wako wa maana ya kwamba kipindi cha ujana ni wakati wa maandalizi.

## SEHEMU YA 9

Bila shaka tamko uliloandika katika sehemu iliyopita linatilia mkazo jinsi ilivyo muhimu kwa vijana kujiandaa kikamilifu kwa ajili ya ulimwengu watakaourithi kwa kupata elimu ya kitaaluma au mafunzo ya kiufundi au kitaalamu. Lakini bila shaka pia uliona kwamba huduma kwa Hoja haiwezi "kusubirishwa" wakati mtu anaendelea na masomo. Mwelekeo kama huo hujipeleka mbele katika mustakabali kadiri mtu anavyoendelea kukua, na huenda mtu anaweza kungojea maisha yake yote kupata hali inayofaa kwa minajili ya kuanza kutoa huduma kwa dhati. Mtazamo huu wa uhusiano kati ya masomo na huduma unaweza kuibuka ikiwa elimu itafafanuliwa kama ujifunzaji wa vitabu pekee yake. Wakati badala yake tuonapo huduma kama ulingo ambamo maarifa yanatumika na akili inakuzwa, basi hapo mawazo kama hayo yanaweza kuepukika kwa urahisi, na huduma huchukuliwa siyo tu kama sehemu ya, bali kiini cha, mchakato wowote mathubuti wa maandalizi kwa ajili ya maisha ya baadaye. Hakika, wakati huduma kwa Hoja huanza mwanzoni mwa ujana wa mtu, huja kuwa kanuni iongozayo katika maisha yote, ikimwezesha mtu kufuata njia inayofaa na kuweka mwelekeo wake wazi.

Utambuzi huu hupelekea kiasilia kuuliza maswali kuhusu aina ya maandalizi wanayoyahitaji vijana ili kuongeza uwezo wao kwa ajili ya huduma. Ingekuwa rahisi kufikiri kwamba kwa kuhudhuria katika mikusanyiko mbalimbali ya jumuiya za Kibahá'í, zikiwemo zile zinazoridhisha hamu ya kiasili ya kutumia muda pamoja na wanarika wao, vijana watakuza uwezo wao na watajiandaa sawasawa kwa maisha ya huduma. Walakini, maandiko hupendekeza kuwa mchakato huo wa elimu usiyo rasmi, ingawa huhitajika, hautoshi.

Kama tukiangalia kwa makini katika mawasiliano yake, tunaona kwamba Shoghi Effendi anaelezea matumaini kwamba vijana watakuwa "wameelimishwa na kufunzwa vyema" katika mafundisho na watapata elimu "kamili" na "imara" ya Imani. Kwa nyongeza, yeye anawahamasisha kupitia "ujifunzaji hai,wa moyo wote na ushiriki endelevu" katika shughuli za jumuiya zao. Kuhusu suala hili, yeye anaeleza kuwa maisha ya jumuiya hutoa "maabara ya lazima," ambamo vijana wanaweza "kutafsiri katika uhai kanuni na vitendo vinavyojenga" wao hukusanya kutoka mafunzo ya Imani. Ni katika "kuwa sehemu halisi ya kile kiumbe hai", yeye huonesha, kwamba wanaweza "kuipata roho halisi iliyomo kupitia Mafundisho yote ya Kibahá'í". Hivyo, mchakato wa elimu rasmi unahitajika kwa ajili ya kuwasaidia vijana kujiandaa wenyewe kwa ajili ya huduma, iliyomo ndani ya uhalisia wa maisha ya jumuiya. Shughuli ili mradi ni shughuli, masomo ili mradi ni masomo, hayakidhi mahitaji.

Jumbe nyingi za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu hueleza katika hali zinazofanana. Uelewa huongezeka zaidi, ujumbe mmoja huweka wazi, "wakati masomo na huduma vinapounganika na kutekelezwa pamoja". "Hapo, katika uwanja wa huduma, elimu hujaribiwa,

maswali huibuka kutokana na mazoezi, na viwango vipya vya uelewa hupatikana.” Katika nchi zote ulimwenguni Taasisi za mafunzo zimesitawishwa kwa kusudi maalum la kukuza rasilimali watu wa Hoja kupitia kozi rasmi za mafunzo. Idadi ya watu inayoendelea kukua kila mahali inajihusisha katika mpangilio wa mchakato wa kielimu kuongeza uwezo wao kwa ajili ya huduma, na vijana mara na tena wameendelea kuwa katika safu za mbele za mchakato huu wa maandalizi. Kuhusu wakala wa Taasisi ya mafunzo, barua moja iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki hueleza:

> **“Hujitahidi kumshughulisha mtu binafsi katika mchakato wa kielimu ambamo tabia adilifu na nidhamu binafsi vinakuzwa katika muktadha wa huduma, hulea upatano na mtindo wa maisha yenye furaha ambao hufuma pamoja masomo, ibada, ufundishaji, ujenzi wa jumuiya na, kwa ujumla, ujihusishaji katika michakato mingine ambayo hutafuta kubadilisha jamii. Kwenye moyo wa mchakato wa kielimu hukutana na Neno la Mungu, ambalo nguvu zake hudumisha jitihada za kila mtu binafsi kusafisha moyo wake na kutembea katika njia ya huduma kwa ‘miguu ya kujitenga’.”[12]**

Barua nyingine iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki hueleza:

> **“. . . kozi za Taasisi zimekusudiwa kumweka mtu binafsi katika njia ambamo sifa na mielekeo, ujuzi na vipawa vinapatikana hatua kwa hatua kupitia huduma — huduma iliyokusudiwa kutuliza nafsi sisitizi, ikisaidia kumwinua mtu binafsi kutoka kwenye mipaka yake na kumweka katika mchakato hai wa ujenzi wa jumuiya.”[13]**

Na, ikirejea kwa makundi ya vijana kila mahali kote ulimwenguni, Nyumba ya Haki huandika:

> **“Bila kujali hali zao mahususi, kila mmoja wao na wote watashiriki katika shauku ya kujitolea muda wao na nguvu, vipaji na uwezo kwa huduma kwa jumuiya yao. Wengi wanapopewa fursa, wangetoa kwa furaha miaka michache ya maisha yao kwa ajili ya utoaji wa elimu ya kiroho kwa vizazi vinavyoibuka. Hivyo basi, katika vijana wa ulimwengu, imo hazina ya uwezo wa kubadilisha jamii inayosubiri kuchotwa. Na uachiliaji wa uwezo huu unapaswa kuchuliwa na kila Taasisi kama jukumu takatifu.”[14]**

## SEHEMU YA 10

Kama tulivyoona katika sehemu mbili zilizopita, lazima tuwe makini wakati wa kufikiria hali yoyote ili tusiivunje vipande vipande kwa namna ambayo tunaanza kutenganisha nyanja za maisha yetu, ambao unaweza kupelekea kwenye mkanganyiko usiyo wa lazima. Kwa ujumla, akili ya mwanadamu ina hulka ya kuugawa ulimwengu ikutanao nao. Uhalisia — wa kimwili, kijamii, na wa kiroho — ni mpana mno kueleweka katika ukubwa wake. Kwa hiyo si jambo la ajabu kuugawa vipande vipande kwa madhumuni ya kuuelewa katika vijisehemu vyake. Hata hivyo, wakati hili likifanyika bila kuzingatia ujumla wa uhalisia, matatizo huibuka. Migogoro miongoni mwa watu wa mbari, rangi, utaifa, na dini mbalimbali ni mifano ya baadhi ya matatizo mengi yanayoweza kuibuka kutoka mtazamo wa maisha uliogawanyika

vipandevipande. Kwani Umoja wa mtu ni halisi, na ugawaji wake kufuatana na misingi ya kimbari, kiitikadi, na kitaifa ni matunda ya akili ya watu na matokeo ya mazingira ya kihistoria.

Tusipokuwa makini na kuishia kuchukua mwelekeo kama huo uliogawanyika kwa maisha yetu, tunaweza kuunda aina za uwili ambao kwa kiasi kikubwa ni wa kufikirika. Kazi, starehe, maisha ya familia, maisha ya kiroho, afya ya kimwili, utafutaji wa mambo ya kiakili, maendeleo ya mtu binafsi, maendeleo ya pamoja na mengine mengi huwa ni vipande ambavyo kwa pamoja huunda maisha yetu. Tunapokubali mgawanyiko huo kuwa halisi, tunajihisi kuvutwa katika mielekeo mingi, tukijaribu kuitikia kwa kile tukichukuliacho kama mahitaji ya sura hizi mbalimbali za maisha. Tunachanganyikiwa mbele ya malengo yanayoshindana kama: Je, nitoe dhabihu maisha yangu ya kifamilia ili kuhudumia Hoja? Je, kuihudumia Imani hakutoingilia juhudi zangu za kulea wanangu? Hii ni mifano miwili baina ya maelfu ya maswali yanayoweza kuibuka.

Ili kutatua uwili tuliyoutengeneza, wakati fulani tunajaribu kuugawa muda wetu sawa sawa miongoni mwa mahitaji mbalimbali yaliyowekwa juu yetu. Wakati mwingine, tunajaribu kuyaweka majukumu katika vipaumbele na kulenga juu ya mambo yale ambayo tunayafikiri kuwa muhimu zaidi katika muda mahususi. Mgawo makini wa muda na uwezo bila shaka ni muhimu. Lakini ni wa manufaa tu iwapo tutabakia wafahamivu wa mwingiliano uliopo kati ya Nyanja nyingi za maisha yetu.Tukishindwa kuona suala kamili, mvutano unaojengeka miongoni mwa pande zote unaweza kupelekea kwenye wasiwasi na kuchanganyikiwa.

Hapa chini ni nyanja mbalimbali za maisha zilizopangwa katika jozi ambazo hupaswa kusaidiana, lakini ambazo wakati mwingine huonekana kama zinapingana. Kwa kila sentensi inayofuata kila jozi, amua kama huwakilisha aina ya mawazo yanayopelekea kwenye njia ya maisha ya upatano au hupelekea kwenye ugawanyikaji: Weka alama “U” (Upatano) na “G” (Gawanyika) ipasavyo:

1. Familia na kazi

_____ Maisha yangu ya familia yatadhurika nikifanya kazi kwa bidii.

_____ Mara nyingi ninajadiliana na familia yangu juu ya mafanikio yangu na changamoto zinazonikabili kazini.

_____ Bila shaka wanawake wanaweza kuwa bora katika taaluma zao, lakini daima watoto ndiyo wanaoteseka.

_____ Ikiwa ninataka kulea watoto wangu vizuri, itanibidi nisahau kuhusu taaluma yangu.

_____ Ninaweza kufikia ubora katika taaluma yangu na kushugulikia kwa uangalifu majukumu yangu ya kifamilia.

2. Elimu na Huduma kwa Hoja

_____ Mafanikio ya kitaaluma ni kigezo cha lazima kwa ajili ya kuingia uwanja wa huduma.

_____ Elimu tunayoipata kupitia masomo yetu ni mali katika uwanja huu wa huduma, na uzoefu tunaoupata katika uwanja wa huduma huongeza kina cha elimu yetu.

_____ Sharti tutelekeze masomo yetu kama kwa kweli tunataka kujitoa kwa Hoja.

_____ Mojawapo ya matarajio yetu makubwa kabisa ni kusoma mafundisho ya Imani na kujifunza kuyatumia katika jitihada zinazoendeleza uboreshaji wa ulimwenguni.

_____ Uwezo tunaokuza katika njia ya huduma wa kuendeleza usitawi wa jumuiya zetu utatusaidia kuchagua nyanja zinazofaa za masomo.

3. Maendeleo ya kiakili na ukuzaji wa sifa za kiroho

_____ Utafutaji huru wa ukweli huhitaji ulezi wa akili, pamoja na upataji wa sifa za kiroho.

_____ Maendeleo ya kiakili huhitaji haki, uaminifu, na utovu wa ubaguzi.

_____ Ili kuendelea kiroho, mtu inabidi aachilie mbali akili yake ya kufikiri.

_____ Akili zetu na mioyo yetu havitenganishwi; huwakilisha sura zinazokamilishana na zinazosaidiana za uhalisia mmoja — roho zetu.

_____ Sifa za kiroho zinakuzwa kupitia elimu ya utambuzi na utekelezaji wa matendo mema.

4. Maisha ya kimwili na maisha ya kiroho

_____ Lazima tujinyime starehe za kimwili ili tuweze kukua kiroho.

_____ Mambo ya kiroho sharti yawekwe kando mpaka tutakapokuwa wazee; katika ujana wetu lazima tuchukue kila fursa kujiendeleza kimwili.

_____ Mahitaji ya kimwili ya watu lazima yatoshelezwe kabla ya kuanza kufikiria mambo ya kiroho.

_____ Kusudi la maisha katika ulimwengu huu wa kimwili ni kukuza sifa na uwezo za kiroho.

_____ Kusudi la maisha katika ulimwengu huu wa kimwili ni kupeleka mbele ustaarabu unaoendelea daima.

_____ Lazima tufurahie majaliwarr yapatikanayo ulimwenguni humu lakini tusiruhusu tamaa za kidunia kutawala mioyo yetu na kutuzuia kumsogelea zaidi na zaidi Mungu.

## SEHEMU YA 11

Katika kitengo hiki hatufikirii sana juu ya sifa zinazowaelezea vijana chipukizi, bali juu ya tabia za vijana wa kiume na wa kike ambazo maandiko yanapendekeza wangepaswa kuwa nazo wakuapo. Tulianza uchunguzi huu kwa kuangalia mateuzi mawili yaliyotupa umaizi kwenye baadhi ya tabia hizi. Halafu tuliona kwamba umri wa miaka kumi na tano huashiria hatua maalum katika maisha ya mtu, kwa sababu huwakilisha kizingiti cha ukomavu, wakati ambapo uwezo mpya na nguvu hudhihirishwa. Tunajua nafasi muhimu vijana wanayoweza kuwa nayo katika maisha ya Hoja na jinsi gani ilivyo muhimu kuuelekeza uwezo wao mkubwa kwenye huduma kwa wanadamu. Pia tumekiri hitaji la vijana kujiandaa kwa utambuzi kwa ajili

ya maisha ya baadaye na tumeona kwamba huduma yenyewe ni sehemu nyeti ya mchakato huu wa maandalizi, sawa na yalivyo masomo yao — yote yale yahitajikayo kwa ajili ya kupata ujuzi na stadi kwa ajili ya kujipatia riziki na yale yatakayo viwezesha vipaji vyao vya kutoa huduma kwa jumuiya zao.

Huenda mtaona ni vyema kusita kidogo hapa na kutafakari juu ya yale mliyoyasoma hadi sasa. Hapa chini yapo matamko kadhaa. Soma kila moja na amua kama ni kweli au si kweli. Ingawa jibu katika baadhi ya matamko huenda likawa dhahiri, tunatumaini kuwa mtalipa zoezi zima umakini wa kutosha. Imekusudiwa kuwapitisha katika mlolongo wa mawazo ambayo yatawasaidia kupangilia mawazo yenu kuhusu masuala tuliyokwisha pitia hadi sasa.

_____ Kwa mtu binafsi, kufikia umri wa miaka 15 humaanisha amefikia umri wa ukomavu, lakini hii zaidi ni alama ya kiishara tu na haiathiri maisha yake katika namna yoyote ile yenye maana.

_____ Vijana wengi ni wachanga na hawawezi kubeba majukumu; huyumbishwa kirahisi na hawawezi kutegemewa.

_____ Vijana wana shauku ya kubeba majukumu ya kazi za Imani, lakini kwa kuwa hawana uzoefu wa kutosha wala ukomavu wanashindwa kufanya mengi.

_____ Vijana wanao uwezo uhitajikao kuinuka na kuhudumia Hoja kwa uthabiti na bila ubinafsi.

_____ Vijana wanaweza kudhihirisha nguvu ya utashi na moyo wa kujituma kufanya utendaji wa kimpangilio katika huduma kwa jumuiya zao.

_____ Wale wainukao kuhudumia Hoja mwanzoni mwa ujana wao wamebarikiwa sana.

_____ Vijana wanapaswa kukazia fikra zao zaidi kwenye masomo yao, muda wao wa ziada unaweza kutolewa kwenye huduma.

_____ Bila kupokea mafunzo ya kitaaluma ya kiwango cha juu kabisa, vijana hawezi kuhudumia jamii ipasavyo.

_____ Nyanja zote za jitihada za kiutu ziko wazi kwa ajili ya vijana; inabidi wachague zile zinazofaa vipaji vyao na mazingira yao, waingie kwa roho ya huduma, na wajitahidi kupata ubora.

_____ Vijana hawana uzoefu wa kutosha na elimu ihitajikayo kujihusisha katika mazungumzo ya maana kuhusu Imani na wale wanaokutana nao; ni bora wahudumie katika njia zingine.

_____ Vijana hawana uzoefu wa kutosha na elimu ihitajikayo kujihusisha katika mazungumzo ya maana kuhusu Imani na wale wanaokutana nao na wanapaswa kuhamasishwa badala yake, kuonesha tabia ya mfano wa kuigwa tu.

_____ Vijana wanao uwezo mkubwa uliomo ndani mwao wa kuelewa mafundisho ya Imani na kushiriki na wanarika wenzao.

_____ Vijana wanao uwezo mkubwa uliomo ndani mwao wa kuelewa mafundisho ya Imani na kushiriki na watu kutoka aina zote za maisha, wote vijana na wazee.

_____ Vijana wanao uwezo mkubwa uliomo ndani mwao wa kuelewa mafundisho ya Imani na kushiriki na watu kutoka aina zote za maisha, wote vijana na wazee na wengine.

_____ Vijana ni miongoni mwa rasilimali kubwa kabisa za Hoja ya Mungu na wanapaswa kusaidiwa, kupitia kozi zinazofaa za mafunzo na uhamasishaji endelevu, kuwa na uwezo wa kuhudumia jumuiya na wanadamu.

_____ Vijana wanahitaji shughuli maalum ambazo zinawaruhusu kuwa na mzaha; ni vigumu kwao kuwa makini kwa kipindi kirefu.

_____ Kujifunza kuwa wenye mpangilio huja baadaye katika maisha, wakati hali ya papo hapo inapoisha.

_____ Uwezo wa vijana kuhimili hali ngumu na kuendana na hali mpya huwafungulia fursa nyingi.

_____ Vijana wana akili ya kudadisi na wanaweza kupata majibu ya maswali yao kwa.kushiriki kikamilifu katika maisha ya jumuiya.

_____ Uwezo mkubwa uliomo ndani ya jumuiya zetu unaweza kukunjulika kupitia roho ya huduma isiyo na ubinafsi inayooneshwa na vijana.

_____ Uwezo wa Neno la Mungu huongeza nguvu za vijana wakati wa kutembea katika njia ya huduma kwa usafi na kujitenga.

_____ Mielekeo na sifa za kiroho, stadi na vipaji vinavyokuzwa na vijana kwa kusoma kozi za taasisi na kwa kufanya shughuli za huduma zinazowiana huwawezesha kuchangia kwa dhati kwa mchakato hai wa ujenzi wa jumuiya.

_____ Hazina ya uwezo wa kubadilisha jamii iliyomo katika vijana wa ulimwengu inaweza.kutumika kupitia ushiriki wao katika mchakato wa kimpangilio wa kielimu ambao unaunganisha kwa usomaji na huduma.

## SEHEMU YA 12

Inatumainiwa kuwa zoezi la sehemu iliyopita limewasaidieni kuimarisha fikira zenu juu ya kipindi cha ujana na kwamba taswira mliyopata juu ya hatua hii ya maisha ni ile ya huduma hai, ikiunganishwa na ujifunzaji — yote yakiwa na maandalizi yenye umakini mkubwa sana ya siku za baadae. Hebu tuangalie dhima hii kwa undani.

Muingiliano tulioujadili baina ya huduma, elimu, na maandalizi yahitajikayo kukunjuka ndani ya muktadha mahususi. Hususani, yanapaswa kuchangia kwenye michakato miwili ya mabadiliko iliyotazamiwa katika maandiko ya Imani: ukuaji wa dhati wa kiakili na wa kiroho wa mtu binafsi na mabadiliko ya jamii. Tunatambua kwamba “kazi kubwa kabisa na ya kipekee” ya Ufunuo wa Bahá’u’lláh “siyo kitu kingine ila kuleta aina mpya ya watu” na kila mmoja wetu hujitahidi kila siku kuweka mawazo na vitendo vyake sawa na vya wale tunaowaona wakielezewa kwenye Maandiko Matakatifu. Maandiko yanatilia mkazo mabadiliko sawa ya kina katika muundo wa jamii. “Punde utaratibu wa hivi sasa utakunjwa.” Bahá’u’lláh hutuambia, “na mpya utakunjuliwa badala yake.” “Watu wote”, Anatangaza, “wameumbwa kuendeleza ustaarabu unaoendelea daima.”

Badiliko hili lenye pande mbili litatokea tu kwa kupitia jitihada za makusudi, na ni muhimu kwamba vijana watambue matokeo yake kwa maisha yao na wapate kujaliwa hisia ya kusudi yenye nguvu, kwa yote mawili, kuwajibika kwa ukuaji wao binafsi na kuchangia katika mabadiliko ya jamii. Kusudi la kimaadili lenye pande mbili kama hilo litajidhihirisha kiasilia katika maisha ya huduma.

Mateuzi yafuatayo hutoa mwanga kwenye nyanja moja wapo ya hisia hii ya kusudi la kimaadili — ihusianayo na ukuaji wetu wenyewe wa kiakili na kiroho:

> **"Kusudi la Mungu mmoja wa kweli katika kujidhihirisha Mwenyewe ni kuwaita watu wote kwenye ukweli na udhati, kwenye ucha mungu na uaminifu, kwenye ridhaa na kujisalimisha kwa Mapenzi ya Mungu, kwenye ustahimilivu na wema, kwenye unyoofu na hekima. Lengo lake ni kumwandaa kila mtu na joho la sifa za utakatifu, na kumremba kwa pambo la matendo matakatifu na mema."[15]**

> **"Jiwe la msingi la maisha ambayo hufuata njia ya Mungu ni utafutaji wa ubora wa kimaadili na upataji wa tabia zilizojaliwa sifa ambazo hupendeza mbele ya uoni Wake."[16]**

> **"Ni juu ya mtu kujipatia elimu, Kufikia ukamilifu wa kiroho mkubwa zaidi, kugundua ukweli uliofichika na kudhihirisha hata sifa za Mungu."[17]**

> **"Kusudi la Mungu katika kumuumba mtu limekuwa na daima litakuwa, kumuwezesha yeye kumjua Muumba wake na kufikia uwepo Wake."[18]**

1. Kamilisha sentensi zifuatazo kutokana na mateuzi ya hapo juu:

   a. Kusudi la Mungu mmoja wa kweli katika kujidhihirisha Mwenyewe ni kuwaita wanadamu wote kwenye ______________________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________ .

   b. Lengo la Mungu ni kumwandaa kila mwanadamu na ________________________

   ______________________ , na kumremba kwa ______________________________

   ___________________________________________ .

   c. Jiwe la msingi la maisha yaliyofuata njia ya Mungu ni ___________________

   ________________________ na ________________________________________

   ______________________________________________________________

   ___________________________________________ .

   d. Ni wajibu wetu kujipatia ___________________ , kufikia __________________

   _____________________________________ , kugundua _____________________

   na kudhihirisha ______________________________________________ .

e. Kusudi la Mungu katika kutuumba limekuwa na daima litakuwa ______________ ________________________________________ na __________________________ _________________________ .

2. Kuwa na muono wa uwezekano uliomo katika roho ya mwanadamu hubumba na kuelekeza hisia ya kusudi la mtu binafsi. Unaweza kueleza ni kwa jinsi gani? ______
__________________________________________________________________________
__________________________________________________________________________

3. Hisia ya kusudi la mtu binafsi huimarishwa kupitia utambuzi kuwa maisha haya ya kidunia ni sehemu ndogo tu ya safari ya milele kuelekea uwepo wa Mungu. Je, mnaweza kueleza ni kwa nini? _______________________________________________
__________________________________________________________________________
__________________________________________________________________________

Jozi ifuatayo ya mateuzi hutoa mwanga juu ya sura nyingine ya hisia hii ya kusudi la kimaadili, ambayo ni, kuchangia katika mabadiliko ya jamii:

**"Mdhulumiwa huyu hushuhudia kuwa kusudi ambalo kwalo walimwengu, kutoka utupu kamili, wamekanyaga katika ufalme wa uwepo, ni kwamba waweze kufanya kazi kwa ajili ya uboreshaji wa ulimwengu na kuishi pamoja kwa ushirikiano na upatano."**[19]

**"Na heshima na utofauti wa mtu hupatikana katika hili, kwamba yeye miongoni mwa umati wote wa ulimwengu awe chanzo cha wema wa kijamii. Je inaweza kufikiriwa baraka kubwa zaidi kuliko hii, kwamba mtu, akijiangalia ndani mwake, aone kwamba kwa neema inayothibitisha ya Mungu yeye amekuwa sababu ya amani na ustawi, ya furaha na faida kwa watu wenzake? Hapana, kwa Mungu mmoja wa kweli, hakuna bashasha kubwa zaidi, hakuna furaha kamili zaidi."**[20]

**"Ni bora kiasi gani, na mwenye heshima kiasi gani mtu, kama atainuka kukamilisha wajibu wake; ni maskini na dhalili kiasi gani, ikiwa atafunga macho yake dhidi ya ustawi wa jamii na kupoteza maisha yake yenye thamani akifuatilia maslahi yake binafsi na faida kwake peke yake."**[21]

**"Msijishughulishe na mambo yenu nyinyi wenyewe; acheni mawazo yenu yakaziwe juu ya kile ambacho kitarekebisha hatima ya jamii ya wanadamu na kutakasa mioyo na roho za watu."**[22]

**"Wale ambao ni watu wa Mungu hawana tamaa isipokuwa kuhuisha ulimwengu, kuyaboresha maisha yake, na kufufua watu wake."**[23]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo kutokana na nukuu za hapo juu:

a. Kusudi ambalo kwalo sisi tunalo, kutoka utupu kamili, tumekanyaga katika ufalme wa uwepo, ni kwamba tuweze ____________________________________________

____________ na ____________________________________________________

______________________ .

b. Heshima na utofauti wa mtu hupatikana katika hili, kwamba __________________

__________________________________________________________________

_______________________________________________ .

c. Hakuna baraka kubwa zaidi kuliko hii, kwamba mtu, akijiangalia ndani mwake, aone kwamba kwa ______________________________________________ yeye amekuwa __________________________________________________________

________________________________________________________________ .

d. Mtu ni mwenye heshima kiasi gani, kama atainuka ________________________ __________ ; ni maskini na dhalili kiasi gani, ikiwa atafunga macho yake dhidi ya _____________ na __________________________________________________

__________________________________________________________________

______________________________________________.

e. Tusijishughulishe wenyewe na _______________________ , bali tukazie mawazo yetu juu ya yale ambayo _____________________________________________

__________________________________________________________________

______________________ .

f. Wale ambao ni watu wa Mungu hawana tamaa isipokuwa ___________________ , ku _________________________ , na _____________________________ .

2. Kuwa na muono wa fursa kubwa zilizo wazi kwa ya jamii ya wanadamu kwenye hatua hii ya maendeleo, ambapo muungano wake wa kuwa familia moja ni uwezekano halisi, hubumba na kuelekeza hisia ya kusudi ya mtu binafsi. Unaweza kueleza ni kwa jinsi gani? ______________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

3. Hisia ya kusudi ya mtu binafsi huimarishwa kwa ufahamu kwamba jamii ya wanadamu ipo katika njia ndefu ya mabadiliko endelevu yanayopelekea kwenye ustaarabu Mtakatifu. Unaweza kueleza ni kwa nini? __________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

## SEHEMU YA 13

Kama ilivyo pendekezwa katika mazoezi ya sehemu iliyopita, uelewa wa asili wa mabadiliko katika mtu na jamii ilivyo elezwa katika maandiko ni msingi muhimu kwa hisia ya kusudi ambayo vijana wanapaswa kuwa nayo. Ili kupata sifa mithili ya vito ambavyo "vimefichwa ndani ya machimbo ya nafsi zao za kweli na za ndani kabisa" na kuchangia kwa uumbaji wa ustaarabu wa ulimwengu ambao una ufanisi wa kimwili na kiroho, wao lazima kwanza wathamini ukubwa wa mabadiliko ambayo Bahá'u'lláh anayataka. Bila shaka, watu kila pahala wanaongelea hitaji la mabadiliko katika wakati huu. Kile tunachopaswa kutambua ni kwamba mabadiliko yaliyokusudiwa kutokea kwa mtu binafsi na jamii chini ya ushawishi wa moja kwa moja wa Ufunuo wa Bahá'u'lláh ni makubwa zaidi kuliko yale ambayo watu wanavyoweza kudhani yangewezekana kuwepo.

Hebu tujaribu kupata kianga cha ukubwa huu wa mabadiliko yatakayotokea katika ngazi ya mtu binafsi kwa kutafakari juu ya mateuzi kadhaa. Bahá'u'lláh hutuambia:

> **"Mbari ya watu, isiyolinganishika katika tabia, itainuliwa, ambayo kwa miguu ya kujitenga, itakanyaga wote walio mbinguni na duniani, na watatawanya mkono wa utakatifu juu ya vyote vilivyoumbwa kwa maji na udongo."**[24]

Na katika kifungu kimoja Anatangaza:

> **"Sema: Yeye hahesabiwi pamoja na watu wa Bahá ambaye hufuata tamaa za kidunia, au yule akaziaye moyo wake kwenye vitu vya kidunia. Yeye ni mfuasi wangu wa kweli, ambaye, kama akija kwenye bonde la dhahabu safi, atapita humo moja kwa moja kwa kujitenga kabisa kama wingu, na hatogeuka, wala kusita. Mtu kama huyo hakika ni Wangu. Kutoka vazi lake Umati wa juu utaweza kuvuta manukato ya utakatifu."**[25]

Katika kifungu kingine Yeye husema:

> **"Wenzi wa Mungu ni, katika siku hii ni, donge ambalo sharti litie chachu watu wa ulimwengu. Sharti waoneshe uaminifu kama huo, ukweli kama huo, na ustahimilivu, matendo na tabia kama hizo ambazo wanadamu wote wanaweza kunufaika kwa mifano yao."**[26]

Na Hueleza zaidi:

> **"Ndani ya pumzi ya roho kama hizo ambazo ni safi na zimetakasika uwezo unaofika mbali umefichwa. Uwezo huu ni mkubwa sana kiasi kwamba wataweza kutumia ushawishi wao juu ya vitu vyote vilivyoumbwa."**[27]

'Abdu'l-Bahá hutuambia:

> **"Ee Enyi rafiki wa Mungu! Fanyeni ninyi jitihada kubwa ambazo watu wote na mbari zote za ulimwengu hata maadui, wataweka imani zao, ujasiri na matumaini ndani mwenu. Endapo roho itafanya makosa mara mia moja elfu, bado itakuwa yenye matumaini ya kusamehewa na isiwe yenye kupoteza matumaini au iliyohuzunishwa. Hii ndiyo tabia na mwenendo wa watu wa Bahá. Huo ndio**

**msingi wa njia bora kabisa! Acheni mienendo yenu na tabia iendane na mashauri ya Abdu'l-Bahá."[28]**

Uzuri ung'aao wa sifa utakao mbainisha mtu huyu mpya, kama ilivyoelezwa katika Maandiko, unastaabisha, na tunaelemewa na dalili tunazozipata za nguvu na uwezo wa hii "mbari mpya ya watu". Baada ya kusoma vifungu kama hivyo tunaweza kuitikia kwa namna tofauti. Tunaweza kulazimika kufikiri kiwango kilichowekwa na Maandiko kiko mbali sana kiasi kwamba tunaona haina maana kufanya jitihada kubwa kuishi kwa mujibu wake na, kama matokeo, tunaangukia katika uduni: katika hali kama hiyo, tunajiruhusu wenyewe kujituliza kwenye kuamini kwamba inatosha tu kukwepa tabia mbaya. Wakati, mtu amejaliwa hisia thabiti ya kusudi, hata hivyo, vifungu kama hivyo vya hapo juu ni chanzo cha mara kwa mara cha hamasa na humchochea mtu kufika kwenye vilele vya juu zaidi.

Hata hivyo pia tumebarikiwa na chanzo kingine cha upuzio katika nafsi ya 'Abdu'l-Bahá, Mfano kamili wa mafundisho ya Baba Yake. Ingawa tunafahamu kuwa 'Abdu'l-Bahá yupo katika mazingira Yake mwenyewe na kwamba hakuna mtu ambaye anaweza kutumaini kufikia daraja Lake lililotukuka, tunaona ndani mwake ukamilisho wa kila sifa ya Kibahá'í na tunajitahidi kufika kwenye kiwango cha tabia ambacho anatuonesha kama mfano. Wewe na rafiki zako mnaosoma kozi hii mnaweza kuona inafaa kuchagua aya kutoka nukuu za hapo juu na kufikiria juu ya matukio kutoka maisha ya 'Abdu'l-Bahá ambayo yanaakisi sifa zilizotajwa kwenye kila moja. Kwa mfano, tunapojaribu kupata taswira ya kutembea "kwa miguu ya kujitenga", hadithi kutoka maisha Yake hutujia akilini ambazo hutuonesha inamaanisha nini kutembea katika ulimwengu huu tukiwa waliojitenga kutoka vitu vyote vilivyoumbwa. Tunapowazia "manukato ya utakatifu," tunajua kwamba inatoka katika "mavazi" Yake ambayo "Umati wa juu" ungeweza kuvuta utamu wake, na tunakumbuka hadithi zinazoonesha utakatifu Wake mkamilifu.

## SEHEMU YA 14

Sasa hebu tufikirie mchakato wa mabadiliko ya kina ambao lazima utokee katika ngazi ya jamii. Bahá'u'lláh husema:

**"Kwa haki yangu Mwenyewe! Siku inakaribia ambapo Tutakuwa tumeukunja ulimwengu na vyote vilivyomo, na kukunjua Utaratibu mpya badala yake."[29]**

Hutuambia zaidi:

**"Mizania ya ulimwengu imevurugika kupitia ushawishi utetemekao wa Utaratibu huu mpya wa Ulimwengu, mkuu kabisa. Maisha yenye mpangilio ya Jamii ya wanadamu yamepinduliwa kupitia uwezo ya Utaratibu huu wa kipekee, mfumo huu wa ajabu - ambao mfano wake macho ya watu hayajawahi kuushuhudia."[30]**

Na 'Abdu'l-Bahá huthibitisha:

**". . . haki na uadilifu vitauzingira ulimwengu; chuki na uadui vitatoweka; chochote kile ambacho ni chanzo cha mgawanyiko miongoni mwa watu, mbari na mataifa kitatokomezwa kabisa; na kile kinachohakikisha umoja, upatano na urafiki kitaendelezwa. Wasiojali wataamka, vipofu wataona, viziwi watasikia, bubu**

**watasema, wagonjwa wataponywa, wafu watafufuka. Vita vitatoa nafasi kwa amani. Uadui utabadilika kuwa upendo, sababu kuu za ugomvi na shida zitaondolewa kabisa, wanadamu watafikia furaha ya kweli; ulimwengu huu utaakisi Ufalme wa Mbinguni; na dunia ya chini itakuwa Kiti cha Enzi cha milki ya juu."**[31]

Na mahali pengine Yeye hueleza:

**"Kile kilichokuwa kinatumika kwa mahitaji ya mwanadamu katika kipindi cha mwanzoni cha historia ya mbari ya wanadamu hakingeweza kukidhi wala kutosheleza mahitaji ya siku hii na kipindi cha upya na ukamilifu. Jamii ya wanadamu imeibuka kutoka viwango vyake vya zamani vya mipaka na mafunzo ya mwanzo. Sasa mtu lazima ajazwe na njema na nguvu mpya, njema mpya, uwezo mpya. Maadili mapya, vipaji vipya, fadhila mpya, majaaliwa, na makamilifu vinamngojea na tayari vinashuka juu yake."**[32]

Na Yeye hutusihi:

**". . . lazima tujitahidi kwa moyo na roho ili giza hili la ulimwengu tegemezi, liweze kuondolewa, ili miangaza ya Ufalme ing'ae juu ya peo zote, ulimwengu wa jamii ya wanadamu uweze kuangazwa, mfano wa Mungu udhihirike ndani ya vioo vya wanadamu, sheria ya Mungu itasitawishwa vyema na kwamba maeneo yote ya ulimwengu yatafurahia amani, faraja na utulivu chini ya ulinzi wa haki wa Mungu."**[33]

Kama ilivyo katika hali ya mtu binafsi, ni vigumu kwetu kufikiria uzuri kamili wa ustaarabu ambao tumeahidiwa. Hakika, ingekuwa vigumu kuwezekana kueleza sura zake. Hata hivyo hatuwezi kuelemewa sana na ukubwa wa mabadiliko yanayohitajika hata tukadhani kuwa yatajitokeza kimiujiza, bila jitihada kutoka kwetu. Macho yetu sharti yabaki yamekazia kwa utaratibu wa ulimwengu wa Bahá'u'lláh, na lazima tutambue kwamba hata kitendo kidogo kabisa kinaweza kuchangia kwenye ujenzi wake. Ili kutafakari zaidi juu ya kiasi cha mabadiliko yatakayotokea katika jamii, jazeni nafasi zilizo wazi katika kila sentensi hapo chini kwa kutumia mojawapo ya maneno au makundi ya maneno yafuatayo:

toweka, tokomezwa, toa nafasi, tawanyika, angazwa,
stawishwa, badilishwa, kutokomezwa, kunjwa, ng'aa,
ondolewa fikia, zingira, endelezwa, furahia, akisi

a. Siku inawadia ambapo ulimwengu na vyote vilivyomo vita ___________________ .

b. Siku inawadia ambamo Utaratibu mpya uta _________________ badala ya ule wa sasa.

c. Haki na uadilifu vita _________________ ulimwengu.

d. Chuki na uadui vita _________________ .

e. Chochote kinachosababisha mgawanyiko miongoni mwa watu, mbari na mataifa kita _______________ .

f. Kile kinachohakikisha muungano, upatano na urafiki kita ___________________ .

g. Vita vita ________________ kwa amani.

h. Uadui uta __________________ kuwa upendo.

i. Sababu kuu za ugomvi na shida zita __________________ .

j. Wanadamu wata _____________________ furaha ya kweli.

k. Ulimwengu huu uta _________________ Ufalme wa Mbinguni.

l. Giza la ulimwengu huu tegemezi, lita ____________________ .

m. Miangaza ya Ufalme ita __________________ juu ya peo zote.

n. Ulimwengu wa jamii ya wanadamu utakuwa __________________ .

o. Sheria ya Mungu ita ___________________ vyema.

p. Maeneo yote ya ulimwengu yata __________________ amani, raha, na utulivu chini ya ulinzi wa haki ya Mungu.

## SEHEMU YA 15

Vifungu na mazoezi katika sehemu mbili zilizopita vimetupatia umaizi wa mabadiliko makubwa yatakayotokea ndani ya mtu binafsi na katika jamii kama matokeo ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Ili kufikiria zaidi juu ya ukubwa wa mabadiliko Aliyoyatarajia, soma matamko yaliyopo hapo chini. Kila moja inaeleza sifa fulani stahiki za mtu binafsi au jamii kama vile haki, kutopendelea, au wema wa upendo. Hata hivyo vifungu vilivyomo katika sehemu zilizotangulia haviachi mashaka kuwa Bahá'u'lláh ameiita jamii ya wanadamu kwa kiwango cha juu zaidi cha tabia ya mtu binafsi na ya pamoja. Jaribu kusahihisha sentensi zifuatazo, ili zioneshe wazi zaidi kiwango kilichowekwa na Ufunuo Wake. Mfano wa tamko la kwanza umetolewa kwa ajili ya kukusaidia.

a. Mtu lazima adhibiti hisia zake za wivu na asimezwe nazo.
b. Sharti tuondoe hata chembe ndogo kabisa ya wivu kutoka mioyo yetu na kuhisi furaha ya kweli katika mafanikio ya wengine.

a. Inatosha kuwa wenye adabu kwa yeyote tunayekutana naye, awe rafiki au mtu usiyemjua.
b. ________________________________________________________________
________________________________________________________________
________________________________________________________________

a. Yatupasa kuwa na shukurani kwa utajiri wa kimwili tuliyopewa na Mungu na daima tuchangie kwenye mashirika ya hisani tunapoombwa.

b. ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

a. Mtu anapaswa kujizuia kuingia katika ugomvi na wengine.

b. ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

a. Kuishi maisha ya kimaadili humaanisha kwamba hatupaswi kusababisha madhara kwa mtu yeyote.

b. ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

a. Kuishi kwa amani, yatupasa tujifunze kuwavumilia watu wa tamaduni, usuli, na dini tofauti.

b. ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

a. Watu sharti wajifunze kusimamia haki zao.

b. ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

a. Sharti serikali zitoe rasilimali zinazohitajika kuunda mipango bora kabisa iwezekanayo kwa ajili ya shule ambazo zinafunda akili za viongozi wetu wa siku zambele.

b. ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

a. Magereza lazima yawe ya kisasa ili kuwarekebisha wahalifu.

b. ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

Sasa tafakari juu ya sentensi ulizoandika hivi punde, kufuatana na vifungu vilivyopo hapo chini. Kifungu cha kwanza hutusaidia kufikiria ni jinsi gani mioyo inapaswa kuwa imetakaswa kutoka tamaa za ulimwengu:

**"Ewe mwana wa dunia! Fahamu, kwa kweli, moyo ambamo mabaki kidogo kabisa ya wivu yangalimo, kamwe hautafikia enzi Yangu ya milele, wala kuvuta manukato matamu ya utakatifu yavumayo kutoka kwenye ufalme Wangu wa utakatifu."[34]**

Juu ya jinsi tupaswavyo kutendeana mmoja kwa mwingine, teuzi lifuatalo hutoa baadhi ya umaizi:

**"Ni roho ya upendo na wema wa upendo lazima viwe vyenye nguvu mno, kiasi kwamba mgeni aweze kujipatia rafiki, adui ajipatie kaka wa kweli, pasiwepo tofauti hata kidogo kati yao."[35]**

Teuzi hili hutoa mwanga juu ya mielekeo ifaayo kwa ajili ya utoaji:

**"Enyi wana wa vumbi! Waambieni matajiri kuhusu kuhema kwa mashaka kwa maskini usiku wa manane, ili ukaidi usije ukawaongoza kwenye njia ya maangamizi, na kuwakosesha Mti wa Utajiri. Kutoa na kuwa mkarimu ni sifa Zangu; heri ni yake yule ajipambaye kwa njema Zangu."[36]**

Kuhusu asili ya mahusiano yetu na wengine, tunasoma:

**"Uwe mwitaji kwa upendo, na uwe mwema kwa mbari zote za wanadamu. Wapende watoto wa watu na shiriki katika huzuni zao. Uwe mmoja wa wale ambao huleta amani. Wape urafiki wako, uwe unayestahili kuaminiwa. Uwe mafuta kwa kila kidonda, uwe dawa kwa kila ugonjwa. Unganisha roho pamoja. Tongoa aya za mwongozo. Jishughulishe katika ibada ya Bwana wako, na inuka kuwaongoza watu kwenye unyoofu. Legeza ulimi wako na fundisha, na acha uso wako uwe mwangavu kwa moto wa upendo wa Mungu. Usipumzike hata sekunde, jitahidi usivute pumzi ya kujipumzisha. Hivyo uweze kuwa alama na ishara ya upendo wa Mungu, na bendera ya neema Yake."[37]**

Na juu ya suala la tabia ya kimaadili, tunashauriwa:

**"Siku ambamo ibada tupu ilionekana kutosha sasa zimekwisha. Wakati umewadia ambamo hakuna kingine bali nia safi, ikisaidiwa na vitendo vya usafi usiyo na doa, vinaweza kupaa kwenye kiti cha enzi cha Yule Aliye Juu Kabisa na kukubalika Kwake."[38]**

Kuhusu kutendeana na watu wa usuli tofauti, kifungu hiki hutupatia umaizi:

**"Andamaneni na watu wote, jamaa na dini za ulimwengu kwa kiwango cha juu kabisa cha ukweli, unyoofu, uaminifu, wema, nia njema na urafiki, ili ulimwengu mzima wa kuwa uweze kujazwa kwa furaha kuu takatifu ya neema ya Bahá, kwamba ujinga, uadui, chuki na husuda vipotee kutoka ulimwenguni na giza la utengano kati ya watu na jamaa wa ulimwengu vitoe njia kwa Mwangaza wa Umoja. Ikiwa watu wengine na mataifa watavunja uaminifu wao kwako, wewe waoneshe uaminifu, ikiwa watakukosea haki, wewe waoneshe haki, wakijiweka mbali kutoka kwenu wavuteni kwenu, wakiwaonesha uadui waonesheni urafiki, ikiwa wataweka sumu katika maisha yenu, ziwekeeni utamu roho zao, wakiwajeruhi ninyi muwe dawa kwa vidonda vyao. Hizi ndizo sifa za wale waaminifu! Hizi ndizo sifa za walio wa kweli."**[39]

Teuzi lililopo hapa chini hutusaidia kuelewa jinsi gani utambuzi wa umoja wa jamii ya watu huathiri mahusiano ya kijamii:

**"Ninatumaini kuwa kila mmoja wenu atakuwa mwenye haki, na kuelekeza fikra zenu kwenye umoja wa jamii ya wanadamu; kwamba kamwe hamtawazuru majirani zenu wala kusema mabaya ya mtu yeyote; kwamba mtaheshimu haki za watu wote, na kushughulika zaidi na maslahi ya wengine kuliko yenu wenyewe."**[40]

Juu ya upatikanaji wa elimu, kifungu kifuatacho hujadili suala hilo:

**"Bahá'u'lláh ametangaza kwamba kwa kuwa ujinga na utovu wa elimu ni vikwazo vya utengano kati ya jamii ya wanadamu, wote lazima wapokee mafunzo na maelekezo. Kupitia amri hii utovu wa maelewano utaondolewa na umoja wa watu kuendelezwa na kukuzwa. Elimu kwa wote ni sheria ya ulimwengu."**[41]

Kuhusu utawala wa haki tunasoma yafuatayo:

**"Hata hivyo Ustaarabu Mtukufu , humfundisha kila mmoja katika jamii kwamba hakuna mtu, isipokuwa wale wachache sana, atakayekubali kutenda uhalifu. Kwa hiyo ipo tofauti kubwa kati ya uzuiaji wa uhalifu kupitia njia za kikatili na za kulipiza, na hivyo kuwafundisha watu, kuwaangazia, na kuwafanya wa kiroho, ili kwamba bila woga wowote wa adhabu au ulipizaji kisasi unaotarajiwa, wao wataachana na vitendo vyote vya kihalifu. Hakika, wataona tendo la uhalifu kama aibu kubwa na tendo lenyewe kuwa adhabu kali kabisa."**[42]

Baada ya kutafakari juu ya vifungu hapo juu, unaweza kupitia matamko uliyoandika na kuona kama unaweza kuyaboresha.

## SEHEMU YA 16

Tumejadili juu ya kusudi la kimaadili lenye pande mbili ambalo huwasukuma watu kuchukua wajibu wa ukuaji wao wenyewe wa kiroho na wa kiakili na kuchangia kwenye ustawi wa jamii. Tumeona jinsi hisia hii ya kusudi, iliyo muhimu sana kwa vijana leo, inavyoimarishwa kwa uelewa wa asili na ukubwa wa mabadiliko ndani ya mtu binafsi na katika jamii kama ilivyotarajiwa katika maandiko. Kile tunachohitaji kutambua pia ni kwamba michakato hii miwili ya mabadiliko imeunganika kwa karibu sana. Kuendeleza uwezo uliyomo

ndani ya mtu na kufanya kazi kwa ajili ya usitawi wa jamii haviwezi kutenganishwa, kwa sababu viwango vya kimaadili vya mtu na tabia zake hubadili mazingira yake, na kwa zamu vinapewa umbo na muundo wa jamii. Barua iliyoandikwa kwa niaba ya Mlinzi inasema:

> **"Hatuwezi kutenganisha moyo wa binadamu kutoka mazingira yetu ya nje na kusema kwamba pale kimojawapo kikirekebishwa vitu vyote vitaboreka. Mtu ameunganika na ulimwengu. Maisha yake ya ndani hubumba mazingira na mwenyewe pia huathiriwa kwa kina na mazingira hayo. Kimoja hutenda juu ya kingine na kila badiliko la kudumu katika maisha ya mtu ni matokeo ya mahusiano ya vitu hivi viwili."[43]**

Juu ya msingi wa teuzi lililopo hapo juu, amua kama kauli zifuatazo ni za kweli au si za kweli:

_____ Mtu binafsi atakuwa amebadilika hapo tu jamii ibadilikapo kikamilifu.

_____ Maovu ya jamii yatapotea kabisa hapo tu watu binafsi watakapo kuwa wa kiroho.

_____ Sheria za haki zikiimarishwa, jamii itakuwa huru kutoka dhuluma, bila kujali desturi za watu binafsi.

_____ Jamii itakuwa huru kutoka dhuluma wakati kila mtu binafsi atakapo jitahidi kuwa mwenye haki.

_____ Wanajamii wote wanaweza kuwa wenye haki hata kama mfumo wa kisheria unaofanya kazi katika jamii yao siyo wa haki.

_____ Tabia ya mtu binafsi huathiri mazingira ya kijamii.

_____ Jamii yenye haki itakuwa ni matokeo ya juhudi za kujenga mifumo ya haki na kuwaelimisha watu binafsi kuwa watu wasiopendelea na wenye kutafuta ukweli.

_____ Hakuna mtu awezaye kuepuka athari za mazingira yake ya kijamii.

_____ Wanadamu, wakisaidiwa na uwezo wao wa kiroho wanaweza kushinda athari hasi za mazingira ya kijamii.

_____ Ubaguzi utatoweka pale ambapo kila mmoja atakapokiri umoja wa jamii ya wanadamu.

_____ Ubaguzi utatoweka pindi jamii itakapo futulia mbali kila dalili ya upendeleo katika sheria na asasi zake.

_____ Kila aina ya ubaguzi inaweza kufutiliwa mbali kupitia usitawishaji wa sheria za haki na ufunzaji wa roho za watu kuchunguza uhalisia na kuambatana na watu wote kwa upendo na urafiki.

_____ Pale ambapo kila mmoja atakapoamini kuwa jamii ya wanadamu ni moja, tutakuwa na umoja.

_____ Ustawishwaji wa umoja ulimwenguni huhitaji mabadiliko ya mtu binafsi na wa muundo wa jamii.

## SEHEMU YA 17

Mawazo yaliyowasilishwa katika sehemu iliyopita huturejesha kwenye suala la huduma, kwani ni ndani ya uwanja wa huduma ambapo tunakuza uwezo wetu na kuleta mabadiliko katika jamii. Ya kwamba kushiriki katika mchakato wa mabadiliko ya kijamii humaanisha maisha yaliyoelekezwa wakfu katika huduma, ni jambo linalohitaji ufafanuzi kidogo. Jambo ambalo lingehitaji kufikiriwa zaidi, hata hivyo, ni uhusiano baina ya huduma na ukuaji wa kiakili na kiroho wa mtu binafsi. Hapo chini ni orodha ya shughuli. Sifa nyingi za kiroho zinahitajika katika utekelezaji wa kila moja na katika kuhakikisha ufanisi wake. Kwa kusudi la zoezi hili maalum, chagua sifa moja au mbili na mielekeo zinazoelekea hasa kuwa na uwiano na kila shughuli na jaribu kueleza jinsi zitakavyo changia kwenye uwezo wa mtu kuzitekeleza.

a. Kuendesha mkutano wa ibada wa mara kwa mara katika ujirani au kijiji: ______

______________________________________________________________

______________________________________________________________

b. Kushiriki katika program iliyosarifiwa ya kuwatembelea marafiki na majirani ili kujadili dhima za kiroho zilizochotwa kutoka kwenye Imani na kuimarisha mafundo ya urafiki: ______________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

c. Uendeshaji wa mara kwa mara wa madarasa ya elimu ya kiroho ya watoto katika kijiji au ujirani: ______________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

d. Kusaidia jitihada za kikundi cha vijana chipukizi kwa kipindi kirefu, sambamba na muhuishaji anaeongoza shughuli zake: __________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

e. Kuwa na ziara za mara kwa mara kwa wazazi ambao wana vijana wadogo katika program za kielimu zinazoendelezwa na taasisi na kuwahusisha katika mazungumzo juu ya dhima kuu za maendeleo ya watoto wao wa kiume na wa kike:

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

Zoezi hapo juu limetusaidia kufikiri kuhusu jinsi sifa za kiroho na mielekeo inavyochangia kwenye uwezo wa mtu binafsi kutekeleza vitendo vya huduma. Lakini vilevile ni kweli kwamba, katika kutoa huduma, mtu anaweza kukuza na kuimarisha sifa kama hizo. Hapo chini zipo sifa chache za kiroho ambazo sisi sote tunajitahidi kuzipata. Kwa kila kikundi, chagua mojawapo ya shughuli hapo juu na eleza katika njia gani unafikiri kuwa itachangia kwa maendeleo ya sifa ya yule anayeitekeleza.

a. Ukweli, uaminifu na haki: ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

b. Ustahamilivu na wema: ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

c. Utakatifu, uadilifu, na ung'aavu: ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

d. Ujasiri, uaminifu kwa Mungu, na unyenyekevu: ______________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

e. Kukubali na kujisalimisha kwa Mapenzi ya Mungu: ___________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## SEHEMU YA 18

Huduma imeungana kwa karibu na hali ya uwepo wetu. Sisi tunapohuishwa na roho ya huduma bila ubinafsi, kila mwingiliano tulionao, kila tendo tufanyalo — katika maisha yetu ya kikazi, katika mahusiano yetu na wengine, kama wana jumuiya zetu — hushawishiwa nayo. Hata hivyo, haijalishi ni huduma gani tuitoayo, kamwe tunabaki kuwa na ufahamu wa ukweli kwamba kuna mpango ulioundwa kwa ajili ya uenezaji wa ujumbe wa Bahá'u'lláh kwa watu wa ulimwengu, ujumbe ambao hutangaza umoja wa mtu, huwaita kwenye muungano wake, na huleta sheria na kanuni, mafundisho ya kiroho na kijamii, ambayo pekee yanaweza kuanzisha mtindo unaofaa wa maisha yajayo ya jamii tofauti kabisa na wowote uliokwisha onekana hapo awali. Ukiasisiwa na 'Abdu'l-Bahá Mwenyewe, mpango huu hautafuti chochote isipokuwa

kuzaliwa upya kiroho kwa ulimwengu, na kadiri unavyoendelea kukunjuka kupitia hatua dhahiri na watu wengi zaidi na Zaidi wanavyoshiriki katika utekelezwaji wake, “ndivyo suluhisho mbadala la matatizo yanayoikumba jamii linaanza kuibuka.” Kwake — Mpango Mtakatifu — tunapaswa kujitolea wenyewe. Kwake Mlinzi hurejea kama “Mpango mkuu kabisa ambao umewahi kutengenezwa kupitia nguvu ya uumbaji ya Jina Kuu Kabisa”. “Unasonga mbele,” hutuambia,

> **“ukiongeza kasi kila siku ipitayo, ukipasulia mbali vizuizi katika hali yoyote na kati ya koo na mbari tofauti, ukipanua bila kupingwa wigo wake wa ufanyaji kazi wenye ukarimu, na ukifunua dalili zenye nguvu zake za kiasili zilizoko ndani yake kadiri usogeavyo kuelekea ushindi wa kiroho wa sayari nzima.”[44]**

Kupitia Mpango Mtakatifu, roho ya Ufunuo wa Bahá’u’lláh itajipenyeza katika kila sehemu ya ulimwengu, ikibadilisha maisha ya mtu binafsi na ya pamoja. Shoghi Effendi huthibitisha zaidi, kwamba

> **“hatua ya mwisho na ya kilele katika maendeleo ya mpango huu uliotengenezwa na Mungu Mwenyewe kwa ajili ya jamii ya wanadamu, kwa wakati wake, itathibitisha kuwa ishara ya kuzaliwa kwa ustaarabu wa ulimwengu, ambao hauwezi kulinganishwa katika ukubwa wake, wala aina yake na nguvu, katika historia ya jamii ya wanadamu — ustaarabu ambao vizazi vijavyo, vitataja kwa sauti moja, kuwa tunda bora kabisa la Zama za Dhahabu za Kipindi Maalum Kitakatifu cha Bahá’u’lláh . . .”[45]**

Kila hatua katika ukunjukaji wa Mpango Mtukufu huashiriwa na mmoja wa Mipango ya Kidunia iliozinduliwa na Mkuu wa Imani. Kila mpango una mahitaji fulani, na unajengwa juu ya mafanikio yaliyo kwishapatikana, na mafunzo yaliyofundwa, katika mpango uliotangulia. Kupitia jitihada zilizofanyika katika Mipango iliyotangulia, “kanuni mbalimbali, dhana, mikakati ya umuhimu wa kiulimwengu”, kwa mradi tunaoshughulika nao zimepata umbo na kuwa “muundo kwa ajili ya utendaji”. Ni muundo huu ambao unaupa umbo utendaji wetu wa pamoja. Na kuhakikisha kuwa tunakuwa thabiti katika tunachokifanya bila kupinda. Mtapata fursa ya kuchunguza asili ya muundo huu unaendelea kukua katika kozi zijazo. Kwa sasa, ni muhimu kutambua kuwa uwepo wake huwawezesha “kiini kinachoendelea kupanuka cha watu binafsi” kwenye ngazi ya umma kuzalisha mjongeo wa watu “kuelekea lengo la Utaratibu Mpya wa Ulimwengu”. Kufuatana na suala hili, ujumbe ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa washiriki kwenye mlolongo wa Makongamano ya vijana yaliyofanyika Ulimwenguni kote mwaka 2013 huelezea:

> **“Baada ya miongo mingi, kazi inayokumbatia dunia ya jumuiya hii iliyoenea sana, ya kupata ufahamu wa kutosha wa Ufunuo wa Bahá’u’lláh na kutumia kanuni zilizomo ndani yake imeishia katika kuibuka kwa mfumo wenye nguvu kwa ajili ya utendaji, ulioboreshwa kupitia uzoefu. Ninyi mna bahati ya kuwa na uzoefu wa mbinu na njia zake ambavyo sasa vimeshamiri vizuri. Kwa kupitia ustahimilivu katika utekelezaji wake, wengi wenu mtakuwa tayari mmejionea wenyewe dalili za uwezo wa ujengaji jamii wa mafundisho ya kiroho. Katika kongamano mnalohudhuria, mnakaribishwa kufikiria mchango ambao unaweza kutolewa na kijana yeyote anayetaka kuitikia mwito wa Bahá’u’lláh na kusaidia kuachilia nguvu hizo.”[46]**

Na ujumbe huo huo unaona zaidi:

**“Uwezekano uliowasilishwa kwa utendaji wa pamoja huonekana wazi hasa katika kazi ya ujenzi wa jumuiya, mchakato ambao unaongeza mwendo katika klasta nyingi na katika ujirani na vijiji ulimwenguni kote ambazo zimekuwa vituo vya shughuli shadidi. Vijana mara nyingi huwa mstari wa mbele kwa kazi kwenye mielekeo hii — siyo vijana wa Kibahá’í pekee, lakini pia wale wenye mawazo yanayofanana nao ambao wanaweza kuona athari chanya za yale ambayo Wabahá’í wameyaanzisha na kupata maono ya kimsingi ya umoja na mabadiliko ya kiroho.Katika sehemu kama hizo, umuhimu wa kushirikiana Ufunuo wa Bahá’u’lláh na mioyo pokevu na kuchunguza maana za ujumbe Wake kwa ulimwengu wa leo, unahitajika sana. Wakati sehemu kubwa ya jamii inakaribisha hali ya utepetevu na kutojali au, mbaya zaidi, kuhamasisha tabia ambazo ni za kuwadhuru wao wenyewe na wengine, tabia tofauti za kupendeza zinatolewa na wale ambao wanakuza uwezo wa watu ili kukuza na kuendeleza ustawi wa ruwaza itajirishayo kiroho ya maisha yajumuiya.”[47]**

Na kwa maneno haya, Nyumba ya Haki, inawahamasisha katika ujumbe mwingine, vijana Wakibahá’í na wale wanaotaka kuungana nao katika kuinua viwango vya maisha ya huduma:

**“Kwa kila kizazi cha waumini vijana hujitokeza fursa ya kuchangia kwenye hatima ya jamii ya wanadamu, ambayo ni ya kipekee katika kipindi cha uhai wao. Kwa kizazi cha sasa, wakati umefika wa kutafakari, kujihimu, kujiweka imara kwa ajili ya maisha ya huduma kutoka kwayo baraka zitamiminika kwa wingi. Katika sala zetu kwenye Kizingiti Kitakatifu, tunamsihi Uzuri wa Kale kwamba, kutoka katika jamii iliyovurugika na kukanganyika, Anaweza kuchuja roho zilizotakasika na zenye kujaliwa mtazamo wazi: vijana ambao uadilifu na unyoofu wao haudhoofishwi kwa kujihusisha na makosa ya wengine na ambao hawazuiliwi na mapungufu yao wenyewe; vijana watakao mtazama Bwana na ‘kuleta wale waliotengwa katika duara la marafiki wa karibu’; vijana ambao utambuzi wao wa kasoro za jamii unawachochea kufanyia kazi mabadiliko yake, siyo kujitenga mbali nayo; vijana ambao, kwa gharama yoyote, watakataa kuupitia ukosefu wa haki katika maumbo yake mengi na watatumia nguvu zao, badala yake, kwamba ‘mwanga wa haki utawanye wangavu wake juu ya ulimwengu mzima.’”[48]**

Vifungu vilivyopo hapo juu haviachi mashaka yoyote akilini mwako juu ya hitaji la muhimu la vijana kusonga mbele hadi safu za mbele za wale wanaohudumia Mpango Mtakatifu. Kuhitimisha sehemu hii, ingekusaidia kutafakari juu ya ujumbe ufuatao ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa mlolongo wa mikusanyiko ya vijana iliyofanyika katika mwaka 2000 kila mahali katika Amerika ya Kilatini:

**“Kadri kizazi hiki cha vijana kinavyowajibika kubeba majukumu ya kuendesha mambo ya jamii, kitakumbana na mazingira ya kinyume cha kukanganya. Kwa upande mmoja kanda inaweza kujivunia kihalali mafanikio mazuri sana katika maeneo ya kiakili, kiteknolojia na kiuchumi. Kwa upande mwingine, imeshindwa kupunguza umaskini ulioenea au kuepusha bahari inayoendelea kuongezeka ya vurugu ambayo inatishia kuzamisha koo zake. Kwa nini — na swali linahitaji kuulizwa kwa uwazi — jamii hii imeishiwa uwezo wake, licha ya utajiri wake mkubwa, kuondoa hali ya kutokuwepo haki ambayo inaendelea kupasua mfumo wa jamii?**

**“Jibu la swali hili, kama ilivyoshuhudiwa dhahiri na miongo mwa historia ya mapigano, haliwezi kupatikana katika ashki ya kisiasa, udhihirisho wa maslahi ya kitabaka yanayokinzana, au njia za kiufundi. Jambo linalohitajika ni ufufuko wa kiroho, kama kigezo cha lazima cha utendaji wenye ufanisi wa vyombo vya kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia. Lakini ipo haja ya kichochezi. Muwe na uhakika kuwa, licha ya idadi yenu ndogo, ninyi ndiyo mifereji ambamo kupitia humo kichochezi hicho kinaweza kutolewa.”**[49]

1. Ujumbe huu wa mwisho unauliza kwa nini jamii pamoja na utajiri huo mkubwa wa kiakili, kiteknolojia na kiuchumi, imeshindwa kuondoa hali ya ukosefu wa haki ambayo unaipasulia mbali, ikiashiria kwamba jibu haliwezi kupatikana katika ashki ya kisiasa, udhihirisho wa maslahi ya kitabaka yanayokinzana, au njia za kiufundi. Fikiria jamii unamoishi na toa mifano ya kila moja ya mambo yafuatayo:

   a. Ashki ya kisiasa, inayoibainisha jamii: ________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   b. Baadhi ya udhihirisho wa maslahi ya kitabaka yanayokinzana katika jamii: ____

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   c. Njia za kiufundi ambazo jamii imefuata: ________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

2. Kufuatana na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, nini kinahitajika kupata utendaji wenye ufanisi wa vyombo vya kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia katika juhudi za kutokomeza maradhi ya jamii? ________________________________________________

   ____________________________________________________________

3. Nyumba ya Haki ya Ulimwengu inatuambia nini kinahitajika ili kuleta ufufuko wa kiroho wa jamii? ________________________________________________

   ____________________________________________________________

4. Nyumba ya Haki ya Ulimwengu inasema ni nani anayekuwa mfereji ambamo kupitia humo Ujumbe wa Bahá’u’lláh unaweza kutolewa? __________________________

   ____________________________________________________________

Sasa, mkiwa na mawazo hayo hapo juu akilini, jadilini pamoja na rafiki zako mnaosoma kozi hii jinsi gani ushiriki katika utekelezaji wa Mpango Mtakatifu unavyowawezesha vijana kutenda kama mfereji kwa ajili ya ufufuaji wa kiroho wa jamii.

## SEHEMU YA 19

Bila shaka mjadala mwisho mwa sehemu iliyopita umewasababisha mfikiri zaidi kuhusu wajibu muhimu wanaotakiwa kutimiza vijana katika usongaji mbele wa Hoja. Katika kifungu cha maneno hapo chini kutoka *Mungu Yu Nasi*, Shoghi Effendi anaeleza taswira ya mashujaa wa mwanzoni wa Imani, ambao vitendo vyao vya kishujaa vinatakiwa kuwapa hamasa jamii ya wanadamu katika zama zote. Tukichukulia kuwa wengi wao walikuwa vijana, ni vyema kutafakari maneno aliyoyatumia Mlinzi kueleza sifa zao maarufu. Kabla ya kufanya hivyo, huenda itakusaidia kusoma faharasa ifuatayo:

| | |
|---|---|
| Mithili ya kimondo: | Kama kimondo; Huacha njia inayong'aa ionekanayo angani na husogea haraka kuvuka anga |
| Katiza: | Safiri kutoka ng'ambo moja hadi nyingine |
| Gubigubi: | Giza na inayotia huzuni |
| Setilaiti: | Chombo kilicho angani kizungukacho chombo kingine kikubwa kuliko chenyewe |
| Galasia: | Kundi kubwa sana la nyota |
| Nururisha: | Tupa miale ya mwanga |
| Ng'arisha: | Toa nuru kwa joto kali inayong'aa kabisa |
| Changa: | Iliyozaliwa hivi karibuni (haijakomaa) |
| Pambano: | Uhangaikaji kupata ushindi |
| Wachonga njia: | Watangulizi |
| Njama: | Mpango wa kisiri |
| Ufisadi: | Rushwa, uovu |
| Kubwa na pana: | Lenye upeo mkubwa, lenye kubumbuaza |
| Uchaji: | Heshima kuu kwa Mung una utii kwa wajibu wa kidini |
| Bidii: | Hisia kali |
| Kisimba: | Kama simba |
| Ukanaji: | Uachiliaji mbali, ukataaji, uasi |
| Uamuzi: | Kusudi lenye nguvu |
| Itale: | Isiyokubali kushindwa kiuimara na inayohimili |
| Kubwa sana: | Yenye ukubwa wakushangaza |
| Heshima kubwa: | Heshima na kicho |
| Inafadhaisha: | Inayobabaisha; inayobumbuwaza |

Mlinzi huandika:

> **"Tunaona, kadri tunavyo chunguza matukio ya mwanzo ya utendaji wake katika riwaya hii bora kabisa, umbo la Shujaa wake Mkubwa, Báb, anainuka kama kimondo juu ya upeo wa <u>Sh</u>íráz, anakatiza anga gubigubi la Uajemi kutoka kusini**

**hadi kaskazini, na kutua kwa kasi kabisa ya kusikitisha na kupotea katika mlipuko wa utukufu. Tunaona setilaiti Zake, galasia ya mashujaa waliokuwa wameleweshwa na Mungu, wakipanda juu ya upeo ule ule, wakinururishwa kwa mwangaza huohuo unaong'arisha, na hata wao wakajimaliza kwa wepesi huohuo, na kwa upande wao kuongeza msukumo kwa mwendo uliokuwa ukiongezeka bila kusita wa Imani changa ya Mungu. . . .**

**"Mashujaa ambao matendo yao hung'aa juu ya kumbukumbu ya mapambano haya makali ya kiroho, yaliyowahusisha kwa wakati huo watu, makasisi, falme na serikali, walikuwa ni wafuasi wateule wa Báb, Herufi za walio Hai, na wenzi wao, wachonganjia wa Siku Mpya, ambao mbele ya njama nyingi, ujinga, ufisadi, ukatili, ushirikina na woga walipinga kwa roho iliyotukuka, isiyozimishwa na inayotisha, ujuzi wa kina cha kustaajabisha, kauli yenye ufasaha iliyobeba kila kitu katika nguvu zake, ucha Mungu usiopitwa bidii yake, ujasiri wa kisimba katika ukali wake, ujikanaji ambao ni mtakatifu katika usafi wake, uamuzi ambao ni imara kama itale, muono mkubwa sana katika upana wake, heshima kubwa kwa Mtume na Maimamu Wake inayowakanganya maadui wake, uwezo wa ushawishi unaowatisha maadui wao, kiwango cha imani na kanuni za tabia ambacho kimewapa changamoto na kupindua maisha ya wananchi wenzao."[50]**

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Herufi za Waliohai na wenzi wao walihusika katika mapambano ____________

   b. Mapambano haya yalihusisha kwa wakati mmoja _____________ , ____________ , _____________ na ___________________ .

   c. Mashujaa wa mwanzo wa Imani walipinga njama, ujinga, ufisadi, ukatili, ushirikina na woga kwa

   – roho ________________ , _________________________ na _____________ ______________________ ,
   – maarifa ________________________________________ ,
   – kauli _______________________________________ ,
   – ucha Mungu, ________________________________________ ,
   – ujasiri _____________________________________________________ ,
   – ujinyimaji _________________________________________________ ,
   – uamuaji _______________________________________________ ,
   – muono ____________________________________________________ ,
   – heshima kubwa kwa Mtume na Maimamu Wake _______________________ _____________________________ ,

– uwezo wa kushawishi ________________________________________ ,

– Kiwango cha imani na kanuni ya tabia ambavyo ________________________
_________________________________ .

2. Ni kwa kusudi gani mashujaa wa mwanzoni wa Imani waliingia katika mapamabano ya kiroho, kama ilivyoelezwa na Mlinzi katika kifungu cha hapo juu? ___________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

3. Je, vijana wa leo wanaojihusisha katika Mpango Mtukufu , kama watangulizi wao wanashughulika na mapambano ya kiroho? _________________________________

4. Mapambano yao yanafananaje na yale ya mashujaa wa mwazoni wa Imani? ______
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

5. Ni jinsi gani vijana wa wa sasa watahakikisha kuwa wao sawa na ndugu zao waliowatangulia wa zama za Ushujaa za imani, wataweza kushinda mapambano ya kiroho wanayojihusisha nayo? ____________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

Kabla ya kujongea kwenye Sehemu ifuatayo, pengine ungependa kutafakari juu ya kifungu kifuatacho kutoka ujumbe ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu:

> **"Wakati Mtukufu Báb, alipokuwa na umri wa miaka ishirini na tano tu, alipoinuka ili kuwasilisha ulimwenguni ujumbe Wake wa mageuzi kabisa, wengi miongoni mwa wale ambao walikubali na kusambaza mafundisho Yake walikuwa ni vijana, wengine hata wadogo kuliko Báb Mwenyewe. Ushujaa wao, umepata umilele katika mwangaza shadidi wa kushangaza katika *Waleta Mapambazuko* na utaangaza kumbukumbu za kihistoria ya wanadamu kwa karne nyingi zijazo. Hivyo ndivyo ilivyoanza ruwaza ambayo kwayo kila rika la vijana, wakichota uvuvio kutoka kwenye msukumo uleule wa kiroho ili kuutengeneza upya ulimwengu, walitwaa fursa kuchangia kwenye hatua mpya katika mchakato unaokunjuka ambao utabadilisha maisha ya jamii ya wanadamu. Ni ruwaza ambayo haijawahi kukatishwa, tangu wakati wa Báb hadi wakati huu wa sasa."[51]**

## SEHEMU YA 20

Kupitia mfululizo wa maduru ya vipindi vya hatari na ushindi, vijana wa kila kizazi wamefuata njia iliyoachwa na Waleta Mapambazuko na wamebaki mstari wa mbele wa shughuli za Kibahá'í, wakifanya kazi kuleta ujumbe wa Bahá'u'lláh kwa jamii ya wanadamu. Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huandika:

> **"Kutoka mwanzo kabisa wa zama za Kibahá'í, vijana wamekuwa sehemu muhimu kabisa katika uenezaji wa Ufunuo wa Mungu. Báb Mwenyewe alikuwa na umri wa miaka ishirini na tano tu wakati alipotangaza Ujumbe Wake, wakati wengi wa Herufi za Walio hai walikuwa pia wadogo zaidi. Bwana, akiwa kama kijana mdogo sana, aliitwa kubeba majukumu mazito katika huduma ya Baba Yake nchini Iraq na Uturuki, na ndugu Yake, Tawi Bora kabisa, aliyatoa maisha yake kwa Mungu katika Gereza Kuu Kabisa akiwa na umri wa miaka ishirini na mbili ili kwamba watumishi wa Mungu waweze 'kuhuishwa, na wote wale waishio duniani waweze kuunganishwa.' Shoghi Effendi alikuwa mwanafunzi katika chuo kikuu cha Oxford wakati alipoitwa kutumikia wadhifa wa ulinzi, na wengi wa mashujaa wa Bahá'u'lláh, ambao walijipatia umaarufu usiopotea katika kipindi cha Mapambano ya Miaka Kumi, walikuwa vijana."[52]**

Katika ujumbe ulioandikwa mnamo mwaka 1984, Nyumba ya Haki huwaenzi mashujaa wa kipindi kilichopita hivi karibuni:

> **"Fikiria, kwa mfano, matukio katika mji wa Shíráz mnamo kiangazi kilichopita ya mabinti wadogo sita, wenye umri kati ya miaka 18 hadi 25, ambao maisha yao yalizimwa kwa kamba ya mnyongaji. Wote walikabiliana na vishawishi vya kuwalazimisha kuikana Imani yao; wote walikataa kumkana Mpendwa wao. Pia tazama visa vya ushujaa wa kushangaza uliyooneshwa tena na tena na watoto na vijana ambao iliwalazimu kustahamili mahojiano na matusi kutoka kwa walimu na maulama na kufukuzwa kutoka shuleni kwa sababu ya kushikilia imani zao. Aidha, inastahiki kuangalia kuwa chini ya makatazo makali sana yanayowekwa kwa ukatili mkubwa juu ya jumuiya zao, vijana walitoa huduma ya kipekee, walielekeza nguvu zao kwenye asasi za Kibahá'í kote nchini. Hakuna kauli nzuri zaidi inayoweza kutoa ushahidi ipasavyo kwa kujidhatiti kwao kiroho na uaminifu kuliko vitendo vyao hivi visafi visivyo na ubinafsi na dhamira. Hakuna sehemu yoyote duniani ambako malipo makubwa kiasi hiki yanadaiwa kwa ajili ya imani kutoka kwa Wabahá'í. Wala hawatapatikana vijana wenye nia, wachukuzi wang'aavu zaidi wa kikombe cha dhabihu kuliko vijana Wabahá'í shujaa wa Iran. Je, hivyo basi, si jambo la kawaida kutarajia kuwa ninyi, vijana wadogo na wakubwa mnaoishi katika wakati wa ajabu usio wa kawaida kama huu, baada ya kushuhudia vitendo vya kishujaa vya wenzenu kutoka Iran, na kwa kutumia uhuru wa kutembea kama huo, 'mtaweza kuingia, bila kizuizi kama upepo', katika uwanja wa utendaji wa Kibahá'í?"[53]**

Fursa za kutafakari juu ya matukio muhimu katika maisha ya roho shujaa kote ulimwenguni zinaweza kusaidia kila kizazi cha vijana kupata hisia ya wito. Mafundo ya karibu huundwa na watu hawa mashuhuri utotoni kupitia masimulizi yanayohadithiwa katika madarasa ya watoto ya kila wiki ya nyumbani, lakini juhudi ya makusudi zaidi inahitajika kukidhi hitaji hili kati ya umri wa miaka kumi na mbili hadi kumi na tano na, bila shaka, katika kipindi chote cha ujana. Mifano iliyochaguliwa kwa uangalifu, baadhi ya kusisimua na mingine

ya kawaida tu, yaweza kuonesha sifa kama ujasiri, dhamira, shauku, na kutokuwa na ubinafsi, ambazo vijana lazima wajitahidi kuiga.

1. Baini ama kutoka historia ya mwanzo wa Imani au kutoka nyakati za karibuni zaidi matukio machache ambayo unahisi vijana wanapaswa kutafakari: ________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

2. Eleza sababu zako za kuchagua matukio haya maalum: ________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

## SEHEMU YA 21

Hata baada ya mwonjo mdogo tu wa aya zilizonukuliwa hapo juu, inaweza kuonekana kuwa maisha ya mashujaa wa mwanzoni wa Imani na roho shujaa zilizowafuatia zilitofautishwa kwa hisia ya kusudi. Hali kadhalika ni dhahiri kuwa kila mmoja wao kwa uhakika alimiliki uelewa wa maana ya kipindi cha historia ambamo waliishi, pia na muono wa ukubwa wa badiliko ambalo wanadamu waliitwa kufanya. Ya kwamba hisia hii ya kusudi ilijitokeza katika maisha ya kujitolea kueneza Ujumbe Mtakatifu pia ni wazi. Walakini, tunapotafakari juu ya matendo ya kishujaa waliyofanya na hatimaye kujitoa muhanga kama wengi wao walivyofanya, hatuwezi kuamini kuwa tabia hizi peke yake ziliwatofautisha viumbe hawa waliotakasika. Kitu gani hasa kiliyaainisha maisha yao zaidi? Shauku gani iliwamiliki, na kitu gani kiliwasukuma kufikia viwango kama hivyo vya huduma isiyo na ubinafsi? Je, haukuwa upendo wa Mungu uliowaka kwa mng’aro mkubwa mioyoni mwao? Je, hawakuleweshwa na uzuri wa Mpendwa wao? Je, tunaweza kamwe kutumaini kuchangia kwenye uwezeshaji wa kiroho wa kizazi kinachofuata cha vijana kama hatulei ndani mwao mvuto kwa uzuri, kama tusipokuza hamu yao ya ndani ya kujitwalia vijito vitiririkavyo kwa ulaini vya elimu ya kweli, kama tusipowasaidia kukuza mahusiano ya karibu na Muumba wao? Hebu tuhitimishe kitengo hiki kwa kujizamisha wenyewe katika maneno yafuatayo:

> **“Kwani mpenzi wa kweli na rafiki thabiti afikapo mbele ya Mpendwa, uzuri unaong’aa wa Yule Mpendwa na moto wa moyo wa mpenzi utawasha moto na kuchomelea mbali utando wote na vizuizi. Naam, vyote alivyonavyo, kutoka kwenye moyo hadi kwenye ngozi, vitawaka, hata kisibaki kitu chochote ila yule Rafiki.”**[54]

> **“Enyi rafiki! Msiutelekeze uzuri wa milele kwa ajili ya uzuri ambao hauna budi ufe, na msiweke huba yenu juu ya dunia hii ya umauti ya vumbi.”**[55]

**“Fahamuni kuwa ni msomi wa kweli yule ambaye amekiri Ufunuo Wangu, na amekunywa kutoka Bahari kuu ya ujuzi Wangu, na kuruka juu kabisa katika anga la upendo Wangu, na ametupilia mbali kila kitu isipokuwa Mimi, na kukishikilia imara kile alichoteremshiwa kutoka kwenye Ufalme wa kauli Yangu nzuri ajabu. Yeye, kwa ukweli ni kama jicho kwa mtu, na sawa na roho ya uhai kwa mwili wa muumbo wote. Atukuzwe Yule Mwenye Rehema zote Ambaye amemwelimisha, na kumsababisha kuinuka na kuhudumia Hoja Yake kuu na yenye uwezo. Kwa kweli, mtu kama huyo amebarikiwa na Umati wa juu, na wale waishio ndani ya Hema la Ufahari, ambae amegugumiza Divai Yangu iliyofungwa katika jina Langu, Mwenyezi, Mwenye Nguvu zote!”[56]**

**“Enyi jeshi la Mungu! Wakati wowote mumuonapo mtu ambaye umakini wake wote umeelekezwa kwa Hoja ya Mungu; ambaye lengo lake pekee ni hili, kuhakikisha Neno la Mungu linafanya kazi; ambaye mchana na usiku, kwa nia safi, anaitumikia Hoja; ambaye kutoka kwenye tabia yake haionekani dalili hata kidogo ya kujipenda ama ya maslahi binafsi — ambaye, anaona ni bora arande katika nyika za upendo wa Mungu, na hunywa kutoka kwenye kikombe cha ujuzi wa Mungu, na anajikita kabisa kusambaza manukato matamu ya Mungu, na anapenda kabisa aya takatifu za ufalme wa Mungu — fahamuni kwa uhakika kuwa mtu kama huyo atasaidiwa na kuimarishwa na mbingu; kwamba mithili ya nyota ya asubuhi, yeye daima atang’aa kwa wangavu kutoka anga za neema ya milele. Lakini yeye akionesha dalili hata kidogo za tamaa za ubinafsi na kujipenda, jitihada zake zitampeleka kwenye utupu na yeye atateketezwa na atabaki bila matumaini hadi mwisho.”[57]**

**“Tambueni kwa ukweli, mkono wa Majaliwa Matakatifu umekuvutieni ninyi kwenye Kiti cha Enzi cha Ufalme, na habari njema tukufu zimekupatia nderemo na furaha kubwa ndani mwenu, kiasi kwamba wewe umeweza kuondoa mfuniko na kuinua utando kutoka Sura ya Uzuri Mtukufu, na kuuona Wajihi ung’aao kupitia umaizi wako, na kutambua siri za usafi na utakatifu katika Hoja hii tukufu!**

**“Sasa, kwa moyo unaofurika kwa upendo wa Mungu, msihi Mungu kwa nderemo zote, na mshukuru Mungu kwa mwongozo huu na zawadi hii ya juu. Na tambua, kwamba kwakweli, vikosi vya safu za mbele vya zawadi za Bwana wako vitakupita kutoka pande zote pale ambapo miguu yenu itakapokuwa imara katika Njia hii.”[58]**

**“Ee Mungu wangu! Ee Mungu wangu! Mtumishi Wako, huyu, amesogea kukuelekea Wewe, anatangatanga kwa shauku katika jangwa la upendo Wako, akitembea katika njia ya huduma Yako, akitarajia fadhila Zako, akitumaini ukarimu Wako, akitegemea ufalme Wako, na akileweshwa kwa divai ya zawadi Yako. Ee Mungu wangu! Ongeza ari ya huba yake Kwako, uthabiti wa kukusifu Wewe, na joto la upendo wake Kwako.**

**“Kwa kweli, wewe u Mkarimu kabisa, Bwana wa neema tele. Hakuna Mungu mwingine ila Wewe, msamehevu, Mwenye Rehema!”[59]**

## MAREJEO


1. ‘Abdu’l-Bahá, katika *Sala na Nyaraka za kibahá’í kwa ajili ya Vijana* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1978), na. 38, uk. 30.

2. ‘Abdu’l-Bahá, katika *Sala za Kibahá’í: Mateuzi ya Sala Zilizofunuliwa na Bahá’u’lláh, Báb, na ‘Abdu’l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2002, 2017 kuchapisha), ku. 246–47.

3. *Chaguo kutoka maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2010, 2015 kuchapisha), na. 225.9, uk. 394.

4. ‘Abdu’l-Bahá, Imenukuliwa katika barua ya tarehe 11 April 1985 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa mtu binafsi, iliyochapishwa kwenye *Jumbe kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu 1963–1986: Awamu Tatu ya Zama za Utungo* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1996), na. 426.3a, uk. 665.

5. ‘Abdu’l-Bahá, kwenye *Sala za Kibahá’í*, uk. 248.

6. Bahá’u’lláh, imenukuliwa kwenye ujumbe wa Riḍván 1982 kwa Wabahá’í wa ulimwengu, iliyochapishwa kwenye *Jumbe za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 1963–1986*, na. 321.5a, uk. 538.

7. Kutoka ujumbe wa tarehe 25 Mei 1975 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa, kama hapo juu., na. 162.34, uk. 310.

8. Kutoka ujumbe wa tarehe 1 Julai 2013 ulioandikwa kwa washiriki wa makongamano 114 yanayokuja kote ulimwenguni, uliochapishwa kwenye *Muundo wa utendaji: jumbe zilizochaguliwa za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na nyenzo za ziada, 2006–2016* (West Palm Beach: Palabra Publications, 2017), na. 27.3, uk. 176.

9. Kutoka ujumbe wa tarehe 10 Juni 1966 ulioandikwa kwa vijana wa Kibahá’í katika kila nchi, uliochapishwa kwenye *Jumbe za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 1963–1986*, na. 37.2, uk. 92.

10. Kutoka barua ya tarehe 23 Februari 1995 ulioandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Mabaraza ya kiroho ya kitaifa yaliyoteuliwa.

11. Kutoka ujumbe wa tarehe 29 Disemba 2015 ulioandikwa kwa kongamano la bodi ya Washauri wa Bara, uliochapishwa kwenye *Muundo wa utendaji*, na. 35.39, uk. 226.

12. Kutoka barua ya tarehe 23 Aprili 2013 ilioandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Baraza la kiroho la kitaifa, kama hapo juu., na. 52.3, uk. 296.

13. Kutoka barua ya tarehe 19 Aprili 2013 ilioandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa kundi dogo la watu binafsi, kama hapo juu., na. 51.9, uk. 293.

14. Kutoka ujumbe wa tarehe 12 Disemba 2011 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Mabaraza yote ya kiroho ya Kitaifa, kama hapo juu., na. 20.21, uk. 138.

15. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1983, 2017 kuchapisha), CXXXVII, aya. 4, uk. 338.

16. Kutoka barua ya tarehe 8 Disemba 1923 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa jumuiya ya Kibahá'í, zilizochapishwa katika "Uaminifu: Njema Kuu za Kibahá'í", iliokusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, iliyochapishwa kwenye *Makusanyo ya Makusanyo* (Maryborough: Kamati ya Uchapishaji la Kibahá'í Australia, 1991), juz. 2, na. 2075, uk. 345.

17. *'Abdu'l-Bahá katika London: Hotuba na Tanbihi za Maongezi* (London: Kamati ya Uchapishaji la Kibahá'í, 1987), uk. 66.

18. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, XXIX, aya. 1, uk. 78.

19. Bahá'u'lláh kwenye "Uaminifu" iliyochapishwa kwenye *Makusanyo ya Makusanyo*, juz. 2, na. 2032, uk. 332.

20. 'Abdu'l-Bahá, *Siri za Ustaarabu Mtakatifu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2007, 2016 kuchapisha), aya. 5, uk. 5.

21. Kama hapo juu., aya. 6, uk. 6.

22. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, XLIII, aya. 4, uk. 105.

23. Kama hapo juu., CXXVI, aya. 2, uk. 306.

24. Bahá'u'lláh, iliyonukuliwa na Shoghi Effendi, *Ujio wa Haki Takatifu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2006, 2018 kuchapisha), aya. 48, uk. 47.

25. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, LX, aya. 3, uk. 133.

26. Bahá'u'lláh, imenukuliwa na Shoghi Effendi, *Ujio wa Haki Takatifu*, aya. 39, uk. 34.

27. Kama hapo juu., aya. 39, ku. 34–35.

28. *Nyaraka za 'Abdu'l-Bahá Abbas* (New York: Kamati ya Uchapishaji la Kibahá'í, 1915, 1940 kuchapisha), juz. 2, uk. 436.

29. *Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXLIII, aya. 3, uk. 354.

30. Kama hapo juu., LXX, aya. 1, uk. 154.

31. 'Abdu'l-Bahá, kwenye *Baadhi ya Maswali Yaliyojibiwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2014, 2016 kuchapisha), na. 10.8, uk. 58.

32. Kutoka hotuba iliyotolewa tarehe 17 Novemba 1912, iliyochapishwa kwenye *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu: Hotuba zilizotolewa na Abdu'l-Baha wakati wa Ziara Yake Amerika na Canada mwaka 1912* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2012), aya. 4, uk. 618.

33. Kutoka hotuba iliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá tarehe 29 Agosti 1912, kama hapo juu., aya. 4, uk. 405.

34. Bahá'u'lláh, katika *Maneno yaliyofichwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2003, 2012 kuchapisha), Kiajemi na. 6, uk. 24.

35. *Wosia na Agano la 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1944, 2013 kuchapisha), ku. 26–27.

36. *Maneno yaliyofichwa*, Kiajemi na. 49, uk. 39.

37. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 10.2, ku. 41–42.

38. Báb, iliyonukuliwa kwenye *Wanamapambazuko*: *Simulizi ya Nabil ya siku za mwanzoni za Ufunuo wa Kibahá'í* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1932, 2018 kuchapisha), uk. 93.

39. *Wosia na Agano la 'Abdu'l-Bahá*, ku. 27–28.

40. Kutoka hotuba iliyotolewa tarehe 17 Novemba 1911, iliyochapishwa kwenye *Mazungumzo ya Paris: Maongezi yaliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá mwaka 1911* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2006, 2016 kuchapisha), na. 49.17, ku. 199−200.

41. Kutoka hotuba iliyotolewa na 'Abdu'l-Baha tarehe 1 Septemba 1912, iliyochapishwa kwenye *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 7, uk. 417.

42. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 105.2, uk. 186.

43. Kutoka barua ya tarehe 17 Februari 1933 ilioandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa mtu binafsi, kwenye *Shughuli za kijamii*: *Makusanyo Yalioandaliwa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2020), na. 90, uk. 44.

44. Kutoka kwenye ujumbe wa Aprili 1955 ulioandikwa na Shoghi Effendi, uliochapishwa kwenye *Jumbe kwa Ulimwengu wa Kibahá'í, 1950–1957* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1971, 1999 kuchapisha), uk. 76.

45. Kutoka barua ya tarehe 4 Mei 1953 ilioandikwa na Shoghi Effendi, kama hapo juu., uk. 155.

46. Kutoka ujumbe wa tarehe 1 Julai 2013 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa washiriki wa makongamano 114 ya vijana yanayokuja kote ulimwenguni, uliochapishwa kwenye *Muundo wa utendaji*, na. 27.2, uk. 175.

47. Kama hapo juu., na. 27.6, uk. 177.

48. Kutoka kwenye ujumbe wa tarehe 8 Februari 2013 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabahá'í wa ulimwengu, kama hapo juu., na. 22.4, uk. 147.

49. Kutoka kwenye ujumbe wa tarehe 8 Januari 2000 ulioandikwa kwa marafiki waliokusanyika kongamano la vijana nchini Paraguay, uliochapishwa kwenye *Kituo cha Kugeukia*: *Jumbe zilizochagulwa za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na nyenzo za ziada*, *1996–2006* (West Palm Beach: Palabra Publications, 2006), na. 20.3–4, ku. 123–24.

50. Shoghi Effendi, *Mungu Yu Nasi* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1974, 2019 kuchapisha), ku. 4–6.

51. Kutoka kwenye ujumbe wa tarehe 1 Julai 2013 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa washiriki wa makongamano 114 ya vijana yanayokuja kote ulimwenguni, uliochapishwa kwenye *Muundo wa utendaji*, na. 27.1, uk. 175.

52. Kutoka ujumbe wa tarehe 10 Juni 1966 ulioandikwa kwa vijana wa Kibahá'í katika kila nchi, uliochapishwa kwenye *Jumbe kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu*, *1963– 1986*, na. 37.1, uk. 92.

53. Kutoka ujumbe wa tarehe 3 Januari 1984 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa vijana wa Kibahá'í wa ulimwengu, kama hapo juu., na. 386.6, uk. 616.

54. *Wito kwa Mpendwa Mtakatifu: Kazi za Mafumbo Zilizochaguliwa za Bahá'u'lláh* (Haifa: Makao Makuu ya Ulimwengu ya Kibahá'í, 2018), na. 2.76 uk. 46.

55. *Maneno yaliyofichwa*, Kiajemi na. 14, uk. 26.

56. *Nyaraka za Bahá'u'lláh zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1988, 2005 kuchapisha), na. 14.4, ku. 207–8.

57. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 35.7, ku. 103-4.

58. *Nyaraka za 'Abdu'l-Bahá Abbas* (New York: Kamati ya Uchapishaji ya Kibahá'í, 1909, 1930 kuchapisha), juz. 1, uk. 182.

59. 'Abdu'l-Bahá, kwenye *Sala za Kibahá'í*, uk. 173.



# Rika la Matumaini

## Kusudi

Kuchunguza uwezo mkubwa wa vijana kati ya miaka kumi na mbili na kumi na tano na kuthamini umuhimu wa kuwapatia mazingira yafaayo kwa uwezeshwaji wao wa kiroho

## SEHEMU YA 1

Katika kitengo kilichopita, tulijadili baadhi ya sifa ambazo huwaainisha vijana. Kusudi la kitengo hiki ni kutafakari juu ya uwezo mkubwa wa vijana chipukizi na nguvu ambazo zinayapa umbo maisha yao. Dhana ambazo mtazichunguza hapa zimeendelea kuimarishwa kupitia miongo ya uzoefu. Mahitaji maalumu ya wale wenye umri kati ya miaka kumi na mbili na kumi na tano yametambuliwa kwa kipindi kirefu sasa na jumuiya ya Kibahá'í. Kutoka majaribio ya awali ya kuwaelimisha wajumbe wa kundi rika hili na juhudi zilizofuatia za kujifunza jinsi ya kufungua uwezo wao na kuelekeza nguvu zao zinazosukasuka, programu ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi tunayoichunguza katika kitabu hiki iliibuka hatua kwa hatua. Pengine unaifahamu programu hii, kwa kushiriki humo ulipokuwa mdogo, kwa kufanya kazi na mmoja wa marafiki zako anaetenda na kikundi cha vijana chipukizi, au kuwa, pamoja na wengine, kuwatembelea wazazi katika Kijiji au ujirani wenu kujadili mbinu na mada zake. Nyenzo unayosoma sasa imekusudiwa kukusaidia kujitolea kwa miaka mitatu ya mwanzo, lakini pengine zaidi, kwa uwanja huu wenye kustahili wa huduma, ikikuwezesha kuwasaidia wajumbe kadhaa wa kundirika waliojaa matumaini katika kuongoza hatua hii muhimu ya maisha yao.

Kuhusiana na programu ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huandika:

> **"Ueneaji wa haraka wa programu ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi bado ni udhihirisho mwingine wa maendeleo ya kiutamaduni katika jumuiya ya Kibahá'í. Wakati mielekeo ya ulimwengu huonesha taswira ya kundirika hili kama tatanishi, lililopotea katika machungu ya mabadiliko ya kimsukosuko ya kimwili na kihisia, lisilojali na lililoteketezwa na nafsi, jumuiya ya Kibahá'í — katika lugha iitumiayo na mbinu itumiazo — kwa vyovyote vile inasonga mbele kuelekea mwelekeo mwingine, ikiona katika vijana chipukizi badala yake utu, hisia kali ya haki, hamu ya kujifunza juu ya ulimwengu na tamaa ya kuchangia kwenye ujenzi wa ulimwengu bora zaidi. Simulizi hadi simulizi, ambamo vijana chipukizi katika nchi zote duniani huelezea fikra zao kama washiriki katika programu hii, huthibitisha juu ya uhalali wa muono huu. Kuna kila dalili kwamba programu hii huhusisha ufahamu wao unaopanuka katika uchunguzi wa uhalisia ambao huwasaidia kuchanganua nguvu za ujengaji na ubomoaji zinazofanya kazi katika jamii na kutambua ushawishi ambao nguvu hizi huuweka kwenye mawazo na vitendo vyao, ikinoa mtazamo wao wa kiroho, ikiimarisha uwezo wao wa kujieleza na ikiboresha miundo ya kimaadili ambayo itawasaidia katika maisha yao yote. Katika umri ambapo nguvu zichipuazo za kiakili, za kiroho na za kimwili hupatikana kwao, wao wanapewa nyenzo zihitajiwazo kupinga nguvu ambazo zingewanyang'anya utambulisho wao wa kweli kama viumbe bora na kufanya kazi kwa manufaa ya wote."[1]**

Dhana nyingi na mawazo yanayotajwa na Nyumba ya Haki katika fungu lililopo hapo juu ndiyo shabaha yenyewe ya kitengo hiki cha mafunzo, na kadri unavyopita humo, zitakuwa wazi zaidi katika akili yako. Kwa sasa, pengine ungependa kujibu maswali yafuatayo:

1. Ni taswira ipi ambayo mielekeo ya kiulimwengu inaonesha ya kundi rika ambalo vijana chipukizi hupatikana? ________________________________________

   ________________________________________________________

2. Jumuiya ya Kibahá'i inaona nini, badala yake, katika kundi la rika hili?

3. Kwa kuhusisha ufahamu upanukao wa vijana chipukizi kwenye uchunguzi wa uhalisia, ni nini programu ya uwezeshwaji wao wa kiroho huwasaidia kufanya?

4. Nyenzo wanazozipata vijana chipukizi kupitia programu hii huwawezesha kufanya nini?

5. Kwa nini unafikiri kuwa vijana wa rika hili la miaka kati ya kumi na mbili na kumi na tano huwakilisha kundi maalumu kama hilo?

6. Kufuatana na yaliopo hapo juu, na kwa kuwakumbuka vijana chipukizi wachache ambao tayari unaowafahamu, je, unaweza kubaini baadhi ya mahitaji maalum ya kizazi hiki cha vijana wadogo?

7. Kitu gani hukuhamasisha kuingia katika ulingo huu mahsusi wa huduma?

## SEHEMU YA 2

Bahá'u'lláh hutuambia kwamba mtu binafsi hufikia mwanzo wa ukomavu kwenye umri wa miaka kumi na tano, ambapo sheria kama zile zinazohusu sala ya faradhi na mfungo zinakuwa za lazima kwake. Ikitazamwa kutoka mtazamo huu, miaka inayotangulia kabla ya umri huo hupata umuhimu maalumu. Ni katika miaka hiyo michache ambamo badiliko la mpito kutoka utoto kwenda kipindi cha ujana hutokea. Mabadiliko ya ghafla na ya haraka ambayo kwa kawaida huhusishwa na kipindi hiki cha mpito — ya kimwili, ya kiakili, na kihisia — hushawishi tabia kwa njia kadhaa.

Wafikiapo umri wa miaka kumi na mbili, dalili za hatua ya badiliko la mpito huanza kutokea. Vijana wengi watakua zaidi kimwili katika kipindi cha miaka mitatu hadi mine ijayo kuliko katika hatua nyingine yoyote ya maisha yao. Wataongezeka katika kimo na uzito wa mwili na watahisi mabadiliko ya homoni. Wavulana watakuza sauti nzito, na mabinti wataanza kupata umbo la usichana. Wote watapitia kipindi cha balehe, na kupata uwezo wa kimaumbile wa kuzaa watoto.

Mabadiliko ya kimwili na kimihemko ambayo mtu hupitia katika kipindi hiki yanaingiliana. Msisimko juu ya uibukaji wa uwezo mpya na shauku ya kuutumia huambatana na mfadhaiko, wepesi wa kuhisi, na hisia za wasiwasi. Mihemko hii inaweza kupelekea kwenye uibukaji wa tabia kinzani. Mtu anaweza kuonekana mwenye aibu, wakati mwingine mchangamfu; pengine anaweza kupenda kuachwa peke yake, na wakati huohuo anakaribisha nadhari; anaweza kuwa na ujasiri wa ajabu katika hali fulani na katika hali nyingine anaweza kuwa mwoga. Wasiwasi unaoendelea kukua kuhusu vipaji na uwezo wa mtu binafsi hatua kwa hatua hujidhihirisha wenyewe, kama vile iongezekavyo hisia ya utambuzi wa nafasi ya mtu ulimwenguni, hususani katika muktadha wa mahusiano ya mtu pamoja na wote wanarika na watu wazima. Jinsi wengine waonavyouona mwonekano wake na wanavyoyaitikia mawazo yake, hupata umuhimu.

Zaidi, mnamo kipindi cha miaka michache kabla ya kufikia umri wa miaka kumi na tano, dhana za kimsingi kuhusu maisha ya mtu binafsi na ya pamoja huundwa katika akili zetu. Uwezo wetu wa uchambuzi unakuwa wenye nguvu zaidi, na pengine tunaweza kuanza kujiuliza juu ya mengi tuliyofundishwa na kuona ukinzani katika ulimwengu unaotuzunguka ambao hapo awali yalipita bila kutiliwa maanani. Hatuko tayari kama hapo kabla kukubali, kufuata bila kufikiri viwango vilivyowekwa na watu wazima. Mtu daima hutafuta majibu kwa maswali, ambayo aghalabu ni ya kifalsafa kiasili, mnamo kipindi hiki cha mabadiliko, na ufahamu mpya hukua kwa haraka.

Kama vijana ni wa kusaidiwa katika kutumia nguvu zao zinazoibuka kwa mafanikio, ni lazima kuepukana na kuwatendea katika njia ambazo huelekea, kwa upande mmoja, hurefusha utoto wao na, kwa upande mwingine, huwahamasisha kuiga aina moja ya utu uzima wa juu juu katika sura zake nyingi — mtindo ambao, kwa bahati mbaya, unapata mizizi katika jamii zaidi na zaidi, 'Abdu'l-Bahá huelekeza:

> **"Baada ya muda yeye huingia kipindi cha ujana, ambamo hali zake za zamani na mahitaji yanapitwa na mahitaji mapya yanayoweza kutumika kuendelea katika kiwango chake. Uwezo wake wa uchunguzi hupanuliwa na huimarishwa; vipaji vyake vya kiakili hufunzwa na kuamshwa; mapungufu na mazingira ya utoto hayazizuii tena nguvu zake na mafanikio yake."**[2]

Kuongeza uelewa wenu wa tofauti kati ya miaka ya utoto na kipindi cha ujana, jadilini maswali yafuatayo katika kikundi chenu:

1. Ina maana gani kwa uwezo wa uchunguzi kupanuka na kuimarika? Je, unaweza kuonesha maoni yako kwa mifano michache? ________________________________

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________

2. Uwezo wa kiakili ya kijana chipukizi hutofautiana vipi na ule wa mtoto? _________

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________

3. Ni yapi baadhi ya mapungufu ya utoto ambayo hayadhibiti tena uwezo za kijana chipukizi? ______________________________________________________________

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 3

Kila mtu binafsi sharti apokee aina ya elimu na malezi katika miaka mara tu kabla ya umri wa miaka kumi na tano ambayo yataruhusu mielekeo iliyomo ndani ya kipindi cha ujana kuibuka. Hitaji la elimu kama hiyo linakuwa wazi zaidi pale ambapo inapotambuliwa kuwa, kufikia umri wa miaka kumi na tano, mitindo mingi ya mawazo na tabia ya mtu binafsi itakuwa tayari imeimarika. Kama ambavyo ‘Abdu’l-Bahá hueleza,

> **“ni vigumu sana kumfundisha mtu binafsi na kuboresha sifa yake baada ya balehe kupita. Hadi wakati huo, kama uzoefu unavyoonesha, hata kama kila juhudi ingefanyika kuboresha baadhi ya tabia yake, hayo yote hayangesaidia chochote. Anaweza, pengine, kuboresha kiasi fulani leo; lakini acha siku chache zipite na yeye husahau, na hugeukia nyuma kwenye hali za tabia yake na njia za kawaida alizozizoea.”**[3]

Wewe unafahamu istilahi “kipindi cha balehe”, ambayo mara nyingi hutumika kwa uhuru kurejelea kwa vijana popote kuanzia umri wa miaka kumi na mbili hadi kufikia miaka kumi na nane. Wakati mwingine kifungu cha maneno “mwanzoni mwa balehe” hutumika kuwabaini wale walio kwenye rika la umri ambao kwa kawaida tunawaita “vijana chipukizi”. Hapa sisi hatutakazia mno hususan kwenye suala hili na kutumia istilahi kwa kubadilishana na

kurejelea kwa vijana kati ya rika la miaka kumi na mbili na kumi na tano. Kufikiri kuhusu umuhimu wa elimu mnamo kipindi cha balehe, amua kama matamko yafuatayo ni kweli:

_____ Hata kama elimu inayofaa haipokelewi katika utoto, malezi yafaayo mnamo kipindi cha balehe yanaweza kusaidia kusahihisha mtindo wowote usiofaa wa tabia iliyostawishwa kabla.

_____ Ni wale watu binafsi tu ambao wamepata elimu ya kiroho na maadili utotoni wanaweza kukuza uwezo wao wote.

_____ Bila umakini unaofaa na uangalizi mnamo kipindi cha balehe, mtu binafsi anaweza kupotea njia, hata kama wakati wa utoto alipata elimu ya maadili na kiroho.

_____ Ni katika kipindi cha balehe kwamba watu binafsi huanza kupatanisha maisha yao na nguvu ambazo zinaendeleza jamii au kujiruhusu wenyewe kupotoshwa kwa nguvu za mmomonyoko wa kijamii.

## SEHEMU YA 4

Ufahamu unaoendelea kukua mnamo kipindi cha balehe unaweza kuelekezwa kuelekea mojawapo ya ncha mbili: kuelekea unyenyekevu kwa Mapenzi ya Mungu na kujitoa dhabihu kwa huduma kwa jamii ya wanadamu au kuelekea kutekwa ndani ya gereza la ubinafsi na ashiki. ‘Abdu’l-Bahá huweka wazi:

> **“Hali ya upekee ya kila kitu kilichoumbwa hutegemea juu ya hekima takatifu, kwa kuwa katika muumbo wa Mungu hakuna kasoro. Hata hivyo, haiba haina hali ya kudumu. Ni sifa inayoweza kubadilika kidogo ndani ya mtu ambayo inaweza kugeuzwa kwenye mwelekeo wowote. Ikiwa kama atapata njema stahiki, hizi zitaimarisha hali ya upekee ya mtu na kutoa nje nguvu zake zilizofichika; lakini ikiwa atapata kasoro, uzuri na ukawaida wa hali ya upekee vitapotea kwake na sifa alizopewa na Mungu zitasongwa katika hali chafu ya ubinafsi.”**[4]

Tunaishi katika zama ambamo tamaduni zenye shari za kidunia zinashambulia kila sura ya maisha. Mshughuliko wa nafsi uliozidishwa ambao umesukwa ndani ya kitambaa cha utamaduni huu ulioenea kote unatuletea changamoto lukuki kadri tunavyojaribu kuwasaidia vijana katika kukuza uwezo wao, kwani hata jitihada ambazo kwa dhati zinatafuta kuwasaidia vijana kutambua uwezo wao na kuelekeza nguvu zao kuelekea kwenye ustawi wa wote zinaweza kusumbuliwa kutokana na ushawishi usiofaa wa muono wa ulimwengu ambao ni wenye ubinafsi kwenye kiini chake. Tatizo hili ni tata. Mfumo wa ulimwengu wa leo huwanyima idadi kubwa ya watu uvumilivu unaohitajika kuishi maisha yenye kusudi; kwahiyo, imani katika nguvu ya maadili ya mtu mwenyewe ni suala la kuangaliwa. Huficha wito wa kweli wa watu; kwahiyo, ufanikishaji wa matarajio bora ya mtu ni wazo halali. Huufanya umati kutotambua maisha ya roho; kwahiyo, ugunduzi wa uwezo wa kweli uliomo ndani ya mtu hustahili umakini. Walakini, programu ambazo husisitiza “nafsi” siyo lazima kurekebisha hali hii. Kile kinachotokea mara kwa mara ni kwamba, kwa kisingizio cha kujitambua, kujigundua, na kujitukuza, programu kama hizi humremba mtu binafsi na kuongeza nguvu za ubinafsi. Changamoto yetu ni kulea hali ya upokevu wa kiroho ndani ya vijana, ili mioyo yao myororo iweze kuguswa kwa mvuto wa Uzuri Mkuu Kabisa na kugeuzwa kuelekea ubora wa juu wa huduma isiyokuwa na ubinafsi kwa jamii ya binadamu. Juhudi zetu za kushughulikia mahitaji

ya kielimu ya awamu hii ya mtungo katika maisha yao lazima zizuie nafsi ng'ang'anizi isiweze kujitetea yenyewe. Ili kuchunguza asili ya changamoto hii, mnaombwa, katika sehemu chache zifuatazo, kutafakari juu ya baadhi ya aya kutoka kwenye maandiko ambazo zinarejelea kwenye nafsi. Kwanza, pengine, mnaweza kuona ya muhimu kujadili katika kikundi chenu maana ya fungu la maneno lisemalo "nafsi ng'ang'anizi ijiteteayo yenyewe". Mtu anaweza kuhakikishaje kuwa huduma haiwi ulingo ambamo nafsi haijikwezi?

## SEHEMU YA 5

Seti ya kwanza ya mateuzi hapa chini inahusiana na nyanja ya "hali ya upekee" ambazo humfurahisha Mungu na zinapaswa kuendelezwa:

> **"Enyi watumishi Wangu! Kama mngelifahamu maajabu yapi ya ukarimu Wangu na fadhila ambazo nimeamuru kukabidhi roho zenu, kwa kweli, mngelijiondoa wenyewe kwenye mwambatano kwa vitu vyote vilivyoumbwa, na mngelipata ujuzi wa kweli juu ya nafsi zenu wenyewe — ujuzi ambao ni sawa na ule ufahamu wa Uwepo wangu Mimi Mwenyewe. Mngelijikuta wenyewe huru kwa vitu vyote isipokuwa Mimi, na mngeliona kwa jicho lenu la ndani na la nje, na dhahiri kama ufunuo wa jina Langu ling'aalo, bahari za wema Wangu wa upendo na fadhila zinazosogea ndani mwenu."[5]**

> **"Mbali, mbali kutoka utukufu Wako uwe uthibitisho wa watu wa umauti kukuhusu Wewe, au sifa Zako, au sifa ambazo kwazo anaweza kukutukuza Wewe! Wajibu wowote ambao wewe umewaandikia watumishi Wako kuutukuza kwa kiwango cha juu kabisa ufahari Wako na utukufu ni ishara ya neema Yako juu yao, ili wawezeshwe kupanda kwenye daraja walilopewa juu ya uwepo wao wa ndani kabisa, daraja la ufahamu wao wenyewe."[6]**

> **"Ṭaráz ya kwanza na mwangaza wa kwanza ambao umechomoza kutoka upeo wa Kitabu Mama ni kwamba mtu sharti ajue nafsi yake mwenyewe na kutambua kwamba kile kinacho mwelekeza kwenye ubora au uduni, utukufu au udhilifu, utajiri au umaskini."[7]**

> **"Ewe mwana wa roho! Nilikuumba tajiri, kwanini unajishusha mwenyewe kwenye umaskini? Nilikuumba bora, kwa nini basi unajidhalilisha? Kutoka kiini cha ujuzi nilikupa uwepo, kwa nini unatafuta elimu kutoka kwa mwingine kando Yangu? Kutoka katika udongo wa upendo Nilikuumba, kwa jinsi gani unajishughulisha na mwingine? Geuzia uoni wako kwako mwenyewe, ili kwamba uweze kuniona nikisimama ndani mwako, mwenye uwezo, mwenye nguvu na ajitoshelezaye."[8]**

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kuzingatia mateuzi yaliyopo hapo juu:

a. Tunapo fahamu ni kwa maajabu gani ukarimu Wake na fadhila za Mungu zimeamuru kukabidhi roho zetu, sisi ______________________________________
______________________________ , na tuta ________________________ .

b. Sisi wenyewe tutajikuta ______________________________________________ ,
na mngeliona kwa jicho lenu la ndani na la nje, __________________________
_________________________________________________________________________
_________________________________________________________________________
____________________________ .

c. Wajibu wowote ambao umeamuriwa juu yetu wa kutukuza ukuu na utukufu wa Mungu ni ishara ya neema yako juu yetu kwamba tuwezeshwe ku _____________
_________________________________________________________________________
_________________________________________________________________________
________________________ .

d. Sharti tujue nafsi zetu wenyewe na kutambua kile ambacho hutuongoza kwenye _____________________ au, _____________ au ________________________ ,
________________ au _________________ .

e. Tumeumbwa ___________________ , na tumefanywa ____________________ .
Kutoka kiini cha _________________________ Mungu ametupa uwepo, na kutoka udongo wa _________________________ Ali _____________________________
sisi. Hutuomba kugeuzia uoni wetu kwetu wenyewe, ili tuweze _______________
_______________________________________________________________ .

Mateuzi yote hapo juu hurejea kwenye nafsi zetu za kweli na umuhimu wa kuelewa asili yake. Sharti tutambue, bila shaka, kwamba ujuzi wa ubora wa uwepo wetu usitupeleke kwenye ukwezwaji wa nafsi bali unyenyekevu mbele ya Mungu na watumishi Wake. Jadilini katika kikundi chenu jinsi gani ujuzi wa nafsi yetu ya kweli hutusaidia katika mapambano yetu dhidi ya ubinafsi.

## SEHEMU YA 6

Seti ya pili ya mateuzi hutuonya juu ya matokeo ya kuendekeza nafsi:

**“Kila roho isiyo kamili ni yenye ubinafsi na hufikiria mazuri yake tu.”**[9]

**“Lakini ikionesha doa japo dogo kabisa la tamaa yenye ubinafsi na kujipenda, juhudi zake zitaipeleka patupu na itaangamizwa na hatimae kuachwa bila matumaini.”**[10]

**“Hususan wewe ungependa kuokolewa kutoka kwenye majivuno. Sifa hii, ambayo ni kiburi, imekuwa njia ya uangamizwaji wa watu wengi muhimu ulimwenguni. Kama mtu amejaa sifa zote njema na stahiki lakini ni mbinafsi, basi, sifa nyingine zote zitapotea na hatimaye zitageuzwa kuwa kasoro mbaya kuliko zote.”**[11]

**“Ukataji tamaa, pote hapa na baada ya hapa, ndicho kitu pekee utakachokipata kutokana na kuendekeza nafsi; fedheha na mateso ndivyo utakavyovuna kutoka ushabiki, kutoka kuwaamini wajinga na wasio na akili.”[12]**

**“Leo, watu wote wa ulimwengu wanajiendekeza katika maslahi binafsi na wanatumia nguvu zao zote katika juhudi na jitihada ya kuendeleza maslahi yao wenyewe ya kimwili. Wanajiabudu wenyewe na siyo uhalisia mtakatifu, wala ulimwengu wa jamii ya binadamu.”[13]**

**“Majaribu haya, kama ulivyoandika, husafisha si kingine ila madoa ya ubinafsi kutoka kwenye kioo cha moyo, hadi jua la Ukweli liweze kuangazia miale juu yake; kwa sababu hakuna utando wenye kuzuia zaidi kuliko nafsi, na hata utando ukiwa mwembamba kiasi gani, hatimaye utamfungia mtu nje kabisa, na kumnyima sehemu yake ya rehema ya milele.”[14]**

**“Tazama jinsi jua linavyong’aa juu ya muumbo wote, lakini ni nyuso zile tu ambazo ni safi na zilizong’arishwa zinazoweza kuakisi utukufu na mwangaza wake. Roho yenye giza haina sehemu ya ufunuo wa mwangaza mtukufu wa uhalisia; na udongo wa nafsi, usiokuwa na uwezo wa kufaidi mwangaza huo, hauwezi kuzalisha ukuaji.”[15]**

**“Imedhalilika kiasi gani roho ambayo inaweza kupata starehe katika giza hili, ambayo inajishughulisha na masuala yake yenyewe, mateka wa nafsi na ashiki, ikigaragara katika tope la ulimwengu wa kimwili!”[16]**

“Ubinafsi”, “kujipenda”, “kujiabudu”, “majivuno”, “kuendekeza maslahi binafsi”, na “mateka wa nafsi na ashiki” huibua ile hali ambayo huzima sifa za upekee wetu tuliopewa na Mungu. Kufuatana na aya zilizopo hapo juu, eleza katika sentensi chache jinsi gani ushughulikaji sana na nafsi huzuia ukuaji wa kiroho na maendeleo ya maadili na hupunguza ufanisi wa huduma.

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

## SEHEMU YA 7

Seti ya tatu ya mateuzi huwakilisha sampuli ndogo ya ushauri mwingi unaopatikana katika maandiko kuhusu jinsi ya kuishugulikia nafsi ng'ang'anizi:

> **"Leo uthibitisho wa Ufalme wa Abhá ni wa wale ambao hujikana wenyewe, husahau maoni yao wenyewe, huweka kando haiba zao na hufikiria ustawi wa wengine. Yeyote ambaye amejipoteza mwenyewe, ameupata ulimwengu na wakaazi wake. Yeyote ambaye anajishughulisha na masuala yake mwenyewe, anatangatanga katika jangwa la kutokujali na majuto. 'Ufunguo mkuu' kwa ajili ya kujitawala ni kujisahau. Barabara ielekeayo kwenye makazi ya kifalme ya maisha ni kupitia njia ya kujikana."[17]**

> **"Yeye ametujalia uwezo wa kupenyeza uhalisia wa vitu; lakini lazima tuwe wenye kujikana, lazima tuwe na roho zilizotakasika, nia safi, na kujitahidi kwa moyo na roho tukiwa katika ulimwengu wa wanaadamu kwa ajili ya kufikia utukufu wa milele."[18]**

> **"Kwahiyo lazima tando za nafsi ya kishetani ziteketezwe kwa moto wa upendo, ili roho iweze kusafishwa na kunadhifishwa na hivyo iweze kujua daraja la Yule Bwana ambaye kama asingekuwapo ulimwengu usingeumbwa."[19]**

> **"Acheni fikra zote za nafsi, na mjitahidi kuwa watiifu na wanyenyekevu kwa Mapenzi ya Mungu tu. Kwa njia hii peke yake tutaweza kuwa raia wa Ufalme wa Mungu, na kuyafikia maisha ya milele."[20]**

> **"Fanyeni kila muwezalo ili muwe mliochoshwa kabisa na nafsi, na mjifunge wenyewe kwa Wajihi wa Miangaza; na pindi mkishafika kwenye vilele kama hivyo vya utumishi, mtavikuta, vitu vyote vilivyoumbwa, vikiwa vimekusanywa pamoja katika kivuli chenu. Hii ni neema isiyokuwa na mipaka; hii ni enzi ya juu kabisa; haya ndiyo maisha yasiyokufa. Vingine vyote isipokuwa hiki mwishowe ni uangamizi dhahiri na hasara kubwa."[21]**

> **"Kwahiyo, ewe rafiki, ikane nafsi yako ili wewe uweze kumpata Yule asiye na kifani, muweze kwenda mbele zaidi kuipita dunia hii ya umauti ili wewe uweze kutafuta kiota chako katika makaazi ya mbinguni. Uwe kama utupu, kama ungependa kuwasha moto wa uwepo na uweze kuwa mwenye kufaa kwa ajili ya njia ya upendo."[22]**

> **"Hebu tuweke kando fikra zote za nafsi; hebu tufumbe macho yetu kwa vyote vilivyomo duniani, hebu tusiyatambulishe mateso yetu wala kulalamika juu ya makosa yetu. Bali hebu tuwe wasiojali nafsi zetu wenyewe, na tunywe mvinyo wa neema ya mbinguni, hebu tupaze sauti za furaha yetu, na kujipoteza sisi wenyewe katika uzuri wa Mwenye Utukufu wote."[23]**

> **"Enyi watu wa ulimwengu! Msifuate vishawishi vya nafsi, kwa sababu vinakuita kwa msisitizo kwenye uovu na ukware; bali mfuate Yule ambaye ni Mmiliki wa vitu vyote vilivyoumbwa, Ambaye anakuamrisha kuonesha ucha mungu, na kudhihirisha kicho cha Mungu."[24]**

Mielekeo ambayo inapendekezwa na mateuzi yaliyopo hapo juu imesimama kinyume kabisa na kuabudu nafsi na upaniaji wa tabia ya kuiridhisha nafsi ambayo huziainisha jamii nyingi za leo. Baini kutoka aya hizi baadhi ya mielekeo tunayopaswa kukuza kuelekea nafsi. Mifano miwili inatolewa kukusaidia.

- Tunapaswa kujifunza kujikana nafsi zetu wenyewe, kusahau maoni yetu wenyewe, kuweka kando haiba zetu na kufikiria ustawi wa wengine.
- Tunapaswa kujifunza kujikana.
- Sharti tujifunze ______________________________
______________________________
- Shari tujifunze ______________________________
______________________________
- Sharti tujifunze ______________________________
______________________________
- Sharti tujifunze ______________________________
______________________________
- Sharti tujifunze ______________________________
______________________________
- Sharti tujifunze ______________________________
______________________________

Jadilini katika kikundi chenu jinsi gani mielekeo mlioibaini inavyochangia kwenye maendeleo ya kiumbe bora na kuvijalia uwezo vitendo vya huduma.

## SEHEMU YA 8

Hatimaye, maneno yafuatayo ya ‘Abdu’l-Bahá hutukumbusha uhusiano wa pamoja kati ya kujitoa dhabihu na uwezo wa kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii:

> **“Umati wa watu unajishughulisha na nafsi na tamaa za kiulimwengu, zimezamishwa katika bahari ya ulimwengu wa chini na ni mateka wa ulimwengu wa asili, ziokoe roho zile ambazo zimeachiliwa huru kutoka minyororo na pingu za ulimwengu wa kimwili na, mithili ya ndege warukao kwa kasi, zinapaa katika milki hii isiyo na mipaka. Wao wako macho na ni waangalifu, wanaepukana na giza la ulimwengu wa asili, matakwa yao ya juu kabisa yanalenga juu ya kutokomeza kutoka miongoni mwa watu huangaikaji kwa ajili ya uwepo, ung’aaji wa kiroho na upendo wa milki ya juu, kutenda wema mkuu kabisa miongoni mwa watu, ufanikishaji wa mahusiano ya karibu kati ya dini na vitendo vya mfano bora wa kujitoa dhabihu ya nafsi. Hapo ndipo ulimwengu wa jamii ya binadamu utabadilishwa kuwa Ufalme wa Mungu.”**[25]

**"Enyi jeshi la Mungu! Leo, katika ulimwengu huu, kila mtu anatangatanga kwa upotofu katika jangwa lake mwenyewe, akienda huku na kule kufuatana na matakwa ya upuuzi wake na mawazo ya kujiendekeza, akifuata mawazo yake mahsusi. Miongoni mwa umati wote uliojaa duniani, jumuiya hii peke yake ya Jina Kuu Kabisa ndiyo huru na haina njama za kiutu na haina kusudi lolote la kibinafsi inaloliendeleza. Peke yake miongoni mwao wote, watu hawa wameinuka pamoja kwa malengo ambayo yametakaswa kutokana na nafsi, wakifuata Mafundisho ya Mungu, wakishughulika kwa shauku kubwa kabisa na kujitahidi kuelekea lengo moja: kubadilisha vumbi hili la chini kuwa mbingu ya juu, kuufanya ulimwengu huu kioo cha Ufalme, ili kubadilisha ulimwengu huu katika ulimwengu tofauti, na kuzisababisha jamii zote za binadamu kuchukua njia za uadilifu na mtindo mpya wa maisha."[26]**

**"Enyi wapendwa wa Mungu! Katika Maongozi haya ya Kibahá'í, Hoja ya Mungu ni roho safi. Hoja Yake siyo mali ya ulimwengu wa kimwili. Haikuja kwa ajili ya ugomvi ama vita, wala kwa ajili ya vitendo vya uchokozi au aibu; siyo kwa ajili ya kugombana na Imani nyingine, wala kwa ajili ya mapigano pamoja na mataifa mengine. Jeshi lake pekee ni upendo wa Mungu, furaha yake pekee ni mvinyo safi wa ujuzi Wake, vita vyake pekee ni uelezaji wa Ukweli; pambano lake moja ni dhidi ya nafsi ng'ang'anizi, vishawishi viovu vya moyo wa mwanadamu. Ushindi wake ni kunyenyekea na kujisalimisha, na utovu wa nafsi ndiyo utukufu wake wa milele."[27]**

Mateuzi yaliyopo hapo juu yanaeleza baadhi ya sifa bainifu za wale ambao 'Abdu'l-Bahá anawafikiria kuwa katika "jeshi la Mungu", ambao Huwarejelea kama "wapendwa wa Mungu", wale ambao wameachiliwa "huru kutoka minyororo na pingu za ulimwengu wa kimwili". Tafakari juu ya tofauti hizi kadiri unavyokamilisha sentensi zilizopo hapa chini.

a. Umati wa watu unajishughulisha na ________________________________ , wamezamishwa katika ____________________________________ na ni mateka ________________________________________________________________ ________________________________________________________________ .

b. Roho zile ambazo zimeachiliwa huru kutoka minyororo na pingu za ulimwengu wa kimwili na, mithili ya ndege warukao kwa kasi, _____________ na __________ ; _______________________________________________ ,wanaepukana na ___________________________ , matakwa yao ya juu kabisa yanalenga juu ya ______________________________________ , _____________________ na __________________ , zoezi la _____________________________________ , ufanikishaji wa ______________________ na vitendo vya __________________ _________________________ .

c. Leo, katika ulimwengu huu, kila mtu ___________________________________ ________________ , akienda ________________________________________ ________________________________________________________________ , wakifuata __________________________ .

d. Jumuiya hii pekee ya Jina Kuu Kabisa ndiyo ________________________________
___________ na ___________________________________________________ .
Peke yake miongoni mwao wote, watu hawa wameinuka pamoja kwa _________________________________________ , wakifuata _______________
____________ , _________________ kwa shauku kubwa kabisa na _____________
______________________ : kubadilisha __________________ kuwa __________
________ , kuufanya ____________________________________________ ,
___________________________________________________ , na kuzisababisha jamii zote za binadamu ________________________________________________ .

e. Hoja ya Mungu na roho ___________ . Siyo mali ya _________________
___________ . Jeshi lake pekee _________________________ , furaha yake pekee _______________________________ , vita vyake pekee ____________________
________ ; pambano lake moja ni ____________________________ , __________
______________________________ . Ushindi wake ni _____________________
_______________ , na ________________________________________________ .

## SEHEMU YA 9

Pengine ungependa kukariri makusanyo yafuatayo kutoka sala zilizofunuliwa na Bahá'u'lláh:

> **"Watie moyo, Ee Bwana wangu, kwa hisia ya unyonge wao wenyewe mbele ya Yule Ambaye ni Mdhihirishaji Wako Mwenyewe, na wafundishe kutambua umaskini wa asili yao wenyewe mbele ya sura ya alama Zako nyingi za utoshelezaji Wako mwenyewe na utajiri, ili waweze kujikusanya pamoja kuzungukia Hoja Yako, na kung'ang'ania pindo la rehema Yako, na kushikilia kamba ya furaha njema ya amri Yako."[28]**

> **"Waondolee, basi, watumishi Wako, Ee Mungu wangu, mavazi ya nafsi na tamaa, au jalia kwamba macho ya watu Wako yaweze kuinuliwa juu kwenye vilele ambavyo vitafanya waone ndani ya tamaa zao siyo kingine ila mpeperuko wa pepo nyanana za umilele wa utukufu Wako, na wanaweza kutambua katika nafsi zao wenyewe siyo kingine isipokuwa ufunuo wa Nafsi yako Mwenyewe yenye rehema, kwamba ardhi na vyote vilivyomo humo viweze kusafishwa kutokana na chochote kile kilicho kigeni Kwako, au chochote kile kidhihirishacho kitu kingine isipokuwa Nafsi Yako."[29]**

## SEHEMU YA 10

Kadiri shauku yako katika kuwalea vijana chipukizi iimarikavyo, utazifahamu nadharia nyingi ambazo zinajaribu kukielezea kipindi cha balehe. Moja ya maneno ambayo utakutana

nayo mara kwa mara ni “misukosuko” — ihusianayo na utambulisho, mihemko, mahusiano na wazazi, mwingiliano na mamlaka, na kadhalika. Mnahitaji kuangalia kwa umakini nadharia hizi, isijetokea mkaichukulia hali hii ya misukosuko kama hali ya lazima ya kila kijana chipukizi. Je, ni muhimu kwa maisha ya kila kijana kimsingi kuanishwa na vurugu ya aina moja au nyingine? Je, vijana chipukizi katika kipindi chote cha historia wamepitia fujo na vurugu, na wanapitia misukosuko kama hiyo katika kila tamaduni na jamii za leo?

Katika kujaribu kujibu maswali haya, mnapaswa kutambua kwamba mafunzo mengi yaliyoenea ya vijana yanatekelezwa ndani ya miundo inayotilia mkazo uliopindukia kwenye nafsi, kwenye kujiridhisha, kwenye mabadiliko ya kibaiolojia, kwenye utambuzi wa kijinsia, na kwenye mafanikio ya kimwili — taaluma, kipato, na daraja la kijamii. Wao aghalabu hulenga kwa ufinyu kwenye tabaka, mbari, na jinsia, wakipuuzia sifa za kiasili walizopewa na Mungu zilizomo katika kila roho ya binadamu. Baadhi ya umaizi ambao utaupata kutoka mafunzo haya, bila shaka, utakuwa wenye msaada kadri utakavyojitahidi kuelewa sifa za kundirika hili. Lakini yapo mashaka kwamba juhudi zilizo hamasishwa na mafunzo kama hayo zitaweza kufanya mengi zaidi kuliko kuwapa uzoefu wa utamaduni vijana juu ya desturi za jamii inayothamini vitu vya kimwili, jamii ambayo, tunajua, huelekea kuharibu upokevu wa kiroho. Kwa kinyume chake, je, dhana ya vijana chipukizi unayoikumbatia, haiwezi kuitisha maendeleo ya utambulisho wa kiroho wa watu binafsi ambao wata “peleka mbele ustaarabu unaoendelea daima” na ambao wata kuwa “wajenzi wa umoja”na “watetezi wa haki”.

Jambo muhimu la kukumbuka katika suala hili ni kwamba namna ambavyo vijana wanavyoonwa na wengine lina athari kubwa kwao. Hivyo ndivyo taswira yenye giza ya kipindi cha balehe iliyoenea kwa upana zaidi katika jamii inavyosadia kujenga katika mazingira ruwaza za tabia zisizo kubalika, zinavyozidi kuenezwa. Chukulia, kwa mfano, tamko ambalo lilisemwa na Sigmund Freud kwamba kipindi cha balehe ni ugonjwa wa akili wa muda mfupi au pendekezo la Anna Freud kwamba, kuwa katika hali ya kawaida mnamo kipindi cha balehe, kwenyewe ni. kutokuwa kawaida. Je, matamko kama hayo hayawi kama tando zinazozuia watu kuona uwezo wa kweli wa vijana chipukizi? Ni uthibitisho gani uliowaongoza wanasayansi hawa kufikia hitimisho la kiujumla kama hilo? Bila shaka, ipo idadi fulani ya waelimishaji ambao wamekizungumzia kipindi cha balehe katika istilahi zinazokubalika zaidi, lakini mawazo yao hayatawali mjadala juu ya mada hii. Taswira zinazoendelea kutawala akili za wazazi na walimu halikadhalika ni za uasi, utovu wa mantiki na upuuzi. Pengine tunaweza kuuliza, ni kwa jinsi gani jamii ambayo ina mawazo kama hayo, yakibubujika katika mishipa yake, itaweza kuwasaidia vijana chipukizi kuwa aina ya vijana walioelezwa katika kitengo cha kwanza cha kitabu hiki?

## SEHEMU YA 11

Katika muktadha wa majadiliano yaliyopo hapo juu, tungependa kupendekeza kwamba mchukue msimamo ufuatao: wakati wowote kikundi chochote cha vijana chipukizi kikuzapo tabia isiyokubalika — ambazo mbali na zile zitokeazo kiasilia kutoka hatua zinazofuatana za misukosuko na ushindi ambayo ni sifa ya mchakato wa ukuaji wa kawaida — sababu zake zinatakiwa kutafutwa katika mazingira ya kijamii, pengine katika mikanganyiko ya waziwazi ambayo akili inayoamka ya vijana hugundua katika maisha ya watu wazima ambao walikuwa wanaaminika hapo awali bila mashaka yoyote, au katika hali ya kutokuweza kwa watu wazima kutambua mantiki ya mtu anayejaribu kuacha nyuma tabia za utoto.

Kwa uhakika msimamo huu, haubishani na kutokuwepo kabisa kwa hali ya kuwa na papara au uasi katika tabia za vijana chipukizi. Kinacho pendekezwa ni kwamba mazingira ya kijamii, hususani tabia za watu wazima, ambazo kwa kiasi kikubwa zinawajibika kwa tabia nyingi zisizopendeza ambazo zimekuja kuhusishwa na rika hili. Ili kuchunguza matokeo ya dai tulilofanya pengine mngependa kujadili katika kikundi chenu uhalali wa matamko yafuatayo na kutunga mengine ambayo yanaeleza zaidi wazo lenyewe:

- Vijana chipukizi huasi dhidi ya watu wazima ambao huwaambia wafuate viwango ambavyo wao wenyewe hawavifuati.

- Vijana chipukizi huonekana waasi wanapopewa ushauri katika sauti ya kukaripiwa.

- Wao huwa wapuuzi pale ambapo ulimwengu hauwapi chochote bali shughuli za kijuujuu zinazozuia maendeleo ya uwezo wao wa kiakili.

- Wao huonesha dharau kwa nidhamu pale ambapo watu wazima wanawalazimisha kufuata sheria kali, hasa kama wao walipewa uhuru usio na mipaka walipokuwa watoto.

- Wao huonekana wenye papara pale ambapo watu wazima wanao wazunguka hawawasaidii kufikiria vyema kuhusu matokeo ya maamuzi yao.

- Wao hukuza kiburi pale ambapo wanafundishwa umuhimu wa nafsi zao wenyewe badala ya huduma isiokuwa na ubinafsi kwa jamii.

- Wao hujiendekeza nafsi pale ambapo propaganda ya kila mara inapowashawishi kuridhisha shauku zao za kimwili.

__________________________________________________________________

## SEHEMU YA 12

Nyumba ya Haki ya Ulimwengu imeongea juu ya "kutokujali na utovu wa maadili" wa "jamii yenye kuendekeza" na hitaji la vijana kujilinda dhidi ya ushawishi wake:

> **". . . Hoja ya Mungu itapata faida kubwa sana pale ambapo itakaonekana kwamba Wabahá'í, na hususani vijana wa Kibahá'í, wanasimama kwa uwazi dhidi ya kutokujali na utovu wa maadili wa jamii yenye kuendekeza, ya kwamba tabia yenye viwango vya juu ambavyo wao hujitahidi kuendeleza vimetia mizizi katika kanuni za kiroho, vikiwapa ujasiri, kujiheshimu na furaha ya kweli. Kwa upande mwingine madhara makubwa kabisa yanaweza kufanywa kwa Hoja ikiwa wafuasi wake wamegubikwa na wimbi la wakati huu."[30]**

Katika teuzi lifuatalo, Mlinzi hutupatia umaizi wa kina kuhusu asili ya jamii kama hizo na ushawishi wake juu yetu sote:

> **"Kwa hakika, sababu kuu ya kuenea kwa maovu katika jamii kwa sasa ni ukosefu wa hali ya kiroho. Ustaarabu wa kimwili wa zama zetu umefyonza sana uwezo na maslahi ya jamii ya mwanadamu, kiasi kwamba watu kwa ujumla hawahisi tena ulazima wa kujiinua juu ya uwezo na hali ya maisha yao ya kila siku ya kimwili. Hakuna madai ya kutosha kwa ajili ya vitu ambavyo tunaweza kuviita vya kiroho ili tuweze kuvitofautisha kutoka mahitaji na matakwa ya uwepo wetu wa kimwili."[31]**

Zipo idadi fulani za dalili za kuanguka kwa maadili ambazo Mlinzi hubaini pale ambapo hueleza juu ya nguvu za ubomoaji zinazofanya kazi katika jamii leo. Miongoni mwa hali ambazo hutilia mkazo katika mawasiliano yake ni mwelekeo usiofaa juu ya ndoa na matokeo ya wimbi liongezekalo la talaka; kudhoofika kwa mshikamano wa familia na kudorora kwa udhibiti wa wazazi unaoenedelea kuongezeka; ufuatiliaji wenye pupa wa starehe za kidunia, utajiri na anasa; kupotoka katika tabia za anasa ya burudani; uharibikaji wa sanaa na muziki; mmomonyo katika kiwango cha fasihi na habari; na chuki ya kimbari na kiburi cha uzalendo. Wakati hakuna mwenye kinga dhidi ya vishawishi vya maovu haya, vishawishi huathiri vijana chipukizi katika njia mahususi. Kwa mfano, fikiria juu ya matokeo ya talaka. Vijana wadogo bila shaka huhisi masikitiko ya kina pale ambapo wazazi wao wanapotalikiana, na wao hutamani kupata usalama na ulinzi wa kaya yenye umoja. Lakini ni katika kipindi cha balehe ambapo watu binafsi ambao huelemewa na mihemko kama vile hatia, hasira, aibu, na udhalilishwaji pale ambapo ndoa ya wazazi wao inapovunjika. Wakati wanawalaumu wazazi wao, hawawezi kujizuia kujilaumu wao wenyewe kwa hatima mbaya ya familia. Mbegu za mashaka juu ya ndoa na maisha ya familia hupandwa katika akili zao, na kutotarajia kwao wema kunathibitishwa na mwendelezo wa talaka zinazoendelea wanaouona katika jamii inayowazunguka.

1. Pengine ingekusaidia kutafakari juu ya namna ambamo baadhi ya hali za kijamii zilizobainishwa hapo juu zinavyoweza kubumba mtazamo wa vijana wa uhalisia, jinsi wanavyojifikiria, mitazamo yao ya maisha, hisia zao na mihemko yao, uwezo wao kutofautisha kati ya mema na mabaya, tabia zao kuelekea wengine, na imani yao katika asasi za jamii. Hali mbalimbali zilizotajwa zimeorodheshwa hapa chini, na nafasi zimetolewa kwa ajili yako ili uandike mawazo yako.

a. Kutokujali na utovu wa maadili wa jamii yenye kuendekeza: ________________

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________

b. Kudhoofika kwa mshikamano wa familia na kudorora kunakoongezeka kwa udhibiti wazazi: ________________________________________________________

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________

c. Ufuatiliaji wenye pupa wa starehe za kidunia, utajiri na anasa; kupotoka katika tabia za anasa ya burudani: ____________________________________________

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________

d. Uharibikaji wa sanaa na muziki; mmomonyoko katika kiwango cha fasihi na habari: ____________________________________________________________

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________

e. Uadui wa kimbari na kiburi cha uzalendo: ____________________

2. Hisia gani zinajaza moyo wako na akili unapo tafakari juu ya jinsi hali ya mmomonyoko wa kijamii inavyoathiri maisha ya vijana chipukizi? Katika njia ipi utambuzi huu unaongeza uwezo za juhudi zako kuwasaidia kukuza uwezo uliyomo katika asili yao ya kweli?

## SEHEMU YA 13

Kuweka umakini kwenye ishara za ulimwengu unaomomonyoka, haina maana ya kukataa matokeo ya nguvu zinazojenga ambazo pia zinafanya kazi katika jamii leo. Kile kinachohitajika ni kuwapa vijana chipukizi, mazingira ambamo uwezo wao wa kiroho unaweza kulelewa kuhakikisha, kwa njia hii, kwamba wao wanavutika kwenye nguvu zinazofaa za kijamii. Majaribio yoyote ya kuwatenga kabisa kutoka hali ya kijamii yenye madhara kwa hakika, lingekuwa bure. Badala yake, wao wanapaswa kusaidiwa kutathmini na kuchambua jinsi ulimwengu unaowazunguka unavyo athiri mawazo yao na mihemko. Kwa mintarafu hii, umakini maalum unatakiwa kutolewa kwa suala la propaganda, kwani katika jamii nyingi, propaganda inazidi kubumba maadili, mielekeo, na maoni ya vijana chipukizi. Mtazamo mfupi juu ya baadhi ya sura za utangazaji unatosha kuangaza kipengele hiki.

Nguvu za vitu vya kimwili ambazo zinatawala propaganda hupotosha uhalisia. Kwa mfano picha zinazo wasilishwa katika matangazo, kuhusu upatikanaji wa mwonekano wa nje wa mtu uliokamilika lakini ambao hauwezi kupatikana, hucheza juu ya hisia za vijana katika wakati ambamo wao utambuzi wao wenyewe huanza kuibuka. Ujumbe baada ya ujumbe huonesha kazi kubwa ya wasichana wadogo kama ile ya kuwavutia wanaume. Aidha, tabia ya kuueleza urijali hasa katika istilahi ya uwezo wa kimwili peke yake umekuzwa sana, aghalabu hadi kufikia hatua ya kukubali vitendo vya kikatili na kujihatarisha na kuhamasisha visa vya kusisimua vya kingono na ushindi. Chochote kile kinachotambulika kama udhaifu hukataliwa katu, na tabia yenye udhalimu uenezwa hatua kwa hatua. Cha kushangaza, aina mahsusi ya ugumu inaoneshwa kuwa kitu cha kupendeza, kwa lengo la kuwafanya wasichana waiige.

Hakuna mashaka kuwa kusudi la kimsingi la sehemu kubwa ya matangazo huelekezwa kwa vijana ili kujenga utamaduni wa kidunia, ambamo wangetamani sana kuwemo ndani yake. Katika utamaduni huu wangejifunza kuongea lugha moja, kufanya vitendo vinavyofanana, na zaidi ya yote, kutumia mkusanyiko mkubwa sana usiokwisha wa bidhaa. Muhimu zaidi, wangeingizwa katika utaratibu wa thamani wenye utata ambao ungeweza kuamua mtindo wao wa utumiaji kwa maisha yao yote. Ni jambo la kutanabahi kuwa istilahi "kijana" yenyewe iliundwa miongo michache iliyopita kwa ajili ya kuliteka soko pokevu ambalo huwakilishwa na tabaka hili la jamii.

Ili kuzitumia kikamilifu shauku zinazoanza kuzinduka, utamaduni ambao unaenezwa katika matangazo huweka mvuto wa kingono kwenye kiini cha maisha ya kijana. Bidhaa kama vile vinywaji laini ambavyo havina uhusiano wowote na mvuto wa kingono hutumika kuleta katika akili ya vijana taswira tupu za mahusiano ya kimapenzi. Hisia ya kutofaa kwa mtu binafsi na wasiwasi wa kukataliwa kwa sababu ya harufu ya mwili, ngozi isiyovutia, au nguo zisizo za kimtindo, huendelezwa kwa ajili ya kutambulisha bidhaa za urembo na mitindo mipya ambazo huahidi mvuto wa kingono na uhuru wa kutoka fedhea. Hata magari huelezwa kwa istilahi kama hizi "motomoto", "mtanashati", "tamu kuendesha" — yote yakiwa na maana ya kingono. Kadiri viwango vya kimaadili vilivyoshuka katika miongo michache iliyopita, maudhui ambayo hayakubaliki kimaadili ya utangazaji yamekuwa wazi zaidi na zaidi. Polepole, ingeonekana kuwa, baadhi ya sura za utumiaji zenyewe zinaendelea kuwa aina ya shughuli za kingono kama zilivyo.

Nafasi ya chapa ya bidhaa ya istilahi "ujana" katika soko la kidunia linaloendelea kupanuka, inastahili kutajwa kwa umaalum. Mafunzo ambayo huchunguza jinsi ya kufaidika na uwezo uliomo ndani soko hili hupendekeza bila aibu kuwa kuabudu nembo za chapa za bidhaa ni kipengele chenye nguvu cha utumiaji. Ni dhahiri kuwa chapa za bidhaa ni nanga katika ulimwengu usio na uhakika wa kipindi cha balehe. Zaidi ya hapo, aghalabu huonwa kama pasi ya kusafiria kuelekea kwenye tamaduni ya ulimwengu wa vijana ambayo hufanywa iwe ya kuvutia kupitia matangazo. Utamaduni ambao unaendelezwa na mbinu hizi za masoko bila shaka haujali umasikini unaozidi kuongezeka miongoni mwa mataifa; huonesha taswira ya wingi unaofurahiwa na watu wachache kati ya umati wa ulimwengu kuwahakikishia vijana kutoka kila usuli kwamba bidhaa ya watumiaji ni chanzo cha furaha isiyokuwa na mwisho.

Katika tafiti fulani za soko la "ujana", vijana wanaainishwa kufuatana na sifa zinazowafanya wakubali utumiaji wa aina maalum ya bidhaa — aina ambazo huruhusu matangazo kuwalenga kwa ufanisi zaidi. Kwa mfano, katika mojawapo ya uchunguzi mahsusi, wamegawanywa katika makundi sita: wale "Waliokata tamaa", wanaoona hatima yao imeshaamuliwa na wanajaribu kuishi kwa juhudi kidogo sana kadiri iwezekanavyo; "Misisimko na Hofu", ambao ni watu wanao tafuta starehe na ambao akili yao ni huru kutoka shughuli za kijamii na kisisasa, wako tayari kujiunga katika kuabudu nembo za chapa; wale waitwao "Wapambanaji", ambao ingawa wanafanana na kundi lililotangulia, hili pia lina msukumo na uwezo wa kufanya kazi ngumu na huona bidhaa na huduma kama njia za kuendeleza na kudumisha mafanikio katika ushindani; "Wafanikishaji wa kimya kimya", ambao ni wafuasi wa utamaduni ambao hukataa ukaidi wa kisiasa na wa kijamii na hubaki wameunganika kwa karibu na familia zao, na ambao ni wanunuzi wabaguzi wanaojali sifa na faida za bidhaa; "Washikiliaji", ambao pia ni wafuasi wa utamaduni lakini ambao hawana mwelekeo wa kitaaluma bali wanajaza akili zao takwimu za michezo na majina ya timu za wanariadha na wachezaji wakiacha nafasi kidogo kwa ajili ya masuala ya kisiasa na kiuchumi; na mwishowe "Waokoaji wa Ulimwengu", ambao wanatamani kufanya mabadiliko chanya

ulimwenguni na ambao umuhimu wao umo katika fursa wanayowapa wauzaji ya kugeuza hoja za kijamii kuwa bidhaa za kuuza.

Ingeonekana kwamba vitu vyote, vinaweza kuathiriwa na uwekaji chapa na utumiaji. Hususan katika ulingo unaobadilika kwa kasi wa mitandao ya kijamii, kila sura ya maisha ya mtu inaweza kuwa zana ya utumiaji. Majukwaa yaliyoundwa kimakusudi ya kuufanya ulimwengu uwe mahali pazuri zaidi kupitia, "ushiriki", "urafiki", na "ubadilishanaji taarifa kimtandao" yamegeuzwa kutumika kama njia za matangazo ya kuchanganya, ambayo yanafika mbali na yenye kupenyeza zaidi. Hatahivyo, hata kama unakanganyaje, uchambuzi mfupi uliowasilishwa hapo juu haukukusudiwa kama lawama kwa matangazo jinsi yalivyo. Kusudi lake ni kuongeza uwezo wako wa kuchunguza propaganda kwa uangalifu — za kibiashara, kisiasa, kimbari, kitamaduni — ili kwamba uweze kuwasaidia vijana chipukizi katika kubaini matokeo yake juu ya mawazo yao na tabia. Mazoezi yafuatayo yanaweza kukusaidia kutafakari zaidi juu ya suala hili tata:

1. Matangazo hutumia lugha na picha kubadilisha bidhaa za kawaida kuwa vyanzo vya msisimko. Alama hutumika kuvipa vitu na matukio umuhimu mkubwa zaidi kuliko vinavyostahili. Kinywaji, kwa mfano, hakiwezi kuelezwa kama kilivyo — kitu cha kukata kiu — lakini kinaoneshwa kama kitu cha kuleta shangwe na mafanikio. Alama zinazotumika na tasnia ya mitindo huzitangaza nguo kuwa zaidi ya mvuto wa urembo. Alama ya uchangamfu wa ujana huuza peremende. Alama za msisimko na ukakamavu wa kiriadha husaidia kuuza sigara na pombe kali. Je, unaweza kufikiria matangazo machache mahsusi na mafungu ya maneno na taswira wanazovitumia kugeuza kitu kimoja kuwa kitu ambacho hakiwezi kuwa kamwe?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

2. Njozi ya furaha inayojengwa kupitia ununuzi wa bidhaa yoyote, haina budi kuwa na maisha mafupi, au sivyo tungeridhika na kile tulicho nacho. Kwahiyo, matangazo yanahitaji kuendelea kujenga shauku na kuhakikisha kuwa haturidhiki kamwe na kuwa wenye furaha. Hili linapatikanaje?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

3. Tumesema kuwa hata hoja za kijamii wakati mwingine hugeuzwa kuwa bidhaa za utumiaji. Je, unaweza kutoa mifano machache?

4. Katika mazingira ya vyombo vya habari vya wakati huu, matarajio ya hali ya juu kwa bahati mbaya yanatumika kwa malengo ya kibiashara. Maneno na misemo yanayoibua ndani mwetu hisia bora, yanatumika kutangaza bidhaa, na sura mbalimbali za urithi wa kiroho wa jamii ya binadamu zinachukuliwa kama bidhaa za kununuliwa. Unaweza kutoa baadhi ya mifano?

5. Fikiria majukwaa ya mitandao ya kijamii yanayotumiwa na vijana chipukizi katika eneo lako. Ushiriki wao katika majukwaa kama hayo unaathirije asili ya urafiki wanaounda, mtazamo wao kuhusu wao wenyewe, na matumaini na matarajio yao? Katika mwangaza huu, fikiria uhalali wa tamko lifuatalo: Kupitia ujihusishaji wao kwenye mitandao ya kijamii, vijana chipukizi bila kujitambua wanaweza kujiona na kujiwasilisha wenyewe kama bidhaa.

## SEHEMU YA 14

Neno la tahadhari ni muhimu hapa. Haijalishi yanaweza kuwa ya madhara kiasi gani matokeo ya jamii ya leo kwa vijana, lingekuwa kosa kutilia msisitizo uliopindukia juu yake katika jitihada zako. Ni rahisi sana kuingia katika tabia ya kuwachukulia vijana chipukizi kama viumbe ambao ni dhaifu na ambao wanahitaji kulindwa kila wakati kutoka maovu ya mazingira yao. Njia kama hiyo haitoweza kamwe kuwaongoza kwenye uwezeshwaji wao wa kiroho. Kile kinachopaswa kuwa shabaha ya jitihada zako ni utambuzi wa uwezo wao wa kutenda kama wakala hai wa mabadiliko ya kijamii na kuchangia kwenye ustawi wa jamii. Hata katika ulimwengu wa sasa wenye matatizo, ipo mifano kadhaa ya vijana chipukizi katika kila tamaduni ambao wameshinda hali zisizokubalika za mazingira wanamoishi na ambao

wameonesha kila mara sifa kama vile shauku kwa ajili ya huduma, hamu ya kujifunza, hisia yenye nguvu ya haki, na mwelekeo wenye nguvu kuelekea ubinadamu.

Idadi fulani ya waelimishaji imeeleza baadhi ya nguvu za kiakili za kuzaliwa na za kiroho ambazo zinaweza kujidhihirisha katika kipindi cha mpito cha balehe. Wapo wachache, kwa mfano, ambao wametilia mkazo shauku vijana chipukizi waioneshayo katika matatizo ya kinadharia. Mwelimishaji mmoja ametilia mkazo nafasi waliyonayo ya kutekeleza katika badiliko la kijamii, akikiita kila kizazi cha vijana chipukizi "mzalishaji muhimu katika mchakato wa ukuaji wa mabadiliko endelevu," ambacho kinaweza "kutoa utiifu na nguvu zake pote pawili kwenye uhifadhi wa kile ambacho kinaendelea kuonekana kuwa ni cha kweli na kwenye masahihisho ya kimapinduzi ya kile kilichopoteza umuhimu wake wa kujihuisha." Na tena mfikiriaji mwingine amewafananisha wale waliomo katika kipindi cha balehe na "vyombo hai vya kiasili, ambavyo vimeundwa kikamilifu ingawa vinaendelea kukua," vyenye uwezo wa kupokea kwa "uwepo" wao wote. Na amevutia umakinifu kwenye uwezo wao wa kusababisha mabadiliko na anasisitiza kuwa elimu sharti ichukue fursa ya njia kadhaa za utambuzi, ikijumuisha nguvu ambayo vijana wanaweza kuileta kwenye tajiriba yoyote, ametanabahi kwamba ushadidi kama huo, "pamoja na ukweli wa uwepo," vinaweza kuifanya jamii ya wanadamu kuwa "kiumbe chenye uhai, kinachoshamiri, chenye upendo wa kweli, kilichojaa furaha na chenye uwezo mkubwa, badala ya dhana baridi, isiyo hai, tupu ya kinadharia." "Hayo ndiyo maajabu ya mabadiliko," ndio maneno yake, "na huo ndio uwezo uliomo ndani ya kipindi cha balehe."

Rejea hizi chache, pamoja na uchambuzi uliofanywa katika sehemu kadhaa zilizopita, huashiria jinsi gani mnahitaji kuwa wangalifu katika kueleza dhana ya kipindi cha balehe. Wakati bila shaka mtachunguza kwa uangalifu maoni tofauti juu ya mada hii katika miaka ya usoni, uelewa wenu wenyewe wa umuhimu wa kipindi hiki nyeti katika maisha ya mwanadamu kwa sehemu kubwa utabumbwa na vifungu kutoka maandiko kama zile zilizonukuliwa katika kitengo hiki na kile kilichopita. Na hapawezi kuwa mashaka yoyote kwamba maamuzi yenu yatathibitishwa na uzoefu wenu wenyewe wa kufanya kazi pamoja na vijana chipukizi.

## SEHEMU YA 15

Seti ya vitabu vilivyokuzwa na Taasisi ya Ruhi kwa ajili ya kusomwa na vijana chipukizi, kama ilivyo kwa sehemu kubwa vitabu vya mlolongo wake mkuu, vinaweza kuonekana rahisi kiudanganyifu kwa kutazama haraka haraka hususani vile vichache vya mwanzo. Urahisi kwa kiwango kikubwa haswa umo katika lugha iliyotumiwa na mazoezi yaliyotolewa. Dhana zinazoongelewa ni zenye utata na za kina. Mkondo wa fikra ambao unatiririka katika nyenzo zote, ambao siyo wa kitoto asilani utawapa changamoto vijana chipukizi watakaozisoma ili watafakari kwa kina juu ya masuala hayo. Ili kuwasaidia kuthamini uwezo wao wa kufanya hivyo, tunawawasilishia katika sehemu hii na sehemu mbili zinazofuata mawazo machache kama yalivyoelezwa na vijana chipukizi kadhaa wenyewe, ambao wote wameathiriwa, kwa njia moja au nyingine, na vurugu. Taswira nyingi mno zinaoneshwa katika vyombo vya habari juu ya tabia katili za vijana chipukizi kama hao kiasi kwamba inatubidi kusikiliza baadhi ya visa vyao ambavyo bado havijasimuliwa vya kupotelewa na matumaini.

Kisa cha kwanza ni katika maneno ya kijana mwenye umri wa miaka kumi na tatu — tumwite Peter ili kuficha jina lake halisi — ambaye ameshuhudia athari za ukatili na vita tangu alipokuwa na umri wa miaka nane. Alipokuwa na umri wa miaka kumi na tatu, alianza

kuhamasisha amani katika shule na mashirika ya vijana, akikubali matokeo, ambayo yalijumuisha kuzomewa kwa ukali na baadhi ya wanarika wenzake:

> *Hakuna kilichonisumbua. Familia yangu iliamini ilikuwa muhimu kujali kuhusu jumuiya na kufanya chochote tuwezacho kusaidia. Ingawa nilikuwa na umri wa miaka kumi na tatu tu, niliweza kuona kuwa matatizo makubwa kabisa yaliyotukabili yalikuwa ni ukatili na vita. Amani ilikuwa inahitajika zaidi kuliko kitu kingine chochote. Kwa uhakika, ni vigumu kwa mtoto kujaribu kuleta amani, lakini kujaribu ndiyo njia pekee ya kutekeleza chochote. . . .*
>
> *Uwongo mwingi umesemwa katika nchi yangu kwa muda wa miaka mingi kiasi kwamba watu hawajui nini au nani wa kumwamini tena. Hawawezi siku zote kuamini magazeti, radio au runinga, wanasiasa, vikundi vyenye silaha — lakini watu wanaposikia watoto wakiongea kuhusu ukatili na jinsi unavyotuathiri na jinsi tunavyotaka amani, kwa namna fulani wao hujua kuwa wanasikiliza ukweli. . . .*
>
> *Baadhi ya watu wanasema wao wanawapigania masikini, lakini masikini wameteseka zaidi kuliko yeyote mwingine vitani. Ninafikiri kuwa baadhi ya watu pia hupigana kwa ajili ya kulipiza kisasi, au kwa ajili ya madaraka, au kwa sababu wao wanahisi kuwa hawana chaguo lingine. Baadhi ya vijana hujiunga na vikundi vyenye silaha kwa sababu familia zao ni masikini na wao hawaoni njia nyingine.*

Peter na familia yake, walikuwa wametishiwa mno kipindi cha vita vya ndani ya nchi vilivyokuwa vinaendelea, walilazimika kuondoka kwenye nyumba yao. Baba yake alienda na kurudi kati ya ofisi yake na mji mpya walikokuwa wakiishi, lakini kiasi kidogo cha utulivu walichofurahia hakikuweza kudumishwa. Msaada hai wa baba yake kwa michakato ya Amani mwishowe uliishia katika kuuawa kwake:

> *Nilifikiri nilielewa kuhusu vita kwa sababu niliishi katikati ya mapigano. Yalikuwepo mapigano mitaani majira ya usiku. Mara nyingi niliamshwa kwa milio ya bunduki. Nilipokwenda shule asubuhi, niliona ushahidi — damu kwenye njia ya miguu, majengo yaliyo jaa risasi. Na nilikuwa nimewaona wahanga kwenye mochuari ambayo haikuwa mbali na ofisi ya baba.*
>
> *Nilikuwa nimeongea kuhusu suala hili kwa kujiamini, kana kwamba nilijua maana ya vita — lakini baba yangu alipouawa, nilivunjika nguvu siyo tu kwa majonzi, lakini kwa sababu sasa nilielewa maana ya vita. Nilijuwa maana ya kutaka kupigana. Nilitambua kuwa hata kama unatamani amani kiasi gani, utachukua hatua dhidi ya ukatili pale ambapo vita itakapokugusa wewe mwenyewe. Huu ni mtego huohuo ambao umewashika watu wengi mno katika nchi yangu. . . .*
>
> *Hakuna kilichokuwa sawa baada ya hapo. Nyumba niliiona kama kasha tupu lisilo na uhai. Mitaa ambayo nilikuwa naifahamu mno yote ilionekana migeni kwangu. Hakuna chochote na popote palipokuwa salama. Nilifikiri kuwa kazi yangu yote niliyoifanya kwa ajili ya amani haikuwa na thamani yoyote kwa sababu haikumwokoa baba yangu. Ukatili wa kuogofya ambao ulikuwa umeufunika mji wetu mwishowe ulikuwa umeshambulia moyo wa familia yangu — na nilikuwa nimeshindwa kuuzuia. Nilijilaumu mwenyewe. Nilijiuliza mwenyewe, "Nini nilifanya kwamba baba yangu afariki kikatili namna hiyo?"*

Familia iliendelea kupokea vitisho, na Peter alinunua bunduki ili aweze kuwalinda wapendwa wake. Jioni moja, kama siku kumi baada ya baba yake kuuawa, wanafamilia ya Peter walikuwa wamekusanyika katika chumba kilichopo kwenye ghorofa la juu la nyumba yao. Peter aliposhuka chini kuelekea jikoni, alimwona mvamizi akiwa na bunduki bustanini akitazama juu kwenye madirisha ya gorofa la pili:

> *Nilijua kuwa ningeweza kuchukua bunduki yangu na kumuuwa mtu huyu. . . . ingekuwa ni kulipiza kisasi kwa ajili ya kifo cha baba yangu. Ningekuwa nailinda familia yangu. Na hakuna mtu katika nchi yangu ambaye angenilaumu kwa kumpiga risasi . . . Bado wakati yote haya yalikuwa kweli, sikufanya chochote. . . . Baba yangu alinitaka nifanye kazi kwa ajili ya amani. Ningewezaje kuwa katili sasa? Njia pekee ambayo ningeweza kuonesha heshima na upendo kwa baba yangu, njia pekee ningeweza kusaidia kuiokoa familia yangu, ingekuwa kwa kujaribu kuleta amani. kumuua mtu huyu kusingeleta amani kwangu, au familia yangu au nchi yangu. Kwa uhakika, kwa kumuua ningepoteza kila kitu. Nisingekuwa bora kuliko alivyokuwa.*

Peter alimfuatilia mvamizi kimya kimya, ambaye, baada ya muda na bila sababu yoyote iliyo wazi, aligeuka na kuondoka. Muda mfupi baada ya tukio hilo, Peter aliachana na bunduki yake na akaapa kuwa hatomiliki nyingine kamwe.

Kabla ya kusoma kisa kinachofuata, pengine mngependa kubaini baadhi ya sifa zinazo muainisha Peter na kusema maneno machache kuhusu uwezo wake wa kutafakari juu ya mada za kina.

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

## SEHEMU YA 16

Mary — pia ni jina la kubuni — alilelewa katika mazingira ambamo kulikuwa tishio la mara kwa mara la migogoro; aligundua gharama ya kutokubaliana na kundi la marafiki katika umri mdogo:

> *Nilipofikisha umri wa miaka kumi na moja, kundi langu lilinisusa, kwa sababu nilikataa kupendelea sehemu moja katika mabishano. Kundi la marafiki zangu walimshutumu msichana mmoja katika darasa letu kwamba aliiba na mgogoro mkubwa ulizuka. Ilibidi uchague kuwa ama upande wa msichana huyu au dhidi yake, na marafiki zangu wote walikuwa dhidi yake. Kila mmoja alifikiria kuwa ningekuwa upande wao, lakini haukuwepo ushahidi kuwa msichana alikuwa mwizi. Sikuweza kuwa na uhakika. Sikutaka kuwapinga marafiki zangu, hatahivyo, kwahiyo*

*sikusema kitu. Kila mmoja alikasirika na, kwa mwaka mzima hakuna aliyeongea na mimi.*

Mary alijenga urafiki na mvulana mmoja, na ingawa wasichanawengine walimchokoza kuhusu yeye, alijenga hisia za upendo kwake. Walizoea kutembea pamoja kwa mda mrefu na kuongelea kuhusu mustakabali wao hadi siku moja alipomkuta anasafisha bunduki ambayo hakujua kama anaimiliki:

*Nilipoingia ndani, alinipa tabasamu, kana kwamba alikuwa hafanyi kitu chochote kisicho cha kawaida. Siku zote nimekuwa nikichukia ukatili, nikichukia bunduki na nikichukia vita. Alijaribu kutafuta visingizio, kama wafanyavyo watu kama yeye, lakini mimi nilimwambia palepale kuwa uhusiano wetu ulikuwa umekwisha, "Mimi sipendi maisha kama haya kwa ajili yangu au kwa ajili ya watoto wangu," nilisema. Nilikuwa mdogo sana inaonekana kama mzaha sasa lakini nilihisi kana kwamba ulimwengu wangu ulivunjika katika vipande viwili.*

Alama za Mary za shuleni zilianza kushuka baada ya tukio hili, na mama yake alianza kuwa na wasiwasi. Kisha Mary aliongea na mmoja wa walimu wake:

*Nilimwambia kisa chote cha rafiki yangu, bunduki, ukimya wa rafiki zangu, uchokozi wa wasichana, fedheha yangu, na moyo uliovunjika. Hakunicheka, au kunifanya nijihisi mdogo na mjinga. . . .*

*"Lazima uelewe," aliniambia, "kwamba unashikilia mustakabali wako mwenyewe mikononi mwako. Mustakabali wako siyo wa mtu mwingine, siyo wa wazazi wako, na haswa siyo wa yule mvulana. Ni wako na unaweza kuufanya kuwa chochote unachotaka."*

Kwenye umri wa miaka kumi na nne, Mary tayari alikuwa mwanafunzi kiongozi katika shule yake, akihamasisha amani miongoni mwa wanarika wenzake na wanafunzi vijana zaidi. Hapa zipo baadhi ya fikra ambazo zilighubika akili yake katika siku hizo:

*Tulijua kwamba kumaliza umasikini kungesaidia kumalizika kwa vita, lakini hatukuweza kufanya chochote kuhusu hilo. Tulijua kwamba upunguzaji wa ukosefu wa ajira ungesaidia, lakini hatukuweza kufanya chochote kuhusu hilo pia. Hatukuweza kuzuia risasi na mapanga. Tusingeweza kumaliza ukatili lakini tuliamini kuwa tungeanza kujenga amani miongoni mwetu wenyewe. . . .*

*Nilijua kwamba kufanya kazi kwa ajili ya amani kungeweza kuwa hatari, na niliguswa na chochote kile ambacho hakikuwa cha kawaida. Wakati fulani hofu kwamba chochote kibaya kinaweza kutokea, haswa kwa familia yangu, kilinifanya nitoe machozi na kuhisi nikimbilie mbali. Walakini watoto wengine walinitegemea, na kwa namna fulani nilihisi kuwa watoto wangu mwenyewe ambao hawajazaliwa walinitegemea pia. Sikuweza kugeukia mbali, haidhuru nilikuwa ninaogopa kiasi gani. Ningeweza kuwa makini tu na kujaribu kukaa salama.*

Ni zipi baadhi ya sifa bainifu za kipekee za Mary?

## SEHEMU YA 17

Hapa vipo visa vilivyosimuliwa na vijana wengine watatu, kila mmoja anaeleza mawazo yake bora kabisa na hisia zake mororo. Cha kwanza kimo katika maneno ya msichana mwenye umri wa miaka kumi na sita, ambaye alipokuwa na umri wa miaka kumi na mbili rafiki yake wa karibu kabisa alinaswa katika ugomvi wa genge na kuchomwa kisu hadi kufa. Hakumsahau kamwe rafiki yake na aliamua kujitoa kwenye uhamasishaji wa amani. Baadaye, alianza kuwasaidia watoto walioathiriwa na ukatili:

> *Watoto wadogo wa kama miaka nane au tisa walijiunga na magenge kwa sababu walifikiri ilikuwa poa au kwa sasababu walifikiri magenge yangewapa ulinzi mtaani. Katika hali nyingi mno walikuwa wanajaribu kuepukana na ukatili nyumbani, lakini walikuta vitu vibaya zaidi mtaani.*
>
> *Lazima nipande basi la kuelekea . . . , lakini madereva wengi wa mabasi wanajua kuhusu kazi ninayojaribu kuifanya. Hunitoza tu kile ninachoweza kulipa kwa ajili ya nauli mara nyingi hunipeleka bila malipo. Barabara ya kuelekea . . . huenda mlimani, hupita mbele ya vibanda vilivyo juu ya miteremko ya milima viking'angania kwa hatari karibu na mwinuko mkali. Vilima vina mashimo mengi pale ambapo majabali makubwa yameondolewa kwa ajili ya kutumika katika miradi ya ujenzi. Kazi kama hiyo ni ngumu, inayovunja mgongo, na isiyolipa vizuri, lakini watoto wengi kutoka familia zilizovunjika hufanya kazi kwenye maeneo haya. Familia zao zimeingia kwenye umasikini mkubwa kiasi kwamba watoto huacha shule na kufanya chochote kile wanachoweza ili wapate pesa.*
>
> *Kutoka barabarani, ninatembea katika matope yanayoteleza na yanayofunika miguu, kuvuka daraja la muda lililopo juu ya mto wenye maji machafu na yanayonuka. Shule ina nusu dazeni ya vyumba vibovu,vilivyokusanyika chini ya paa la bati. Madawati ya mbao ni machakavu na yamevunjika. Takataka zimejaa katika pembe za madarasa. Hakuna umeme. Mojawapo ya madarasa ina mwangaza unapita kwenye dirisha lililopo kwenye tundu la paa. Sakafu ni ya udongo. Mvua hupiga makelele juu ya paa la bati kiasi kwamba kila mmoja lazima apige kelele ili aweze kusikika, na maji huvuja kila mahali. Ukuta wa darasa moja umepambwa na michoro ya nyumba nzuri iliyochorwa na watoto,inayotofautiana sana na mazingira yanayo wazunguka. Pengine hizi ni taswira za makazi ambamo waliwahi kuishi zamani au yale ambayo wangependa kuwa nayo katika siku za mbele. . . .*

*Wazazi wengi wana huzuni katika nyuso zao. Huongea kwa ukali na watoto wao, wakiwaita majina mabaya. Lakini mnamo kipindi cha warsha wao wakati Fulani huanza kubadilika. Baadhi yao hufikiri kuwa ni lazima kuwapiga watoto wao ili kuwafanya wawe watiifu, lakini wao wanatambua kuwa kumpiga pia kunaweza kumfukuza mtoto mbali na kukimbilia mitaani.*

Aya inayofuata ni fikra za binti ambaye alitoroka kutoka nyumbani alipokuwa na umri wa miaka kumi na moja,na akawa ni mraibu wa madawa ya kulevya, aliokolewa kwa msaada usiokoma wa rafiki yake, na mwishowe akajiunga na harakati ya vijana waliojikita kuleta amani:

*Ilikuwa vigumu sana kueleza maisha yetu yalikuwa ya aina gani. Niliogopa kukiri kuwa haijalishi unajaribu kiasi gani kuleta amani, unaweza kuburuzwa kurudi katika ukatili. . . . Siku zote nimetamani kuondoka kwenye maisha haya. Ni vigumu kukubali lakini hivi sasa ni kweli kuwa nina ondoka tena polepole kutoka harakati ya kuleta amani. Nimekuwa nikijidanganya na kujifanya mbele ya marafiki zangu kuwa kila kitu kiko sawa. Jambo hili siyo kweli wakati mwingine ninalewa. Kila usiku kuna ugomvi nyumbani. Kama hawanifokei mimi, mama yangu na baba wa kambo wanafokeana. Siwezi kuvumilia, kwahiyo ninatoroka na kwenda mitaani, na huko yapo mengi yanayoweza kumdhuru kijana mdogo. . . . Ninatembea katika njia mbili kwa wakati mmoja na bado ninatamani ningeweza kutembea njia ya amani wakati wote. Ninafikiri kwamba kupambana kwangu na jinsi nilivyoweza kunusurika vinapaswa kuwa na thamani ya kitu fulani. . . . Ninaamini kuwa vijana wangeweza kufanya mengi zaidi ya hayo kusaidia amani kama watu wazima wangekuwa tayari kushirikiana, kusikiliza yale ambayo tumejifunza na kufanya kazi pamoja nasi. Kama tungekuwa na amani nyumbani, huo ungeweza kuwa mwanzo mzuri sana.*

Kifungu cha mwisho kinaeleza kisa cha mvulana mwenye umri wa miaka kumi na tano ambaye kaka yake alitekwa na kikundi cha wanamageuzi. Baada ya muda fulani, familia ilipokea habari kutoka kwake, na waliruhusiwa kuwasiliana naye:

*Nimemtumia mashairi, kwa ajili ya kumhamasisha kubakia kuwa mwenye ujasiri na matumaini. Ninamwambia kuwa nina sikiliza ushauri wake na nina soma kwa bidii. Nilifurahi sana alipoijibu barua yangu hivi karibuni na kusema, "nimefurahi sana kuwa unaendelea vizuri shuleni. . . . Hapo ndipo nilipokosea. Najuta kwa kutokutumia fursa ya masomo yangu ilivyonipasa. . . . Kwa kweli sikupenda kusoma, kwa mfano . . . hata hivyo hapa nimesoma zaidi ya vitabu thelathini vyote juu ya mada tofauti na bado vingalipo vingine vya kusoma. Huwa ninapata kamusi pia na kuangalia maneno ya ajabu nisiyoyajua. . . . nisingefanya hivyo mimi peke yangu hapo zamani. . . ."*

*Ingawa anaonekana salama, bado nina wasiwasi. Kama ningeweza kuongea na watu ambao wanamshikilia kaka yangu, ningewaomba wawe wenye huruma na kuelewa mateso waliyosababishia.*

*Ninafikiri kuwa msamaha ni wa kimsingi ikiwa tunataka kupata amani. Vita haiwezi kumalizika bila msamaha. Ni muhimu haswa kwa watu kama sisi ambao tumeteseka kusamehe.*

*Ninafikiri hiki ndicho ninachofanyia kazi — ninafanyia kazi msamaha.*

Jadilini katika kikundi chenu baadhi ya sifa zilizooneshwa kama mfano na vijana zilizoandikwa katika sehemu hii, na andika mawazo yenu machache.

## SEHEMU YA 18

Mwishowe, hakuna uchunguzi juu ya asili ya kipindi cha balehe, hata kama kifupi kiasi gani, unaoweza kupuuzia maisha ya Rúḥu'lláh, kijana shujaa wa Imani ambaye, katika umri wa miaka kumi na mbili, kwa furaha alikunywa kutoka kikombe cha ufia dini. Katika umri mdogo wa miaka saba, Rúḥu'lláh alipewa heshima ya kuambatana na baba yake, Mkono wa Hoja ya Mungu Varqá, na kaka yake mkubwa kwenda hija kwenye Nchi Takatifu. Rúḥu'lláh alishamiri kiroho katika mazingira hayo matakatifu na kuota katika mwangaza wa jua la uwepo wa Bahá'u'lláh. Siku moja tunaambiwa, Bahá'u'lláh alimuuliza Rúḥu'lláh, "Umefanya nini leo?"

"Nilikuwa napata masomo kutoka [kwa mwalimu fulani]" Ndilo lilikuwa jibu.

"Ulikuwa unajifunza somo gani?" Bahá'u'lláh aliuliza zaidi.

"Kuhusu 'kurudi' kwa [mitume]", Rúḥu'lláh alijibu.

"Unaweza kueleza hii ina maana gani?" aliuliza Bahá'u'lláh.

"Kwa 'kurudi' ina maanisha kurudi kwa uhalisia na sifa," alijibu.

"Hayo ni maneno halisi ya mwalimu wako," Bahá'u'lláh alihoji. "Niambie katika maneno yako mwenyewe uelewa wako wa mada."

Kwa hili Rúḥu'lláh alijibu: "Ni sawa na kuchuma ua kutoka kwenye mmea mwaka huu. Ua la mwaka ujao litakuwa sawasawa na ua hili lakini halitakuwa lile lile."

Jibu la kiakili la Rúḥu'lláh lilimfurahisha Bahá'u'lláh, Ambaye mara nyingi alimwita kwa jina la Jináb-i-Muballigh (Mheshimiwa, Mwalimu wa Kibahá'í).

Vipo visa vingine kadhaa vya kuangaza sifa bora za Rúḥu'lláh. Kwa uhakika ni kweli kwamba, ili kukwea vilele vya dhabihu alivyovifikia katika umri mdogo wa miaka kumi na mbili, bila shaka hakuwa kijana wa kawaida. Kujitoa kwake kwa Hoja na dhabihu katika njia ya Mpendwa haina haja, bila shaka, kuhusishwa na ufia dini. Hata hivyo ni kwa shauku gani

na furaha isiyo na mipaka kwamba Rúḥu'lláh anaeleza uhalisia wake katika shairi lake maarufu ambalo limenukuliwa kwa sehemu hapa chini.

> Kutoka kikombe cha fadhila tukufu nipe ninywe
> na niondolee dhambi na udhaifu;
> Kwani ingawa kwa uhakika dhambi zangu ni nyingi,
> Rehema za Bwana wangu bado ni kubwa zaidi.
>
> Nikaribishe kwako, mchukuzi wa kikombe cha dhifa tukufu!
> Njoo wewe, changamsha roho yangu na
> Nifanye niwe mstahiki wa kutolewa dhabihu
> Katika njia ya Mpendwa Kabisa.

Vijana chipukizi katika kikundi ambacho utakiandaa hivi karibuni hawataishi maisha ya Rúḥu'lláh. Hata hivyo vifungu vilivyo nukuliwa katika sehemu chache zilizopita, vinatoa dalili ya aina ya ubora ambao mwanadamu anaweza kudhihirisha kutoka umri mdogo sana. Tunakumbushwa juu ya tamko lililotolewa hapo awali katika kitengo hiki kuhusu utambuzi unaoendelea kuibuka mnamo kipindi cha balehe unaweza kuelekea kwenye mojawapo ya ncha mbili — kuelekea unyenyekevu kwa Amri ya Mungu na huduma yenye dhabihu kwa jamii ya binadamu au kuelekea utumwa katika mahabusu ya ubinafsi na ashiki. Katika majadiliano yaliyofuata juu ya sehemu kadhaa zilizofuata, tulichunguza asili ya kipindi cha balehe, uwezo wa vijana chipukizi, na athari za mazingira juu ya maisha yao. Itakuwa ya manufaa kwako kusita hapa na kuandika aya chache juu ya kile unachochukulia kuwa ni uwezo wa kuzaliwa uliomo ndani ya vijana chipukizi na kile kinachohitaji kufanyika, kama tunahitaji kukuza nguvu zao za kiroho na za kiakili.

## SEHEMU YA 19

Baada ya kuchunguza katika kitengo hiki kwa sehemu kubwa zaidi juu ya uwezo uliomo ndani ya vijana chipukizi, sasa tunaweza kusema maneno machache kuhusu ushiriki wenu katika programu ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi. Mojawapo ya shauku yenye nguvu kabisa ya wale waliomo katika rika hili ni kuwa sehemu ya kikundi cha wanarika. Vijana wanapata uhakika kugeuka kwa ajili ya ushauri kwa rafiki zao wanao waelewa na kuwahurumia. Hivyo basi, ni jibu la kawaida kwa hitaji halali, kwamba programu hii imeandaliwa kuzungukia dhana ya "kikundi cha vijana chipukizi", ambacho wajumbe wake hukutana kila mara na huongozwa kimpangilio kutenda na kujifunza. Mandhari ya mikutano, wakati ni yenye furaha, kirafiki na ukaribu, haipaswi kuwa ya mzaha. Inapaswa kuchangia, badala yake, kwenye uwezeshaji kwa zile sifa na mielekeo ambayo maisha ya huduma kwa Hoja na jamii ya wanadamu huhitaji. Katika mpangilio kama huo, wajumbe wa kikundi, wakiwa huru kutoka hofu ya kukosolewa au dhihaka, wanaweza kueleza mawazo yao na kutafuta majibu kwa maswali ya kiuchunguzi yaliyotawala katika akili zao. Wanajifunza kusikiliza, kuongea, kutafakari, kuchambua, kufanya maamuzi, na kuyatekeleza.

Katika kila kikundi, lipo hitaji kwa ajili ya mtu mkubwa zaidi ambaye, kama rafiki wa kweli kwa vijana, anaweza kuwasaidia katika kukuza uwezo wao. Wale ambao hufanya shughuli hii hujulikana kama "wahuishaji". Uwepo wa mhuishaji huwasaidia wajumbe wa kikundi kubakia wenye matumaini na wenye uhakika kwamba siyo tu wanaweza kujilinda wenyewe dhidi ya nguvu za mmomonyoko wa maadili zinazofanya kazi katika jamii inayowazunguka bali pia huchangia kwenye uboreshaji wake. Ingawa kuhudumu katika nafasi hii siyo jukumu pekee la rika lolote maalum, vijana wenye umri wa miaka kumi na saba na kuendelea huwa wahuishaji wazuri sana kwa sababu wao huona kuwa ni rahisi kuwachukulia vijana chipukizi kama wenzao, siyo kama watoto, wakiwatia moyo kuuliza maswali, kuibua dukuduku, na kujihusisha katika uchunguzi wa uhalisia. Katika teuzi lililopo hapa chini, 'Abdu'l-Bahá anaeleza matumaini Yake kwamba roho za ujana zinaweza kulelewa kwa namna hiyo:

> **"Ni matumaini ya 'Abdu'l-Bahá kwamba zile roho za ujana katika chumba cha shule cha ujuzi wa kina zaidi zitaangaliwa na yule ambaye atawafunza kupenda.**

**Tunawaombea wao wote, kupitia njia ya kiroho, kujifunza vizuri mafumbo yaliyofichika; vizuri sana kiasi kwamba katika Ufalme wa mwenye Utukufu wote, kila mmoja wao, kama shorwe aliyejaaliwa na kauli, ataimba kwa sauti kubwa siri za milki ya mbinguni, na sawa na mpenzi mwenye shauku atamimina hitaji lake kuu na hitaji lake la Mpendwa."**[32]

Kikundi cha vijana chipukizi siyo darasa la watoto. Kina baadhi ya sura za kikundi cha mafunzo, lakini kazi yake ya msingi ni kutumika kama mazingira ya msaada wa pamoja kwa wajumbe wake, ambamo wanaweza kukuza mtazamo wa kiroho na mitindo ya fikra na tabia ambayo itawaainisha katika maisha yao yote. Baada ya kushiriki katika kozi mbalimbali za Taasisi ya Ruhi, wewe unao uzoefu wa moja kwa moja kama mjumbe wa kikundi cha mafunzo na bila shaka umefundisha baadhi ya madarasa ya watoto katika kutekeleza kipengele cha mazoezi ya kozi ya tatu. Angalia katika orodha ya sifa zilizopo hapa chini. Kwa kila moja, jadili na washiriki wenzako katika kozi hii mfanano na utofauti upi unatarajia kuuona kati ya darasa la watoto, kikundi cha vijana chipukizi na kikundi cha mafunzo.

- Asili ya shughuli
- Uhusiano miongoni mwa washiriki
- Mandhari ya mikusanyiko
- Nafasi ya yule anayefanya huduma — kama ni mwalimu, mhuishaji, au mkufunzi.

## SEHEMU YA 20

Kadiri ujitoavyo kwenye eneo hili la huduma, punde tu utatambua kuwa ufaaji wa juhudi zako hutegemea, kwa kiasi kubwa, juu ya ubora wa uhusiano unaoujenga na wajumbe wa kikundi cha vijana chipukizi utakachosaidia kukiunda. Bila shaka, utakuwa tayari kuwasikiliza, kuwapa ushauri na ikibidi kuwafariji. Imani yako thabiti katika uadilifu wao, na heshima na upendo wa kweli ulionao kwa ajili ya kila mmoja wao, utawahamasisha kujitahidi kwa ajili ya ubora. Utahitaji kuonesha uthabiti wako kwa ustawi wao na maendeleo, bila hata chembe ya ubaba, ya kujigamba, au udhibiti mkali wa kimamlaka — mielekeo ambayo haiachi nafasi ya kuwaruhusu vijana chipukizi kushamiri. Utahitaji kutumia kila fursa kuimarisha msingi wa Imani ya kweli katika mioyo na akili zao na kuingiza ndani mwao matumaini katika mustakabali angavu. 'Abdu'l-Bahá hutuhimiza:

**"Kabla ya yote, muwe tayari kutoa dhabihu maisha yenu mmoja kwa ajili ya mwingine, kupendelea ustawi wa wote kuliko ustawi wako binafsi. Jenga mahusiano ambayo hakuna kinachoweza kuyatikisa; unda mkusanyiko ambao hakuna kinachoweza kuusambaratisha; uwe na akili ambayo haisiti kamwe kupata utajiri ambao hakuna kinachoweza kuuharibu. Kama upendo usingekuwepo, uhalisia gani basi ungebaki? Ni moto wa upendo wa Mungu ambao huwapa watu daraja la juu kuliko wanyama. Imarisha nguvu hii bora zaidi ambayo kupitia kwayo maendeleo yote ya ulimwengu yanaweza kupatikana."**[33]

Jadilini jinsi gani mielekeo ifuatayo ingeondoa uwezo wa wajumbe wa kikundi cha vijana chipukizi na mawazo yapi, hisia zipi, na tabia zingemsaidia mhuishaji kukataa mielekeo kama hiyo.

Ubaba: ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

Mwenye kujigamba: ______________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

Udhibiti mkali wa kimamlaka: ______________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## SEHEMU YA 21

Uhusiano wako na wajumbe wa kikundi chochote cha vijana chipukizi pia utaathiriwa kwa kiasi kikubwa na mfano utakaouweka. Ushawishi wa mfano katika maisha ya kijana hauwezi kukadiriwa kwa kiwango cha juu. Hivyo, juhudi zetu wenyewe, za kuisafisha mioyo yetu hupata maana zaidi katika uhusiano huu. "Mwambatano na malimwengu", "kujiambatanisha kwa vitu vya kiulimwengu ambavyo hufunika roho za watu", "hofu na wasiwasi ambavyo huvuruga akili zao", "starehe na ufujaji ambavyo vinajaza muda wao", "ubaguzi na chuki ambavyo hutia giza mitazamo yao, utepetevu na uchovu ambavyo hupooza vipawa vyao vya kiroho" ni "miongoni mwa vikwazo vigumu", ambavyo Mlinzi anasema, "husimama katika njia ya kila mpiganaji mtarajiwa katika huduma kwa Bahá'u'lláh". Anatukumbusha zaidi kuwa uwezo wetu wa kukataa nguvu kama hizo utategemea juu ya kiwango ambacho sisi wenyewe tumesafishika kutoka "najisi hizi," tukiwa huru kutoka "mihangaiko hii midogo midogo na wasiwasi unaokera," tukiachiliwa kutoka "ubaguzi huu na ukinzani," "tukiwa wenye utupu wa ubinafsi," na "waliojazwa na nguvu ya Mungu iponyayo na idumishayo".

Ni yapi baadhi ya matokeo ya uhamasishaji wa Mlinzi kwa juhudi zako za kuchangia kwenye uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi?

## SEHEMU YA 22

Kama rafiki wa kweli kwa vijana chipukizi pia na mshauri mwenye busara, itakuwa lazima kwako kuambatana nao katika kipindi cha furaha na kupitia vipindi vigumu. Wao daima watahitaji kutiwa moyo, kama wanatakiwa kukwea vilele vikubwa zaidi na zaidi vya ubora. Kadiri utakavyolenga juu ya mafanikio yao, kuliko juu ya mapungufu na makosa, ndivyo utakavyoweza kuwasaidia. Utawatia moyo, lakini siyo, bila shaka, katika namna ambayo itaongeza kiburi chao. Utalenga juu ya mafanikio, walakini hutaogopa kutoa ushauri kama utawaona katika hali ambazo zinaweza kuhatarisha unyoofu wa kimaadili.

Kufikiria kuhusu asili ya urafiki wako na kikundi, soma teuzi lifuatalo kutoka barua iliyoandikwa kwa niaba ya Mlinzi. Ingawa inaelezea uhusiano wa asasi za Imani kwa mtu binafsi, ina uwiano na jitihada zako kama mhuishaji wa kikundi cha vijana chipukizi:

> **"Waumini, kwa sehemu kubwa, ni wachanga katika Hoja, na kama wao wakifanya makosa, hilo halifikii hata nusu kwa umuhimu, ukilinganisha na kama roho zao zimevunjwa kwa kuambiwa kila mara — fanya hiki usifanye kile!"[34]**

Jadilini kwa nini roho ya kijana inaweza kuvunjika kwa kukumbushwa mara kwa mara makosa yake na kuaambiwa kila mara fanya hiki usifanye kile. Andika baadhi ya mawazo yako hapa chini.

Utiaji moyo siyo sawa na kusifiwa kiholela; ni lazima uwe wa kweli na huru kutoka unafiki, vinginevyo utapelekea ama kwenye majivuno au ukosefu wa uaminifu. Hapa chini

kuna baadhi ya mifano ya jinsi gani 'Abdu'l-Bahá aliwatia moyo waumini katika juhudi zao za kuhudumia Hoja.

**"Kwa kweli Ninamtukuza Mungu kwa kuwa Yeye amekuthibitisha katika huduma ya Hoja ya Mungu katika shamba Lake kuu la mizabibu."[35]**

**"Kwa kweli Ninamtukuza Bwana wangu Mkuu kabisa kwa kukuchagua kutaja Jina Lake miongoni mwa watu, kwa ajili ya kukuvutia kwenye uzuri wa Mtukufu kabisa na kukuimarisha katika kuipatia Hoja Yake ushindi."[36]**

**"Kwakweli, Mungu amekusafisha kutoka dhambi, alipokuzamisha katika bahari ya rehema Yake na kukufanya unywe kikombe cha Imani na mvinyo safi wa utambuzi. Umefanya vizuri sana! Umefanya vizuri sana! kwa sababu umetamani kuyafifisha matakwa yako kwa ajili ya matakwa ya Mungu, umetafuta upendo wa Mungu, ukuzaji wa ujuzi wako wa Yeye, na kubaki imara kwenye njia Yake."[37]**

**"Enyi wapendwa wangu wa kiroho! Sifa ziwe kwa Mungu! Ninyi mmesukuma kando tando na kumtambua mpendwa mwenye huruma, na mmeharakia mbali kutoka makazi haya na kwenda kwa milki isiyo kuwa na mahali. Mmesimika mahema yenu katika ulimwengu wa Mungu, na kumtukuza Yeye Aliyepo Mwenyewe, mmepaza sauti zenu tamu na kuimba nyimbo zilizopenya mioyo. Mmefanya vizuri sana! Mmefanya vizuri sana mara elfu moja! Kwa kuwa ninyi mmeutazama mwangaza uliodhihirishwa, na katika uwepo wenu uliozaliwa upya mmepaza sauti, 'abarikiwe Bwana, Aliye bora wa waumbaji wote!'"[38]**

**"Enyi waaminifu, wenye shauku, mnaovutwa kama kwa sumaku, ninyi ambao mmeinuka kuihudumia Hoja ya Mungu, kutukuza Neno Lake na kusambaza manukato Yake matamu mbali kwa marefu na kwa mapana! Nimesoma barua yenu bora kabisa, nzuri kwa mtindo, yenye ufasaha wa maneno, yenye kina cha maana, na ninamtukuza Mungu na kumshukuru kwa ajili ya kuwasaidia na kuwawezesha kumtumikia Yeye katika shamba Lake la mizabibu lililoenea kwa mapana."[39]**

**"Barua yako ilikuwa kama shada la maua yenye kunukia likipukutisha ng'ambo manukato ya Imani na yakini. Umefanya vizuri sana! Umefanya vizuri sana! Wewe umegeuzia sura yako kwenye Ufalme usioonekana. Vizuri sana! Vizuri sana! kwamba wewe unavutiwa kwenye Uzuri wa Mweza! Ajabu! Ajabu! Bahati ilioje kwamba wewe umefika kwenye fadhila hii kuu Kabisa!"[40]**

Mkiwa mliohamasika na namna ambavyo 'Abdu'l-Bahá aliwasifia marafiki, elezeni katika sentensi chache jinsi gani utakavyokuwa unawatia moyo wajumbe wa kikundi utakachokuwa unakisaidia hivi punde.

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

## SEHEMU YA 23

Hatimaye, unahitaji kukumbuka kwamba juhudi zako za kusitawisha mafundo ya kina ya urafiki wenye upendo na wajumbe wa kikundi cha vijana chipukizi na kuwatia moyo kujitahidi kuwa bora zaidi zitazaa matunda ya kiwango kikubwa kiasi kwamba utajenga mazingira yenye furaha.

> **"Furaha hutupa mabawa! Katika nyakati za furaha uimara wetu huwa wenye uwezo, akili zetu makini zaidi, na uelewa wetu ambao haukufunikwa. Tunaonekana wenye uwezo zaidi wa kukabiliana na ulimwengu na kupata nafasi yetu ya ufaaji."[41]**

Kwa minajili ya kujenga mazingira yenye furaha kwa ajili ya kikundi, mnahitaji kuhisi furaha. Fikiria juu ya kikundi cha vijana chipukizi ambao utakuwa unafanya nao kazi hivi punde. Mawazo yapi yanakuja akilini mwako kuwahusu wao ambayo yanakuletea furaha?

Ni zipi baadhi ya hatua za kivitendo unazoweza kuchukua ili kuijaza kwa furaha mikutano ya kikundi hicho, bila kuifanya kuwa ya kipuuzi?

Pamoja na mawazo haya akilini hebu soma kifungu kilichopo hapa chini kutoka barua iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu:

**“Furaha ya ndani ambayo kila mtu binafsi huitafuta, tofauti na mhemko wa kupita, haitegemei ushawishi wa nje; ni hali, inayozaliwa kutokana na yakini na ujuzi wenye utambuzi, ikiendelezwa na moyo safi, ambao unaweza kutofautisha kati ya kile ambacho ni cha kudumu na kile ambacho ni cha juu juu.”**[42]

Hebu tuhitimishe usomaji wa kitengo chetu kwa kutafakari juu ya maneno yafuatayo ya ‘Abdu’l-Bahá:

**“Zawadi kuu kabisa ya mwanadamu ni upendo wa wote — ile sumaku ambayo huyafanya maisha yawe ya milele. Huvutia uhalisia na hutawanya katika maisha furaha isiyo na kikomo. Kama upendo huu utapenya ndani ya moyo wa mtu, nguvu zote za ulimwengu zitatambulika ndani yake, kwa kuwa ni uwezo mtakatifu ambao humsafirisha hadi kwenye daraja takatifu na hataweza kuendelea mpaka pale atakapo angaziwa nazo. Jitahidi kuongeza nguvu ya upendo wa uhalisia, kuifanya mioyo yenu iwe vitovu vikubwa zaidi vya mvuto na kujenga mawazo mapya na mahusiano.”**[43]

## MAREJEO


1. Kutoka Riḍván 2010 ujumbe ulioandikwa kwa Wabahá'í wa ulimwengu, uliochapishwa katika *Muundo wa utendaji: jumbe zilizochaguliwa kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na nyenzo za ziada, 2006–2016* (West Palm Beach: Palabra Publications, 2017), na. 14.16, uk. 82.

2. Kutoka hotuba iliyotolewa tarehe 17 Novemba 1912, iliyochapishwa kwenye *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu: Hotuba zilizotolewa na 'Abdu'l-Bahá mnamo kipindi cha Ziara Yake Amerika na Canada katika 1912* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2012), aya. 3, uk. 617.

3. *Mateuzi kutoka maandiko ya 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2010, 2015 kuchapisha), na. 111.7, uk. 192.

4. *'Abdu'l-Bahá juu ya Falsafa Tukufu* (Boston: The Tudor Press, 1918), ku. 131–32.

5. *Mikusanyo kutoka maandiko ya Bahá'u'lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1983, 2017 kuchapisha), CLIII, aya. 6, uk. 370.

6 Kama hapo juu., na. 1, aya. 5, uk. 3.

7. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1988, 2005 kuchapisha), na. 4.7, ku. 34–35.

8. Bahá'u'lláh, *Maneno Yaliyofichwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2003, 2012 kuchapisha), Kiarabu na. 13, ku. 6–7.

9. *Mateuzi kutoka maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 34.2, uk. 100.

10. Kama hapo juu., na. 35.7, uk. 104.

11. *Nyaraka za 'Abdu'l-Bahá Abbas* (New York: Kamati ya Uchapishaji ya Kibahá'í, 1909, 1930 kuchapisha), juz. 1, uk. 136.

12. 'Abdu'l-Bahá, *Siri za Ustaarabu Mtakatifu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2007, 2017 kuchapisha), aya. 186, uk. 136.

13. *Mateuzi kutoka maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 68.3, ku. 147–48.

14. Kama hapo juu., no. 155, uk. 253.

15. Kutoka hotuba iliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá tarehe 26 Mei 1912, iliyochapishwa kwenye *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 3, uk. 205.

16. Kutoka hotuba iliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá tarehe 11 Juni 1912, kama hapo juu., aya. 4, uk. 258.

17. 'Abdu'l-Bahá, *katika Maandiko Bahá'í*: *Mateuzi kutoka Kauli za Bahá'u'lláh na 'Abdu'l-Bahá* (New York: Kamati ya Uchapishaji ya Kibahá'í, 1928), na. 992, uk. 548.

18. Kutoka hotuba iliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá tarehe 11 Juni 1912, iliyochapishwa kwenye *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 6, uk. 261.

19. *Wito wa Mpendwa Mtakatifu: Kazi za Mafumbo Zilizochaguliwa za Bahá’u’lláh* (Haifa: Makao Makuu ya Ulimwengu ya Kibahá’í, 2018), na. 2.22, uk. 21.

20. Kutoka hotuba iliyotolewa tarehe 28 Oktoba 1911, iliyochapishwa kwenye *Mazungumzo ya Paris: hotuba zilizotolewa na ‘Abdu’l-Bahá mwaka 1911* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2006, 2016 kuchapisha), na. 15.12, uk. 53.

21. *Mateuzi kutoka maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá*, na. 36.5, uk. 111.

22. *Wito wa Mpendwa Mtakatifu*, na. 2.19, uk. 19.

23. *Mateuzi kutoka maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá*, na. 195.5, uk. 327.

24. Bahá’u’lláh, kwenye *Kitáb-i-Aqdas*: *Kitabu Kitakatifu Kabisa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1993, 2013 kuchapisha), aya. 64, ku. 42–43.

25. *Mateuzi kutoka maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá*, na. 223.1, ku. 388–89.

26. Kama hapo juu., na. 35.4, uk. 102.

27. Kama hapo juu., na. 206.9, uk. 354.

28. *Sala na Tafakari za Bahá’u’lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1987, 2008 kuchapisha), XXXVI, aya. 4, uk. 47.

29. Kama hapo juu., CLXXXIV, aya. 2, uk. 324.

30. Kutoka barua ya tarehe 23 Novemba 1983 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa mtu binafsi, iliyochapishwa kwenye *Miangaza ya Uongozi* (New Delhi: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1988, 2010 kuchapisha), na. 1206, ku. 359–60.

31. Kutoka barua ya tarehe 8 Disemba 1935 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa mtu binafsi, iliyochapishwa kwenye *Sala na Maisha ya Kiibada: Makusanyo ya Dondoo kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh, Báb, na ‘Abdu’l-Bahá na Barua za Shoghi Effendi na za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu*, zilizokusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2019), na. 71, uk. 30.

32. *Mateuzi kutoka maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá*, na. 107.1, uk. 188.

33. *‘Abdu’l-Bahá juu ya Falsafa Takatifu*, uk. 112.

34. Kutoka barua ya tarehe 30 Juni 1957, iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa Baraza la Kiroho la Kitaifa, kwenye “Baraza la Kiroho la Kitaifa”, iliyochapishwa kwenye *Makusanyo ya Makusanyo* (Maryborough: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í Australia, 1991), juz. 2, na. 1502, uk. 128.

35. *Nyaraka za 'Abdu'l-Bahá Abbas*, juz. 1, uk. 11.

36. Kama hapo juu., uk. 18.

37. *Nyaraka za 'Abdu'l-Bahá Abbas* (New York: Kamati ya Uchapishaji ya Kibahá'í, 1915, 1940 kuchapisha), juz. 2, ku. 266–67.

38. *Mateuzi kutoka maandiko ya 'Abdu'l-Bahá*, na. 236.4, uk. 439.

39. Kama hapo juu., na. 199.1, ku. 332–33.

40. *Nyaraka za 'Abdu'l-Bahá Abbas* (New York: Kamati ya Uchapishaji ya Kibahá'í, 1916, 1930 kuchapisha), juz. 3, uk. 530.

41. Kutoka hotuba iliyotolewa na y 'Abdu'l-Baha tarehe 22 Novemba 1911, iliyochapishwa kwenye *Mazungumzo ya Paris*, na. 35.2, uk. 135.

42. Kutoka barua ya tarehe 19 Aprili 2013 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa kundi dogo la watu binafsi, iliyochapishwa kwenye *Muundo wa Utendaji*, na. 51.7, uk. 292.

43. *'Abdu'l-Bahá juu ya Falsafa Takatifu*, ku. 111–12.



# Kuhudumia kama Mhuishaji

## Kusudi

Kutafakari juu ya dhana ambazo hubumba
programu kwa ajili ya uwezeshwaji
wa kiroho wa vijana chipukizi

## SEHEMU YA 1

Katika kitengo cha pili cha kitabu hiki tulijadili umuhimu wa mazingira ya kijamii katika maisha ya kijana katika kipindi cha mwanzoni cha balehe. Programu ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi kufuatana na hilo, imeandaliwa kuzunguka dhana ya "kikundi cha vijana chipukizi". Kikundi cha vijana chipukizi, tumesema,sio darasa la watoto. Kina baadhi ya sura za kikundi cha mafunzo, lakini kazi yake ya msingi ni kutumika kama mazingira ya msaada wa pamoja kwa wajumbe wake, yale ambamo wanaweza kukuza mtazamo wa kiroho na mitindo ya fikra na tabia ambayo itawainisha katika maisha yao yote.

Kikundi cha vijana chipukizi hukutana mara kwa mara, angalau mara moja kwa juma, na hushiriki kambi kadhaa kila mwaka katika kipindi cha miaka mitatu. Katika muda ambao wajumbe huutumia pamoja kama kikundi wao hujifunza nyenzo zilizoandaliwa maalumu kwa ajili ya rika la umri kati ya miaka kumi na mbili na kumi na tano. Vijana pia hushauriana kupanga na kufanya miradi ya huduma katika jumuiya, hushiriki katika michezo, na hujihusisha katika shughuli za kitamaduni, kama vile maigizo na stadi za mikono, zinazoendana na mazingira yao ya karibu. Katika makambi ambayo hufanyika siku kadhaa kila mmoja wao hufanya masomo shadidi kama kikundi na huhudhuria matukio maalumu ya ujumla na shughuli pamoja na vikundi vingine kutoka katika ujirani au kijiji chao wanaopitia program hii. Katika kitengo hiki, tutachunguza Nyanja mbalimbali za programu ya uwezeshaji wa kiroho ambazo unapaswa kuzifahamu vizuri.

## SEHEMU YA 2

Hebu kwanza tufikirie uwanachama wa kikundi. Pale ambapo vijana chipukizi wa jumuiya fulani waoneshapo shauku kwa programu, kwa kawaida iwezekana kuunda kikundi cha wajumbe kumi hadi kumi na tano. Wakati umri wa wengi utakuwa kati kumi na mbili na kumi na tatu, baadhi ya vijana wanaweza kuwa chini kidogo ya kumi na mbili na wengine wenye kumi na nne. Uzoefu unapendekeza kuwa programu hii inakuwa yenye manufaa kabisa pale ambapo wajumbe wake bila kujali umri wao wanabakia pamoja kwa kipindi chote cha miaka mitatu na wanahitimu kama kikundi. Kufikia hatua hiyo, wale wanaopenda wanaweza kuendelea pamoja katika hatua inayofuata ya mchakato wa kielimu wakijifunza mlolongo mkuu wa kozi za taasisi wakifuata njia ya huduma uifunguayo kwao.

Katika baadhi ya sehemu vijana ambao hujiunga na kikundi watakuwa wameisha shiriki katika madarasa ya watoto ya Kibahá'í, lakini inapaswa ikumbukwe kuwa, katika hali nyingi, vijana wanaokutana na programu hii watakuwa hawajawahi kukutana na Imani hapo mapema. Hivyo, mbali na utofauti wa umri, mara nyingi kutakuwa na baadhi ya tofauti katika usuli na uzoefu. Kamwe hakuna kikundi kinachoweza kufanana kwa kila kitu, na wahuishaji mara kwa mara hukabiliana na changamoto ya kuitikia kwenye shauku mbalimbali za vijana. Kiasi kikubwa cha unyumbulifu na ubunifu kinahitajika katika muktadha huu, na utahitaji kujiandaa kushughulikia changamoto hii kila wakati mnapokusanyika pamoja na kikundi. Ungekabilianaje, kwa mfano, na hali zifuatazo?

- Baadhi ya wajumbe wa kikundi cha vijana chipukizi unachokisaidia wanapata ugumu katika ufahamu wao wa kusoma.

- Wajumbe wadogo zaidi wa kikundi hujihisi kuwa wamedhalilishwa unapojaribu kufanya kazi nao kwa kuwatenganisha.

- Mjumbe mmoja au wawili wakubwa zaidi hawaoni kuwa shughuli fulani za kikundi zina changamoto ya kutosha.

- Baadhi ya wajumbe wa kikundi wanakataa kushiriki katika shughuli fulani.

- Wajumbe wachache wa kikundi huonesha uwezo wa kupitia nyenzo kwa kasi kubwa zaidi kuliko wengine.

- Wasichana na wavulana katika kikundi wagoma kushiriki katika shughuli fulani pamoja.

- Wajumbe kadhaa hawana pesa za kutosha kwa ajili ya kuchangia, tuseme, kwa ajili yakutumia kwenye mtoko wa kikundi.

- Mjumbe mmoja au wawili mahudhurio yao siyo ya mara kwa mara.

- Mjumbe mmoja anaanzisha utani usiostahili wakati wa mikutano.

- Wajumbe wachache wa kikundi huwaleta wadogo zao kwenye mkutano.

- Mjumbe mmoja au wawili hawashiriki katika majadiliano ya kikundi.

Jadilini katika kikundi chenu hali hizi na nyingine kama hizi. Bila shaka, kadri unavyopata uzoefu katika eneo hili la huduma, utaweza kuchunguza changamoto hizo katika mikutano ya tafakari ya vipindi pamoja na wahuishaji wenzako na kupata umaizi mpya.

## SEHEMU YA 3

Vitabu ambavyo usomaji wake upo kwenye moyo wa programu — ambavyo baadhi yao pengine umeshavisoma, kwa kufuata mapendekezo ya kufanya hivyo katika Kitabu cha 2 — vimepangwa katikampangilio unaoweza kubadilika kwa kiwango cha ugumu, kufuatana na vyote viwili, kulingana na lugha na dhana zinazochunguzwa. Vimegawanywa katika makundi mawili.Vile vilivyo katika kundi la kwanza huwasilisha mada kutoka mtazamo wa Kibahá'í, lakini siyo katika mtindo wa maagizo ya kidini. Katika maana hii vinaweza kuitwa vyenye "mwelekeo wa Kibahá'í". Vinaunda sehemu kubwa ya programu. Kundi lingine hujumuisha vitabu, vichache zaidi kiidadi ambavyo hutoa kwa udhahiri kipengele cha Kibahá'í. Tutachunguza kipengele hicho katika Sehemu inayofuata na hapa tutamakinikia juu ya asili ya vitabu vyenye mwelekeo wa Kibahá'i.

Kwa kawaida nyenzo za kielimu za aina hii zimetengenezwa kwa imani kwamba, katika bahari kuu ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh, kuna lulu za busara zisizohesabika ambazo zinapaswa kutolewa kwa watu wenye shauku, hata pale ambapo bado hawajatambua Daraja Lake. Tayari unaifahamu dhana hii kama ambavyo, katika kitengo cha pili cha Kitabu cha 2, "Mazungumzo Yainuayo",ulisoma vifungu vinavyotokana na hotuba na Nyaraka za 'Abdu'l-Bahá kwa ajili ya kukuza uwezo wa kuhusisha ujuzi wa kiroho na umaizi uliopatikana katika mazungumzo yako ya kila siku.

Kama unavyojua kutoka uzoefu wako mwenyewe, katika kujadiliana pamoja na wengine dhima zilizochunguzwa katika kitengo hicho, unaweza katika mazingira fulan kutaja chanzo cha hamasa yako katika njia ya kiasilia, ingawa wakati mwingine, unaweza kufiri ni bora kutokufanya hivyo — hili, kulingana na mahitaji ya kila hali. Kanuni hiyohiyo hutumiwa katika suala la nyenzo zenye mwelekeo wa Kibahá'í. Barua iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu inasisitiza katika uhusiano huu:

> **"Mojawapo ya kanuni za msingi inayotawala maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Kibahá'i ni kwamba marafiki sharti wayatoe Mafundisho ya Bahá'u'lláh kwa uhuru na bila masharti kwa jamii ya wanadamu, ili kwamba watu kila mahali waweza kuyatumia katika masuala muhimu na kuboresha maisha yao ya mtu binafsi na kwa ujumla, katika nyanja zote za kimwili na za kiroho. Ufikiaji kwa Neno la Mungu haupaswi kuwekewa juu ya masharti ya kumkubali Bahá'u'lláh kama Mdhihirishaji wa Mungu kwa siku leo. Aidha, lisingekuwa jambo lisilofaa kujizuia kutaja kwa uwazi Chanzo cha hamasa iliopo kwenye msingi wa programu ya kielimu inayokuzwa juu ya msingi wa Mafundisho Yake pale hali inapodai. Katika muangazaa huu, zipo chaguzi nyingi, ambazo marafiki wangeweza kuzifikiria wanapotengeneza nyenzo za kielimu ambazo zinachota kutoka kwenye mafundisho na kanuni za Imani."**[1]

Na barua nyingine iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki unasema:

> **"Tumeombwa kuwajulisheni kwamba hakuna hitaji la kumtaja mwandishi unapotumia teuzi kutoka maandiko ya Kibahá'í katika nyenzo za mitaala yenye mwelekeo wa Kibahá'í pale ambapo busara ya kutokufanya hivyo inapoibuka."**[2]

Hivyo, wakati nyenzo zote zenye mwelekeo wa Kibahá'í huzalishwa chini ya ushawishi wa moja kwa moja wa Ufunuo wa Bahá'u'lláh, asili ya kila seti ya nyenzo na matumizi yake yaliyokusudiwa huamua ni kwa kiasi gani Imani inaweza kutajwa wazi wazi.

Katika baadhi, ni sawa kabisa kujumuisha vifungu kutoka maandiko matakatifu. Katika vingine, mafundisho ya Kibahá'í yanaweza kuelezwa bila mateuzi yoyote. Katika hali yoyote, marejeo kwenye vyanzo vya asili yanaweza kujumuishwa au kutokujumuishwa. Hata hivyo, ni muhimu kutambua, kwamba hata katika hali ambamo Imani haikutajwa waziwazi, muktadha wa uzoefu wa ufundishaji — ujifunzaji huweka wazi kwamba nyenzo hizi kwa uhakika zimehamasishwa na Ufunuo wa Bahá'u'lláh.

Nyenzo zenye mwelekeo wa Kibahá'í tunazofikria hapa huchota kwa kiasi kikubwa kutoka kwenye nguvu ya Neno la Mungu, kwa vyote viwili, kwa kunukuu moja kwa moja kutoka maandiko na kwa kufuma mafundisho ya Imani katika uwasilishaji wa dhima za kiakili, kimaadili, na kiroho. Vitabu vyenyewe havitoi marejeo, na kwa kawaida imeachwa kwa mhuishaji kuamua, kufuatana na hali ya kikundi na mielekeo, na shauku zake, kama anatakiwa kutaja vyanzo vya mateuzi na kama inafaa, wafanye hivyo wakati gani. Hapa chini ipo dondoo kutoka somo la *Pepo Nyanana za Uthibitisho*, kwa kawaida ni kitabu cha kwanza kinachosomwa na vikundi vya vijana chipukizi. Isome na jadilini maswali yanayofuata.

Godwin ana rafiki yake wa karibu anayesoma naye darasa moja ambaye jina lake ni Chishimba. Yeye mara kwa mara huwatembelea wakina Mulenga, na usiku wa leo anashiriki nao chakula cha jioni. Mazungumzo mezani yanahama kutoka somo moja hadi lingine. Musonda anataka kuleta somo la uthibitisho, na anakosa subira. Hatinaye, kuna dakika chache za ukimya. "Rose na mimi tumekuwa tukiongelea juu ya uthibitisho," anasema Musonda.

"Ameshaanza huyo dada yangu mdogo!" anasema Godwin, akisafisha koo lake. Lakini alishangazwa, Chishimba alionekana kuvutiwa.

"Neno hilo humaanisha nini kwako?" humuuliza Musonda.

Musonda pia alishangazwa, alimwangalia Rose, akitumaini kuwa atakuwa na jibu.

"Uthibitisho . . . Mungu hututhibitisha na hutusaidia katika yale tufanyayo," anasema Rose.

Chishimba hasemi kitu chochote kwa kitambo. Kuna huzuni machoni mwake. "Miezi michache iliyopita," yeye alianza kusema taratibu, "baba yangu alipoteza kazi yake. Yeye ni mwaminifu na mwajibikaji, na kila mmoja analijua hili. Kwa miaka kumi na nane amefanya kazi kama mlinzi katika kampuni, na ghafla bila kutegemea, walimfukuza. Sisi sote tunaijua sababu. Kama angeendelea kwa miaka miwili zaidi, angestaafu na kampuni ingetakiwa kumlipa mafao. Hatuna akiba kubwa ya fedha. Ingawa kaka yangu mkubwa anatusaidia, inaonekana kuwa sitaweza kurudi shuleni mwakani kwa sababu siwezi kulipia chumba changu na bweni. Napenda sana shule. Nashangaa kwanini Mungu hanisaidii."

Kila mmoja anaangalia upande wa Bwana Mulenga, wakimtegemea kujibu swali hili.

Bwana Mulenga anatabasamu na kusema, “Vile Mungu hututhibitisha tunapofanya jitihada haimaanishi kuwa maisha ni rahisi. Maisha yenu yatajaa shida, na hatima mbaya, nyingi zao zitasababishwa na ukosefu wa haki. Lakini mtahitaji kushughulika kwa bidii, na hata kama kwa muda mambo yanaweza yasiwe vile ninyi mngetamani yawe, muwe na uhakika wa uthibitisho wa Mungu. Atawathibitisha hasa katika jitihada yenu ya kuondokana na dhuluma.” Anamgeukia Chishimba na anasema, “Familia yenu imeungana na ni yenye bidii. Moyo wangu unaniambia kuwa mambo yatakubadilikia. Utamaliza masomo yako. Amini maneno yangu katika hili.”

Katika Sehemu ya 20 na 21 tutaangalia *Pepo Nyanana za Uthibitisho* kwa kina zaidi, lakini kwa sasa pengine mngependa kujadiliana maswali yafuatayo katika kikundi chenu:

1. Ni dhana kuu ipi ya kiroho inayongelewa katika maongezi ya hapo juu?

2. Je, dhana imewasilishwa katika njia inayoweza kueleweka na vijana chipukizi?

3. Katika kitengo cha pili cha kitabu hiki tulifikiria kuhusu hatari ya kuweka mkazo mkubwa juu ya “nafsi”. Ni kwa jinsi gani mchakato wa kielimu ambao unatilia mkazo umuhimu wa kufanya jitihada na kuvutia uthibitisho wa Mungu ni tofauti kutoka ule ulioandaliwa kuzungukia dhana za kujitambua, kujigundua, na kujithamini kamazilivyoelezwa katika kitengo hicho?

4. Je, vijana chipukizi wote, bila kujali usuli wao, ukijumuisha wale kutoka familia za Kibahá’í, hufaidi kutoka usomaji wa aina ya nyenzo zenye mwelekeo wa Kibahá’í zinazofikiriwa hapa? Kwa nini?

## SEHEMU YA 4

Vitabu katika kundi la pili hutoa maudhui kwa ajili ya mwendelezo wa elimu ya kiroho iliyopatikana katika madarasa ya watoto ya Kibahá’í. Viko wazi katika namna vinavyoelezea itikadi za kimsingi za Kibahá’í na kujadili namna ambamo itikadi hizi zinapaswa kutafsiriwa katika utendaji kwenye muktadha wa maisha ya jumuiya. Daraja la Bahá’u’lláh kama Mdhihirishaji wa Mungu kwa zama hizi, imani kamili katika utambuzi wa msingi wa kusudi Lake kwa jamii ya wanadamu, uhakika wa uhuru pasi na kikomo na furaha tunayoipata kupitia utiifu kwa sheria Zake, na yakini katika uwezo wa Agano Lake — haya ni miongoni mwa mathibitisho ambayo hujulisha jinsi mada zinavyotumika kwenye vitabu.

Katika kufikiria kuhusu kundi hili la nyenzo, utaona kifungu kifuatacho kilichoandikwa kwa niaba ya Mlinzi kuwa chenye manufaa:

> **“. . . hatari zinazowakabili vijana wa sasa zinaendelea kuwa mbaya zaidi na zaidi, na zinaitisha suluhisho la haraka. Lakini, kama ambavyo uzoefu huonesha waziwazi, tiba ya hali hii ya kusikitisha na yenye kukanganya haipatikani katika dini za kitamaduni na kikasisi. Mifumo ya kikanisa imeondolewa kabisa. Kile kinachoweza kuudhibiti ujana na kuuokoa kutoka mitego isiyojali ya masuala ya kimwili ya zama hii ni nguvu ya Imani ya kweli, inayo jenga na iliyo hai kama ile iliyofunuliwa kwa ulimwengu na Bahá’u’lláh. Dini, kama ilivyo kuwa katika siku zilizopita, bado ni tumaini la pekee la ulimwengu, lakini siyo aina ile ya dini ambayo makasisi wanajitahidi bure kuhubiri. Yakiwa yametengwa kutoka dini ya kweli, maadili hupoteza ufanisi wake na hukoma kuongoza na kuthibiti maisha ya mtu binafsi na ya kijamii. Lakini pale ambapo dini ya kweli inapounganika pamoja na kanuni za kweli, ndipo maendeleo ya maadili yanakuwa uwezekano na siyo wazo tu.”[3]**

Kifungu kilichopo hapo juu huweka wazi kuwa, kinyume na ushawishi unaoendelea kupungua wa dini ya kitamaduni, nguvu ya Imani hai inaweza kuwalinda vijana kutoka “mitego isiyojali ya masuala ya kimwili” iliyotapakaa mno katika jamii ya leo. Nguvu hii inapaswa kuakisiwa katika vyote viwili, maudhui ya kile kinachosomwa na vijana na katika namna ambavyo wanasaidiwa katika kukuza uwezo wao wa kiroho. Kwa minajili ya kufikiria mawazo haya zaidi, hebu tuangalie dondoo kutoka *Roho ya Imani* — mojawapo ya vitabu katika kundi hili linalochunguzwa hapa.

*Roho ya Imani* hushughulika na mada za kifalsafa kiasili, kwa kuwa vijana waliomo katika rika hili bila shaka hupambana na maswali ya kimsingi ya uwepo, maswali ambayo lazima yajibiwe ipaswavyo kama mkanganyiko na hata upotezaji wa Imani vinatakiwa kuepukwa baadaye maishani. Ni katika mafundisho ya Kibahá’í ambamo majibu yanatakiwa kupatikana kwa maswali mengi yanayotatiza ambayo huchanganya akili ya mtu: asili ya kweli ya mwanadamu, mema na maovu, hiari na hatima, ukuaji endelevu na utokeaji wa roho ya mtu, akili yenye kufikiri ya mwanadamu, na roho ya Imani. Kitabu huchota kutoka umaizi uliokusanywa kutoka Maandiko, hususani kutoka maelezo yanayopenya ya ‘Abdu’l- Bahá katika *Baadhi ya Maswali Yaliyojibiwa*, kwa minajili ya kutoa mwanga juu ya mada hizi. Hukuza kila mada kupitia mazungumzo ya kikundi cha vijana chipukizi katika wakati wa mikutano yao ya kila juma na baadaye pale wanapokutana mwisho wa juma pamoja katika kambi. Sehemu ifuatayo imechukuliwa kutoka somo ambamo vijana wanajadili suala la hatima pamoja na mhuishaji wa kikundi chao, Natalia Petrovna:

> “Hebu tuangalie kile tulichoelewa hadi sasa.” Natalia Petrovna anasema. “Tuna ari uhuru au hiari ya kuamua kufanya mazuri au mabaya na sisi tunatumia utashi wetu kuendesha maisha bora. Lakini kuwa na hiari haimaanishi tunaweza kuchunga kila kitu. Yapo mambo yatakayojitokeza ambayo juu yake hatuna uwezo wowote. Sasa ninataka kuwauliza wazo lingine. Mnaelewa nini mkisikia neno, ‘hatima’?”

“Ninafikiri hatima ni kitu ambacho hatuwezi kukibadilisha katika maisha yetu, kwa vyovyote vile,” Igor hujiibu.

“Hiyo ni sawa. Yupo yeyote anayeweza kutoa mifano michache?” Natalia anauliza.

“Hatuchagui wazazi wetu,” Nadya anasema.

“Hatuwezi kuchagua mahali tunapozaliwa.” Anton anaongeza.

“Wazazi wangu huniambia mara kwa mara kuwa ni hatima yangu kuwa mcheza piano mahiri,” Vadik anasema.

“Lakini sio lazima ufanye hivyo, unaweza kuchagua kuwa kitu kingine,” Marina alisema.

“Hilo ni sawa. Hatima siyo rahisi hivyo,” Natalia anasema. “Upo mfano mzuri ambao hueleza jinsi hatma ifanyavyo kazi. Kuna yeyote kati yenu amewahi kuona jinsi zulia linavyofumwa?”

Kila mmoja anaonesha sura ya mshangao, kwa hiyo Natalia anaendelea kueleza: “Haya basi, kwanza kuna fremu. Juu ya fremu, au kitanda cha mfumi, hii nyuzi hupangwa sambamba kutoka juu kwenda chini na kukazwa vizuri. Mfumaji hutumia nyuzi za aina mbalimbali zenye rangi tofauti kufuma kupitia nyuzi hizi na kuunda bombwe. Muumini mmoja wa mwanzoni alimsikia ‘Abdu’l-Bahá akisema kuwa sisi sote ni kama wafumaji. Tumepewa fremu na nyuzi zikiwa zimewekwa juu yake. Pia tumepewa nyuzi zinazohitajika kwa ajili ya kufuma, ambazo unaweza kusema ni vipaji na uwezo wote ambao tumezaliwa nao. Hii ndio hatma yetu. Lakini sisi ndiyo tunachagua mtindo tutakaoufuma kwenye kitanda cha mfumi. Tunao uhuru juu ya vitendo vyetu. Kila tendo huunda sehemu ndogo ya bombwe. Kazi iliyokamilika ni jinsi tukuwavyo kuwa. Kupitia hiari na ridhaa, tunakuza uwezo na vipaji tulivyopewa na Mungu.”

---

**Tafakari**:

Mungu ametupatia wote vipaji na uwezo fulani. Mtu mmoja anaweza kuwa mahiri katika baiolojia, wakati mtu mwingine anaweza kuwa na kipaji cha muziki. Lakini wote tumepewa kile ambacho tunahitaji ili kuendelea kama viumbe bora. Siyo sahihi, kwahiyo, kulaumu hatima kwaajili ya mapungufu yetu. Tunapofanya hivyo, tunaacha kufanya jitihada za kujiboresha. Katika kila

hali iliyoandikwa hapo chini, chagua wazo liwezalo kumsaidia mtu kubadilisha hali yake:

a. Mtu huugua mara kwa mara kwa sababu hula chakula kisicho salama. Yeye hufikiri:

______Ni hatima yangu kuwa mnyonge na dhaifu.

______Inanibidi kuacha kuweka visingizio na kubadilisha tabia zangu za kula.

b. Mtu fulani hasomi, kwa hiyo anashindwa mtihani. Yeye hufikiri:

______Mimi siyo mwanafunzi bora, lakini kwa bidii ninaweza kufanya vizuri zaidi.

______Siyo hatima yangu kufaulu shuleni.

c. Mtu fulani anakunywa pombe kila wakati anapokumbana na matatizo. Akiwa hajalewa hufikiri:

______ Maisha hunilazimisha kunywa.

______ Ninaweza kujifunza kutatua matatizo kwenye maisha yangu, sihitaji pombe.

d. Mtu fulani amezoea kuwakosoa marafiki zake. Kwa hiyo wanamkwepa. Yeye hufikiri:

______Hakuna anaenipenda.

______Inabidi niache kuwakosoa marafiki zangu na kuona mazuri yaliyomo ndani mwao.

e. Mtu fulani anadanganya katika mtihani na anakamatwa. Yeye hufikiri:

______Mimi nina bahati mbaya! Wengine wadanganya na hawajawahi kukamatwa.

______Nimewezaje kufanya kitu kama hicho? Ninapaswa kujipamba na vazi la uaminifu.

---

“Tunataka kusema kuwa siyo hatima ya mtu kuwa mhalifu?” Ivan anauliza.

“La hasha,” Natalia Petrovna anajibu. “Katika mfano niliotumia hivi punde, kila mmoja anaweza kufuma bombwe nzuri kwa kutumia fremu na nyuzi ambazo

amepatiwa. Ingawa tofauti, sote tuna uwezo wa kukuza tabia zetu na kuwa watu wema."

Ivan anakubaliana na yote yanayosemwa. Hata hivyo, kuna kitu kinachomtatiza, na hajui ni nini hicho haswa. Halafu, ghafla anajisikia akisema, "Lakini yote haya ni magumu sana."

Hakuna anayeelewa Ivan anachomaanisha.

"Kitu gani ni kigumu?" Natalia anauliza.

"Kufanya sana juhudi muda wote kuwa imara, kuwa wema," Ivan anajibu.

"Uko sahihi Ivan,"Natalia anasema huku akitafakari jibu la Ivan. "Lakini kumbuka kuwa Mungu anatusaidia wakati wote. Hatuachi peke yetu kamwe. Fikiria kuhusu mtumbwi wa tanga; uwezo ya kuusogeza hutoka kwenye upepo na siyo kutoka kwenye mtumbwi wenyewe. Lakini ni nahodha ambae lazima akamate upepo kwenye tanga na kuendesha mtumbwi hadi mwisho wa safari yake. Uwezo wote hutoka kwa Mungu. Bila msaada Wake, sisi hatuna uwezo. Pale tunapojiangalia sisi wenyewe tu, chote tukionacho ni udhaifu. Lakini tukimgeukia Mungu na kumuomba msaada Wake na auni, tunapata nguvu kufanya kile kimpendezacho Yeye."

Kisha vijana hujigawa katika jozi kwa ajili ya kukariri vifungu vifuatavyo:

> **"Muumba asiye na kifani Amewaumba watu wote kutokana na kitu kile kile, na kuinua hadhi yao juu ya viumbe Wake wengine. Ushindi au kushindwa, kupata au kukosa, havina budi basi kutegemea juhudi za mtu mwenyewe. Kadiri anavyojibidiisha mwenyewe ndivyo kwa kiasi hicho yatakavyo kuwa makubwa maendeleo yake."**

> **"Ee Mungu wangu! Ee Mungu wangu! Wewe waniona katika udhilifu wangu na udhaifu wangu, nikijishughulisha na kazi kubwa kabisa, nikiwa nimedhamiria kuinua neno Lako miongoni mwa umati na kusambaza mafundisho Yako miongoni mwa watu Wako. Nitafanikiwaje isipokuwa kama Wewe ukinisaidia kwa pumzi ya Roho Mtakatifu, nisaidie kushinda kwa majeshi ya ufalme Wako mtukufu, na ninyeshee juu yangu mathibitisho Yako, ambayo peke yake yanaweza kubadilisha kisubi kuwa tai, tone la maji kuwa mito na bahari, na atomu moja kuwa miangaza na jua? Ee Bwana wangu!**

**Nisaidie kwa ushindi na UwezoWako, ili ulimi wangu useme sifa na maadili Yako miongoni mwa watu wote na roho yangu ifurike kwa mvinyo wa upendo na ujuzi Wako.**

**"Wewe ni Mwenyezi Muweza na Ufanyaye lolote Wewe upendalo."**

Ingawa utapata fursa kusoma kitabu kizima cha *Roho ya Imani* katika Sehemu ya 22, ingekufaa kusita hapa na kuchunguza maudhui ya dondoo ya hapo juu na kujadiliana vipengele vifuatavyo:

1. Nyenzo hiyo inawasilishaje dhana ya hatima? Je, huo ni msimamo mkali?

2. Uwasilishaji wenye msimamo mkali wa dhana ungekuwa wa namna gani?

3. Je, nyenzo zinaweka mkazo sahihi juu ya kuwasaidia vijana chipukizi kuchunguza dhana za kiroho, au mawazo yamewasilishwa kwa msimamo mkali?

4. Nyenzo hizi zinawasaidiaje kuona matokeo ya maandiko yanayohusu hatima na hiyari kwa ajili ya maisha yao?

5. Je, hadithi hii inaonesha ustahimilivu kwa maoni yanayotofautiana na hisia zilizooneshwa na vijana wahusika ambao wanajaribu kuelewa dhana hizi? Kama ndivyo, unaoneshwaje?

6. Nini kingetokea kama wajumbe wa kikundi cha vijana chipukizi wasingeruhusiwa kueleza mawazo yao kwa uhuru katika suala hili?

7. Jinsi gani Natalia Petrovna anawasaidia marafiki zake wadogo kukuza uwazi wa fikra?

8. Je, maswali yanayojadiliwa kati ya vijana wadogo kwenye hadithi yanawafaa vijana chipukizi wote, bila kujali usuli wao?

## SEHEMU YA 5

Kipindi cha mwanzo cha balehe ni kipindi cha maisha ambamo uwezo wetu wa kuangalia mbele zaidi ya mwonekano wa nje wa vitu umeimarishwa sana; tunatafuta uelewa wa kina zaidi wa yale tunayoshuhudia na yale tunayofanya. Hii inamaanisha kuwa vijana chipukizi wanahitaji mtazamo wa kiroho; wanapaswa kusaidiwa katika kutambua nguvu za kiroho, kwa kuona uhalisia wa kiroho wa kila hali, na katika kubaini kanuni za kiroho husika. Maandiko ya imani, hurejerea vipawa kama hivyo kama "muono wa ndani", "uoni wa ndani" na kwa "jicho la roho". Hivyo, kwa mfano, ndivyo 'Abdu'l-Bahá aliishauri Shule ya Tarbíyat ya Ṭihrán:

**“Waache wafanye maendeleo makubwa kabisa katika muda mfupi kabisa, waache wafungue macho yao wazi kabisa na kufunua uhalisia wa ndani wa vitu vyote, kuwa wenye umahiri katika kila sanaa na ustadi, na kujifunza kuelewa siri ya vitu vyote vile kama vilivyo — kipawa hiki ni mojawapo ya athari wazi za utumishi kwenye Kizingiti Kitakatifu.”**[4]

‘Abdu’l-Bahá hutaja mtazamo wa kiroho kama moja ya nguvu unaowatofautisha watu kutoka wanyama:

**“Ni dhahiri kabisa kuwa ingawa mtu anamiliki uwezo kama ule wa mnyama, yeye hutofautishwa kutoka kwa mnyama kwa kuwa yeye ana uwezo wa kiakili, mtazamo wa kiroho, upatikanaji wa njema, uwezo wa kupokea majaliwa ya Kimungu, fadhila za heshima na upatikanaji wa rehema za mbinguni. Hili ndilo pambo la mtu, heshima yake na ubora. Jamii ya binadamu lazima ijitahidi kuelekea daraja hili kuu kabisa.”**[5]

Na Anarejea kwenye muono wa ndani na usikivu wa ndani kama neema za kiroho:

**“Ametupa zawadi za kimwili na neema za kiroho, uoni wa nje kuona miangaza ya jua na muono wa ndani ambao kwao pengine tunaweza kuuona utukufu wa Mungu. Ametengeneza sikio la nje kufurahia mlio mtamu wa sauti na usikivu wa ndani ambao kwao pengine tunaweza kusikia sauti ya Muumba wetu.”**[6]

Katika tukio lingine Yeye anatukumbusha jinsi ilivyo muhimu kufungua uoni wetu wa ndani:

**“Utambuzi wetu wa kiroho, uoni wetu wa ndani lazima ufunguliwe, ili kwamba tuweze kuona ishara na dalili za roho ya Mungu katika kila kitu. Kila kitu kinaweza kuakisi kwetu mwangaza wa roho.”**[7]

Na katika kifungu hiki ‘Abdu’l-Bahá hueleza kisa kimoja ambamo utambuzi wa kiroho hukuza uelewa:

**“Wazo la uangamizaji mkubwa ni kipengele katika udhalilishaji wa wanadamu, sababu ya ushushaji na udhilifu wa mtu, chanzo cha hofu na unyonge wa wanadamu. Limekuwa la kufaa kwenye usambaratishaji na udhoofishaji wa fikra za wanadamu, ambapo utambuzi wa uwepo na uendelevu umemuinua mwanadamu kwa kilele cha ubora wa mawazo, umesitawisha misingi wa maendeleo ya wanadamu na kuchochea maendeleo ya sifa njema za kimbingu; kwahiyo, inampasa mtu kuachana na fikra za hali ya kutokuwepo na kifo, ambazo za dhania kabisa, na kujiona kuwa ataishi milele, daima akiishi katika kusudi tukufu la uumbwaji wake. Lazima ageukie mbali kutoka mawazo yanayodhalilisha roho ya mwanadamu ili kwamba siku hadi siku na saa hadi saa aweze kuendelea kuelekea juu na juu zaidi kwenye utambuzi wa kiroho wa uendelevu wa uhalisia wa mwanadamu.”**[8]

Je, unaweza kusema maneno machache kuhusu jinsi mtazamo wa kiroho unavyoleta nyanja mpya kwa uelewa ambao haupatikani kupitia zoezi la uwezo wa kiakili peke yake?

## SEHEMU YA 6

Baada ya kuchunguza umuhimu wa kuwa na mtazamo wa kiroho, sasa tujiulize namna unavyokuzwa. Swali hili, bila shaka, halikubali jibu rahisi, na hapa tunaweza kufikiria tu, mawazo machache yenye uwiano.

Ni wazi kuwa utambuzi wa kiroho ni sifa ya moyo safi. 'Abdu'l-Bahá hutuambia:

> **"Kadiri moyo wa mtu unavyokuwa safi na ulivyotakasika zaidi, ndivyo unavyo mkaribia zaidi Mungu, na mwangaza wa Jua la Uhalisia unafunuliwa ndani yake. Mwangaza huu huifanya mioyo ing'ae kwa moto wa upendo wa Mungu, hufungua ndani mwao milango ya ujuzi na hufungua siri takatifu ili kwamba vumbuzi za kiroho ziwezekane."[9]**

Kwamba ujuzi wa Mungu ni wa muhimu kwa maendeleo ya utambuzi wa kiroho pia ni dhahiri:

> **"Kwani uelewa wa uhalisia wa vitu huleta faida ya kimwili katika milki ya uwepo, na huleta maendeleo ya ustaarabu wa nje; lakini ujuzi wa Mungu ni chanzo cha maendeleo ya kiroho na mvuto, muono wa kweli na umaizi, utukuzaji wa jamii ya binadamu, kuonekana kwa ustaarabu mtukufu, uboreshaji wa maadili na mwangaza wa ufahamu."[10]**

Na upendo wa Mungu ni wazi kuwa ni wa lazima kama uoni wa ndani unahitaji kuimarishwa:

> **"Ewe rafiki yangu! Mshukuru Mungu kwamba ameuangaza uoni wako kwa mionzi ing'aayo iliyomiminwa kutoka Jua la Ukweli, na kwa kukuhuisha na kukubatiza kwa maji ya uzima na kwa moto wa upendo wa Mungu."[11]**

> **"Upendo wa Mungu unaongelewa kama moto, kwakuwa huteketeza tando, na kama maji kwakuwa ni chanzo cha uhai. Kwa kifupi, upendo wa Mungu ni uhalisia wa ndani kabisa wa njema za ulimwengu wa jamii ya binadamu. Kupitia humo, asili ya mwanadamu hutakasika. Kupitia upendo wa Mungu, mtu hukombolewa kutoka kasoro za ulimwengu wa wanadamu. Kupitia upendo wa Mungu, mtu anaweza kuendelea katika milki ya njema. Upendo wa Mungu, ni sababu ya mwangaza wa ulimwengu."[12]**

Pengine mazoezi haya yatakuwa yenye msaada kadiri mnavyotafakari juu ya maana ya ushauri uliopo hapo juu.

1. Andika sentensi chache zikielezea namna kila moja ya zifuatazo zinavyoongeza mtazamo wa kiroho:

   a. Usafi wa moyo: ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   b. Ujuzi wa Mungu: ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   c. Upendo wa Mungu: ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

2. Amua kama sentensi zifuatazo ni kweli:

_____ Kupitia kufikiria kimantiki peke yake, bila msaada wa mafundisho ya Mungu, tunaweza kutofautisha mema kutoka mabaya.

_____ Ni utambuzi ya Wadhihirishaji wa Mungu na utiifu kwa mafundisho yao ambavyo vinatuwezesha kuona ukweli.

_____ Usafi wa moyo humfanya mtu awe mjinga.

_____ Moyo unavyokuwa safi zaidi, ndivyo unavyoakisi kwa uaminifu sifa takatifu zaidi, ambazo mwangaza wake hutuwezesha kuona uhalisia wa ndani wa vitu.

_____ Moto wa upendo wa Mungu huteketezea mbali utando wa nafsi, hivyo kuuwezesha uoni wa ndani kuona ukweli.

_____ Nguvu za upendo wa Mungu hutusaidia tunapojitahidi tukiwa na muono ulio wazi kutii Matakwa Yake na kutimiza kusudi Lake.

_____ Woga wa kutoweka hudhoofisha uwezo wetu wa kiakili na kiroho, na kwahiyo mtazamo wetu wa kiroho unanolewa pale tunapohakikishiwa juu ya uendelevu wa uwepo wetu.

_____ Huduma isiyo na ubinafsi kwenye Kizingiti Kitakatifu itatusaidia kuona uhalisia wa ndani wa vitu.

_____ Kwa uoni wa ndani, tunaweza kuona uthibitisho mtakatifu.

## SEHEMU YA 7

Teuzi la mwisho katika sehemu iliyopita linaelezea dhana ya msingi yenye uhusiano mahsusi kwa uchunguzi wetu — yaani, kwamba tando nyingi zinazuia jicho la ndani kuona uhalisia wa vitu. Maendeleo ya mtazamo wa kiroho humaanisha uondoaji wa tando hizo ‘Abdu’l-Bahá huonesha:

> **“Majaliwa ya Mungu ambayo yanajidhihirisha katika nyanja zote za maisha wakati mwingine hufichwa kwa tando za muono wa kiakili na wa umauti ambao humfanya mtu kuwa kipofu wa kiroho na asiyejiweza, lakini wakati magamba yanapoondolewa na tando kupasuliwa mbali, ishara kuu za Mungu zitaonekana, na yeye atashuhudia mwangaza wa milele ukijaza dunia. Majaliwa ya Mungu yote na daima ni dhahiri. Ahadi za mbinguni zipo daima. Fadhila za Mungu zote zinatuzunguka lakini ikiwa jicho lenye ufahamu la roho la mtu likibaki limefunikwa na kutiwa giza, ataongozwa kukana ishara hizi za ulimwengu na kubaki amejinyima madhihirisho haya ya fadhila takatifu. Kwahiyo, lazima tujitahidi kwa moyo na roho ili kwamba utando unaofunika jicho la muono wa ndani uweze kuondolewa, kwamba tuweze kuona madhihirisho ya ishara za Mungu, zikishushwa neema zake za ajabu na kutambua kwamba baraka za kimwili zikilinganishwa na fadhila za kiroho ni kama si kitu.”[13]**

> **“Kila jicho lazima lijitahidi kwamba tando zinazofunika macho ya wanadamu zipasuliwe mbali na kwamba papo hapo jua liweze kuonekana na kwamba moyo na uoni viweze kuangazwa kutokana na hilo.”[14]**

Fasiri ya neno kwa neno, fikra tupu, kuiga, nafsi, na kutafuta ashiki na uchu, tamaa na husuda na ubaguzi — hizi ni miongoni mwa tando zilizotajwa katika maandiko. Hivyo, pia, hisia zetu za kimwili zinaweza kuwa tando.

> **“Sala Yangu kwenu ni kwamba vipawa vyenu vya kiroho na matarajio yenu yaweze kuongezeka kila siku, na kwamba kamwe hamtaruhusu hisia za kimwili kufunika kutoka macho yenu mwangaza wa utukufu wa Mbinguni.”[15]**

> **“Moja ya tando ni fasiri ya neno kwa neno. Kupenyeza kwenye maana ya ndani juhudi kubwa inahitajika.”[16]**

> **“Mtukuze Mungu wako kwamba umepata njia yako kuingia ndani ya Ufalme wa Miangaza, na umepasulia mbali utando wa fikra tupu, na kwamba kiini cha fumbo la ndani limefanywa lijulikane kwako.”[17]**

> **“Ninamsihi Mungu, kwa dhati, kuondoa utando kutoka Jicho lako la ndani na kukuonesha ishara Zake kuu kabisa na kukufanya bendera ya muongozo, Ambaye umeondolewa kutoka mengine yote isipokuwa Yeye, ukiwa umewashwa kwa moto wa upendo Wake, ukijishughulisha na kumbukumbu Yake na kufahamu uhalisia wa vitu, kwamba uweze kuona kwa macho yako, usikie kwa masikio yako, na kuepuka kuiga chochote cha Mababu zenu. Tazama kwa umaizi kwenye Hoja ya Bwana wako, kwa watu wamefunikwa katika tando za giza.”[18]**

**“. . . kwa kuwa hakuna utando ambao ni kikwazo zaidi kuliko nafsi, na hata kama huo utando uwe mwembamba kiasi gani, mwishowe utamfungia kabisa mtu nje, na kumnyima sehemu yake ya neema ya milele.”[19]**

**“Bado ufuataji wa ashiki na tamaa utayazingira macho katika tando elfu moja ambazo huibuka kutoka moyoni kupofusha uoni na umaizi vile vile.”[20]**

**“Enyi wana wa uelewa! Kama kigubiko cha jicho, japokuwa kikiwa chembamba kiasi gani, kinaweza kulinyima jicho la nje la mtu kuuona ulimwengu na yaliyomo humo, Hivyo fikiria kile ambacho kingetokea kama utando wa tamaa ungelifunika jicho lake la ndani. Sema: Enyi watu! Giza la tamaa na husuda hufunika mnururiko wa roho kama vile mawingu yanavyozuia mwangaza wa jua.”[21]**

**“Natumaini kwamba mtageuka na kwa macho yasiyo na utando kuelekea Jua la Ukweli, bila kutazama vitu vya dunia . . . ; acha Jua lile liwape nguvu Zake. Ndipo mawingu ya ubaguzi hayatafunika mwangaza Wake kutoka macho yenu! Ndipo Jua litakapokuwa bila mawingu mbele yenu.”[22]**

Katika kifungu cha kwanza hapo juu, ‘Abdu’l-Bahá hutuambia kuwa “majaliwa ya Mungu yote na siku zote hujidhihirisha”, “ahadi za mbinguni zipo daima”, na “fadhila za Mungu zinatuzunguka kila mahali”. Hueleza zaidi kuwa, “endapo jicho la ufahamu la roho ya mtu likibaki limefunikwa na kutiwa giza”, ataongozwa kukana ishara kuu za Mungu na atanyimwa fadhila hizi dhahiri.

1. Unafikiri ni yapi baadhi ya majaliwa na fadhila ambazo ‘Abdu’l-Bahá anazirejerea?

   ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

2. Sasa elezea jinsi tando zilizotajwa hapa chini zinavyotunyima kuona majaliwa haya na fadhila.

   a. Fasiri ya neno kwa neno ya maandiko matakatifu: ______________

      ______________________________

      ______________________________

      ______________________________

   b. Fikra tupu: ______________________________

      ______________________________

      ______________________________

      ______________________________

   c. Kuiga kwa upofu: ______________________________

      ______________________________

d. Nafsi: ____________________

e. Ufuataji wa ashiki na tamaa: ____________________

f. Tamaa na husuda: ____________________

g. Ubaguzi: ____________________

3. Amua kama sentensi zifuatazo ni kweli:

_____ Jicho letu la ndani linaona hata bila msaada wa vipawa vyetu vya kiakili na macho ya kimwili.

_____ Hisia zetu za kimwili na vipawa vya kiakili daima hutuzuia kuuona uhalisia wa kiroho.

_____ Kutakasa hisia zetu za kimwili kutokana na yote yale yasiyo kuwa ya Mungu husaidia vipawa vyetu vya ndani kuuona ukweli.

4. Mwishowe, tafakari juu ya tamko hili kutoka maandiko ya 'Abdu'l-Bahá kupata umaizi zaidi katika asili za tando ambazo zinaweza kuzuia mtazamo wa kiroho. Likariri kama ukipenda.

**"Jueni kwamba, kwakweli, kuna tando nyingi ambamo Ukweli umezingirwa: tando za kuhuzunisha; halafu tando dhaifu na wazi; halafu hufungiwa kwa Mwanga, uoni ambao hupumbaza macho, kama lifanyavyo jua ambalo limezingirwa katika mwangaza wake lenyewe na, tunapolitazama, uoni hupofuliwa na macho hupumbazwa.**

**"Namuomba Mungu kuondoa tando zote na kuyazoesha macho yote mwangaza, ili kwamba mtu asiweze kufungiwa kutoka kushuhudia Jua la Ukweli."[23]**

## SEHEMU YA 8

Hapa chini ni moja ya masomo kutoka *Dalili za Matumaini*, kitabu kingine chenye mwelekeo wa Kibahá'í kinachosomwa na vijana chipukizi. Kinasimulia hadithi ya Kibomi, mvulana mwenye umri wa miaka kumi na mbili ambaye, baada ya kupoteza wazazi wake, anaanza safari kumtafuta dada yake. Kibomi ni wa kabila la Adumbu. Wazazi wake waliuawa katikati ya mapigano ya wenyewe kwa wenyewe na watu wa kabila la Wakungu. Somo lililotangulia kabla ya hili huelezea mkutano wake pamoja na mzee mmoja kutoka kabila la Wakungu ambaye humtendea kwa wema mkubwa. Hapa anakutana na kikundi la wanajeshi kutoka kabila lake mwenyewe.

Baada ya kula chakula, Kibomi ana nguvu zaidi na anatembea kwa haraka. Wakati Alipokuwa anakimbia kutoka kijijini kwake, zaidi alihisi hofu na hasira. Sasa anaanza kuzirudisha hisia nzuri ambazo daima alikuwa nazo kuhusu watu. Yule mzee alikuwa Mkungu, ila alikuwa mwema na mwenye hekima. Alimgawia chakula chake. Maneno aliyozungumza yalikuwa mazuri na yaliyojaa matumaini: "inabidi tufanye maamuzi." "Tuliumbwa kupenda, siyo kuchukia."

Kibomi anaendelea kuufuata mto kuelekea Nangata. Baada ya kutembea kitambo kidogo, anasikia sauti na haraka anajificha nyuma ya mti mkubwa. Kikundi cha vijana wadogo kinakaribia. Wanazungumza lugha ya ki Adumba Kibomi anafurahi kusikia lugha yake na taratibu anajitokeza kutoka nyuma ya mti. Wale vijana wamevaa sare. Ni askari wa jeshi la waasi la Waadumba. Baadhi yao ni wadogo kabisa, na mmoja wao anaonekana ana umri sawa na Kibomi. Maaskari wakasimama mara tu walipomuona Kibomi na kushika bunduki zao. "Ngojeni!" akasema Kibomi. "Mimi ni mu Adumba kama ninyi!"

"Unafanya nini peke yako hapa?" akauliza kiongozi wao bila subira.

"Wakungu walivamia kijiji chetu na kuwauwa wazazi wangu. Ilinibidi nikimbie," akajibu Kibomi.

"Njoo ujiunge nasi basi," akasema kiongozi yule. "Lazima tuwafundishe Wakungu somo. Tuwafanye walipe kwa kile walichokifanya kwa familia yako."

Kibomi alishawishika. Anafikiria kidogo na alikuwa karibu akubali. Yule askari mtoto akaja mbele na kumpa mkono wake. Kibomi anamtazama machoni na anatatizwa na ukataji tamaa auonao machoni mwake. Anasita. "Naweza kujiunga nanyi baadaye," akasema kwa sauti ya kutetemeka. "Ila kwa sasa lazima niende kumtafuta dada yangu."

Wakati wanajeshi wanaondoka, mmoja akageuka na kusema, “Kumbuka kupigana ndiyo njia pekee.” Kibomi hakujibu.

**Maswali**

1. Kibomi alihisi nini alipoondoka kijijini kwake?
2. Kwa nini hisia zake zimebadilika baada ya kumuona yule mzee?
3. Kwanini Kibomi anajificha nyuma ya mti?
4. Wale vijana wadogo aliokutana nao wamevaa sare ni akina nani?
5. Kiongozi anamwambia Kibomi afanye nini?
6. Kibomi anaona nini kwenye macho ya yule askari jeshi mdogo?

**Shughuli**

1. Kibomi anaona ukataji tamaa kwenye macho ya kijana mdogo mwanajeshi ambaye akiwa na hofu na hasira kama yeye, amechagua kupigana na kuua. Sisi wote huwa tuna nyakati za huzuni na kukata tamaa. Katika nyakati kama hizo, tusichague njia za giza ila tutafute mwanga ambao hurudisha matumaini. Soma sala ifuatayo na utafakari maneno yake.

   **“Yeye ni Mwenye huruma, Mkarimu Kabisa! Ee Mungu, Mungu wangu! Wewe waniona, wewe wanijua. Wewe u mahali pangu pa usalama na kimbilio. Sijamtafuta yeyote wala hakuna yeyote nitakaye mtafuta ila Wewe; hakuna njia niliyoikanyaga wala sitaikanyaga njia yeyote ile ila njia ya upendo Wako. Katika usiku wa giza na ukataji tamaa, macho yangu yanageukia kwa matarajio na kujawa na matumaini katika asubuhi ya fadhila zako zisizo na mipaka na katika muda wa alfajiri roho yangu ififiayo huchangamshwa na kuimarishwa katika kukumbuka uzuri Wako na ukamilifu.”**

   Sasa pengine ungependa kukariri sala iliyopo hapo juu.

2. Kwa kila hali zifuatazo, amua mawazo na vitendo vipi vitaleta ukataji tamaa na vipi vitarudisha matumaini:

a. Unafanya vibaya katika mtihani wa somo mojawapo.

| | *Matumaini* | *Kukata tamaa* |
|---|---|---|
| – Unaacha kusoma na kutumia muda wako mwingi kucheza. | ☐ | ☐ |
| – Unajiambia mwenyewe kuwa u mjinga. | ☐ | ☐ |
| – Unamuomba mwanafunzi mwingine akusaidie. | ☐ | ☐ |
| – Unakuwa na subira na unajaribu kwa bidii zaidi kuelewa somo. | ☐ | ☐ |
| – Unamlaumu mwalimu wako kwa kutokukusaidia zaidi. | ☐ | ☐ |

b. Unajihisi mpweke na inaonekana kama huna rafiki yeyote.

| | *Matumaini* | *Kukata tamaa* |
|---|---|---|
| – Unajiweka pekee na kujisikia huzuni wakati mwingi. | ☐ | ☐ |
| – Unatumia muda mchache kujifikiria na kujali zaidi wengine. | ☐ | ☐ |
| – Unawaza juu ya makosa ulani ine wakati wote. | ☐ | ☐ |
| – Unatafuta mazuri ndani ya watu wengine. | ☐ | ☐ |
| – Unachukua hatua ya kwanza kuzungumza na kujenga urafiki na wengine. | ☐ | ☐ |

c. Unaona wivu na ugomvi kati ya baadhi ya ndugu zako. Matumaini Kukata tamaa.

| | *Matumaini* | *Kukata tamaa* |
|---|---|---|
| – Wewe pia, unahisi wivu na unagombana nao. | ☐ | ☐ |
| – Unajaribu kuwa mkarimu zaidi kwao. | ☐ | ☐ |
| – Unasali kuwaombea wanafamilia yako waungane. | ☐ | ☐ |
| – Unawafundisha watoto kwenye familia juu ya upendo na ukarimu. | ☐ | ☐ |
| – Unajiambia mwenyewe kwamba hakuna unaloweza kufanya kuwabadili ndugu zako. | ☐ | ☐ |

d. Rafiki anafanya kitu ulani kukuumiza.

| | *Matumaini* | *Kukata tamaa* |
|---|---|---|
| – Unaamua kulipiza kisasi na kumuumiza rafiki yako. | ☐ | ☐ |
| – Unamsamehe rafiki yako. | ☐ | ☐ |
| – Unaamua kamwe kutokumuumiza mtu yeyote kama hivyo. | ☐ | ☐ |
| – Unawaambia wengine jinsi gani rafiki yako alivyo mtu mbaya. | ☐ | ☐ |
| – Unavunja urafiki wenu. | ☐ | ☐ |

Taja baadhi ya kweli za kiroho ambazo vijana chipukizi wanaweza kuzigundua katika somo hili. Zinatendewaje dhima za matumaini na ukataji tamaa, ambazo zinalinganishwa na mwangaza na giza? Katika njia zipi unafikiri kuwa hadithi na shughuli zinazoambatana husaidia kunoa mtazamo wa kiroho wa vijana chipukizi?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## SEHEMU YA 9

"Tumaini" na "uthibitisho" ni mifano miwili ya dhima nyingi ambazo programu ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi inahitaji kuziongelea. Majadiliano makini ya dhima

kama hizo yanaweza kuimarisha mtazamo wa kiroho na kuchangia kwenye upanuzi wa ufahamu.'Abdu'l-Bahá husema:

> **"Zipo baadhi ya nguzo ambazo zimewekwa kama msaada usiotikisika wa Imani ya Mungu. Yenye nguvu kabisa kati ya hizi ni ujifunzaji na utumiaji wa akili, upanuzi wa ufahamu, na umaizi kwa uhalisia wa ulimwengu na mafumbo yaliyofichwa ya Mungu Mwenye nguvu zote."[24]**

Mtu anaweza kuishi katika viwango tofauti vya ufahamu. Kuwa na utambuzi wa amri takatifu na kusudi, kutambua nguvu zinazotushawishi na jumuiya zetu, na kujitahidi kutumia nguvu zetu za kiakili na kiroho kujenga ulimwengu mpya — hizi humaanisha kiwango cha juu cha ufahamu kuliko maisha yaliyokaziwa kwenye masuala ya kimwili. Moja ya changamoto kubwa ya mhuishaji wa kikundi cha vijana chipukizi ni kuwasaidia wajumbe wake kufikia viwango vya juu na juu zaidi vya ufahamu. Ikiwa wanatakiwa kufanya hivyo, vijana wanahitaji kuelewa dhana hizo ambazo huhusiana na dhima ambazo ni muhimu kwa maisha ya kiroho. Hivyo, pia, sharti wanapaswa kuongeza uwezo wao wa kutafakari na kuchambua dhana hizo na kuzitumia katika uhalisia wao. Kwa kuongezea kwenye tumaini na uthibitisho, ni zipi baadhi ya dhima na dhana zinazohusiana ambazo vijana chipukizi wanapaswa kuzifanya lengo lao la tafakari?

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

## SEHEMU YA 10

Katika sehemu chache zilizopita, tumechunguza swali la mtazamo wa kiroho na baadhi ya sifa zinazohusiana nao — usafi wa moyo, ujuzi wa Mungu, na upendo wa Mungu. Pia tumefikiria kuhusu "tando" ambazo zinaweza kutuzuia kuona kwa "macho yetu ya ndani" na tumefikiria namna uelewa wa dhana fulani unavyo tusaidia kuimarisha mtazamo wetu wa kiroho na kupanua ufahamu wetu.

Mnamo kipindi cha balehe nguvu zilizomo katika roho ya mwanadamu huzidi kujidhihirisha zenyewe zaidi. Miongoni mwa hizi, nguvu za fikra na kauli zina umuhimu mahususi, na kuzilea pia ni muhimu sawasawa na upanuzi wa ufahamu. Kuna uhusiano wa karibu sana kati ya lugha na fikra. Nguvu ya fikra hufunuliwa kupitia kauli, na ukuzaji wa nguvu ya kauli ni wa lazima kwa uendelezaji wa uelewa. Ukuzaji wa uwezo wa kujieleza na uongezaji kina cha uelewa wa uhalisia wa mtu huenda bega kwa bega. Uelewa huhitaji baada

ya yote, taamali na tafakari, shughuli zilizofungamana bila kutenganishwa pamoja na lugha. Bahá'u'lláh anasema:

> **"Enyi watu wa Bahá! Chanzo cha stadi za mikono, sayansi na sanaa ni uwezo wa kutafakari. Fanyeni kila juhudi ambazo kutoka ndani ya machimbo haya bora ziweze kung'aa lulu za busara na kauli ambazo zitaendeleza ustawi na upatano wa koo zote duniani."[25]**

Uelewa wa mwanadamu na uwezo wa kujieleza, bila shaka, unahitaji mwangaza kutoka kauli Takatifu. Bahá'u'lláh hutuambia:

> **"Yeye amekuja kwa ajili ya wokovu wenu, na amevumilia mateso ili ninyi muweze kupanda, kwa ngazi ya kauli, hadi kwenye kilele cha uelewa."[26]**

Ukuzaji wa uwezo wa kujieleza unahusisha zaidi ya upatikanaji tu wa ujuzi wa kiufundi wa usomaji, kuandika, na kuongea. Huhitaji vipaji kadhaa: kusoma kwa ufahamu mzuri, kueleza mawazo kwa uwazi na ufasaha, na kufafanua dhana kwa usahihi wenye mantiki. Katika utekelezaji wa vipaji hivi, vijana chipukizi hujifunza kutumia dhana husika za kisayansi, za kimaadili, na za kiroho kwa ajili ya uchambuzi wa ulimwengu unaowazunguka na kwenye uundaji wa mathibitisho binafsi ambamo juu yake mustakabali wa itikadi ya kijamii unaweza kujengwa.

'Abdu'l-Bahá anaeleza kuwa "umati wa watu hauna habari juu ya mawakala hawa muhimu ambao ndio tiba ya papo hapo kwa jamii yenye magonjwa sugu. "Kwa sasa," Yeye pia anaeleza, "kwa sababu ya mapungufu katika elimu yao, idadi kubwa ya watu inakosa hata msamiati wa kuelezea kile wanachokitaka." Hivyo, wana bahati iliyoje, wale ambao, katika ujana wa awali, wanaweza kukuza uwezo wa kujieleza na, kwa kuwa wanatambua tiba takatifu kwa ajili ya magonjwa sugu ya jamii ya binadamu, wakijaza akili zao kwa fikra za mbinguni, wakiongeza kwa namna hii uelewa wao na upanuzi wa ufahamu wao.

Katika somo lililopo hapa chini kutoka *Kuchota kutoka Nguvu ya Neno*, kitabu chenye mwelekeo wa Kibahá'í mara nyingi kinasomwa na vijana chipukizi ambao tayari wamesha pitia vitabu kadhaa vya mwanzo, kikundi cha vijana wanajadili dhana ya "neno". Soma somo na jaribu kuona jinsi linavyoongeza uelewa na kukuza ufahamu.

Shughuli mojawapo zinazosisimua sana zinazofanywa na kikundi cha vijana wa Alegrías mnamo miezi ya mwanzo ya uwepo wake ilikuwa ni mradi wa upandaji miti. Pindi walipomaliza kupanda miti hamsini ya matunda kuzungukia shule yao, waliwaalika wazazi wao, rafiki na majirani kwenye sherehe ambapo Elisa alitoa hotuba fupi juu ya umuhimu wa uboreshaji wa mazingira. Jumuiya ilifurahia mradi huu kwa sababu miti iliyopandwa ingezaa matunda na kuremba kijiji.

Siku iliyofuata baada ya sherehe, kabla ya kuondoka Alegrías, Elisa aliomba mkutano maalum pamoja na vijana. "Leo ningependa tuongelee mada ambayo itakuwa kiini cha majadiliano yetu kwa miezi ijayo," aliwaambia kwa shauku

kubwa. “Ili kuitambulisha, hebu niwaulizeni swali: Mnafikiri kwa nini Mungu ametuumba?”

Mariela alijibu mara moja, “Mungu alituumba kwa sababu anatupenda. ‘Nilipendezwa na kuumbwa kwako na ndipo nikakakuumba.’ Nilijifunza nukuu hii nilipokuwa ningali mtoto na sijaisahau kamwe.”

“Vizuri sana,” alijibu Elisa. “Mungu ametuumba kutokana na upendo Wake usiyo na kikomo kwetu. Na kwa sababu ya upendo huu, amejalia juu ya kila mmoja wetu zawadi za ajabu kabisa. Mojawapo ya zawadi Zake kubwa kabisa kwetu ni uwezo wa kutumia ‘neno’. Hakuna kiumbe hai kingine kilichopewa uwezo huu wa kuongea maneno, kusoma maneno, kuandika maneno, na kuyaelewa. Kupitia maneno, tunawasiliana na kila mmoja na tunafahamishana tunachofikiri na tunachohisi. Juu ya yote, ni kupitia maneno kwamba mafundisho matakatifu huelezwa. Tunayaelewa mafundisho haya kwa kusikiliza na kusoma Neno la Mungu lililofunuliwa kupitia Mdhihirishaji Wake. Hivyo, mada niliyonayo akilini kwa ajili ya majadiliano yetu, ni, uwezo wa neno.”

“Nimesikia kuwa neno lina uwezo zaidi kuliko upanga,” alisema Carlota.

“Hiyo ni kweli,” aliongeza Antonio. “Lakini ili maneno yawe na nguvu, sharti yaambatane na vitendo. La sivyo, maneno ni matupu na yanaweza kupeperushwa kwa urahisi na upepo. Mojawapo ya nukuu niipendayo anasema hivi, ‘tujihadhari, tusije tukatembea katika njia za wale ambao maneno yao hutofautiana na vitendo vyao.’”

“Ndiyo,” anaongeza Ana Maria. “Unaweza kumwambia mtu kuwa yeye ni rafiki yako kuliko wote, lakini ikiwa humsaidii anapokuwa anakuhitaji, basi labda wewe siyo rafiki yake kama ulivyokuwa ukidai.”

Wazo la Ana Maria liliwasha cheche ya mawazo katika akili za kila mmoja na wote wakaanza kutoa mifano ya maneno matupu na maneno ambayo yameambatana na vitendo.

Hatimaye, Elisa alisema, “Vizuri. Nyote mnaamini kuwa maneno yanayoambatana na vitendo yana uwezo mkubwa sana. Maneno yana uwezo wa ajabu — yanawezakubadilisha ulimwengu. Ndiyo maana ninyi, ambao mnataka kujenga ulimwengu bora zaidi, mnapaswa kujifunza kutumia maneno vizuri. Hii ina maana kufikiri neno, kuelewa neno, kusema neno, kusambaza neno na kuweka neno katika vitendo.”

Kwa muda kidogo vijana walikaa kimya, wakitafakari alichokuwa amesema Elisa. Halafu Diego ghafla alipata wazo. Kwa msisimko, aliruka juu mbele ya kikundi na kusema, “Sasa ninajua jinsi tutakavyopata maendeleo ya kimwili na ya kiroho: kwa uwezo wa neno ambalo linaambatana na vitendo safi.”

Kimya. Hakuna aliyesema kitu. Diego hatimaye aliishia kusimama tu hapo, kwa wasiwasi .Hakujua aketi au abaki amesimama. Alimwangalia Elisa kwa ajili ya msaada. Elisa alisimama polepole, alimwendea na kuushika mkono wake. “Wewe umegundua ukweli wa kina kabisa,” alimwambia. “Kadiri upitavyo muda utaelewa ni muhimu kiasi gani.

**Mazoezi**

1. Tumia maneno yafuatayo kukamilisha sentensi hapo chini:

ambatana, dhania, eleza, vitendo, wasiliana,
boresha, jalia, unda, mazingira, izungukayo,
zawadi, iliyofunuliwa, shawishi, kina

a. Ni kupitia nguvu ya neno kwamba tunaweza ______________________ sisi wenyewe.

b. Julia hakutaka mdogo wake wa kiume aende dukani peke yake, kwa hiyo aliamua ________________________________ nae.

c. Daktari alifurahi kuona afya ya msichana mdogo imeanza ____________ .

d. Ni baada tu ya kumuuliza mara kadhaa ndiyo Luis Enrique hatimaye aliweza __________________________ kutoa hotuba mkutanoni.

e. Mungu ametupa _____________________ ya uhai, na sharti tusiipoteze.

f. Wakati wowote Juan Carlos atoapo ahadi, hujitahidi sana kuitimiza. Maneno yake mara nyingi hufuatwa na _________________ .

g. Kwa ajili ya upendo Wake kwetu, Mungu ametupatia zawadi nyingi. Uwezo wa kutumia neno ni mojawapo ya zawadi kubwa kabisa. Yeye ametu ____________________ .

h. Hadithi fupi iliandikwa kutoka __________________ ya akili ya mtunzi pekee.

i. Ili kuweza ____________________ na wengine, lazima tujifunze kusikiliza.

j. Cecilia anafikiria kuhusu ________________________ na anaamua kutoa mafunzo kwa jamii kuhusu usafi.

k. Wakati wowote pakiwepo na mradi wa kutekelezwa, Diego anaweza kuwasisimua wote kuhusu mradi. Ana uwezo wa _____________________ shauku.

l. Roberto alichoka sana baada ya kufanya kazi sana siku nzima hata akaenda kulala na hakuna aliyeweza kumuamsha. Alikuwa katika usingizi wa _______________________ .

m. Bibi yangu kamwe hakupenda kumwambia mtu yeyote umri wake, lakini alipofikisha miaka 100, hatimaye ali _______________ umri wake.

n. Anna alipanda bustani kuzunguka nyumba yake, kwa hiyo yalikuwepo maua mazuri ya rangi na aina mbalimbali ________________________ nyumba.

2. Andika sentensi kwa kutumia vifungu vya maneno vilivyopo hapo chini:

   vitendo visafi:_______________________________________________________

   _____________________________________________________________________

   kuboresha mazingira: _________________________________________________

   _____________________________________________________________________

   kwa shauku kubwa: ___________________________________________________

   _____________________________________________________________________

   kuweka maneno katika vitendo: ________________________________________

   _____________________________________________________________________

   kutafakari juu ya kilichosemwa: ______________________________________

   _____________________________________________________________________

3. Maneno yana nguvu kupelekea kwenye wema au ubaya, na kulingana na maneno tunayotumia, tunaweza kutoa ushauri mzuri au mbaya kwa wengine. Weka alama “Z” mbele ya maelezo ya ushauri mzuri, “B” mbele ya ushauri mbaya.

_______ Lazima tuwe na umoja na kamwe tusigombane.

_______ Kama unakihitaji kichukue. Usijali mwenyewe anasemaje.

_______ Usisengenye.

_______ Sisi sote wakati mwingine tunahisi uvivu, tunapokuwa na siku kama hiyo ni bora tusifanye kitu.

_______ Usiahirishe hadi kesho unachoweza kufanya leo.

_______ Haijalisha kama utachelewa kidogo kwenda mkutanoni.

_______ Hata kama kazi ni ndogo kiasi gani, lazima ifanywe kwa ubora.

_______ Ni sahihi kusema uwongo mdogomdogo mara moja moja.

_______ Usimfanyie mtu yeyote kitu; hailipi.

_______ Kusudi pekee la maisha ni kujifurahisha.

_______ Lazima tujitahidi kila siku kujiboresha wenyewe.

_______ Kazi ni adhabu.

_______ Kwa nini tutii sheria; sisi sote tunajua kinachotufaa zaidi.

_______ Kusudi letu duniani ni kumjua na kumuabudu Mungu.

_______ Tunamuabudu Mungu tunapofanya kazi yetu kwa moyo wa huduma.

_______ Kila mtu ajali maisha yake mwenyewe, na tusisumbuliwe na matatizo ya watu wengine.

_______ Wazazi wako ni wazee; wanajua nini kuhusu maisha ya leo!

_______ Kunywa pombe siku moja moja kamwe hakumuumizi mtu yeyote.

_______ Maisha ni mafupi. Kwa nini ujiue kwa kufanya kazi!

1. Somo hili linalenga kupanua ufahamu wa vijana chipukizi kwa kuwasaidia kutafakari juu ya dhana ya “neno”. Je hili linafanikishwaje? ______________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

2. Baada ya kuchunguza somo la hapo juu, ni aina gani ya uhusiano unaoweza kuuona kati ya nguvu ya fikra na nguvu ya kauli? ____________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 11

Vijana chipukizi wanahitaji kukuza uwezo wa kusoma kwa urahisi na kuelewa vizuri maana ya wanachokisoma. Katika sehemu nyingi za ulimwengu, vipo viwango tofauti vya fasihi kwa ajili ya rika hili, kutoka vitabu vya kiada hadi magazeti ya vibonzo. Wakati vipengele vingi vya chombo hiki kipana cha fasihi vinachangia kwenye maendeleo imara ya vijana chipukizi, athari zao haziwezi kulinganishwa na ushawishi ambao ukweli unaopatikana katika maandiko unauweka juu ya roho ya kijana. Tunajua kwamba, katika Maongozi haya, Bahá'u'lláh amejalia kila neno katika Ufunuo Wake uwezo mpya. Yeye husema:

> **"Kupitia mjongeo wa Kalamu Yetu ya utukufu, Sisi, kwa amri ya Mwamuru mwenye uwezo wote, tulipulizia uhai mpya ndani ya kila umbo la mwanadamu, na kuingiza katika kila neno uwezo mpya. Vitu vyote vilivyoumbwa hutangaza ushahidi wa kuzaliwa upya kwa kila kitu ulimwenguni."[27]**

Dhima au dhana zozote zinazotumika katika nyenzo kukuza uwezo wa kujieleza katika vijana chipukizi, maana inayoelezwa inapaswa kuakisi kwa ukaribu maandiko ya Imani. Uelewa wetu wa wazo la haki, kwa mfano, kama ukiangaziwa na mafundisho ya Bahá'u'lláh, ungepenyeza katika vina vya maana ambavyo siyo rahisi kupatikana kwa ulimwengu ambao umepoteza mahusiano na uhalisia wa kiroho. Ugunduaji wa vito vya busara vilivyomo katika maandiko, kwa msaada wa nyenzo za kielimu zilizoelezwa kwa ubunifu, huaangazia akili za vijana chipukizi na kutengeneza furaha katika mioyo yao. 'Abdu'l-Bahá hueleza:

> **"Roho zenu ziweze kuangaziwa kwa mwangaza wa Maneno ya Mungu, na muweze kuwa hazina za siri za Mungu, kwani hakuna faraja kubwa zaidi wala furaha tamu zaidi kuliko ufahamu wa kiroho wa mafundisho matakatifu. Ikiwa mtu anaelewa maana ya halisi ya beti za mshairi kama vile Shakespeare, amefurahishwa na**

**kushangilia. Furaha na shangwe yake ni kubwa kiasi gani anapoona uhalisia wa Maandiko Matakatifu na kuwa aliyetaarifiwa siri za Ufalme!”[28]**

Dondoo zilizopo hapa chini zimetolewa katika kitabu kiitwacho *Kuchota Kutoka Nguvu ya Neno*. Dhima ya “maendeleo” inapatikana katika kitabu chote. Nyenzo hujitahidi kusaidia akili changa kupata uelewa wa dhana ya maendeleo ambao unapatana na mafundisho ya Imani. Mnaombwa kujaribu kubaini tofauti kati ya maana ya maendeleo, kwa mfano, yanayoongelewa katika vyombo vya habari leo, na maana yake kama inavyoelezwa katika dondoo inayofuata:

Muda kidogo uliopita, watu wa kijiji walipokea ziara ya Mwalimu mmoja mwenye heshima ambaye aliwaambia, “Alegrías inaweza kuwa jumuiya ya mfano, ambamo tunaweza kupata maendeleo ya kimwili na ya kiroho.” Mwanzoni, Diego hakuelewa hasa maana ya “maendeleo ya kimwili na ya kiroho”, lakini alishiriki katika furaha ya jumuiya nzima. Tangu hapo amejifunza mambo mengi kuhusu suala hilo. Ametambua kuwa, ingawa kimwili yeye ni mdogo, lakini siyo mtoto tena na anaweza kusaidia kijiji chake kufikia shauku ya maendeleo ya kimwili na kiroho.

Ilikuwa ni wakati wa mojawapo ya mazungumzo haya ambapo Diego aliamua kumuuliza kila mmoja walichofikiri kuhusu maendeleo ya kimwili na ya kiroho. Mariela, ambaye kila wakati ana jambo la kuvutia la kusema alijibu mara moja: “Mimi najua hasa maendeleo ya kimwili humaanisha nini. Humaanisha sisi ni masikini na tunahitaji fedha zaidi kuweza kupata vitu vitakavyo tufurahisha.”

Wazo la Mariela lilimsisimua kila mmoja, na wote walianza kushirikiana maoni yao. Waliyoyasema ni zaidi au pungufu ya haya:

Antonio: “Siamini kwamba ili kuwa na furaha lazima uwe tajiri. Nawafahamu watu wengi ambao ni masikini lakini wana furaha.”

Carlota: “Kaka yangu yupo likizo kutoka chuo kikuu, naye anasema kuwa matajiri walibuni wazo, ‘maskini wenye furaha’ ili kutufanya turidhike kuendelea kuwafanyia kazi.”

Ana Maria: “Labda hilo ni kweli, lakini mimi najua kuwa furaha hutoka ndani na haitegemei juu ya vitu vingapi anavyomiliki mtu.”

Diego: “Lakini pamoja na hayo, bila shaka siyo raha kuwa maskini. Lazima tujitahidi kadiri tunavyoweza kuboresha maisha yetu.”

Antonio: “Lakini lazima tuwe na furaha wakati tunapojaribu kufanya hivi. Mimi nataka kufanya kazi kwa bidii kwa ajili yangu mwenyewe na kwa ajili ya jumuiya, lakini pia nataka kuhisi furaha wakati ninafanya hivyo. Nilizoea kufurahia kutumia muda wangu na kaka yake Carlota, lakini tangu ameanza kuongea mambo ya matajiri na maskini, sipendi kumsikiliza tena. Amejawa hasira nyingi sana.”

Roberto: “Najua kuwa furaha halisi ni kuwa karibu na Mungu na utii kwa Sheria Zake.”

Diego: “Hilo ni kweli, lakini hatuwezi kusahau kuwa ili kumpenda Mungu sharti tuwapende watu wenzetu na kuwasaidia.”

Carlota: “Na tukumbuke kuwa kutii sheria za Mungu pia humaanisha kufanya kazi pamoja kujenga ulimwengu bora mbamo watu hawatakuwa maskini tena.”

Halafu, ghafla Diego alielewa kuwa mpaka kufikia hapo wao wote walikuwa wamejadili maendeleo ya kimwili. “Nini kimetokea kwa maendeleo ya kiroho?” aliuliza. Lakini kila mmoja tayari alikuwa amechoka, na waliamua kuendeleza majadiliano wakati mwingine.

Vijana walitenga mikutano kadhaa kujadili maendeleo ya kimwili na kiroho. Mwezi mmoja baadaye, mara kabla ya ziara ya Elisa, waliandaa mkutano maalum kupitia matokeo mbalimbali. Wakati vijana walipowasilisha mawazo yao kwa Elisa, alifurahi sana. Aliwasaidia kuandaa hitimisho lao zuri na kuandika azimio lifuatalo:

**Azimio la Vijana**

Sisi siyo watoto tena na tunapaswa kufikiria kwa uzito kuhusu mustakabali wetu. Ulimwengu ambamo tunaishi umejaa mateso na umeathiriwa na utengano. Tunataka kujenga ulimwengu mpya ambamo watu wataishi kwa

upatano na ambamo hakuna tena vita na umasikini. Ili kujenga ulimwengu mpya inatubidi kuanza na jumuiya yetu wenyewe. Ndiyo maana sasa tunajadili maendeleo ya kimwili na ya kiroho katika kijiji chetu kidogo, Alegrías. Ili tuendelee kimwili, inatupasa kuboresha kilimo chetu, kutunza afya zetu vizuri zaidi, kuwa na shule nyingi na kuendelea katika biashara na viwanda. Kwa matunda ya kazi zetu, tunaweza kugeuza nyumba zetu, kijiji chetu, na maeneo yanayotuzunguka kuwa mahali pa uzuri mkubwa, ambamo wote tunaweza kufurahia mazingira safi na salama.

Maendeleo ya kimwili kwa ajili ya watu wote hayapatikani tusipopata maendeleo ya kiroho. Bila hali ya kiroho, watu wachache watatajirika wakati wengine wote wataendelea kuishi katika hali ya umaskini. Ili kufikia malengo yetu kama jumuiya inatubidi kuungana, tutende kwa haki, kushirikiana na kuwa marafiki mmoja kwa mwingine, na kuwa wakarimu, wakweli na wakuaminika. Haki, ukarimu, upendo na wema, ukweli na kuaminika ni sifa za kiroho ambazo kwazo tunafikia maendeleo ya kimwili na ya kiroho.

Tunahitaji sifa njema za kiroho siyo tu kwa ajili ya kujenga ulimwengu bora. Pia tunazihitaji kwa ajili ya maisha ya roho zetu ambayo hayaishii hapa duniani. Maendeleo ya kimwili na kiroho humaanisha kuwa kila siku tunajitahidi kupata ubora katika hali za kimwili na kiroho za maisha yetu, ya kwamba tunafanya kazi kwa bidii kujenga ulimwengu wenye haki na amani na kwamba tunajiandaa wenyewe kwa ajili ya maisha ya milele ya shangwe na furaha.

Diego alitumia saa nyingi kufikiria juu ya hotuba yake. Kiasilia, “Maendeleo ya kimwili na kiroho kwa ajili ya Alegrías” ndiyo mada aliyotaka kuijadili. Hata hivyo, yeye hakutaka kutoa hotuba nzito juu ya mada na hakutaka kuwahubiria rafiki zake. Kwa hiyo yeye alichagua njia hii ya kuwasilisha mawazo yake:

Kuwa sehemu ya kikundi cha vijana cha Alegrías limekuwa jambo muhimu kwangu. Washiriki wake ni marafiki bora kabisa ambao nimewahi kuwa nao, na baadhi ya nyakati zangu za furaha kabisa huwa pale ninapokuwa nao. Nadhani sote tumebadilika tangu tumeanza kukutana na kufanya mambo mbalimbali pamoja. Tulikuwa tungali watoto tulipoanza, na kukutana kwetu

kumetusaidia kuingia hatua inayofuata ya maisha yetu kwa jinsi yenye maana. Tunashukuru kwa shughuli zetu na majadiliano, hatutaingia katika hatua ya ujana katika hali ya kuchanganyikiwa na kukosa matumaini. Tunajua tunakusudi maishani, na tutaweza kusaidiana mmoja kwa mwingine kutimiza malengo yetu. Nadhani tutakuwa marafiki daima.

Mojawapo ya mawazo ambayo tumefikiria mara kwa mara tangu tumeunda kikundi chetu ni maendeleo ya kiroho na kimwili ya Alegrías. Nadhani mwanzoni tulikuwa tunataka kudadisi tu kuhusu maana yake. Lakini sasa, kwa wengi wetu, maendeleo ya jumuiya yetu ni jambo ambalo tungependa kulitilia nguvu zetu. Tunatumaini kwamba shauku yetu inaambukiza na itamwathiri kila mtu kijijini.

Tunamshukuru Elisa amabaye ametuongoza kwa upendo, sasa tunajua mambo muhimu kuhusu maendeleo. Tunajua kuwa daima tunatakiwa kuungana, la sivyo juhudi zetu zote zitapotea bure. Tunajua kuwa inatubidi kujitahidi kupata ubora; kila siku inapaswa iwe bora zaidi kuliko siku iliyopita. Pia tunajua kuwa maneno yaliyoangaziwa na matendo safi yana nguvu ya kuleta mabadiliko. Lakini kwa nini maneno yana uwezo kama huo? Mojawapo ya sababu muhimu kabisa ni kwamba kupitia hayo tunagundua, tunapata na kusambaza ujuzi. Kiini cha maendeleo ni ujuzi.

Siku moja nilikuwa naangalia baadhi ya ng'ombe wakichungwa katika malisho karibu na nyumbani kwangu. Nikafikiri mwenyewe, "Ng'ombe hawa wana kila kitu wanachokihitaji. Majani yote wanayotamani yapo kwa ajili yao. Kuna kijito cha maji kipitacho katika malisho, ambamo wanaweza kunywa wakati wowote wapendapo. Wanaweza kulala juani au kivulini wakati wowote wapendapo. Wanahitaji nini zaidi?" Lakini tena nilitambua kuwa wao walikuwa na hayo tu. Hawana ujuzi au uelewa wa kile wanachokifanya. Wao ni watumwa wa asili. Niliamua kuwa bila shaka sikutaka kabisa kuishi kama ng'ombe. Kisha nikajisemea, "Itakuwaje kama nikiwa tajiri kupindukia na mwenye nguvu lakini nikabaki mjinga? Itasaidia nini? Hata nikiwa na utajiri huo wote na nguvu sitakuwa kitu kingine isipokuwa mtumwa — mtumwa wa ashiki zangu mwenyewe ambazo zitanipelekea kufanya mambo ambayo hata sielewi, mtumwa wa tamaa, mtumwa wa watu wengine ambao ni matajiri na wana nguvu zaidi kuliko mimi." Ndiyo maana ujuzi ndiyo kiini cha maendeleo. Ujuzi hutupa uhuru.

Katika nafasi hapa chini, andika aya chache zinazoelezea nini unachofikiria vijana chipukizi wanapaswa kuelewa kuhusu dhima ya maendeleo, na kwa nini.

## SEHEMU YA 12

Katika maandiko ya Imani, "kauli" mara nyingi huvumishwa na istilahi kama vile "wazi kama kioo", "fasaha", "yenye kupenya", "ya kuvutia" na ikiambatana na misemo ambayo inaelekeza kwenye uhitaji wa "ukadirifu", "hekima", na "uelewa". Maneno yenye sifa hizi yanategemewa kuwa na matokeo ya kipekee kama "kushinda utando wa nafsi na ashiki" na "kuzima moto wa uadui na chuki". Zaidi, maneno hutoa ushawishi kufuatana na hali na sifa za kiroho za yule anayeyatamka.

> **"Sema: kauli ya mwanadamu ni kiini ambacho hutarajia kutoa ushawishi na huhitaji kiasi. Kuhusu ushawishi wake, hili hutegemea unadhifu ambao nao hutegemea mioyo ambayo imejitenga na ni safi."[29]**

> **"Aidha, maneno na kauli sharti zote ziwe zenye kuvutia na zinazopenya. Hata hivyo, hakuna neno ambalo litakuwa na sifa hizi mbili isipokuwa likisemwa kwa ajili ya Mungu peke Yake na likikidhi mahitaji ya tukio na ya watu."[30]**

> **"Namsihi Mungu kumimina juu ya vichwa vyenu lulu za fadhila Zake, kuwasha mioyoni mwenu moto wa upendo wa Mungu, kuweka huru ndimi zenu katika kauli za maneno yenye ufasaha na maana bora kabisa na siri katika mikusanyiko ya watakatifu, kuwafanya maua ya paradiso ya Abha na malaika wa mbinguni, mlioungana kwa mawazo yenu na fikra zenu kupatana; na kudhihirisha kwenye nyuso zenu ishara za utakatifu wa Ufalme Wake miongoni mwa watu wote."[31]**

> **"Ikiwa mnataka maneno na kauli zenu viwe na athari katika mioyo migumu, jitengeni na mambo yote ya ulimwengu huu na geukieni Ufalme wa Mungu."[32]**

1. Baini kutoka mateuzi yaliyopo hapo juu baadhi ya sifa za kiroho zinazojalia nguvu maneno ya mwanadamu ____________________

2. Unafikiri ni namna gani uchunguzi wa dhana katika vitabu vinavyosomwa na vijana chipukizi kwenye programu ya uwezeshwaji wa kiroho huwasaidia kukuza sifa hizi?

## SEHEMU YA 13

Katika maandiko tunaambiwa kuwa nguvu ya kauli inatakiwa kuelekezwa kwenye utambuzi wa malengo ya juu:

> **"Sasa ndiyo muda wa kujitakasa wewe mwenyewe kwa maji ya kujitenga ambayo yametiririka kutoka kwenye Kalamu Kuu, na kutafakari, kwa ajili ya Mungu peke yake, mambo yale ambayo, tena na tena, yameteremshwa au kudhihirishwa, na halafu kujitahidi kadiri iwezekanavyo ndani mwako, kuzima, kupitia uwezo wa busara na nguvu ya kauli yako, moto wa uadui na chuki ambavyo vinawaka chinichini katika mioyo ya watu wote wa ulimwengu."[33]**

> **"Mtumishi huyu anazisihi roho zote ambazo zinabidii na ni jasiri kutumia jitihada zake zote kuinuka kurekebisha hali za kanda zote na kuhuisha wafu kwa maji ya uzima ya hekima na kauli, kwa njema ya upendo alionao kwa Mungu, Mmoja, Asiye na Kifani, Mwenyezi, Mpaji."[34]**

> **"Kila neno limejaliwa roho, kwa hiyo msemaji au mwelezaji inampasa kuwa mwangalifu kutoa neno katika muda na mahali panapofaa, kwani mvuto ambao kila neno litatoa ni wazi kabisa na linasikika. Yule aliye Mkuu anasema: neno moja linaweza kufananishwa na moto, lingine kama mwangaza, na ushawishi ambao yote mawili hutoa ni dhahiri ulimwenguni. Kwa hiyo mtu mwenye hekima aliyeangaziwa kimsingi sharti aseme kwa maneno yenye upole mithili ya maziwa, kwamba watoto wa watu waweze kulelewa na kusaidiana kutoka humo na waweze kupata lengo lililokusudiwa la uwepo wa mwanadamu ambalo ni daraja la uelewa wa kweli na ubora. Na kadhalika Yeye anasema: Neno moja ni kama msimu wa mchipuo unaosababisha miche michanga ya bustani ya mawaridi ya elimu kuwa kijani na kustawi, wakati neno lingine ni kama sumu inayoua. Inampasa mtu mwenye hekima kuongea kwa upole na ustahamilivu mkubwa ili utamu wa maneno yake umwezeshe mtu kupata kile kinachostahili daraja lake."[35]**

1. Amua kama kauli zifuatazo ni Kweli: Uwezo wa kujieleza unapaswam orci. uelekezwe kuelekea.

   _____ kushinda mabishano.

   _____ kueleza ukweli kwa kuweka wazi hoja.

   _____ kuzima moto wa uadui na chuki ndani ya mioyo ya watu.

   _____ kulaghai wengine.

   _____ kuficha ukweli.

   _____ kueleza siri za ulimwengu.

   _____ kueleza mambo yenye utata.

   _____ kufafanua sintofahamu na kujenga umoja wa muono.

   _____ kuonesha ubora wa mawazo ya mtu.

   _____ kujitwalia sifa na kupendwa.

   _____ kuchunguza uhalisia.

_____ kuboresha hali za watu.

_____ kutetea haki za wanyonge.

2. Sema maneno machache kuhusu jinsi ukuzaji wa uwezo wa kujieleza huwasaidia vijana chipukizi katika njia ya mabadiliko binafsi na vilevile katika juhudi za kuchangia kwenye mabadiliko ya jamii.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 14

Katika kuwasaidia vijana chipukizi kukuza uwezo wa kujieleza, kamwe tusisahau kuwa ni Neno la Mungu ambalo hujaza nguvu ndani ya maneno ya mtu na huupatia moyo na akili ya mtu uelewa wa kweli. Mnaombwa kusita hapa na kutafakari juu ya vifungu hapa chini:

**"Nyota ya Mchana ya kauli, inayong'aa kwa wangavu kutoka chemichemi ya mchana ya Ufunuo mtakatifu imeyaangazia mno Magombo na Nyaraka kana kwamba ufalme wa kauli na milki iliyotukuka ya uelewa vinatetema kwa shangwe na upeo wa furaha na kumeremeta kwa uzuri wa mwangaza Wake. . ."[36]**

**"Sema: Tumesababisha mito ya kauli Takatifu kutoka kwenye Kiti Chetu cha Enzi, kwamba miche michanga ya hekima na uelewa iweze kuchipua kutoka kwenye udongo wa mioyo yenu."[37]**

**"Kupitia pumzi ya kauli Yako mbingu ya uelewa imepambwa, na kwa mmiminiko wa kalamu Yako kila mfupa uozao umehuishwa."[38]**

**"Ni wazi na dhahiri, kwa hiyo, kwamba majaliwa ya kwanza ya Mungu ni Neno, na mvumbuzi na mpokeaji wake ni uwezo wa kuelewa. Neno hili ni mkufunzi wa kwanza kabisa katika shule ya uhai na mfunuaji wa Yeye Ambaye ni Mwenye Nguvu. Vyote vinavyoonekana ni wazi kupitia tu mwangaza wa hekima yake. Vyote ambavyo vimedhihirika ni ishara ya ujuzi wake. Majina yote ni jina lake tu, na mwanzo na mwisho wa mambo yote huhitaji kutegemea juu yake."[39]**

Pengine ungependa kukariri mateuzi ya hapo juu, mengi kadiri uwezavyo.

# SEHEMU YA 15

Tunaishi katika kipindi ambamo jamii ya wanadamu inakabiliana na ufilisikaji wa kimaadili. Viwango ambavyo vimewaongoza wanadamu kwa mamia ya miaka vinaendelea kupoteza ushawishi wao, na maadili yaliyosambaa ya masuala ya kimwili na itikadi zilizojengwa juu ya ulinganishaji uliokithiri na ubinafsi usiyo na kikomo taratibu vinachukua nafasi yake. Hebu tufikiri zaidi kuhusu hali hii kabla ya kuangalia athari zake juu ya vijana.

Inawezekana kuona katika historia kwenye miongo michache iliyopita uhuru wa hatua kwa hatua wa jamii ya binadamu kutoka minyororo mingi ambayo imeikandamiza kwa muda mrefu — kutoka itikadi potofu, kutoka udhalimu, kutoka ushirikina, kwa kutaja machache. Ingawa mengi bado yanahitaji kutimizwa, ubaguzi uliojikita umeshaondolewa, sheria za kusimamia haki zimeundwa, na haki za watu binafsi na makundi zimetambuliwa. Kwa bahati mbaya, mjongeo huu wa thamani wa kihistoria sasa umeharibika, na kuendelea kuwa hivyo hadi kupindukia zaidi. Ikijongea kuelekea katika kiini ni ulinganishaji wa kupindukia na ubinafsi ambao hauna kikomo, na uwepo wa ukamilifu unasukumwa kando. Kuwa huru kufuata matakwa ya mtu binafsi huchukuliwa kama wazo la juu kabisa, na kama matokeo tofauti kati ya mema na mabaya inaanza kufifia. Ruwaza za tabia zinazotegemea utofauti mkubwa sana wa seti za maadili, katika sehemu nyingi zaidi na zaidi, zimechukuliwa kuwa sawa, na mafundo ambayo kiutamaduni yalikuwa yakiwaunganisha wajumbe wa jumuiya, sasa polepole yamepoteza nguvu zake.

Katika hali hii, vijana wanaachwa bila muongozo wa maadili na wanapata ugumu kutenganisha ukweli kutoka uwongo. Hakuna kingine isipokuwa Neno la Mungu linaloweza kuamsha mielekeo ya kiroho inayowawezesha binadamu kubaini utofauti. ‘Abdu’l-Bahá hutuambia kwamba Neno la Mungu huangaza milki ya fikra na maadili:

> **“. . . katika ufalme wa kiroho wa kiakili na nadharia, lazima pawepo na kiini cha mwangaza, na kiini hicho ni cha milele, ni Jua ling’aalo daima, Neno la Mungu. Miangaza yake ni miangaza ya uhalisia ambayo imeng’aa juu ya jamii ya wanadamu, ikiangazia milki ya fikra na maadili, ikimimina majaaliwa ya ulimwengu mtakatifu juu ya mtu.”[40]**

Ili kuweza kufanya chaguo za kimaadili, mtu huhitaji zaidi ya seti za kanuni; muundo mzima wa maadili unapaswa kujengwa akilini na moyo wa kijana ambaye amejaaliwa kusudi lenye nguvu ya kijamii — muundo ambao unaunganisha dhana za kiroho, ruwaza za tabia, na ujuzi wa matokeo na ambayo yanashikiliwa kwa uimara na nguvu za utashi na ujasiri. Muundo kama huo wa maadili unaonekana kuwa una uhusiano wa karibu na muundo wa lugha ambao hufanya kazi katika akili ya mtu binafsi. Lugha hii, kama ilivyoelezwa katika sehemu chache zilizopita, inatakiwa kuwa tajiri ya kutosha kuwawezesha vijana kutambua nguvu za kijamii, kitamaduni, na kiitikadi zinazobumba maadili ya watu katika ulimwengu unaomomonyoka na kuelewa asili ya nguvu za kiroho zinazohitajika kuwabadilisha.

Uhusiano wa karibu kabisa kati ya muundo wa lugha ambamo mtu huwasilisha mawazo na muundo wa kimaadili ambao huongoza fikra na tabia zake una matokeo muhimu kwa jinsi vyote viwili lugha na maadili vinavyopaswa kufundishwa. Maudhui ya nyenzo zinazotumika kufundishia lugha hayana budi kubadilika kulingana na maadili ya wale ambao wanayatayarisha. Yanaweza kuleta ujumbe uliowazi wa maadili, unaweza kutatanisha kimaadili, au hata kuleta madhara ya kiroho. Maudhui ya elimu ya maadili, pia, yanaweza kubadilika kufuatana na uelewa wa kimaadili unaosambazwa. Mtu anaweza kubaini, kwa

mfano, matoleo ya nyenzo ya kielimu ambamo dhana za maadili huwasilishwa kama mlolongo wa njema, wajibu, kanuni, na taarifa sahihi zinazolenga kuboresha tabia bila umakini kwa vipengele vya lugha na fikra ambavyo hukuza mtazamo wa kiroho na kulea uwajibikaji kwa mabadiliko ya kijamii. Pia mtu anaweza kuziona programu za elimu ya maadili kama zinazowataka wanafunzi kujadili wanavyovipenda na wanavyopendelea kwa matarajio kuwa wakati wa kuvifafanua, wao watakuja kuelewa wao ni kina nani na kutambua uwezo wao. Kuishusha elimu ya maadili kwa mojawapo ya njia hizo mbili siyo lazima. Programu iliyowekwa kwa ajili ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi, haiwezi, bila shaka, haiwezi kupuuzia viwango vya juu vya maadili, wala haiwezi kupuuzia kile ambacho kiwango kama hicho kinadai bila kukosea kutoka kwa mtu binafsi. Wakati huo huo, programu kama hiyo inahitaji kuruhusu kama tulivyotanabahi mapema, majadiliano ya ziada ya dhana za kiroho. Inahitaji hata hivyo, kwenda mbele zaidi. Hususan, lazima iwe makini juu ya nafasi ya lugha katika kutengeneza muundo wa kimaadili, na tutafikiri kuhusu wajibu huu katika sehemu mbili zifuatazo.

## SEHEMU YA 16

Nyenzo zilizotumika katika programu ya kielimu zinazohusu uwezeshwaji wa kiroho lazima ziandikwe katika lugha ambayo ni wazi na yenye kuchunguza na wakati huohuo inalinda dhidi ya aina ya ulinganishaji ambao kwao elimu ya maadili imeshambuliwa sana katika miongo ya hivi karibuni.

*Kutembea katika Njia Iliyonyooka* ni kitabu kingine chenye mwelekeo wa Kibahá'í ambacho kinaunda sehemu ya programu ya vijana chipukizi. Kinajumuisha hadithi ishirini, kila moja ikihusiana na mada ya maadili. Katika tamaduni nyingi sana, hadithi hutumika kama njia ya kurithisha hekima kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Katika kitabu hiki, baadhi ya hadithi ambazo ni maarufu zimeandikwa upya ili kuondoa jumbe zenye utata zilizosimuliwa kitamaduni. Kila somo pia linajumuisha mazoezi ya kuongeza stadi na uwezo wa lugha muhimu sana kwa maendeleo thabiti ya muundo wa maadili. Somo lililopo hapa chini linaanza na hadithi ambayo unaweza kuwa unaifahamu. Imeandikwa upya kwa kusudi la kulea muundo wa fikra na tabia ambazo zinaendana na ujumbe mahususi wa kimaadili. Soma somo na jadilini jinsi ujumbe uliofikishwa na hadithi unavyoepukana na udumishaji wa tabia potofu za desturi za kitamaduni.

> *Wenye busara hawadanganywi na kilemba cha ukoka. Kila mmoja, kwa uhakika, huhamasika akisifiwa. Lakini hebu tukumbuke kuwa tamaa ya sifa hudhoofisha uwezo wetu wa kuamua.*
>
> Mbweha siku moja alimwona kunguru akiruka na kipande cha jibini mdomoni mwake. "Lazima niipate jibini ile," Mbweha alijiambia mwenyewe na hivyo alifuata kivuli cha ndege huyo hadi alipotua juu ya tawi la mti.
>
> "Habari za kutwa, rafiki yangu mpendwa," Mbweha alisema, kwa adabu mno. "Unaonekana mzuri sana leo. Manyoya yako yanang'aa, na macho yako

yanameremeta mithili ya vito. Kwa kweli, pia una sauti nzuri sana. Oh! Kama tu ningeweza kukusikia ukiimba."

Maneno haya yalikuwa kama maji safi ya kutuliza kiu ya sifa ya kunguru. Kwa hiyo aliinua kichwa chake kwa madaha na kuanza kuimba kwa heshima ya rafiki yake mcheshi.

Kwa kweli, mara tu alipofungua mdomo wake, kile kipande cha jibini kilianguka. Na mbweha alikidaka mara moja kabla hakijafika chini na kukimbia, wakati sauti ya mwewe ambayo siyo nzuri sana ilisikika hewani.

**UFAHAMU**

Jibu maswali hapo chini kwa sentensi kamili.

1. Mbweha aliona nini? ____________________________________________
   ____________________________________________

2. Kunguru alikuwa na nini mdomoni mwake? ______________________
   ____________________________________________

3. Mbweha alifanya nini kupata jibini? ____________________________
   ____________________________________________

4. Je, ni kweli kwamba kunguru alikuwa na sauti inayo vutia?__________
   ____________________________________________

5. Mbwea alikuwa mkweli katika kumsifu kunguru? _________________
   ____________________________________________

6. Hadithi hii ilitokea mjini, kijijini au msituni?______________________
   ____________________________________________

**MSAMIATI**

Kamilisha kila sentensi hapo chini kwa kutumia moja wapo ya maneno yafuatayo:

hamasishwa, tamani, cheshi, kivuli, sifa,
ridhika, kiburi, furahia, uamuzi, dhoofika

1. Mwalimu alifikiri kuwa wanafunzi wake walikuwa wachapa kazi na daima alikuwa mwenye ______________ kwa ajili yao.

2. Armando na kaka yake walitumia siku nzima waki ___________________ pamoja. Wakifanya kazi mashambani na kujadili mipango yao ya baadaye.

3. Hong Mei alipenda kusafiri na ali ___________________ kuona sehemu mpya.

4. Alikuwa na sauti nzuri, na Mwalimu wake alim ___________________ kusomea muziki.

5. Mkulima alionesha ___________________ mzuri katika kupanda mbegu mara baada ya mvua za kwanza.

6. Chandu haku ___________________ na alama alizopata katika mtihani kwa hiyo aliamua kusoma kwa bidii zaidi.

7. Zhong Jiang alikuwa katika matatizo, lakini kwa sababu alikuwa ana ___________________ , sana alikataa msaada wa mtu yeyote.

8. Hatimaye, ___________________ kirefu cha mti kilikuawa kwenye bustani.

9. Ilikuwa hadithi _____________ , na watoto walitaka kuisikia tena na tena.

10. Alikuwa ame ___________________ sana na maradhi, lakini punde alianza kufanya kazi tena akijua kuwa angepata nafuu kadri muda ulivyopita.

**MAJADILIANO**

Tutahakikishaje kuwa hatudanganywi na sifa za uwongo?

**KUKARIRI**

**"Jilindeni kwa uangalifu mkubwa, ili msije mkanaswa katika mtego wa uwongo na udanganyifu."**

Jadilini maswali yafuatayo katika kikundi chako:

1. Kama mtu siyo mwangalifu, hadithi hii inaweza kusimuliwa — kwa uhakika, imeelezwa — katika njia ambayo inahusisha sifa za ujanja dhahiri wa mbweha. Mfumo wa hadithi uliotolewa hapo juu unaepukanaje kutoa wazo kama hilo? _____________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

2. Ni upi ujumbe wa maadili wa hadithi? ____________________

3. Ni zipi baadhi ya dhana zinazohusiana na ujumbe? ____________________

4. Hadithi kama hii inafaaje katika kuwasaidia vijana chipukizi kuelewa dhana za kimaadili? ____________________

5. Mazoezi yanakuza uwezo gani kwa vijana chipukizi? ____________________

6. Ni kwa jinsi gani zoezi la majadiliano linachangia kwenye uendelezaji wa nguvu ya fikra na tafakari — pale majadiliano yanapofanywa siyo katika utupu bali katika muktadha wa ujumbe wa kimaadili? Linakuzaje uwezo wa kujieleza? ____________________

7. Ni kwa jinsi gani kukariri teuzi lililopo mwishoni mwa somo kunasaidia kuimarisha nguvu hizi? ____________________

## SEHEMU YA 17

Kama vijana chipukizi wanatakiwa kusaidiwa kutambua kanuni za kimaadili zinazohusiana na chaguzi wanazofanya, ni muhimu kuziwasilisha kwa hali ambazo ziko karibu

na uhalisia wao. Hata hivyo, hii haimaanishi kuwa, katika jina la uhalisia, umakini unavutwa kwenye udhihirisho wa asili ya chini ya mtu. Hali zilizochunguzwa, ingawa zinapatikana kwa vijana chipukizi, siyo lazima kuwa ni za kawaida kabisa katika jamii inayoendelea kuoza, bali zinapaswa kuwakilisha, badala yake, vile viwango vya fikra na tabia ambazo zingeweza kuwahamasisha kujitahidi kupata ubora. Kwa hatma hii, nyenzo zinazotumika katika programu kwa ajili ya uwezeshwaji wao wa kiroho lazima ziepuke mielekeo ya ubaba na maongezi ya kitoto, kwa upande mmoja, na lugha ya mahubiri juu ya tabia njema kwa upande mwingine. Fikiria somo lifuatalo kutoka kitabu kingine chenye mwelekeo wa Kibahá'í kinachoitwa *Kujifunza Kuhusu Ubora.* Katika somo hilo, Bi. Chen anaeleza wazo la usafi kwa wajukuu wake na kuwasaidia kwa msaada wa mazoezi machache, kupata uelewa zaidi wa umuhimu wake.

Bi. Chen anataja kuwa sharti la pili la ubora, ni maisha ya ubikira na utakatifu, ambayo humaanisha, staha, usafi, ukadirifu, heshima, na akili-safi. Yeye anaanza kwa kueleza usafi, msingi ambao juu yake maisha ya ubikira yanapaswa kujengwa:

"Fikiria kioo. Mkikisafisha na kuondoa vumbi lote, huakisi mwanga. Kwa namna hiyo hiyo, moyo ukisafishwa kutokana na mapungufu kama vile husuda, chuki, na kiburi, huwa safi na kuakisi mwangaza wa mbinguni. Mencius amesema kuwa muungwana hapotezi moyo wake wa kitoto. Jambo hili ni kweli bila shaka, lakini lazima tukumbuke kuwa moyo wa mtoto ni msafi kutokana na hatia na udhaifu na kwamba usafi wa mtoto bado haujajaribiwa. Sasa mmefikia umri ambao hamuwezi kuchukuliwa tena kama watoto. Kadiri mkuavyo, mtakuwa wenye busara na wenye nguvu. Walakini kila mmoja wenu itampasa kuwa mwangalifu na kuchunga sana asipoteze usafi wake wa moyo. Msiruhusu kioo cha moyo wenu kichafuliwe na uchafu wa ulimwengu huu. Lakini hili mnapaswa kulifanya kupitia uwezo wa mantiki na imani. Mnaweza kubakia wasafi kupitia juhudi na kwa kuonesha nia tu."

Bi. Chen kisha anaeleza kuwa dhana ya usafi aghalabu hueleweka vibaya na huwaomba wajukuu zake vijana kubaini kutoka orodha iliyopo hapo chini sifa zile ambazo zinamaanisha usafi na zile ambazo zinahusishwa na usafi kimakosa:

- Kuwa halisi
- Kuwa mnyoofu
- Kuwa wajinga
- Kuwa huru kutokana na unafiki
- Kuwa na akili safi

- Kuwa na mwili msafi
- Kuwa mpumbavu
- Kutokuwa na kiburi
- Kuwa mwenye msimamo mkali
- Kuwa na akili ya kawaida
- Kuwa huru kutokana na udanganyifu
- Kutokuwa mbinafsi
- Kuwa dhaifu
- Kuwa mwenye hisia za karibu
- Kuwa mwenye akili
- Kuwa mwema
- Kutokuwa mwenye majigambo

Vijana wanakariri mateuzi yaliyopo hapa chini na kujadili pamoja na babu na bibi zao maswali yanayofuata:

> **"Ushauri Wangu wa kwanza ni huu: uwe na moyo safi, mwema na ung'aao, ili yako iwe enzi ya kale, isiyopotea na inayodumu milele."**

> **"Wa kwanza katika njia ya maisha ya mwanadamu lazima iwe usafi, kisha ubichi, unadhifu, na uhuru wa roho. Kwanza inabidi mkondo wa mto usafishwe, ndipo maji matamu ya mto yataweza kupita humo."**

1. Mnafiki ni mtu yule ambaye hudai kuwa mnyoofu wakati siyo. Ni kipi kibaya zaidi, kuwa na kasoro nyingi au kuwa mnafiki?
2. Ni upi baadhi ya uchafu ambao kutoka kwao inatupasa kusafisha fikra zetu?
3. Ni nani hasa atimizaye zaidi katika ulimwengu huu, msafi wa moyo au yule mdanganyifu?

Jadilini katika kikundi chenu maswali yafuatayo:

1. Ni jinsi gani somo husaidia kuondoa sintofahamu zilizo zoeleka kuhusu dhana ya usafi?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

2. Ni zipi baadhi ya sifa za lugha ambayo inatumiwa na Bi. Chen? ____________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

3. Ni jinsi gani somo hili huwasaidia vijana chipukizi katika kujitahidi kupata ubora wa kiroho? ____________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

## SEHEMU YA 18

Katika sehemu mbili zilizotangulia tulifikiria, japo kwa ufupi tu, wajibu wa lugha katika kuunda muundo wa maadili. Uchunguzi wetu wa masomo mawili, mmoja kutoka *Kutembea katika Njia Iliyonyooka* na mwingine kutoka *Kujifunza Kuhusu Ubora*, umetusaidia kuona jinsi majadiliano ya mada na dhana fulani, pamoja na mazoezi yaliyobuniwa kuongeza stadi na ujuzi wa lugha, yanaweza kuongeza nguvu za ruwaza za fikra zinazosaidia chaguo thabiti za kimaadili. Hata kama ni muhimu kuongeza ufasaha wa lugha kwa njia hii, tunapaswa kukumbuka kuwa muundo wa maadili wa mtu binafsi hutegemea juu ya vipengele vingi vinavyoingiliana. Hasa, ni vigumu kutenganisha ruwaza za kufikiri zinazoongelewa hapa, na kufikiri kisayansi. Vijana wanahitaji kujiandaa kuuendea uchunguzi wa uhalisia kwa njia ya kisayansi. Idadi ya vitabu watakavyosoma, kwa hiyo, vitaingia katika maeneo ya hisabati na sayansi — siyo katika jitihada ya kuwafundisha kama masomo bali kuongeza nguvu za aina ya mantiki itokanayo humo. Katika kozi zinazochepuka kutoka kitabu hiki, zinazokusudiwa kwa ajili ya wale wanaotaka kujitoa wenyewe kufanya kazi pamoja na vijana chipukizi kwa kipindi kirefu cha miaka kadhaa, vitabu hivi vitaongelewa kwa kirefu kiasi. Kwa sasa, inatosha kuwa mtambue tu kuhusu kipengele hiki cha mchakato wa kielimu ambamo vijana chipukizi watajihusisha.

## SEHEMU YA 19

Kuendeleza mtazamo wa kiroho, kukuza uwezo wa kujieleza, na kujenga muundo thabiti wa maadili, vyote ni muhimu kwa mchakato wa uwezeshwaji wa kiroho. Kwa bahati mbaya, kumiliki uwezo aghalabu huhusishwa pamoja na maadili ambayo yanakwenda kinyume na asili

ya kiroho ya mtu. Taswira zinazo kuja akilini kwa kawaida pale dhana inapotambulishwa, ni zile za kudhibiti, kulaghai, kuwatawala, kuongoza, ukuu, na ukandamizaji. Hata hivyo, lengo lako, ni kuwasaidia vijana chipukizi kuchota kutoka nguvu ya aina mbalimbali. Nguvu ya maadili huchipuka kutoka kwenye upendo, haki, ujuzi, uelewa, mtazamo wa kina, huduma na, juu ya yote,unyenyekevu. Kwa uhakika, unyenyekevu ni sharti la lazima la mchakato wa uwezeshwaji tunaouzungumzia hapa, kwa sababu ni kupitia msaada kutoka juu tu kwamba kisubi anaweza kuwa tai, tone la maji libadilishwe kuwa mito na bahari, na chembe ndogo kuwa miangaza na jua. Kutafakari juu ya dondoo kutoka sala zilizofunuliwa na Bahá'u'lláh na 'Abdu'l-Bahá, ambamo tunamsihi Mungu kutujalia sifa fulani na vipawa, hutupa umaizi katika uwezeshwaji wa asili ya kiroho na maadili:

> **"Ninakuomba, Ewe Ambaye u Bwana wa majina yote na Mtawala wa vyote viwili ardhi na mbingu, kujalia kwamba wote ambao ni wapendwa Wako waweze kila mmoja wao kuwa kikombe cha rehema Yako katika siku Zako, ili waweze kuhuisha mioyo ya watumishi Wako. Wawezeshe pia, Ee Mungu wangu, kuwa kama mvua inyeshayo kutoka mawingu ya neema Yako, na mithili ya upepo upulizao manukato ya msimu wa machipuo ya wema — Wako wenye upendo, ili kwamba kupitia humo udongo wa mioyo ya viumbe Wako uweze kuvishwa kijani kibichi, na uweze kuzaa kile kitakochosambaza manukato yake juu ya milki Yako yote, ili kwamba kila mmoja aweze kuhisi harufu tamu ya Joho la Ufunuo Wako."[41]**

> **"Tuwezeshe, basi, Ee Mungu wangu, kusambaza kote ishara Zako miongoni mwa viumbe Vyako, na kulinda Imani Yako ndani ya milki Yako."[42]**

> **"Niwezeshe, basi, Ee Mungu wangu, kuhesabiwa miongoni mwa wale ambao wameshikilia kwenye sheria Zako na kanuni kwa ajili Yako peke Yako, na wamekazia macho yao juu ya Uso Wako."[43]**

> **"Tuwezeshe, basi, Ee Mungu wangu, kujitelekeza wenyewe na kushikilia imara kwa Yule ambaye ni Mdhihirishaji wa Nafsi Yako mwenyewe, Aliyetukuka kabisa, Aliye Juu Kabisa."[44]**

> **"Ninakusihi Wewe, kwa Yule Ambaye ni Chemchemi ya mchana ya majina Yako na mahali pa Pambazuko la sifa Zako, kuamuru kwa ajili yangu kile kitakachoniwezesha kuinuka kukutumikia Wewe na kutukuza njema Zako."[45]**

> **"Niwezeshe kuwa mmoja wa vijakazi Wako ambao wamefikia mapenzi Yako mema."[46]**

> **"Walinde watoto hawa, wasaidie kwa neema kuelimika na wawezeshe kutoa huduma kwa ulimwengu wa jamii ya wanadamu."[47]**

> **"Nitelemshie basi, Ee Mpendwa wangu, kile kitakachoniwezesha kuwa imara katika Hoja Yako, ili mashaka yote ya makafiri yasiweze kunizuia kukugeukia Wewe."[48]**

> **"Niwezeshe, basi, kupata kiti cha ukweli Mbele Yako, nijalie zawadi ya huruma Yako niruhusu nijiunge na wale miongoni mwa Watumishi Wako ambao hawataogopa wala hawatahuzunishwa."[49]**

**“E Mungu wangu, msaidie mtumishi wako kuinua Neno, na kukataa yale ya upuuzi na uwongo, kusimamisha ukweli, kusambaza mbali aya takatifu, kuwafunulia uzuri, na kufanya mwangaza wa asubuhi kupambazuka ndani ya mioyo ya wanyoofu.”**[50]

**“Wawezeshe kujitofautisha miongoni mwa watu Wako ili, watukuze neno Lako na kuendeleza Hoja Yako. Wasaidie, Ee Mungu wangu, kutimiza Amri Yako na mapenzi Yako.”**[51]

## SEHEMU YA 20

Wakati tunakumbuka akilini mwetu majadiliano ya sehemu kadhaa zilizopita — uchunguzi wetu katika asili ya mtazamo wa kiroho, ambao ni wa lazima sana kwa uelewa wa uhalisia; utafiti wetu katika uwezo wa kujieleza, ambao ni muhimu sana kwa mafanikio ya malengo ya juu; uchambuzi wetu wa uhusiano kati ya lugha na muundo wa maadili, ambao ni wa maana sana katika kufanya chaguzi; na tafakari zetu juu ya mchakato wa uwezeshaji wa kimaadili — hebu sasa tufikirie kwa kina vitabu viwili vinavyosomwa na vijana chipukizi. Katika sehemu hii na ile inayofuata tutaangalia kitabu cha *Pepo Nyanana za Uthibitisho*, na katika sehemu ya 22 na 23 tutachunguza kitabu cha Roho ya Imani. Kiujumla vyote viwili ni miongoni mwa vitabu vinavyosomwa na vikundi katika mwaka wa kwanza wa program ya uwezeshwaji wa kiroho.

Kitabu chenye mwelekeo wa Kibahá’í *Pepo Nyanana za Uthibitisho* kinasimulia hadithi ya Musonda, binti ambaye ndiyo kwanza ametimiza umri wa miaka kumi na tatu, na binamu yake mkubwa Rose, ambaye amekuja kumtembelea wakati wa likizo. Pamoja na kaka yake Musonda Godwin na rafiki yake Chishimba wasichana wanafikiri juu ya mustakabali wao na kujadili matumaini na fursa zao. Yapo mawazo kadhaa ambayo utahitaji kuchunguza katika kikundi chako yanayohusu kitabu hiki. Hata hivyo, kwanza, unahamasishwa kukisoma mara moja na tena kwa umakini zaidi, kufanya mazoezi. Baada ya kufanya hivyo, unaweza kuendelea pamoja na mapitio yanayofuata.

Kama ulivyotanabahi bila shaka, dhima inayoongelewa katika kitabu chote ni “uthibitisho”. Hapa chini yapo yale mafungu katika kitabu ambayo yanaongelea mada hii, ama kupitia majadiliano miongoni mwa wahusika wakuu katika hadithi, au kupitia matukio yanayoonesha uthibitisho mtakatifu unavyofanya kazi. Vifungu, ambavyo kila moja vimetolewa kutoka mojawapo ya masomo, vimewasilishwa katika mtiririko wao kama unavyoonekana ndani ya kitabu. Eleza katika nafasi iliyotolewa jinsi dhana ya uthibitisho inavyo shughulikiwa katika kila kifungu, na jinsi unavyofikiri uelewa wa dhana kwa vijana chipukizi utakavyokuzwa kadiri watakavyopitia masomo.

> “Nafikiria kuhusu huduma. Ninataka kufanya kitu ambacho kitawasaidia watu wengine. Ningependa kuwa muuguzi, lakini lazima usome sana. Ni ghali pia na sidhani kama wazazi wangu wana fedha za kutosha,” Musonda anaeleza.

“Ndiyo, lakini unaweza kujaribu, Musonda,” anasema Rose. “Kuna neno, ‘uthibitisho’, ambalo nimejifunza majuma machache yaliyopita katika mojawapo ya madarasa yangu. Mwalimu wangu anasema kuwa Mungu hututhibitisha na hutusaidia katika kile tunachokifanya. Sasa ninalipenda sana neno hili. Nina hakika kuwa utapokea uthibitisho wa Mungu ikiwa moyo wako umepania kuwa muuguzi.”

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

Baadaye usiku ule wasichana walipokuwa kitandani, Musonda alimnong’oneza Rose, “Rose, umesema neno ‘uthibitisho’. Unamaanisha kwamba ikiwa nitajitahidi sana katika masomo yangu, Mungu atatutumia fedha ili niweze kusomea uuguzi?”

Rose anajigeuza na kumtazama Musonda. “Sidhani kuwa ni hivyo hasa. Namaanisha, sijui. Tunapaswa kujaribu mambo na kuona milango ipi itafunguka. Lakini ninajua kwamba Mungu humpatia kila mmoja wetu vipaji. Lazima tujaribu kuelewa tuna vipaji vipi na halafu tujifunze kuvitumia,” anajibu Rose.

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

Godwin ana rafiki yake wa karibu anayesoma naye darasa moja ambaye jina lake ni Chishimba. Yeye huwatembelea wakina Mulenga mara kwa mara, na

usiku wa leo anashiriki nao chakula cha jioni. Mazungumzo mezani yanahama kutoka somo moja hadi lingine. Musonda anataka kuleta somo la uthibitisho, na anakosa subira. Mwishowe, kuna dakika chache za ukimya. “Rose na mimi tumekuwa tukiongelea juu ya uthibitisho,” anasema Musonda.

“Ameshaanza huyo dada yangu mdogo!” anasema Godwin, akisafisha koo lake. Lakini alishangazwa, Chishimba alionekana kuvutiwa.

“Neno hilo humaanisha nini kwako?” humuuliza Musonda.

Musonda pia alishangazwa, alimwangalia Rose, akitumaini kuwa atakuwa na jibu.

“Uthibitisho . . . Mungu hututhibitisha na hutusaidia katika yale tufanyayo,” anasema Rose.

Chishimba hasemi kitu chochote kwa kitambo. Kuna huzuni machoni mwake. “Miezi michache iliyopita,” huanza taratibu, “baba yangu alipoteza kazi yake. Yeye ni mwaminifu na mwajibikaji, na kila mmoja analijua hili. Kwa miaka kumi na nane amefanya kazi kama mlinzi katika kampuni, na mara bila kutazamiwa, walimfukuza. Sisi sote tunaijua sababu. Kama angeendelea kwa miaka miwili zaidi, angestaafu na kampuni ingetakiwa kumlipa mafao. Hatuna akiba kubwa. Ingawa kaka yangu mkubwa hutusaidia, inaonekana kuwa sitaweza kurudi shuleni mwakani kwa sababu siwezi kulipia chumba changu na bweni na chakula. Napenda sana shule. Nashangaa kwanini Mungu hanisaidii.”

Kila mmoja anaangalia upande wa Bwana Mulenga, wakimtegemea kujibu swali hili.

Bwana Mulenga anatabasamu na kusema, “Vile Mungu hututhibitisha tunapofanya jitihada haimaanishi kuwa maisha ni rahisi. Maisha yenu yatajaa shida, na kwa bahati mbaya, nyingi zao zitasababishwa na ukosefu wa haki. Lakini mtahitaji kushughulika kwa bidii, na hata kama kwa muda mambo yanaweza yasiwe vile ninyi mngetamani yawe, muwe na uhakika wa uthibitisho wa Mungu. Atawathibitisha hasa katika jitihada yenu ya kuondokana na dhuluma.” Anamgeukia Chishimba na anasema, “Familia yenu imeungana na ni yenye bidii. Moyo wangu unaniambia kuwa mambo yatakubadilikia. Utamaliza masomo yako. Amini maneno yangu katika hili.”

Jumatatu iliyofuata wasichana wawili walikwenda pamoja na Bi. Phiri kliniki. Muda ulipofika kwa kina mama kuanza darasa lao, Musonda na Rose wanawapeleka watoto nje na kukaa nao katika kivuli cha mti mmoja. Wanaimba nyimbo na kucheza michezo pamoja, na Rose anawasimulia hadithi. Punde hadithi ilipokwisha, kina mama wanafika kuwachukua watoto wao. Kila mmoja ni mwenye furaha. Bi. Phiri na wahudumu wengine wa afya wanafurahi kuwakaribisha wasichana kurudi juma linalofuata.

Njiani walipokuwa wanarudi nyumbani, Musonda ana mawazo mengi. Hatimae ana vunja ukimya na kumwambia Rose, “Je, unafikiri kilichotokea leo kinahusiana na ‘uthibitisho’? Wewe unataka kuwa Mwalimu na mimi nataka kuwa muuguzi, na tupo hapo katika kliniki tunafundisha na kuwaangalia watoto.”

Katika majuma ambamo Rose amekuja kukaa naye, wasichana hawa wawili wameongelea mambo mengi, na kichwa cha Musonda kimejaa mawazo. Kwa hiyo, asubuhi moja anaamua kwenda sehemu moja aliyoipenda sana. Anajilaza juu ya jabali, anakumbuka siku hiyo alipokwenda kliniki. “Lilikuwa jambo zuri

kutenda kitu kinachosaidia," anajiambia kimoyomoyo. Anakumbuka baba yake alichozoea kusema, kuwa miti lazima izae matunda. Naye anashangaa, "Nitahakikishaje kuwa maisha yangu yanazaa matunda mazuri?" Mara moja analifikiria neno "uthibitisho".

Ghafla kuna dhoruba ya upepo mkali.  Unapeperusha majani hewani. Katikati ya majani Musonda anamuona ndege mdogo wa rangi ya manjano. Upepo unapotulia, majani yote yanaanguka ndani ya maji, lakini ndege anaendelea kuruka. Anapomwangalia ndege, wazo linamjia akilini mwake. Upepo umemsukuma ndege mdogo, na sasa anaruka juu zaidi na zaidi. Labda hiyo ndiyo maana ya uthibitisho. Ndege alijitahidi kuruka na upepo ukamsaidia.

"Je, unafikiria juu ya mustakabali wako Godwin?" Musonda anauliza. "Unataka kuwa nani?"

Godwin anaendelea kuitengeneza baiskeli. "Sijui. Nataka kupata pesa, nataka kuwasaidia wazazi wetu na kuwa na familia siku moja," yeye anajibu.

"Lakini umewahi kufikiria juu ya vipaji vyako na jinsi utakavyo vitumia?" Musonda anauliza. "Rose na mimi tunaliongelea sana suala hili."

"Najua, najua!" Yeye anasema wakati akichukua spana yake. "Na wakati wote mnaongelea kuhusu 'uthibitisho'. . . 'Mungu hutusaidia tunapojitahidi'."

"Lakini Godwin, ni kweli." Halafu anamsimulia hadithi ya yule ndege wa manjano na upepo. Pia anamueleza kuhusu kazi ambayo yeye na Rose wamekuwa wakiifanya pamoja na watoto kule zahanati.

Mara Chishimba anafika. “Hallo,” anasema. “Baiskeli inaendeleaje? Umegundua tatizo?” anauliza.

“Tatizo lilikuwa kwenye gia. Bado ninalishughulikia,” Godwin alisema huku akiendelea kukaza nati.

“Nilijua kuwa ungeweza kuitengeneza!” Chishimba anasema, na kisha anamwangalia Musonda. “Unajua kuwa kaka yako ni fundi makanika?”

Rose anatoka nje ya nyumba na anasikia sehemu ya maongezi. “Godwin,” anasema, “hicho ni mojawapo ya vipaji vyako! Wewe ni hodari kutengeneza vitu. Wewe unaweza kuwa fundi makanika mzuri!”

“Kwa kuwa tu ninajua kutengeneza baiskeli,” Godwin anasema, “Haimaanishi kuwa mimi ni fundi makanika. Nitahitaji mafunzo.”

Wale wengine watatu wanatabasamu na kusema, “Kwa hiyo, jitahidi basi!” Kila mmoja anacheka, hata Godwin.

“Godwin, kwa nini usiongee na Bw. Chiyesu, fundi mwenye duka karibu na soko? Huenda akakufundisha,” anasema Chishimba kwa sauti yenye shauku.

“Ndiyo, huo unaweza kuwa mwanzo,” Rose anaongeza.

“Nini?” Godwin anauliza. “Siwezi tu kwenda pale na kumwambia namna hiyo. Kwanza mtu mwenyewe simfahamu.”

“Ninamfahamu. Naweza kukutambulisha. Tunaweza kwenda pamoja kesho,” Chishimba anasema.

Baadaye, wanapokuwa peke yao, Rose anamwambia Musonda, “kesho Godwin ataelewa maana ya uthibitisho.” Wanacheka, lakini wanaamua kutowaambia kitu chochote wavulana.

Bw. Chiyesu, ambaye ni mwanaume mfupi, wa makamo, amekaa nje ya duka lake, akisafisha vipande vya injini ndogo na anaimba lahani anavyofanya kazi. Sura yake inafurahi anapomuona Chishimba, na wanapeana mikono.

Chishimba anamtambulisha Godwin na anaeleza kuwa ni hodari wa kutengeneza vitu. Godwin ana wasiwasi, lakini anapata ujasiri wa kusema. Anasafisha koo lake na kusema, "Bw. Chiyesu, ningependa kuwa fundi makanika. Kwa hiyo nilidhani ninaweza kukusaidia hapa dukani na kujifunza kutoka kwako."

"Sawa, ninaweza kukusaidia," anajibu Bw. Chiyesu. "Lakini, sina hela ya kukulipa."

"Haijalishi. Ninapenda kujifunza tu," Godwin anasema. "Lini naweza kuanza?"

"Hakuna muda bora zaidi ya sasa!" Bw. Chiyesu anajibu. "Unaweza kubaki asubuhi hii? Vipande hivi vinahitaji kupakwa oili, na kisha tunatakiwa kuifunga injini pamoja."

"Sasa hivi? Ninaweza kuanza sasa hivi?" Godwin anauliza kwa mshangao.

"Haswa!" anacheka Bw. Chiyesu. "Kunja mikono ya shati na anza kazi!"

Godwin anaanza kazi yake mpya kwa shauku. Baada ya dakika chache Chishimba alisimama akiwa tayari kuondoka. Anamuaga Bw. Chiyesu. Anainama na kunong'oneza "uthibitisho" katika sikio la Godwin.

Wakati anarudi nyumbani, Chishimba anapitia zahanati kumuona Rose na Musonda wakiwasaidia watoto. Wasichana hawa wanapenda kujua kilichotokea. "Mambo yameendaje?" wanauliza.

"Godwin amejitahidi na amefanikiwa. yupo kule hivi sasa. Ninafikiri Bw. Chiyesu alitaka kumjaribu," Chishimba anajibu.

Asubuhi moja Chishimba anaelekea sokoni kununua samaki kwa ajili ya mama yake. Kwa siku kadhaa alikuwa anafikiria jinsi ya kujipatia fedha kwa ajili ya shule. Alifikiria kupanda zao la kuuza, lakini msimu wa upanzi ulikuwa umekwisha. Alifikiria kuuza mkaa kandokando ya barabara, lakini watu wengi walikuwa wakifanya hivyo. "Jaribu kufanya kitu ambacho hakuna mtu anayekifanya," anakumbuka kile alichosema Rose.

Anapofika kwenye meza ya Bi. Musole kununua samaki, anagundua kuwa hayupo. "Amekwenda mjini kununua samaki," anasema mwanamke wa meza ya jirani. "Yeye huenda mara mbili kila juma." Chishimba anajua kuwa pia Bw. Chiyesu huenda mjini wakati mwingine kununua vifaa vya gari.

Anapata wazo "Pengine ninaweza kujitolea kwenda mjini kwa niaba yao," anawaza moyoni mwake, "na kuwaletea vitu wanavyohitaji. Kama wao watabaki na kuendelea na kazi hawatapoteza fedha."

Usiku huo nyumbani Chishimba anashauriana na wazazi wake, na wao wanalipenda wazo hilo. Kwa hiyo siku iliyofuata anakwenda sokoni kuongea na Bi. Musole na Bw. Chiyesu. "Ikiwa ninyi wawili mtanipa fedha ambazo kwa kawaida mnazitumia kulipia nauli, mimi nitatumia nusu ya hizo kama nauli ya kwenda mjini na kuwaletea mnachohitaji. Nitahifadhi fedha inayobaki kwa ajili ya shule." Wanakubali kuwa wazo hilo lilistahili kujaribiwa na wanamwambia arudi baada ya siku mbili. "Kama wazo hili litafanya kazi vizuri," anasema Bw. Chiyesu, "basi, utakuwa umejipatia kazi!"

Wakati anarudi nyumbani kuwaambia wazazi wake habari njema, Chishimba anapitia kwa Godwin na familia yake. Ana shauku kubwa kuwataarifu mpango wake. Baada ya kusikiliza maelezo yake, Bi. Mulenga anampa Chishimba taarifa nyingine nzuri. Anamueleza kuwa Bw. Mulenga alihitajika huko Kabwe juzi na

aliongea na binamu yake huko. Alisema kuwa Chishimba anakaribishwa kuishi pamoja na yeye na familia yake, kama kilomita moja kutoka shuleni. “Na kuchangia chakula na sehemu ya kulala,” anasema Bi. Mulenga, “unaweza kuwasaidia kwa kazi za mashambani.”

“Hii ni nzuri!” anasema Chishimba. “Asante, Bi. Mulenga.”

“Chishimba,” anasema Bw. Mulenga, “Inaonekana kuwa baada ya muda mfupi tu utakuwa unajipatia pesa. Itabidi uhakikishe kuwa unaweka fedha kwa ajili ya shule, hata kama wakati mwingine itakuwa vigumu. Usishawishike kuitumia kwa vitu vidogo vidogo vya kipuuzi.”

“Usihofu, Bw. Mulenga,” anajibu Chishimba, uso wake ukiwaka kwa tabasamu. “Ninaahidi kuwa sitaruhusu hilo litokee.” Anawapungia mkono wa kwaheri, anawaangalia Rose na Musonda na kusema, “Milango inafunguka!”

Likizo zinafikia mwisho. Muda umefika wa Rose kurudi nyumbani na kuanza tena shule. Anapokuwa anajiandaa kuondoka, yeye na Musonda wanaongea.

“Natamani usingeondoka,” Musonda anasema.

“Hata mimi,” anasema Rose. “Kweli ilikuwa likizo nzuri sana. Siwezi kuamini mambo yote haya yametokea.”

“Ndiyo,” Musonda anasema. “Mtazame Godwin. Amefurahia sana kazi yake kiasi kwamba anaongelea juu ya kupata mafunzo ya kiufundi baada ya kumaliza

shule. Na wazo la Chishimba limefanikiwa vizuri kabisa. Ana wateja wengi kiasi kwamba anakwenda mjini karibu kila siku."

"Na tuangalie sisi," anasema Rose. "Kufanya kazi katika kituo cha afya tumepata uzoefu mzuri. Sasa nina hakika zaidi kuwa nataka kuwa mwalimu. Halmashauri ya kijiji changu huandaa madarasa ya kila juma kwa ajili ya watoto wa rika tofauti, na karibu watoto wote hushiriki. Mwaka huu nitajitolea kufundisha mojawapo ya madarasa hayo."

"Na mimi nitajaribu kuendelea kufanya kazi katika zahanati," Musonda anasema. "Siwezi kwenda Jumatatu tena kwa sababu ya shule, lakini labda ninaweza kusaidia siku nyingine wakati wa mchana. Unajua Rose, siku ile ya kwanza tuliongelea juu ya 'uthibitisho', nisingeweza kufikiria ni wa umuhimu kiasi gani na namna ya uelewa wa neno hilo ungebadilisha maisha yetu."

"Ni kweli," Rose anakubali. "Tazama jinsi tulivyobadilika sote kwa sababu tumejifunza juu ya kufanya jitihada na kutegemea uthibitisho."

Walipokuwa wakielekea nyumbani, Musonda anauliza kama anaweza kwenda mtoni. Anakimbilia mahala pake maalum, anapanda juu ya jabali na kulala chali, akiangalia angani. Mawazo mengi yanapita kichwani mwake. Anafikiria juu ya likizo na kujiuliza kile kitakachotokea mwaka ujao. Ni siku yenye upepo na anamkumbuka ndege wa njano. "Chochote nitakachojaribu," akajinong'oneza mwenyewe, "Mungu atanisaidia." Alipoinuka kuondoka, upepo unampuliza mgongoni na kumpa nguvu.

## SEHEMU YA 21

Kwa kawaida, kuwa na ufahamu mzuri wa maudhui ya vitabu — katika hili, *Pepo Nyanana za Uthibitisho* — na kuwa na uelewa mzuri wa jinsi vinavyojaribu kukamilisha madhumuni yao kutakuwezesha kuchukua majukumu yako kama mhuishaji wa kikundi cha vijana chipukizi kwa kujiamini. Kwa kuongezea, utahitaji kutafakari juu ya mbinu utakazotumia kusaidia kikundi katika kusoma vitabu na kunufaika kutokana na yaliyomo. Ujuzi na uwezo utakavyohitaji kwa ajili ya kusudi hili, bila shaka, vitakuzwa hatua kwa hatua kadri utakavyopata uzoefu, lakini mazoezi yafuatayo, yanahusiana hasa na *Pepo Nyanana za Uthibitisho*, yatakupatia umaizi mwingi katika suala hili:

1. Masomo yaliyomo katika kitabu hiki yanajaribu kudumisha kiwango fulani cha urahisi katika muundo na mtiririko wa sentensi. Hata hivyo, pale panapohitajika, maneno magumu na vifungu vya maneno vinatumika kwa urahisi. Masomo yanatoa maana ya maneno hayo kwa kuyaweka katika muktadha tofauti na kupitia matumizi ya mazoezi. Kwa kuruhusu misamiati mingi ya namna hii, hadithi inaepukana na mwelekeo wa kuonekana ya kitoto na ya kijuujuu. Kwa mfano, uonevu, ni dhana tata, ingawa ni neon linatumika mara nyingi katika mazungumzo ya kila siku. Katika muktadha ambamo Somo la 6 limetambulishwa na mazoezi yahusianayo yanawasaidia vijana chipukizi kupata uelewa fulani wa dhana. Je, unaona njia hii inafaa kwa ajili ya vijana mwanzoni mwa kipindi cha balehe, au unafikiri kuwa ni lazima upitie kila somo na kufafanua maneno "magumu" kwa ajili yao?

2. Masomo ya kitabu hiki yaliandikwa ili yasomwe kwa mwendo wa uchangamfu katika hali ya furaha na tafakari ya kina. Inatarajiwa kuwa vijana chipukizi watasoma hadithi na kutimiza mazoezi, yaliyotengenezwa kwa minajili ya kukuza stadi zao za lugha, na

kuimarisha uelewa wao wa maneno na dhana, mapema iwezekanavyo lakini kwa uangalifu unaohitajika. Nini kingetokea kama ungejaribu kutimiza zaidi ya lengo lililokusudiwa kwa kila somo na kusisitiza kila wazo linalotoa?

3. Kiasi cha umakini cha vijana chipukizi siyo kifupi, kama inavyofikiriwa mara nyingi. Wakati wakifurahia vitu vya kawaida vya maisha pia wanaweza kufikiri kwa kina kuhusu mawazo yanayowapa changamoto. Kama mandhari ya kikundi ni ile ya uaminifu na msaada — huru kutoka aina yoyote ya wasiwasi wa ushindani na shinikizo ya kupata matokeo fulani ambayo yameamuliwa mapema — usomaji wa masomo yaliyomo katika *Pepo Nyanana za Uthibitisho* utaibua mjadala na tafakari kwa kiwango kinachofaa kulingana na mahitaji na uwezo wa vijana chipukizi. Utachukua hatua zipi kujenga mandhari inayotakiwa?

4. Usomaji wa kitabu hautarajii "kazi ya kufanyia nyumbani". Mazoezi yanatakiwa kufanyika wakati wa mikutano ya kikundi na kujadiliwa kwa msaada wa mhuishaji. Ipo faida gani ya kufuata mbinu hii badala ya kuwaachia vijana chipukizi wafanye mazoezi kama kazi ya kufanyia nyumbani?

5. Masomo mengi katika kitabu hiki yanajumuisha shughuli ambamo vijana chipukizi wanaombwa kuandika sentensi chache, ama kuhusu sehemu ya hadithi ambayo wao wameisoma hivi punde au kuhusu wazo mahususi na matumizi yake katika maisha yao. Ungewasaidiaje vijana chipukizi katika kutekeleza aina hii ya shughuli, kuwasaidia kukuza uwezo wa kujieleza wenyewe kwa uwazi?

6. Somo la 2, 5, 9, 10, 13, na 14 ya kitabu kila moja huishia na teuzi kutoka maandiko ambalo vijana chipukizi wanahamasishwa kukariri. Itawasaidia kurejea kwenye moja au mbili ya dondoo hizo ili kuchunguza jinsi shughuli hii ya mwisho inavyoimarisha dhana kuu inayowasilishwa katika masomo.

7. Kwa kuongezea kwenye dhima kuu, kitabu kinagusa juu ya dhana nyingi za kimaadili na hujaribu kutilia mkazo juu ya sifa stahiki na mielekeo. Rose, kwa mfano, anagawana chakula chake na mtoto ndani ya basi. Godwin na Chishimba wanamsaidia mwanamke kumbebea kuni. Rose na Musonda wanafundisha watoto wakati mama zao wanahudhuria madarasa juu ya lishe kwenye zahanati. Mchezo wa mpira wa miguu ni tukio la kirafiki ambamo "ushindi" siyo kusudi. Mawazo haya yanatakiwa kupewa umakini wa kiasi gani? Je, kila kipengele kinahitaji kuainishwa na kufikiriwa kwa undani? Au, inatosha kuviruhusu vijitokeze kiasilia wakati wa majadiliano?

8. Hadithi inakunjuka katika kijiji kimoja cha Kiafrika. Vitabu vinavyounda sehemu ya programu ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi huonesha uhalisia katika idadi fulani ya mandhari za kitamaduni na za kijamii katika mabara mbalimbali. Hii inaongezea kwenye utajiri wa programu. Baadhi wanaweza kupendekeza kuwa ipo haja ya "kuvitumia vitabu kwa uhalisia wa vijana katika kila nchi" kwa mfano, kwa kubadilisha majina ya wahusika katika hadithi. Walakini watu wamesoma vitabu kutoka tamaduni nyingine tofauti na zile zao kwa kipindi cha karne nyingi, wamevifurahia na kujifunza kutoka humo. Bila shaka, wamefanya hivyo kwa ufahamu kabisa. Utawawezeshaje vijana chipukizi kutambua sura hii ya programu? Ni yapi

mawazo yako juu ya imani walionayo baadhi kwamba watoto na vijana hujifunza tu kutoka nyenzo zilizoandikwa katika muktadha wa utamaduni wao wenyewe?

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

## SEHEMU YA 22

*Roho ya Imani*, kama tulivyotanabahi hapo awali, ni mojawapo kati ya vitabu kadhaa ambavyo huleta maudhui kwa ajili ya uendelezaji wa Madarasa ya watoto ya Kibahá'í na ambamo marejeo dhahiri yanafanywa kwa Wakuu wa Imani. Tumetaja hapo awali kwamba kipindi cha balehe ni hatua katika maisha ambamo mtu binafsi anapenda sana kuchunguza maswali ya asili ya kifalsafa, haswa yale yanayohusu kusudi na asili ya mwanadamu. *Roho ya Imani* inaanza kwa kuuliza swali, "Nini maana ya kuwa binadamu?" Katika kujaribu kujibu swali hili, masomo kadhaa ya kitabu huchunguza mlolongo wa mawazo husika: ubora wa mwanadamu; asili ya juu na ya chini ya mwanadamu; kutokuwepo kwa uovu; asili ya utashi; hiari na hatima; uwezo wa kiakili; wa uchunguzi wa kisayansi; mabadiliko ya kimwili; roho ya mtu; na, hatimaye, roho ya Imani.

Kama ilivyokuwa katika kitabu cha *Pepo Nyanana za Uthibitisho*, mnahitaji kupitia kitabu mara moja na tena kukisoma tena kwa umakini zaidi, awamu hii utaweka umakini mahususi kwenye sehemu zinazorejewa kama "tafakari". Baada ya kufanya hivyo, unatakiwa kuchambua jinsi kitabu kinavyoonesha kufikia lengo lake, kwa kujibu maswali yafuatayo:

1. Mateuzi kadhaa kutoka maandiko ya Bahá'u'lláh yamenukuliwa katika Somo la 1 ambayo yana taswira ambazo zinaweza kuwasaidia vijana chipukizi kufikiri kuhusu utambulisho wao wa kweli. Ni umaizi gani kila taswira inautoa katika uhusiano huu? Ni kwa namna gani tafakari zilizomo katika somo zinaongeza uelewa wao wa mada?

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

2. Vijana chipukizi wanathaminije muumbo wa Mungu na ubora wa mwanadamu kutoka sehemu ya kwanza ya Somo la 2? ______________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

3. Tafakari ya kwanza ya somo hilo inawasaidiaje kuona utumiaji wa dhana ya ubora katika maisha yao? ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

4. Katika sehemu inayofuata ya somo wanafikiri kuhusu kile ambacho kina wasababisha watu kujishusha wenyewe. Ni kitu gani? ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

5. Ni uelewa gani unatumaini kijana chipukizi angeupata kutoka usomaji huu mfupi wa asili ya juu na ya chini ya binadamu? ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

6. Vijana chipukizi wanajifunza nini kuhusu maendeleo ya asili yao ya juu kupitia tafakari ya pili ya somo? ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

7. Inawasaidiaje vijana chipukizi kutambua kuwa asili ya chini ya binadamu siyo uovu ili wasijihisi wenye hatia kila wafanyapo kosa? Mifano ipi inatumika kusaidia kuongeza kina cha uelewa wao wa mada? ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

8. Umaizi upi unapatikana kutoka sehemu inayofuata ya Somo la 2, hasa tafakari mbili za mwisho, juu ya namna ya kudhibiti tamaa za asili ya chini? ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

9. Dhana ya utashi limeshughulikiwaje katika Somo la 3? Unadhani hali iliyoelezwa mwanzoni mwa somo ina uwiano katika maisha ya vijana? ______________________________

______________________________

______________________________

10. Vijana chipukizi wanajifunza nini katika Somo la 3 kuhusu nafasi ya hiyari katika maendeleo ya asili yao ya juu?

11. Katika maeneo gani ya maisha yao vijana chipukizi wataelewa kuwa wanaweza kutumia hiyari? Kwanini ni muhimu kwao kujua mipaka ya hiyari yao?

12. Umaizi upi zaidi wanaoupata katika matumizi ya hiyari yao kutoka tafakari ya pili katika somo?

13. Kwa nini ni muhimu kwa vijana chipukizi kuona tofauti kati ya kuwadhibiti wengine na kutumia ushawishi chanya? Unafikiri majadiliano yanayofanywa katika tafakari ya tatu huwasaidiaje vijana chipukizi katika jitihada zao za kutumia ushawishi chanya juu ya mazingira yao?

14. Somo la 3 linawafundisha nini vijana chipukizi kuhusu dhana ya hatima?

15. Somo linajaribu kuondoa dhana gani potofu kuhusu asili ya hatima?

16. Ni ya kufaa kiasi gani sitiari ya mtumbwi katika kuwasaidia vijana chipukizi kupata mtazamo unaofaa juu ya thamani ya juhudi zao wenyewe na nguvu za msaada mtakatifu katika maisha yao?

17. Ni kwa njia gani sehemu ya kwanza ya somo la nne husaidia vijana chipukizi kugundua mipaka ya asili? ____________________

18. Somo linasemaje kuhusu jinsi wanadamu wanavyoweza kuishinda mipaka hii? ____

19. Hoja inawasilishwa kwenye somo kwamba sayansi ni mali ya jamii yote ya wanadamu. Hoja hii ni ipi? ____________________

20. Katika fungu linalohusu sayansi lililonukuliwa katika Somo la 4, lipo tamko linalosema, au ameweka upendo huu wa uhalisia ndani ya mwanadamu.” Ni muhimu kiasi gani kulea upendo huu wa uhalisia katika vijana chipukizi?________________

21. Uwezo wa kuchunguza umeelezwaje kwa vijana chipukizi?____________________

22. Mfano uliotolewa kwenye Somo la 4 unawasaidiaje vijana chipukizi katika kuthamini nafasi ya uchunguzi na kufanya majaribio katika maendeleo ya sayansi?__________

23. Je, somo linamaanisha kuwa wao wanaweza kutumia uwezo wao wa kuchunguza katika kila sura ya maisha? Unafikiri kwa nini maswali yaliyoulizwa katika tafakari ya

tatu, ambayo yanawahamasisha kutumia uwezo huu, yote yanailenga asili ya juu ya mwanadamu? ____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

24. Mifano iliyotolewa katika tafakari ya nne inaashiria kuwa ufanyaji majaribio hauwezi kutumika katika kila nyanja ya maisha. Inawasaidiaje vijana chipukizi kuthamini umuhimu wa kanuni hii? ____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

25. Mifano tofauti iliotumika kwenye Somo la 5 na 6 inawasaidiaje vijana chipukizi kupata umaizi katika nadharia tata sana za mabadiliko endelevu ya viumbe? ____________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

26. Uonekanaji wa roho ya mtu unaelezwaje katika mchakato huu wa mabadiliko endelevu? ____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

27. Katika Somo la 6 mhuishaji, Natalia Petrovna, anasoma mateuzi mawili kutoka maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá kwa kikundi cha vijana chipukizi kwenye hadithi na kuwasaidia kusoma na kuyaelewa. Hakuna dalili ya jinsi anavyofanya hivyo. Ungefanyaje kuelezea mateuzi haya?________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

28. Ni zipi sifa bainifu za roho ya mwanadamu kama ilivyoelezwa katika sehemu ya kwanza ya Somo la 7? ____________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

29. Ni jinsi gani ufahamu umetambulishwa katika tafakari ya kwanza ya somo hilo? Mazoezi mawili katika tafakari yana uwiano gani na maisha ya vijana chipukizi?

30. Uwezo wa akili ya watu unakuwaje chombo cha asili ya juu? Je, uwasilishwaji wa ukinzani, kama ilivyofanyika kwenye tafakari ya pili, ni njia inayofaa ya kutilia mkazo juu ya umuhimu wa kuongoza akili ya mtu?

31. Roho ya Imani ni nini?

32. Tafakari mbili za mwisho za Somo la 7 zinawasaidiaje vijana chipukizi kuona matumizi ya roho ya imani katika maisha yao?

## SEHEMU YA 23

Kwenye moyo wa kitabu cha *Roho ya Imani* kuna kanuni ya upatano kati ya sayansi na dini. Matokeo ya kanuni hii kwa ajili ya maisha ya jamii ya wanadamu ni ya kina na sisi tunapaswa kila mmoja wetu, kujitahidi kupata umaizi mpya katika utendaji wake. Bila shaka, ipo baadhi ya mitazamo kati ya dini na sayansi, ambayo ingawa haipingani kwa uwazi, ni dhahiri kuwa haikidhi mahitaji ya uhusiano wenye upatano kati yao kwa mfano, dai la kuwa mafumbo yoyote yale yanayoelezwa na dini leo, siku moja yataelezwa na sayansi kadiri inavyoendelea kukuwa, au kwa upande mwingine, imani kwamba ukweli wote wa kisanyansi mwishowe utavumbulika kwa kusoma vitabu vya dini kwa kuwa vinatoka kwa Mungu Ajuaye yote. Bila kuingia katika dhana potofu zilizopo nyuma ya kila mtazamo, sisi kwa urahisi kabisa tunaweza kuona kuwa, katika zote mbili, chanzo kimoja cha ujuzi kinawekwa chini ya kingine, kitu ambacho hakiwezi kuitwa upatano wa kweli. Lakini hata kama mitazamo hii ingekataliwa, tunahitaji kujiuliza wenyewe tunawezaje kuona kuwa sayansi na dini vinakamilishana. Kwa mwangaza huu tamko lililopo hapa chini limeletwa kwenu kwa ajili ya tafakari yenu. Lisomeni na kisha kamilisheni mazoezi yanayofuata.

> *Uwezekano mmoja ni kusema kuwa kweli zilizomo katika sayansi na dini zinafunika maeneo mawili tofauti na ya kipekee ya uzoefu. Sayansi huchunguza ulimwengu wa kimwili, siyo tu jinsi asili inavyofanya kazi, bali pia matukio fulani yanayohusiana na jumuiya za wanadamu, mashirika, na miingiliano. Ujuzi uunaopatikana unakuwa msingi wa maendeleo ya kiteknolojia, na teknolojia inaweza kutumika ama kwa*

*mema ya jamii ya watu au ya kuiangamiza, Haijalishi sayansi ya kijamii imeendelea kiasi gani, sayansi yenyewe haina uwezo wa kujitosheleza kuamua jinsi matumizi ya bidhaa zake yanavyopaswa kuwa. Dini, kwa upande mwingine, inahusika hasa na sura ya kiroho ya uwepo wa mwanadamu. Kazi yake ni kuangaza maisha ya ndani ya mtu binafsi, kugusa mizizi ya motisha, kuunda utaratibu wa kanuni na maadili ambayo yanafaa kuongoza tabia za mwanadamu. Mchakato wa kuleta ustaarabu unategemea juu ya mifumo yote miwili ya ujuzi; hadi hapo kila kimoja kinavyobaki ndani ya eneo la akili maalumu, hakuna sababu ya kwazo kufikia migogoro moja kwa nyingine.*

*Mtazamo huu wa upatano kati ya sayansi na dini ni halali, lakini zaidi katika kiwango cha utekelezaji. Hatimaye, katika njia hii, sayansi na dini vinatenganishwa na kuachiwa kufuata njia zao zenyewe,na kile kinachochukua umuhimu ni mwingiliano kati ya teknolojia na maadili. Lakini uchambuzi wa namna hii wa uhusiano kati ya sayansi na dini punde hufikia mipaka yake kwani kwa hakika, kuna matukio mengi ambayo yote mawili yanajaribu kuelewa na kueleza. Wakati hali hii siyo wazi sana katika uhusiano wa asili, ni wazi katika usomaji wa binadamu na jamii. Aidha, kuna mambo mengi yanayofanana kati ya sayansi na dini kwa jinsi zinavyouendea uhalisia. Kwa mfano, zote mbili zinaamini uwepo wa mpangilio katika muumbo na kuamini kwamba, angalau kwa kiasi fulani, akili ya mwanadamu ina uwezo wa kuelewa mpangilio huu. Mbinu za kisayansi zimethibitisha kuwa zinafaa sana katika kugundua jinsi muumbo unavyofanya kazi. Lakini inabidi pia dini itumie njia hizi wakati inajitahidi kuwaongoza wanadamu kuchangia katika ustaarabu uendeleao daima. Sayansi na dini havifanani, lakini vina mambo mengi yanayofanana yanayoviwezesha kuongea pamoja, kuwa na upatano, kuathiriana na kukamilishana moja kwa nyingine na mbinu zinazotumika.*

1. Uhusiano kati ya sayansi na dini ulioelezwa katika tamko lililopo hapo juu unatazamia maeneo ya ujuzi ambayo vyote sayansi na dini zinaufanyia uchunguzi. Miongoni mwa masuala haya yanayohusu uwezo wa akili ya binadamu, ukuaji endelevu wa spishi ya mwanadamu, na maendeleo ya kiakili na maadili. Jadilini jinsi gani, katika kushughulikia masuala kama hayo, *Roho ya Imani* kinaheshimu uhalali wa sayansi na wakati huohuo kinaruhusu mwangaza wa dini kuuangazia uelewa.

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

2. Kanuni ya upatano kati ya sayansi na dini inamaanisha kwamba, pale itakapofaa, nyenzo za kielimu zinaweza kuhusisha dhana za kiroho na za kisayansi, bila shaka katika njia ambayo inaepukana na mambo ya kijuujuu na ambayo siyo ya kiholela. Ushirikiano kama huo wa ujuzi unakuza uelewa na unaondoa mkanganyiko wa uwili wa uwongo. Chunguza jinsi *Roho ya Imani* inavyofanikisha kiasi hiki cha mwingiliano. Unaweza kurejea hasa kwenye tafakari za Somo la 5 na la 6.

3. Pengine ungependa kuchunguza tena *Roho ya Imani* na kuamua kiasi ambacho kinasababisha mielekeo fulani ambayo ni ya lazima kwa ajili ya yule ambaye anataka kuwa mtafutaji wa ukweli na mchunguzi wa uhalisia. Ni ipi baadhi ya mielekeo hii, na ni kwa ufanisi gani nyenzo imeichunguza?

## SEHEMU YA 24

Tutamalizia hapa majadiliano ambayo tuliyaanza katika Sehemu ya 3 kuhusu vitabu vilivyosomwa katika programu ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi. Uchambuzi wa kina tuliofanya wa *Pepo Nyanana za Uthibitisho* na *Roho ya Imani* unatupa dalili ya kiwango cha uzoefu wako unaohitaji kufikia pamoja na kila moja ya vitabu katika program. Katika kozi zinazochepuka kutoka Kitabu cha 5, sisi tutaingia katika majadiliano kama hayo ya vitabu vingine, ambayo yatawasaidia katika muunganiko huu; hata hivyo, mbali na mafunzo kama hayo, unapaswa kutenga muda wa kutosha kusoma vitabu na kuchunguza jinsi vinavyojitahidi kutekeleza malengo yao. Mikutano ya mara kwa mara ya tafakari pamoja na wengine ambao wanaohudumu kama wahuishaji itawapa baadhi ya fursa zenye tija kabisa kwa ajili kuimarisha uelewa wenu wa nyenzo hizi. Wewe na wahuishaji wenzako mtakuta, katika matukio kama hayo, shehena ya tajiriba za wengi ambamo unaweza kuchota. Kwani, katika uchambuzi wa mwisho, ni katika uumbaji tu wa mandhari ya usaidizi na msaada wa pamoja, ambapo kujidhatiti kwa ujifunzaji hupata kujieleza kupitia hiari ya kuambatana na wengine katika jitihada zao, ili uwezo uliyomo ndani ya vitabu uweze kuchunguzwa kikamilifu na hatimaye kutambuliwa.

## SEHEMU YA 25

Ilitajwa hapo awali katika kitengo hiki kwamba, zaidi ya usomaji wa nyenzo, vijana chipukizi hushiriki katika shughuli za huduma, michezo, na aina tofauti za sanaa na stadi za mikono hususan zile za utamaduni wa maeneo yao. Katika kitengo cha pili cha kitabu hiki,

ulikuwa na fursa ya kufikiria, kwa kiasi fulani, athari ya mazingira ya kijamii juu ya vijana, na ulitahadharishwa haswa ya baadhi ya athari zake zenye madhara, Mkazo uliotiliwa juu ya hali inayozidi kuwa mbaya ya jamii ya leo haupaswi kuruhusiwa, hata hivyo, kugubika ukweli kwamba vipo vipengele vingi katika kila mazingira ambavyo, kama vikitumika vyema, vinaweza kukuza uwezo wa kujieleza, uwezo wa kuchambua michakato ya kijamii, na utayari wa kuihudumia jamii. Makala yafuatayo ya gazeti yanatusimulia hadithi ambayo inatuonesha vizuri jinsi vyombo vya habari, kwa mfano, vinaweza kutumika katika kuendeleza ustawi wa jamii:

> Sauti ya Wasio na Sauti
>
> Katika Afrika Magharibi radio ya transista ingali inaongea kwa niaba ya jumuiya.
>
> Wakiwa wamejikusanya kukizungukia kinasa sauti katika studio ndogo ya stesheni ya radio ya kijiji cha Nzérékoré katika msitu wa jimbo la Guinea, vijana watatu wanajadili elimu ya wasichana.
>
> "Wasichana sharti waende shule, kwa sababu watakuwa mama siku moja, na kama wakielimika, watawaelimisha watoto wao wenyewe na wataweza kuwalea vizuri zaidi," Moriko Kaké anasema. "Unapomwelimisha msichana, unaelimisha taifa zima," yeye anaongeza kwa mkazo. Lancei Touré, mkaribishaji wa programu hii mwenye miaka kumi na sita, anatingisha kichwa kwa kukubali, ingawa wazazi wake wanataka aache shule ili aanze kazi mashambani.
>
> Maongezi wazi na fasaha ya vijana, yanarushwa mubashara kwa vijiji jirani vya mipaka ya Liberia na Ivory Coast. Ni jioni, na chemli za mafuta ya taa zinametameta ndani ya vibanda vya udongo. Wanakijiji wamerudi kutoka mashambani au sokoni. Wote wanasikiliza radio wanapokuwa wanapika chakula cha jioni na kujiandaa kwa ajili ya usiku. . . .
>
> Katika nchi kama Guinea — ambamo sehemu kubwa ya watu wazima hawajasoma, watoto wengi hawana fursa ya kwenda shule na umeme ni nadra — vituo vya radio ya kijiji vinavyoendeshwa kwa jenereta ni kiungo muhimu cha kuokoa maisha katika jumuiya.
>
> "Radio ni kila kitu hapa," anasema Gnouma Camara, mkurugenzi wa vipindi katika kituo cha radio cha kijiji cha Nzérékoré, ambacho hutangaza siku sita kwa juma katika moja ya lugha tano za mkoa na kwa lugha ya Kifaransa ndani ya kipenyo cha kilometa100. Familia mbili kati ya tatu za mkoa zina miliki transista, na pale ambapo kituo kinapotangaza asubuhi mapema na jioni, kijiji kizima husikiliza.
>
> "Tunaongea lugha yao, tunajua tamaduni na mila zao, tunafikisha jumbe zao, tunatangaza vizazi na vifo, tunajadili ukulima na masuala ya kilimo, na matatizo ya jumuiya," Camara anaongeza. "Sisi ni sauti ya jumuiya. Sauti ya wasio na sauti." . . .
>
> "Mimi ninasikiliza vipindi kwa sababu vinawasilishwa na watoto na kwa sababu huongea kwa lugha yangu mwenyewe," anasema Mamadou Malic, kijana mwenye umri wa miaka kumi na tano katika lugha yake asili ya Kipular. . . . "Vipindi vinapoanza, ninawaita kaka zangu na dada zangu wote ili tusikilize pamoja. Ninajifunza mengi kwa njia hiyo."

> “Wazazi na viongozi wa jumuiya wanasikiliza pia,” Camara anasema. “Katika tamaduni zetu, watoto mara nyingi hawasikilizwi, lakini sasa watu wazima wanaanza kuwasikiliza. Watoto huwashauri wazazi umuhimu wa usafi, kwa mfano. . . . Kama baba akimpiga mtoto, majirani zake sasa wanasema: ‘Husikilizi radio?’”

Hadithi hii inaashiria kwa njia moja tu miongoni mwa njia lukuki ambamo kutoka humo vinaweza kuchotwa vipengele tofauti vya mazingira ya kijamii vya kuongoza vipawa na uwezo wa vijana kuelekea kutoa huduma kwa jumuiya zao. Muziki, vyombo vya habari, na teknolojia vinaathiri maisha ya vijana zaidi na zaidi katika kila sehemu ya dunia. Kama mhuishaji, utahitaji kuendelea kutambua vipengele hivi vyenye uwezo na kujifunza kusaidia vijana chipukizi kuvitumia kujenga shughuli zinazofaa. Fikiria kuhusu mazingira yako mwenyewe ya kijamii. Ni uwezekano gani unafunguliwa kwa vijana chipukizi kufanya kazi pamoja na mawazo yafuatayo? Jadilini mawazo yako katika kundi lako, na andika baadhi ya mawazo yako katika nafasi iliyotolewa.

Muziki: ____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

Vyombo vya habari: ____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

Teknolojia: ____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

## SEHEMU YA 26

Kama vijana chipukizi wanatakiwa kuwezeshwa kusimamia maendeleo yao wenyewe na kuchangia kwenye maendeleo ya jumuiya zao, wanahitaji kushiriki siyo tu katika utekelezaji wa shughuli zenye maana kama kikundi lakini pia katika uundaji wake. Kuongezea kwenye miradi ya huduma, na sanaa na stadi za mikono, shughuli kama hizo, kwa mfano zinaweza

kujumuisha, matukio maalumu ya kusherehekea umalizaji wa kitabu kimoja au kingine, ambamo vijana chipukizi huwasilisha maigizo, kuimba, kutongoa mashahiri, na kutoa hotuba. Daima utapendelea sana kujadili na wahuishaji wengine jinsi unavyoweza kuwahamasisha marafiki vijana kuandaa na kutekeleza shughuli ambazo hufunza vipawa vyao vya kiakili na kiroho, zinawasaidia kueleza katika mazoezi baadhi ya dhana kupitia huduma, na kuimarisha juhudi zao za kujitahidi kuelekea ubora. Aina ya maswali ambayo utahitaji kufikiria pamoja na wahuishaji wenzako ni pamoja na yafuatayo: Je, unawasaidiaje vijana chipukizi kubuni na kutekeleza mradi wa huduma na kutafakari juu ya jinsi unavyokunjuka? Unawasaidiaje vijana chipukizi kuandika muswada na kuigiza maigizo rahisi? Utahakikishaje kuwa michezo ya kitoto haiwasilishwi kama mbadala wa sanaa na stadi za mikono na kwamba vijana wanasaidiwa kupata thamani ya kweli ya "sanaa, stadi za mikono na sayansi" ambazo "huuinua ulimwengu wa uwepo, na hufaa kwenye utukuzaji wake"?

Ingawa huu siyo muda wa kuingia katika majadiliano ya shughuli ya kisanii, ni muhimu kwako kutambua kuwa shughuli kama hiyo, ni kielelezo cha utamaduni, hubeba thamani yake. Hivyo, kwa asili yake yenyewe, inaweza kushawishi mchakato wa kielimu zaidi. Kama mhuishaji wa kikundi cha vijana chipukizi, utapenda kuchukua tahadhari ya kuwasaidia rafiki zako vijana kubaini shughuli za kisanii zinazofaa, zile ambazo haziishi bila kukusudia zinazowalazimisha tabia ambazo zinaenda kinyume, kwa njia za kichinichini, na mchakato wa kielimu ambamo wao wanajihusisha.

## SEHEMU YA 27

Tajiriba inaonesha kuwa kikundi cha vijana chipukizi kilichoundwa na wajumbe kumi hadi kumi na tano aghalabu huanza na wajumbe wachache tu ambao wameonesha uwezo wa kukusanya marafiki zao katika hoja stahiki. Ambapo vijana hawa wanahamasishwa kuungana, wao wataanza kukutana kila mara pamoja na mhuishaji. Ushiriki katika kikundi unaweza kuimarishwa kwa msaada kutoka kwa kiini kinachoendelea kupanuka cha marafiki wanaofanya kazi katika ujirani au kijiji, hususan vijana wenye umri kati ya miaka 16 hadi 19, ambao wanaendelea katika masomo ya vitabu vichache vya kozi za mwanzo za Taasisi. Katika sehemu fulani za ulimwengu, kuwakaribisha wajumbe vijana wa kijiji au ujirani kwenye mlolongo wa matukio kabla ya ustawishaji wa vikundi rasmi umethibitika kuwa njia yenye ufanisi Njia nyingine ni kutambulisha programu shuleni. Pale shule inapoonesha upokevu kwenye wazo, na uwasilishaji mmoja au zaidi kwa wanafunzi na walimu wa madaraja husika kwa kawaida una matokeo ya uundaji wa vikundi kadhaa vya vijana chipukizi. Halafu, wanaweza, kuichukulia program kama shughuli ya ziada, iwe wanakutana kwenye majengo ya shule au la. Shule, kwa vyovyote hutambua mchango wa thamani wa programu kwa maendeleo thabiti ya maadili na uwezo wakiakili kwa wanafunzi wake.

Fikiria kuhusu hali yako mwenyewe na eleza baadhi ya mbinu ambazo ungeweza kutumia, kama mhuishaji mwenye shauku, kwenye kusaidia kuunda kikundi cha vijana chipukizi.

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

## SEHEMU YA 28

Hitaji muhimu la kudumisha kikundi hai cha vijana chipukizi ni ujenzi wa uhusiano wa uaminifu na urafiki pamoja na wazazi. Wahuishaji wanahitaji kuwatembelea wazazi ama kabla au mara baada ya kuunda vikundi na kuwaeleza kusudi la program. Wanapaswa kuendelea kutembelea kila kaya mara kwa mara na kujadiliana na wajumbe wake matarajio na uwezo uliomo ndani ya vijana chipukizi — mada zilizoandikwa katika kitengo cha tatu cha Kitabu cha 2, lakini zinachunguzwa kwa tondoti nyingi zaidi hapa. Ziara kama hizi pia zinaweza kutoa fursa ya kushauriana pamoja na wazazi kuhusu ustawi na maendeleo ya watoto wao wa kiume na wa kike. Aghalabu, kama inavyoshauriwa katika Kitabu cha 2, wahuishaji wanawaonesha wazazi kitabu kimoja au vitabu viwili vinavyosomwa katika program, ili wao waweze kuona kile ambacho vijana wao wanajifunza. Ingawa kila mhuishaji atahitaji kujenga mafundo ya urafiki pamoja na wazazi katika kipindi cha miezi kadhaa, yeye anaweza kuambatana na mtu mwenye uzoefu zaidi katika ziara zake chache za mwanzoni**.**

Wewe unahamasishwa kugeukia kwenye Sehemu ya 14 ya kitengo cha tatu cha Kitabu cha 2, kwa ajili ya kujikumbusha dhana zinazounda msingi wa maongezi endelevu pamoja na wazazi wa vijana waliomo katika program ya uwezeshaji wa kiroho. Kisha pamoja na washiriki wengine wa kozi, jadili tajiriba uliyoipata katika kijiji au ujirani wako wakati wa kuzitembelea familia za vijana chipukizi. Mawazo gani ya nyongeza kutoka usomaji wa kitabu hiki ambayo yangeweza kutajirisha maongezi wakati wa ziara?

## SEHEMU YA 29

Mazungumzo ambayo mhuishaji huanzisha miongoni mwa kikundi cha vijana chipukizi hapo mwanzoni, yanaweza kuwa yenye umuhimu maalum. Sharti katika mikutano mitatu au minne ya mwanzo, wajumbe waongelee kusudi la kundi na wabaini malengo machache ambayo wangependa kufanikisha kwa pamoja. Pia wanapaswa wafikie baadhi ya maamuzi kuhusu aina ya shughuli wanazopenda kufanya. Mada zinazoongelewa katika mikutano hii inaweza kuwa tofauti kutoka kikundi kimoja hadi kingine. Walakini zipo dhana fulani kama vile “ubora” na “huduma”, ambazo lazima zitiliwe mkazo zaidi katika mikutano yote kama hiyo. Vipengele vilivyopo hapa chini pengine vitakusaidia, basi, kupanga maongezi yako machache ya mwanzo ambayo utafanya na wajumbe wa vikundi ambavyo ulisaidia kuviunda. Wewe unapaswa kuchunguza kila kipengele kwa umakini. Pamoja na washiriki wengine katika kozi hii, na andika baadhi ya mawazo yako ya mwanzo kuhusu jinsi utakavyoanzisha majadiliano na kikundi cha vijana chipukizi, ambao unatarajia kushughulika nao hivi punde.

- Wahuishaji wengi wanaona kuwa ni msaada mkubwa kuwahamasisha vijana chipukizi kukiona kikundi kama nafasi ambamo wao wanaweza kutarajia kupata ubora wa kiroho na wa kiakili. Kujitahidi kupata ubora wa kiroho, wao wanaeleza, sisi tunahitaji kukuza sifa ambazo ni sehemu ya asili yetu ya juu, kama vile upendo, ukarimu, ukweli, na unyenyekevu. Kujitahidi kupata ubora wa kiakili, sisi tunatakiwa kupata ujuzi na stadi za kivitendo ambazo zitatusaidia kuboresha maisha yetu, na maisha ya wengine. Kwa kutafakari juu ya dondoo kama hizi “Acha kila asubuhi iwe nzuri zaidi kuliko jioni yake na kila kesho iwe tajiri zaidi kuliko jana yake,” na kuzikumbuka akilini aghalabu husaidia uelewa wa dhana ya ubora.

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

- Baada ya kupata uwazi fulani kuhusu kusudi la kikundi, wajumbe wake wanaweza kusaidiwa na mhuishaji kuamua ni shughuli zipi — za kiakili, za kimichezo, na kitamaduni — ambazo wao wangependa kufuata katika utafiti wa ubora.

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

- Katika uhusiano na ubora wa kiakili na kiroho, suala la lugha, ambayo imeungana kwa karibu na ruwaza za fikra, litahitaji kuongelewa kwa kirefu kiasi. Katika maongezi juu ya mada hii pamoja na vijana chipukizi, kwa kawaida inatosha kueleza kuwa, kwa minajili ya kupata viwango vya juu zaidi na zaidi vya ubora, sisi lazima tukuze uwezo wetu wa kujieleza. Sisi tunatakiwa tuweze kusoma na kuelewa, tunapaswa kujifunza kueleza mawazo yetu kwa uwazi. Ni katika muktadha huu ambao wahuishaji aghalabu huona kuwa unafaa kwa ajili ya kutambulisha vitabu ambavyo vijana chipukizi watasoma, ambavyo baadhi yao umevichunguza, kwa ujumla au kwa sehemu, mapema katika kitengo hiki.

- Kukariri vifungu kutoka katika maandiko lazima upewe umuhimu stahiki katika program kwa ajili ya uwezeshwaji wa kiroho wa vijana chipukizi. Suala la kukariri, kwa hiyo linapaswa kuwa mada ya mazungumzo katika mojawapo ya mikutano ya kikundi ya awali. Wahuishaji wanapaswa wawasaidie rafiki zao vijana kutambua uwezo wa kipekee wa Neno la Mungu na athari zake juu ya maisha yao, kadiri wanavyojitahidi kupata ubora. Kupitia majadiliano kama haya wao wataweza kutambua faida za kujua vifungu vingi kutoka katika maandiko, kimoyomoyo.

- Inawasaidia wahuishaji kutilia mkazo katika mikutano ya mwanzo kwamba, ili kikundi kiweze kujitahidi kupata ubora wa kiroho, wajumbe wake wanahitaji kukuza mafundo yenye nguvu ya urafiki na kufanikisha umoja mkubwa zaidi na zaidi. Wahuishaji aghalabu huona kuwa inafaa kwa ajili ya kuwasaidia vijana chipukizi kuchunguza

mada za urafiki, umoja, na upatano katika mwanga wa dondoo kutoka maandiko, ambayo wanaweza kuhamasishwa kukariri.

- Majadiliano juu ya mada za urafiki na umoja yanaweza kutoa fursa ya kawaida kwa ajili ya maongezi kuhusu jinsi wajumbe wa kikundi wanavyofanya kazi pamoja kati yao. Kwamba mmoja anaweza kumsikiliza mwingine kwa uangalifu; kwamba daima watajitahidi kuelewana, hata kama wakati mwingine ni vigumu kueleza mawazo walionayo, kwamba kamwe hawatabeza mawazo ya mtu mwingine — hii ndio mifano ya baadhi ya maamuzi wanayoweza kuyafikia kama kikundi katika mazungumzo kama hayo.

- Huduma ni mada muhimu haswa ambayo inahitaji kujadiliwa katika mojawapo ya mikutano ya awali ya kikundi. Vijana chipukizi wanaweza kukumbushwa kuwa, kama wanadamu, sisi sote tunategemeana. Sisi sote ni wajumbe wa familia moja ya wanadamu na sharti tujitahidi kadiri tuwezavyo kuboresha hali ya jumuiya yetu. Kufikiria ingekuwaje kama tusingepokea msaada wowote kutoka wale waaotuzunguka, wakati mwingine inaweza kuwasaidia vijana chipukizi kutambua umuhimu wa huduma.

- Majadiliano juu ya huduma yanapaswa kwenda mbele zaidi ya suala la jitihada za mtu binafsi za kuwahudumia wengine na kufikiria kile ambacho vijana chipukizi wanaweza kufanya kama kikundi. Bila shaka, ni muhimu kwamba jitihada zao za mwanzo ziwe za vipindi vifupi, vyenye malengo yanayoweza kupatikana kwa urahisi. Kwa jinsi hii, wao wataweza kuwa na imani katika uwezo wao wa pamoja na watajifunza kufanya kazi pamoja, wakifungua fursa kwa ajili yao za kufanya miradi migumu na iliyosarifiwa. Tangu mwanzoni, wahuishaji wanapaswa kuwaongoza vijana kuanzisha mchakato ambamo wao wanayafikiria maisha ya jumuiya zao na jinsi wanavyoweza kuchangia katika uboreshaji wake. Wakiulizwa maswali ambayo yanawalazimisha kutoa maoni kuhusu jumuiya, itawasaidia katika suala hili. Hivyo, wao wangeweza kuanza kufanya vitendo vya huduma kama kuwatembelea wagonjwa katika jumuiya na polepole waweze kufanya mradi fulani — kwa mfano wa kupanda miti — mradi ambao utawalazimu kushauriana na mashirika husika ya eneo, kutafuta msaada kutoka kwa marafiki na wazazi, na kufanya mipango ya muda mrefu. Ni kawaida kwamba katika mikutano michache ya mwanzo ya kikundi, baadhi ya stadi na vipaji na sifa zinazohitajika kwa ajili ya ushirikiano unaofaa vinaongelewa.

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

- Burudani maridhawa, hususan michezo, ni mada nyingine inayoweza kuongelewa katika mikutano ya mwanzo ya kikundi cha vijana chipukizi. Kwa mara nyingine tena, kuongeza kwa uchunguzi wa dhana na vipengele husika, wahuishaji watataka kukisaidia kikundi kubaini aina ya shughuli za burudani ambazo zinaweza kufanywa ama wakati wa mkutano au wakati mwingine maalum. Neno moja la tahadhari linahitajika hapa. Shughuli shadidi za kimwili ni uelezaji wa kawaida wa nguvu walizonazo vijana chipukizi. Tajiriba ya duniani kote imeweka wazi kwamba, kupendelea shughuli za kisanii kuliko michezo, katika kikundi, ni mwanzo wa mchakato wa kuchagua, ambamo baadhi ya vijana hatimaye watasita kuendelea kushiriki.

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

Kuhusiana na vipengele vyote vilivyowasilishwa hapo juu, ni muhimu kutambua kwamba, kadiri wahuishaji wanavyopata tajiriba, ndivyo wanavyoweza kuwasaidia vizuri zaidi vijana chipukizi kuunda na kutekeleza shughuli zao zinazokamilishana — shughuli ambazo maelezo ya utendaji ya umaizi ambao wameupata kupitia usomaji wa vitabu tofauti na fikra za juu wanazojitahidi kufuata.

## SEHEMU YA 30

Kutokana na majadiliano yetu ya vitengo viwili vya mwanzo vya kitabu hiki, ambayo kimsingi yalikua mawazo kiasili,maandalizi yako ya kutoa huduma kama mhuishaji, katika kitengo hiki, pia yamesogea katika sura fulani za utendaji. Kadiri unavyopata uzoefu katika uwanja huu wa huduma, kurasa za kitabu hiki zitaendelea kukupa mawazo kwa ajili ya kutafakari. Wahuishaji wengi wanakuta vipengele vilivyomo katika sehemu zilizotangulia zenye msaada mkubwa na huzirejelea tena na tena, wakidumisha daftari ambamo wanaandika uzoefu wao na majadiliano pamoja na wahuishaji wenzao. Kwa sasa unashauriwa kumaliza kitengo hiki kwa kutafakari juu ya athari za jitihada unayoifanya kwa wakati huu. Maneno ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, yaliyoandikwa kwa vijana kote ulimweguni, yanawahusu wale wote wanaotaka kufuata njia hii ya huduma:

> **"Haishangazi kuwa ni kundi la rika lenu ambalo linapata tajiriba zaidi katika kuwasaidia vijana chipukizi, na watoto pia, na maendeleo yao kimaadili na ya kiroho, ikilea ndani yao uwezo wa huduma ya pamoja, na urafiki wa kweli. Baada ya yote, kwa kuutambua ulimwengu ambamo hizi roho changa zitahitaji kupita, pamoja na mitego yake yote na pia fursa zake, ninyi mtathamini umuhimu wa uongezaji nguvu wa kiroho na maandalizi. Kwa kutambua kwamba Bahá'u'lláh amekuja kubadilisha vyote viwili maisha ya ndani na hali za nje katika jamii ya wanadamu, ninyi mnawasaidia wale ambao ni wadogo kuliko ninyi kuboresha tabia zao na kuwaandaa kubeba majukumu kwa ajili usitawi wa jumuiya zao. Kadiri wanavyoingia katika balehe, ninyi mnawasaidia kukuza uwezo wao wa kujieleza, pia na kuwezesha hisia zenye nguvu za maadili zijikite ndani mwao. Katika kufanya hivyo, hisia zenu wenyewe za kusudi zinakuwa wazi zaidi kadiri mnavyojali agizo la Bahá'u'lláh: 'Acha vitendo, siyo maneno viwe pambo lenu.'"[52]**

# MAREJEO


1. Kutoka barua ya tarehe 11 June 2006 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa mtu binafsi, kwenye *Shughuli za kijamii*: *Makusanyo yaliyoandaliwa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2020), na. 117, uk. 62.

2. Kutoka barua ya tarehe 19 Julai 2006 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa watu binafsi wawili.

3. Kutoka barua ya tarehe 17 April 1936 ilioandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwamtu binafsi, iliyochapishwa katika *Maagizo kutoka Mlinzi* (New Delhi: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1973), uk. 84.

4. 'Abdu'l-Bahá, katika makusanyo *Shughuli za kijamii*, na. 190, uk. 112–13.

5. Kutoka hotuba iliyotolewa tarehe 20 Septemba 1912, yaliyochapishwa kwenye *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*: *Hotuba zilizotolewa na 'Abdu'l-Bahá mnamo kipindi cha Ziara Yake Amerika na Canada katika mwaka 1912* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2012), aya. 9, uk. 471.

6. Kutoka hotuba iliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá tarehe 4 Mei 1912, kama hapo juu., aya. 9, uk. 125.

7. Taarifa ya maneno ya 'Abdu'l-Bahá kama ilivyotongolewa na J. E. Esslemont, *Bahá'u'lláh na wakati mpya: Utambulisho wa Imani ya Kibahá'í* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2006, 2017 kuchapisha), uk. 101.

8. Kutoka hotuba iliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá tarehe 4 Mei 1912, iliyochapishwa kwenye *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 7, uk. 123.

9. Kutoka hotuba iliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá tarehe 26 Mei 1912, kama hapo juu., aya. 1, uk. 204.

10. 'Abdu'l-Bahá, kwenye *Baadhi ya maswali yaliyojibiwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2014, 2016 kuchapisha) na. 84.2, uk. 440.

11. *Nyaraka za 'Abdu'l-Bahá Abbas* (New York: Kamati ya Uchapishaji ya Kibahá'í, 1915, 1940 kuchapisha) juz. 2, uk. 276.

12. *Khitábát: Hotuba za 'Abdu'l-Bahá* (Hofheim-Langenhain: Bahá'í-Verlag, 1984), ku. 131–32.

13. Kutoka hotuba iliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá mnamo tarehe 4 Mei 1912, ilichapishwa kwenye *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 8, uk. 124.

14. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2010, 2015 kuchapisha), na. 230.1, uk. 428.

15. Kutoka hotuba iliyolewa tarehe 10 Novemba 1911, iliyochapishwa kwenye *Mazungumzo ya Paris*: *hotuba zilizotolewa na ‘Abdu’l-Bahá mwaka 1911* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2006, 2016 kuchapisha), na. 29.41, uk. 113.

16. *‘Abdu’l-Bahá kwenye Falsafa Takatifu* (Boston: The Tudor Press, 1918), uk. 30.

17. *Mateuzi kutoka Maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá*, na. 24.1, ku. 78–79.

18. *Nyaraka za Abdul-Baha Abbas* (New York: Kamati ya Uchapishaji la Kibahá’í, 1909, 1930 kuchapisha), juz. 1, uk. 63.

19. *Mateuzi kutoka Maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá*, na. 155.4, uk. 253.

20. ‘Abdu’l-Bahá, *Siri za Ustaarabu Mtukufu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2007, 2016 kuchapisha), aya. 118, uk. 83.

21. *Hema la Umoja: Majibu ya: Bahá’u’lláh kwa Mánikchí Ṣáḥib na Maandiko mengine* (Haifa: Makao Makuu ya Ulimwengu ya Kibahá’í, 2006), na. 1.11, ku. 7–8.

22. Kutoka hotuba iliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá tarehe 27 Oktoba 1911, iliyochapishwa kwenye *Mazungumzo ya Paris*, na. 12.8, uk. 42.

23. *Nyaraka za ‘Abdu’l-Bahá Abbas*, juz. 1, ku. 71–72.

24. *Mateuzi kutoka Mandiko ya ‘Abdu’l-Bahá*, na. 97.1, ku. 177–78.

25. *Nyaraka za Bahá’u’lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1988, 2005 kuchapisha), na. 6.40, uk. 72.

26. *Tangazo la Bahá’u’lláh kwa Wafalme na Viongozi wa ulimwenguni* (Haifa: Bahá’í World Centre, 1967, 1978 kuchapisha), uk. 78.

27. *Makusanyo kutoka maandiko ya Bahá’u’lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1983, 2017 kuchapisha), XLIII, aya. 2, uk. 104.

28. Kutoka hotuba iliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá tarehe 3 Disemba 1912, iliyochapishwa kwenye *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu,* aya. 3, ku. 648–49.

29. *Nyaraka za Bahá’u’lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 9.20, uk. 143.

30. Kama hapo juu., na. 11.28, uk. 172.

31. *Nyaraka za ‘Abdu’l-Bahá Abbas*, juz. 1, uk. 31.

32. Kama hapo juu., uk. 194.

33. Bahá’u’lláh, *Waraka kwa mwana wa mbwa mwitu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1988, 2016 kuchapisha), uk. 12.

34. *Nyaraka za Bahá’u’lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas*, na. 11.27, uk. 172.

35. Kama hapo juu., na. 11.30, ku. 172–73.

36. Kama hapo juu., na. 13.15, uk. 199.

37. *Makusanyo kutoka maandiko ya Bahá'u'lláh*, XVIII, aya. 1, uk. 47.

38. *Sala na Tafakari za Bahá'u'lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1987, 2008 kuchapisha), XXXII, uk. 41.

39. *Hema la Umoja*, na. 1.2, uk. 4.

40. Kutoka hotuba iliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá tarehe 5 Mei 1912, iliyochapishwa kwenye *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 3, uk. 130.

41. *Sala na Tafakari*, CXIII, uk. 191.

42. Bahá'u'lláh, kwenye *Sala za Kibahá'í: Makusanyo kutoka Sala zilizofunuliwa na Bahá'u'lláh, Báb na 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2002, 2017 kuchapisha), ku. 181–82.

43. *Sala na Tafakari*, CLXXVIII, uk. 299.

44. Kama hapo juu., LXXIX, ku. 131–32.

45. Bahá'u'lláh, kwenye *Sala za Kibahá'í*, ku. 219–20.

46. 'Abdu'l-Bahá, kama hapo juu., ku. 243–44.

47. Kama hapo juu., uk. 28.

48. Bahá'u'lláh, kama hapo juu., uk. 183.

49. Báb, kama hapo juu., uk. 186.

50. 'Abdu'l-Bahá, kama hapo juu., uk. 197.

51. *Sala na Tafakari*, XCI, ku. 154–55.

52. Kutoka ujumbe wa tarehe 1 Julai 2013 ulioandikwa kwa washiriki wa makongamano 114 kote ulimwenguni, uliochapishwa kwenye *Muundo wa Utendaji: Jumbe za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu zilizochaguliwa na nyenzo ya ziada, 2006–2016* (West Palm Beach: Palabra Publications, 2017), na. 27.4, uk. 176.